**7 SEPTEMBA, 2023**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA MBILI**

**Kikao cha Nane – Tarehe 7 Septemba, 2023**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. NENELWA J. MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) K.n.y. WAZIRI WA FEDHA:**

Maelezo ya Waziri wa Fedha kuhusu Muswada wa Sheria ya Ununuzi wa Umma wa mwaka 2023.

**MHE. MARIAM M. NYOKA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Muswada wa Sheria ya Ununuzi wa Umma wa Mwaka 2023.

**SPIKA:** Ahsante sana.

Katibu.

**NDG. NENELWA J. MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

**MASWALI KWA WAZIRI MKUU**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, aje hapa mbele. *(Makofi)*

Ahsanteni sana, Waheshimiwa Wabunge tutaanza na Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mbunge wa Mlalo.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, nishati ya mafuta ni nishati ambayo ni muhimu sana kwa Taifa letu, kwanza kwa sababu ni sehemu ya ulinzi na usalama wa nchi, lakini pili pia ni sehemu ambayo inachangia kwa mawanda mapana shughuli zote za kiuchumi katika nchi yetu. Lakini miezi ya hivi karibuni kuanzia Mwezi wa Saba, Mwezi wa Nane na hata Mwezi huu wa Tisa kumekuwa na sintofahamu kwenye eneo hili la sekta ya nishati. Upatikanaji wa mafuta umekuwa ni wa mashaka pia bei zimekuwa zikibadilika bila ya kuwa na mpangilio maalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hali ambayo ni ya kushangaza zaidi ni kwamba wiki moja ama mbili kabla ya kutangazwa bei ya mafuta kama utaratibu ulivyo kwamba kila Jumatano ya kwanza ya mwezi mpya bei ya mafuta zinatangazwa, mafuta huwa hayapatikani, bei ikishatangazwa tayari mafuta yanaanza kupatikana.

Mheshimiwa Spika, nataka kufahamu ni upi mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba Taifa linakuwa na mafuta wakati wote, lakini pia kuhakikisha kwamba yanapatikana kwa bei ambayo Watanzania kote nchini wanaweza kuimudu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kwanza ninakiri kwamba tunazo changamoto za upatikanaji wa mafuta nchini, kwa sababu baadhi ya vituo kwenye maeneo mbalimbali vimekuwa vikikosa mafuta na Watanzania wanaohitaji huduma hii maeneo kadhaa tumeona wakiwa wanalalamika kukosekana kwa mafuta.

Mheshimiwa Spika, ziko jitihada kadhaa zinafanywa na Serikali kupitia mifumo yetu ya upatikanaji wa mafuta, Wizara imekuwa ikifanya jitihada pia za kuona upatikanaji wa nishati hii unakuwepo, pia hata Kamati ya Bunge ya Nishati imekaa mara kadhaa na Wizara kuona mwenendo wa upatikanaji wa nishati hii. Nasi tunajua nishati hii ina msaada mkubwa kwenye maeneo mengi na ndiyo inasaidia pia kufanya shughuli za kiuchumi ziweze kwenda.

Mheshimiwa Spika, kufuatia mabadiliko ya Mheshimiwa Rais aliyoyafanya juzi, tumeanza kumwona Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu akifanya vikao kadhaa ndani ya Wizara kukutana na wadau. Sasa kwa kuwa ameshaanza hii kazi, niendelee kumuagiza Naibu Waziri Mkuu kushughulikia hili. Muhimu zaidi nishati yenyewe ipatikane nchini, suala la bei tunajua bei zinabadilika wakati wowote, lakini kwanza nishati ipatikane kwenye vituo vyote na maeneo yote nchini. Pili Watanzania wapate hii huduma na upatikanaji huu ni muhimu kuhusisha pia taasisi zote za mafuta, *EWURA* na taasisi nyingine zote wale wanunuaji wa mafuta kwa *bulk,* lakini pia Taasisi ya Ununuaji wa Mafuta tutengeneza kikao kikubwa na Wizara kadhaa zinazohusika, Wizara ya Fedha, Ofisi ya Uratibu, Ofisi ya Waziri Mkuu mkae pamoja, muone namna ya upatikanaji wa mafuta, suala la bei tutaanza kuliangalia hapo baadae kwa sababu bei zinabadilika kutegemeana na upatikanaji.

Mheshimiwa Spika, pia tupanue wigo wa waagizaji wa mafuta ili tuwe na mafuta mengi nchini kwa usalama wa Taifa letu. Kama hili litafanyika ndani ya wiki moja tutakuwa tumeshapata majibu na tutawapa taarifa Watanzania, lakini tutahakikisha kwamba nishati hii ya mafuta inapatikana na Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu atashughulikia hilo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Shangazi naona ameketi, kwa hivyo hana swali la nyongeza. Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo, Mbunge wa Mwanga, sasa aulize swali lake.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi hii ya kuuliza swali.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, nchi yetu kupitia Bunge hili ilitunga sheria nyingi nzuri za kulinda uhifadhi hapa nchini na hasa kuzuia uwindaji haramu kwa ajili ya kukuza utalii, kulinda ikolojia na pia kuongeza Pato la Taifa kupitia mapato yanayotokana na utalii. Hivi karibuni Mheshimiwa Waziri Mkuu, wanyamapori hawa ambao tumewahifadhi kwa mujibu wa sheria zetu na pia kwa kuheshimu mikataba ya Kimataifa katika eneo hili wamegeuka kuwa janga kwa kuharibu mali za watu, kuvuruga miundombinu na hata kusababisha watu wengi kupoteza maisha.

Je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha kwamba tunapitia upya sheria hizi ambazo tuliziweka kwa ajili ya kulinda uhifadhi ili pia ziwalinde wananchi wetu na hata ikibidi kujitoa kwenye baadhi ya mikataba ya Kimataifa ambayo inatushurutisha kuweka sheria za namna hii ambazo zinawadhuru wananchi wetu na mali zao? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tadayo, Mbunge wa Mwanga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kupitia vikao vyetu vya Bunge hapa na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakieleza usumbufu ambao wananchi kwenye maeneo yetu wanaupata kwa wanyama waliohifadhiwa kwenye maeneo mbalimbali kwenye misitu yetu kuhamia kwenye makazi ya watu na kusababisha uharibifu wa mali, lakini pia hata maisha ya watu, na tumepata taarifa hizi mara nyingi kwenye miji iliyoko kando kando na hifadhi zetu.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba tunazo sheria zinazosimamia utekelezaji huu wa kuhakikisha kwamba wanyama

wanabaki porini na wananchi wanaendesha maisha yao kwenye maeneo yao rasmi. Pia kumekuwa na wimbi kubwa la ongezeko kubwa la wanyama kwenye misitu yetu na hii ilitokana na jitihada tulizozifanya kupitia sheria zetu hizo hizo za kulinda uwindaji haramu, hili ndiyo limepelekea kuwa na idadi kubwa ya Wanyama.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Wizara ya Maliasili imekuwa ikifanya taratibu kadhaa kukutana na vikao na Wizara ambata zinazohusika kwenye uhifadhi wa mazingira yetu, wa misitu yetu, wanyama wetu na kuona kuwa wanyama wanabaki huko, jitihada kadhaa ambazo zimechukuliwa ni pamoja na kuongeza idadi ya Maaskari ambao pia wameweka vituo kando kando ya maeneo haya ili kuzuia wanyama kuingia, lakini pia tumeona jitihada za kutumia hata ndege kufukuza wanyama kuingiza porini.

Mheshimiwa Spika, tunajua ziko sheria zinalinda haya na Mheshimiwa Mbunge ametaka tubadilishe sheria, lakini muhimu sasa ni Wizara kuhakikisha kuwa maeneo yote yaliyohifadhiwa kwa ajili ya kuweka wanyama yanaendelea kusimamiwa na sheria zake, lakini na taratibu hizo ambazo wamezipanga kwa ajili ya kudhibiti wanyama hawa kuingia kwenye makazi. Hii ni pamoja na kulinda ile *buffer* ambayo tuliitenga kilometa tano kutoka makazi kuingia kwenye msitu na baadaye tukaruhusu wananchi wafanye shughuli zao za uzalishaji mali, shughuli za maendeleo kwenye hifadhi ile ya kilometa tano, lakini sasa inaonekana pia wanyama wanavuka hifadhi hiyo na kuingia kwenye makazi ya watu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ziko jitihada zimechukuliwa na Wizara ya Maliasili na Utalii na wameunda timu ya kufanya ukaguzi wa maeneo haya na kubaini tatizo *exactly* ni nini hasa kinapelekea wanyama kutoka kule kuingia huku, baada ya kamati ile kukamilisha kazi yao tutapata majibu. Kwa hiyo, niwaahidi kwamba hili ilimradi Wizara imeshaanza kuunda timu ya kwenda kukagua na kugundua tatizo ni nini, baada ya kubaini tatizo, kama tatizo hilo pia litagusa kwenye sheria basi Wizara itatuongoza katika kuleta sheria hapa tufanye mabadiliko ili tuweze kuhifadhi, lakini pia tuhakikishe kwamba wananchi

wanaendesha shughuli zao na maisha yao yanaendelea kuimarishwa na kulindwa kama ambavyo tuliweka sheria hizi awali na hatukuwa na tatizo hili hapo mwanzo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nilitaka nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa ushauri wake kwa Serikali sisi tunauchukua, lakini kwa kuwa timu ilishaanza kazi, tuipe muda timu yetu ikamilishe kazi, halafu ije na mkakati ambao imeuweka na tutaona mkakati huo na jinsi ambavyo utaweza kulinda maisha ya watu, utaweza kulinda pia na hawa wanyamapori wakiwa kwenye maeneo yao. Hii ndiyo njia sahihi ambayo itatusaidia katika kuzuia madhara yaliyojitokeza kwenye makazi ya watu hasa yale makazi yaliyopo karibu na sehemu za hifadhi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda, Mbunge wa Kigoma Mjini, sasa aulize swali lake kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi ya kumuuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, sera yetu ya viwanda hapa nchini imetuwezesha kupata viwanda vingi sana na kuwafanya Watanzania watumie bidhaa nyingi ambazo zinatengenezwa hapa nchini. Hata hivyo, sera hii bado haijapiga hatua kubwa katika viwanda vinavyoongeza thamani ya mazao ya wakulima, wafugaji na wavuvi. Tunataka tuone viwanda vya maziwa, vya nyama, tunataka kuona viwanda vya kusindika samaki, dagaa, na viwanda vya kusindika matunda.

Je, ni nini mpango wa Serikali katika kuongeza viwanda vya kusindika au kuongeza thamani ya mazao ya wakulima? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ng'enda Kilumbe, Mbunge wa Kigoma Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu imeendelea kutafuta mbinu mbalimbali za kuwawezesha Watanzania wanaojishughulisha kwenye sekta zote zinazozalisha mali na kuongeza uchumi, kuhakikisha kwamba tunaongeza thamani ili mapato yawe makubwa zaidi ikiwemo na sekta ambazo Mheshimiwa Mbunge amezieleza, Sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Spika, sekta hizi zimekuwa na manufaa makubwa kwa sababu sekta hizi ndiyo zina uwezekano wa kuwa na viwanda vingi kwa sababu zinakuwa na malighafi nyingi, na kwa hiyo, mkakati wa Serikali kuongeza viwanda zaidi ya viwanda tulivyonavyo, ni kuhakikisha kuwa na hili tumeshalifanya la kujenga mazingira mazuri ya uwekezaji hapa nchini ili kuweza kuwavutia wawekezaji wanaotaka kujenga viwanda, awe Mtanzania au yeyote kutoka nje ya nchi kwa maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, pia tumefungua wigo wa kuhakikisha kuwa, wawekezaji wote wanapokuja nchini tunawahakikishia uwekezaji wao kuwa salama. Kwa hiyo suala la usalama kwa wawekezaji wetu tumelipa nafasi kubwa ili kuwakaribisha walio wengi sana. Hata hivyo, tumeimarisha miundombinu inayowawezesha wafanyabiashara wanaotaka kujenga viwanda kuendesha viwanda vyao na kupata faida, kama vile barabara na Watanzania mnaona barabara zote nchini zimejengwa na zinaendelea kujengwa, reli lakini pia njia ya anga, tumeshanunua na ndege ya kupeleka mazao nje ya nchi. Hii yote ni kuvutia wawekezaji wetu, hata pia ukanda wa bahari na maziwa tumeongeza meli ili kuwezesha kusafirisha bidhaa zao kwa ajili ya kufuata masoko. Uboreshaji wa mazingira haya ya miundombinu unamuwezesha kumpa uhakika muwekezaji kujenga kiwanda popote nchini ili aweze kutumia malighafi tulizonazo aweze kufanya biashara yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, tulikuwa tunaangalia wafanyabiashara wengi, wawekezaji wengi wa viwanda wanakwazwa wapi? Tukagundua kwamba tulikuwa na tozo nyingi sana za uwekezaji. Tumepunguza tozo ili kumuwezesha yeye kufanyabiashara na kupata faida na bado mkakati wetu wa kufanya mapitio ya mara kwa mara ya uwekezaji wetu unafanywa kuvutia wawekezaji hao.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nitoe wito tena kwa Watanzania wenye uwezo kujenga viwanda ndani ya nchi, malighafi tunazo kwa sababu Sekta ya Kilimo imepata mabadiliko makubwa, Mifugo nako pia tuna malighafi za kutosha na uvuvi nako pia tumeimarisha uvuvi bora na wa kisasa kwa lengo la kupata malighafi nyingi za kuendesha kwenye viwanda vyetu, lakini pia tunajaribu kuhakikisha kwamba tuna tunasikiliza kero za wawekezaji. Hii inatoa fursa sasa ya Mwekezaji kufanya maamuzi kuja nchini na ndiyo kwa sababu wakati wote tumekuwa na maonyesho ya viwanda, maonyesho ya kilimo ili kuwahakikishia kwamba viwanda vina nafasi vilivyopo na vile ambavyo vinakuja, lakini kwenye maonesho ya mazao kuonesha uwepo wa malighafi hapa nchini. Tunaendelea kufanya haya kwa kutoa wito na kufanya maboresho ya maeneo yote niliyoyatamka ili kukaribisha viwanda zaidi hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, huo ndiyo mpango wetu ambao tunao wa kuwezesha kuongeza viwanda viweze kuleta faida nchini na sisi tunaamini kwamba tukiwa na viwanda kwanza tunatengeneza ajira kwa Watanzania, mbili, tunapata kodi ya hawa wawekezaji wanalipia, tatu tunahakikisha kuwa huduma mbalimbali zinazohitajika viwandani wale majirani wananufaika nazo. Hayo yote ni manufaa ambayo tunayapata na kwa hiyo wito wako uliotokana na swali lako, tutaendelea kuusimamia na kuyasimamia hayo maboresho tunayoyafanya kwa lengo la kuvutia wawekezaji zaidi wa kujenga viwanda hapa nchini. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Zainab Athman Katimba, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA:** Mheshimiwa Spika ahsante, zao la chikichi ni zao ambalo linaweza kuleta ukombozi mkubwa kwa Taifa katika kujitosheleza katika uzalishaji wa mafuta ya kula nchini, hasa ukizingatia kwamba kujitosheleza katika uzalishaji wa mafuta ya kula nchini kutasaidia kupunguza changamoto ya nakisi ya urari wa malipo inayotokana na uagizaji wa bidhaa nyingi kutoka nje ya nchi.

Je, ni upi mkakati wa Serikali wa kuhakikisha kunakuwa na programu endelevu ya kukuza zao la chikichi katika Ukanda wa Ziwa Tanganyika ikiwa ni pamoja na maeneo mengine ya nchi ambapo zao la chikichi linastawi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zainab Katimba, Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge amezungumzia zao la mchikichi, ni kweli kwamba Serikali yetu tulishaanza mkakati wa kulirudisha zao hili kwa wakulima kwa kulima kisasa na kupata mbegu bora ili tuongeze uzalishaji ukilinganisha na uzalishaji tuliokuwanao awali ambao ulikuwa unatumia mbegu ambazo hazizalishi na kutoa mafuta mengi, lakini pia hata hamasa ya kilimo cha chikichi ilipungua sana.

Mheshimiwa Spika, tulipokuwa tunaanza kurudisha zao hili liwe kwenye mpango wetu wa kiserikali, inatokana na mahitaji makubwa ya mafuta hapa nchini. Kwa hiyo, mkakati wa kupata mafuta ya kula hapa nchini unatokana na mkakati wa ndani kwa mazao hayo ya chikichi na mazao mengine kama vile alizeti na mazao yote yanayotoa mafuta.

Mheshimiwa Spika, mkakati wa Serikali katika kulipanua zao hili, kwanza tumeimarisha kuwa na kituo cha utafiti, na kule Kigoma tumejenga kituo cha utafiti na ndicho ambacho kimeleta mafanikio makubwa kwa kupata mbegu yetu wenyewe Watanzania kutoka kwenye vituo vyetu. Ndiyo hiyo ambayo tumeipanda na sasa inaendelea vizuri na tunafanya ukaguzi wa mara kwa mara na tumethibitisha kwamba mbegu yetu inafanya vizuri.

Mheshimiwa Spika, pia utafiti huu unakwenda sambamba na kutafiti udongo unaoweza kumea mchikichi na kupata matunda, siyo tu kwa ukanda wa Ziwa Tanganyika bali na maeneo mengine yote nchini ili tulipande zao hili, liwe pana, na watu wanaoshughulika na kilimo waweze kuingia kwenye sekta

hiyo wakiwa na uhakika kwamba wanapanda mchikichi kwenye ardhi ambayo inaweza kuzalisha zaidi. Hiyo ni moja.

Mheshimiwa Spika, pili, tumeanza kampeni ya zao hili na sasa imeanza kuleta matunda. Tunaona pia Mkoa wa Tabora wanalima, tumeona Mikoa ya Pwani, Mkoa wa Pwani wenyewe, Dar es Salaam, ndiyo twende Lindi, Mtwara, tunaona maeneo yote yanayopanda zao la minazi pia tunaambiwa yanaweza kustawisha zao la mchikichi. Huu ni mpango wa kupanua zao hili ili tupate mazao mengi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia tunapoanza na mkakati huu kupitia kituo chetu cha utafiti na kuzalisha mbegu nyingi, tumeanza kutoa mbegu inayozalishwa bure kwa wakulima katika kipindi kisichozidi mwaka mmoja ili kupanua wigo wa watu ambao wanaanzisha kilimo hiki ili waweze kupanda zao hili la mchikichi, huku pia tukiimarisha uwekaji wa viwanda vidogo vidogo kwa ajili ya wachakataji, kwa sababu baada ya kuwa tumezalisha, tunahitaji sasa tuone matokeo. Hii itasaidia watu wengi kuingia kwenye kilimo na kuwezesha kulima zao hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mkakati huu wa kukuza zao hili tunausimamia toka tulipoanza kulima zao hili Kigoma, na Mkoa wa Kigoma ni watu ambao wameanza mara moja kulilima zao hili na mafanikio tunayaona na tunaona mikoa mingine nao pia wanachukua miche na upandaji tunaona maendeleo yake. Kwa hiyo, tunataka tuhakikishe kwamba zao la chikichi sasa linaanza kuchangia upatikanaji wa mafuta ndani ya nchi na mazao yake mengine na kunufaisha yeyote ambaye anaingia kwenye kilimo cha chikichi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wakulima wa zao la chikichi kwamba Serikali itaendelea kusimamia maendeleo ya zao hili na hapo baadaye litakapokuwa kubwa tunaweza tukaliundia chombo chake cha usimamizi wa zao hili ili pia liweze kusimamiwa kwa ukaribu zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, malengo yetu ni kwamba tunatoa fursa kwa Watanzania wanaotaka kulima kilimo wawekeze kwenye

mashamba makubwa, wanaotaka kujenga viwanda na tumehusisha pia na taasisi za umma na taasisi binafsi kulima zao hili. Kule Kigoma tuna Magereza, Magereza zote zinalima chikichi, shule za msingi nyingi zimekuwa na mashamba yao, wanalima chikichi, pia Jeshi la Kujenga Taifa, JKT Bulombora nao wana shamba kubwa zaidi ya ekari 4,000 na tunaendelea kuhamasisha taasisi zote zilime zao hili lilete manufaa makubwa.

Mheshimiwa Spika, niwahamasishe Watanzania kulima mchikichi kwa faida yao. Tulime mchikichi kwa ajili ya kupata mafuta mengi, tulime mchikichi kwa sababu na yenyewe inatoa sabuni na bidhaa nyingine ambazo pia zinaleta faida kwenye zao hili.

Mheshimiwa Spika, huo ndiyo mkakati wa Serikali wa kupanua zao hili. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Jackson Gideon Kiswaga, Mbunge wa Kalenga.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi kumwuliza Waziri Mkuu swali. Kwa kuwa tabia za watu za uharibifu wa mazingira zimesababisha kuwa na nchangamoto za ukosefu wa mvua na hivyo kuhatarisha pengine usalama wa chakula katika Taifa letu na hivyo kusababisha pia mabadiliko ya tabianchi: Je, ni mpango gani wa Serikali sasa kuzuia kabisha shughuli za kibinadamu kwenye milima yote na vilima vyote ili sasa tuwe na mvua za uhakika na hivyo kulifanya Taifa liendelee kuwa imara katika emneo hilo? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kiswaga Mbunge wa Kalenga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala la uhifadhi wa mazingira Serikali yetu tumeliwekea nguvu kwa sababu tunataka tulinde mazingira haya kwa misitu yetu, mito na vyanzo vya maji kwa lengo la kufanya Taifa hili kuwa endelevu na kutoa fursa za upatikanaji wa maji na pia tupate mvua za kutosha kupitia misitu.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais eneo la Mazingira wamefanya kazi kubwa na wanaendelea kufanya kazi kubwa kukabiliana na uharibifu wa mazingira. Kwanza ziko sheria zinasimamia uhifadha wa mazingira ambapo pia wenyewe tumeendelea kushirikisha mpaka kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa; mkoani, wilayani na kwenye halmashauri zote na vijijini ambapo ndiyo misitu ilipo, kila mmoja ashiriki katika uhifadhi wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, pia tumeendelea kutoa elimu kwa Watanzania kuhusu umuhimu wa uhifadhi wa mazingira, misitu yetu pamoja na vyanzo vya maji kwa sababu vyote hivi vina umuhimu mkubwa kwenye maisha ya kila siku ya binadamu. Hata hivyo, tumekuwa tunashirikisha taasisi mbalimbali za umma na zile za binafsi kwenye uhifadhi wa mazingira na kwenye eneo hili tunaungwa mkono sana. Malengo yetu ni kukabiliana na changamoto ya mabadiliko ya tabianchi

Mheshimiwa Spika, kubwa zaidi ni programu mbalimbali zilizoko ndani ya Serikali zinazosimamia uhifadhi wa mazingira kwenye milima hiyo ya miinuko, kwenye mabonde na maeneo yote ambayo yana misitu ambayo tunaitumia kwa ajili ya kuhifadhi mazingira yetu. Kwa hiyo, nitoe wito kwa Watanzania, kwanza kuona umuhimu wa uhifadhi wa mazingira kwa maslahi yetu.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko ya kupatikana kwa mvua yanatokana na uharibifu wa mazingira ambao sasa unaendelea; pia ukosefu wa maji kwenye maeneo ambayo tulikuwa tunatarajia tupate maji kama vyanzo ili tujenge miradi ya maji inatokana na uharibifu wa mazingira. Madhara haya na madhara mengine ndiyo yanasababisha sasa kuwa na mabadiliko ya majira, kuhamahama kwa wanyama kutoka kwenye maeneo yao kuhamia kwenye maeneo mengine wakitafuta maji na aina nyingine yoyote ya usumbufu ambao tunaupata.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, nataka niwakikishie kwamba Serikali inao mpango huo wa kuhifadhi mazingira, kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais na tumeipeleka hiyo mpaka TAMISEMI, tusimamie kwa pamoja

tuhakikishe kwamba nchi yetu tunakabiliana na uharibifu wa mazingira. Kwa kufanya haya, tunaweza sasa tukaokoa mazingira yetu na tukaanza kunufaika na uwepo wa misitu hii, vyanzo vya maji na aina nyingine yoyote ya uhifadhi ambayo tumeiwekea sheria, na tutaendelea kuimarisha sheria zetu na kusimamia sheria zetu. Vile vile taasisi zote ambazo zinahusika katika uhifadhi zisimamie kikamilifu. Huo ndiyo mkakati wetu tulionao ndani ya Serikali, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Serikali imekuwa ikitekeleza miradi ya elimu na afya nchini kwa kujenga majengo mbalimbali, lakini pamoja na Serikali kutekeleza miradi hiyo pia wananchi wamekuwa wakitumia nguvu kubwa kuhakikisha wanasaidiana na Serikali katika kuhakikisha wanajenga majengo hayo kwenye maeneo yao: Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha wanabainisha majengo yote ambayo ni maboma nchini ili yaweze kumaliziwa na wananchi waweze kuona thamani ya nguvu yao lakini na fedha ya Serikali inayokwenda kwenye maeneo yao ili wananchi waweze kutumia? Nashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala la ujenzi wa miradi, iwe ya elimu au afya ambayo inahusisha majengo na yasipokamilika sasa yanakuwa ni maboma, ni mkakati ambao sisi Serikali tumeuelekeza zaidi kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Tuna upatikanaji wa vyanzo vya fedha wa aina mbili; moja, kutoka Serikali Kuu. Kutoka Serikali Kuu, tunapeleka fedha kwenye halmashauri za kujenga majengo haya kwa thamani ya jengo lenyewe na kwa hiyo basi, kunatakiwa kuwa na usimamizi baada ya fedha hizi kuzipokea kuhakikisha kwamba jengo lenyewe linajengwa kwa thamani ile ile ambayo wao walitoa makadirio na

Serikali Kuu kupeleka fedha kwenye Sekta ya Elimu na Afya tunapojenga vyumba vya madarasa, nyumba za walimu, matundu ya vyoo na majengo mengine, kwenye afya pia zahanati, vituo vya afya na hospitali.

Mheshimiwa Spika, pia kuna fedha ya aina ya pili inayotokana na mapato ya ndani ya halmashauri zenyewe ambapo wao halmashauri hupanga mpango wa maendeleo yao kupitia bajeti yao kwenda kujenga. Maboma mengi yanatokana na mipango ya fedha hizi za halmashauri. Kwa nini mpango wa Serikali haukukamilisha maboma?

Mheshimiwa Spika, nataka niiagize sasa TAMISEMI, kwanza iendelee na utaratibu wa kubaini maboma yote ambayo wao waliyajenga na hayakukamilika na wahakikishe wanaendelea kutenga bajeti za kukamilisha maboma hayo kwa sababu yametokana na bajeti zao. Uzoefu tulioupata wakati wa ukaguzi wa miradi hii, majengo yote yaliyopelekewa fedha za Serikali Kuu yamekwenda kama yalivyo na pale ambapo hayakukamilika hatua kali zimechukuliwa. Nao wametakiwa kukamilisha fedha kwa kuwa wameshindwa kukamilisha ujenzi wa jengo hilo kwa fedha ambayo ilikuwa imepelekwa. Sasa kwa kuwa maboma mengi yanatokana na mipango yao na kushindwa kuiendeleza, bado wanatakiwa kuweka bajeti ya kukamilisha majengo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mkakati wa Serikali sasa ni kuhakikisha maboma hayo yanakamilika kwa agizo hili ninalolitoa kwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Kila halmashauri ifanye tathmini ya miradi yake, ione maeneo gani walianza miradi na wameshindwa kukamilisha na yamebaki maboma ambayo Waheshimiwa Wabunge sasa wanataka waone mpango wa Serikali, ili sasa wapange bajeti ya kila mwaka kuhakikisha kwamba maboma haya yanakamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunajua kwamba zahanati ni shilingi milioni 50, vyumba vya madarasa ni shilingi milioni 20 na fedha zote zinapatikana kwenye halmashauri. Zipo halmashauri zinapata zaidi ya shilingi bilioni tatu mpaka nne kwa mwaka, hawawezi kushindwa kupata shilingi milioni 20 ya kukamilisha chumba cha

darasa, au shilingi milioni Hamsini za zahanati, au shilingi milioni 300 kwa ajili ya kujenga zahanati na kituo cha afya. Kwa hiyo, agizo langu bado linabaki pale pale kwamba tunahitaji sasa halmashauri zisimamie.

Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali ni kuhakikisha kwamba maboma yote haya yanakamilika ili huduma zianze kutolewa kwa wananchi walioko kwenye maeneo hayo, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Hassan Seleman Mtenga, Mbunge wa Mtwara Mjini, sasa aulize swali lake.

**MHE. HASSAN S. MTENGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kumwuliza swali Waziri Mkuu. Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuwa nchi yetu imeamua kuongeza wigo wa diplomasia wa uchumi kwa kufungua milango ya kibiashara na kimawasiliano: Ni upi mkakati wa Serikali katika kutekeleza miradi ya ujenzi wa madaraja yanayounganisha nchi kuendana na uchumi ambao sasa tunautarajia katika nchi yetu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Mtenga, Mbunge wa Mtwara Manispaa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge anahitaji kujua mpango wa Serikali wa kuimarisha ujenzi wa madaraja kwa lengo la kuimarisha diplomasia ya kiuchumi na mawasiliano kati ya nchi yetu na nchi jirani. Mkakati wa Serikali katika kuimarisha diplomasia ya kiuchumi na mawasiliano ni mkakati endelevu na hakika kwenye eneo hili lazima nimpongeze kwanza Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye ameifungua nchi kwa kuimarisha diplomasia ya kiuchumi na mahusiano na mataifa mengi duniani na tumeanza kuona manufaa ya marafiki wengi kuja nchini kuwekeza katika maeneo mbalimbali. Hii inatokana na jitihada hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa Mheshimiwa Mbunge anataka kujua mpango wa kuendelea kujenga daraja. Najua anachotaka kukiuliza ni nini? Wiki mbili zilizopita nilikuwa Mkoani Mtwara, na moja kati ya jambo ambalo yeye aliliuliza hadharani ni ujenzi wa daraja wanalolihitaji wakazi wa Mkoa wa Mtwara kwenda nchini Msumbiji. Tuna madaraja mengi. Kule Mkoani Mtwara tuna Daraja la Umoja lile linalotoka Wilaya ya Nanyumbu kwenda Msumbiji. Linaitwa Daraja la Umoja, daraja zuri, kubwa, linalounganisha hizi nchi.

Mheshimiwa Spika, pia tuna madaraja mengine; kule Mkoani Mbeya Wilaya ya Kyela tuna daraja pale Kasumulu, linaunganisha na Malawi; Ileje tuna daraja la Mto Songwe linaunganisha na Malawi pia; na kule Ngara tumefanya ziara kwenye mradi mkubwa wa umeme wa Rusumo, tuna daraja kubwa linaungfanisha na Rwanda. Tunatarajia kuimarisha ujenzi wa madaraja haya ikiwemo na Mkoa wa Mtwara.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa za Wizara ya Ujenzi kupitia Meneja wa Mkoa wa Mtwara wa *TANROAD* alituhakikishia kwamba liko eneo la Mtwara Vijijini ambalo ndiyo karibu zaidi na Msumbiji, karibu zaidi na maeneo ambayo yana huduma nyingi za kibiashara na mkoa mmoja unaitwa Cabo Delgado, moja kati ya mikoa iliyoko nchini Msumbiji kwamba tayari wameshaanza upembuzi yakinifu ili kujenga daraja kwenye eneo la Kikole, Kikombo ambalo pia litakwenda mpaka Msumbiji. Huo ndiyo mkakati wa kuimarisha ile diplomasia ya kiuchumi na Msumbiji na diplomasia ya mawasiliano na msumbiji kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge anatoka Mkoa wa Mtwara alisisitiza kwamba Wanamtwara wanahitaji zaidi.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa daraja hili siyo kwa Wanamtwara tu, ni taifa zima, kwa sababu sisi na Msumbiji tuna mahusiano na maeneo yote yanayohitaji kujengwa daraja, maeneo yote ambayo yanahitaji kuimarishwa vivuko, na maeneo yote yanayohitaji kuimarishwa malango ya uhamiaji kwa lengo la kujenga mahusiano rahisi na nchi jirani ili kuimarisha uchumi na mawasiliano kwenye nchi hizi.

Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imelichukua jambo hili na kuendeleza jitihada hizi ambazo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wetu amezianzisha na tunataka tuone sasa Watanzania wananufaika na diplomasia hii ya kiuchumi na mawasiliano na nchi jirani na nchi zote ambazo zinajenga mahusiano mazuri na Tanzania.

Mheshimiwa Spika, huo ndiyo mkakati ambao tunao kwa sasa kwenye eneo hili la kuimarisha mahusiano na hasa kwenye maeneo ambayo Mheshimiwa Mbunge anahitaji zaidi Serikali ianze kujenga daraja la kwenda nchini Msumbiji, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na ratiba yetu. Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc*. – KATIBU WA BUNGE:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na maswali ya kawaida. Tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Michael Mwita Kembaki, Mbunge wa Tarime Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 112

**Hitaji la Shule ya Bweni ya Wasichana Tarime Mjini**

**MHE. MICHAEL M. KEMBAKI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Shule ya Bweni ya Wasichana Tarime Mjini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Deo Ndejembi, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Michael Mwita Kembaki, Mbunge wa Jimbo la Tarime Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2021/2022 na 2022/2023, Serikali kupitia Mradi wa *SEQUIP* ilitoa shilingi bilioni 1.054 kwa ajili ya ujenzi wa shule mbili za Gicheri na Nyagisese zenye miundombinu yote ya madarasa, maabara, jengo la utawala na chumba cha kompyuta. Shule hizo zitakapokamilika zitaongezewa miundombinu ya mabweni ili ziweze kudahili wanafunzi wa kike.

**SPIKA:** Mheshimiwa Michael Mwita Kembaki, swali la nyongeza.

**MHE. MICHAEL M. KEMBAKI:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza. Nishukuru Serikali kwa majibu mazuri lakini napenda kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, ni lini Serikali itapeleka fedha kukamilisha ujenzi wa mabweni katika Shule ya Sekondari ya Mogabiri? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, katika Shule ya Sekondari Tarime mabweni yana uwezo wa ku-*accommodate* watoto 750 lakini wanafunzi waliopo katika shule ile ni zaidi ya 1,500. Je, ni lini Serikali itajenga mabweni zaidi ili kutoa huduma ya mabweni mazuri katika Shule ya Sekondari Tarime?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kembaki. La kwanza kuhusu mabweni katika Shule ya Sekondari Mogabiri kwamba ni lini Serikali itapeleka fedha kumalizia ujenzi wa mabweni.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge anafahamu kwamba Serikali Kuu ilipeleka shilingi milioni 200 kwa ajili ya ujenzi wa mabweni na madarasa mawili katika shule hii. Walibadilisha eneo ambalo lilikuwa limewekwa mwanzo kwa ajili ya ujenzi wa mabweni haya hivyo kupelekea gharama za ujenzi kuongezeka.

Mheshimiwa Spika, tathmini imeshafanyika na Halmashauri ya Tarime Mji na imefahamika kwamba inahitajika shilingi milioni 120 kwa ajili ya ukamilishaji wa mabweni haya. Serikali iko katika mchakato wa kutafuta fedha hizi kupitia mapato ya ndani ya halmashauri yenyewe na Serikali Kuu ili kuweza kumalizia ujenzi wa mabweni haya. Mkurugenzi wa Halmashauri hii tayari ameshaleta maombi hayo Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili la Shule ya Sekondari ya Tarime kuwa na wanafunzi wengi, ni kweli kwamba shule hii ina wanafunzi wengi. Kwa kulitambua hilo, Serikali kupitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI katika kupanga wanafunzi wa kidato cha tano mwaka huu shule hii ilipelekewa wanafunzi wachache kulingana na miundombinu ambayo ipo. Tunaendelea kutafuta fedha ili kuona ni namna gani ambavyo tunaweza tukapeleka kwa ajili ya kuongeza mabweni katika shule hii ya Tarime Sekondari.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali mafupi majibu mafupi. Mheshimiwa Aysharose Mattembe.

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi. Kwa kuwa wanafunzi wanaosoma katika Shule ya Sekondari ya Masinda, Kata ya Ihanja, Jimbo la Ikungi Magharibi hutembea umbali mrefu kufuata huduma za masomo. Napenda kujua je, ni lini Serikali itajenga bweni katika shule hiyo ili kuwawezesha wanafunzi kusoma kwa utulivu? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, Serikali itajenga mabweni katika Kata hizi za Msinda na Ihanja ambazo wanafunzi wanatembea umbali mrefu kufuata

elimu kadri ya upatikanaji wa fedha. Natoa wito kwa halmashauri hii waanze kujenga kwa mapato yao ya ndani wakati Serikali Kuu inatafuta fedha kwa ajili ya kwenda kumalizia majengo haya.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, Serikali hii ya Dkt. Samia Suluhu Hassan imepeleka shilingi bilioni tatu katika Mkoa wa Singida kwa ajili ya ujenzi wa shule ya wasichana pale Solya. Ambayo watoto wote wa kike katika Mkoa wa Singida wataenda pale Solya kwa ajili ya kupata elimu ambapo tayari kuna mabweni. Hivi karibuni kuna shilingi bilioni moja nyingine imeongezwa na Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za walimu katika shule ile ya Mkoa wa Solya**.**

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ya kwanza umesema imepeleka kiasi gani?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, Serikali ilipeleka shilingi bilioni tatu na sasa imepeleka shilingi bilioni moja.

**SPIKA:** Sawa, maana ulisema shilingi milioni tatu sasa nataka Taarifa zetu Rasmi za Bunge zikae sawa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, ni shilingi bilioni tatu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Florence George Samizi, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI:** Mheshimiwa Spika ahsante kwa kunipa nafasi. Je, ni lini Serikali itajenga mabweni katika Shule ya Sekondari ya Busagara na Shule ya Sekondari Kumgogo ili tuweze kutoa huduma…

**SPIKA:** Mheshimiwa Samizi subiri kidogo, kwa sababu ni swali la nyongeza, shule moja.

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI:** Mheshimiwa Spika, Je, ni lini Serikali itajenga bweni katika shule ya sekondari ya Busagara ili tuweze kutoa huduma ya Kidato cha Tano na cha Sita kama tulivyoomba?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, Serikali itajenga mabweni katika shule hii ya Busagara kadri ya upatikanaji wa fedha. Mkurugenzi wa Halmashauri aanze kutenga fedha kwenye mapato ya ndani kwa ajili ya ujenzi wa mabweni haya na kisha kuleta maombi Serikali Kuu kwa ajili ya kumalizia mabweni haya ambayo yataanza kwa jitihada za halmashauri yenyewe.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwantumu Zodo, swali la nyongeza.

**MHE. MWANTUMU M. ZODO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa Serikali imepeleka shilingi milioni 470 kwa shule za Kata 231. Je, ni lini sasa Serikali itapeleka fedha za mabweni kwa ajili ya shule hizo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, shilingi milioni 470 zilizopelekwa kwenye shule hizi 231 nchini ilikuwa ni kwa ajili ya kata ambazo hazina sekondari bado katika Taifa letu hili la Tanzania. Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan aliona kuna umuhimu wa kuhakikisha kata ambazo bado hazikuwa na sekondari zinapata sekondari na ndiyo maana ametoa shilingi milioni 470 na mwaka huu kuna shilingi milioni 560 na kuna wengine wamepata hadi shilingi milioni 603 kwa ajili ya ujenzi wa shule hizi za Kata.

Mheshimiwa Spika, tutakapomaliza ujenzi wa shule hizi za kata Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya mabweni kwenye shule hizi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Salome Wycliffe Makamba, swali la nyongeza.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona. Serikali itapeleka lini fedha za kumalizia ujenzi wa bwalo la chakula katika shule ya sekondari ya mfano ya wasichana ambayo ipo katika Jimbo la Shinyanga Mjini?

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Hapo natafakari, swali linahusu mabweni wewe unataka bwalo. Mheshimiwa Naibu Waziri inaonekana majibu anayo, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, Serikali kwanza inamalizia miundombinu mingine, hii ni shule kama niliyosema mwanzo ya Singida ya shilingi bilioni tatu ambayo imejengwa pale Shinyanga Mjini.

Mheshimiwa Spika, Shinyanga Mjini walipata bilioni tatu kwa ajili ya ujenzi wa shule hii ya wasichana ya Mkoa wa Shinyanga, na tayari kuna shilingi bilioni moja nyingine Serikali hii ya Awamu ya Sita imepeleka kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu iliyokuwa imesalia na baada ya hapo itafanyika tathmini nchi nzima kwa ajili ya mabwalo ambayo yanakuwa bado hayajakamilika ili Serikali iweze kutafuta fedha na kuipeleka kwenye ukamilishaji huo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Subira Mgalu, swali la nyongeza.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Spika ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa hizi shilingi milioni 470 kuna baadhi ya maeneo sekondari hizi hazikukamilika bado maabara nyingine hazikukamilika, je, Serikali ina mpango gani wa kufanya tathmini ya kina na kuweza kuongeza ili miundombinu ya shule hizi mpya ikamilike? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, nayaruhusu haya maswali kwa sababu umeshajibu la Mheshimiwa Salome Makamba na ulionyesha utayari, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Subira Mgalu. Hizi shilingi milioni 470 ambazo zilikwenda kwenye ujenzi wa shule za Kata kwenye kata ambazo hazikuwa na shule zilienda na maelekezo maalum na zilitakiwa kutosha. Kuna Halmashauri kwa mfano pale Kongwa Mkoani Dodoma na Bahi Mkoani Dodoma walimaliza kwa shilingi milioni 470. Ni wao kule chini ambao hawakutekeleza maelekezo yaliyopelekwa na Ofisi ya Rais, TAMISEMI na wakategemea kuna fedha nyingine ya kuja kumalizia.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilishafanya tahmini na baada ya tathmini hiyo ikaongeza fedha kwenye awamu hii ya pili kutoka shilingi milioni 470 mpaka kwenye *minimum* ya shilingi milioni 560 katika halmashauri zote hapa nchini. Tutaendelea na tathmini kuona ni namna gani tunaweza tukatafuta fedha kwa ajili ya kumalizia kule ambapo hawakumalizia lakini wengine ilikuwa ni uzembe wao wenyewe.

**SPIKA:** Naamini hao mnaosema ni uzembe wao mtawachukulia hatua. Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, swali la nyongeza.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa fedha hizi shilingi milioni 470 ziligawanywa kwa kiwango sawa nchi nzima wakati gharama za ujenzi hazifanani kati ya Dar es Salaam na mikoa mingine, ni upi mkakati wa Serikali katika kuhakikisha kwamba wanapogawa fedha zisifananishwe katika mikoa yote? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyokuwa nimemjibu Mheshimiwa Subira Mgalu namjibu Mheshimiwa Kanyasu. Baada ya shilingi milioni 470 hii

kwenda na kuonekana kuna changamoto baadhi ya maeneo kwa mfano Makete kwa Mheshimiwa Festo Tuntemeke Sanga, wao mchanga wanauchukua Makambako kuweza kwenda kujenga kule Makete kwa hiyo, gharama inakuwa tofauti.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana kwenye awamu hii ya pili fedha ikaongezwa kwa kulingana na maeneo. Fedha waliyopata Dar es Salaam siyo aliyopata Mheshimiwa Sanga kule Makete na siyo aliyoipata Mheshimiwa kule Mbinga Vijijini.

**SPIKA:** Mheshimiwa George Natany Malima swali la nyongeza.

**MHE. GEORGE N. MALIMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Shule ya Sekondari ya Berege yenye Kidato cha Tano na cha Sita ina idadi kubwa ya wanafunzi lakini ina upungufu mkubwa wa mabweni. Je, ni lini Serikali itajenga mabweni katika shule hii? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, Serikali itajenga mabweni katika Shule ya Sekondari Berege kule Wilayani Mpwapwa kadri ya upatikanaji wa fedha. Nitoe wito kwa Mkurugenzi wa Halmashauri kuanza kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa mabweni haya katika Shule ya Sekondari Berege na kisha kuleta maombi vilevile Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa ajili ya kuweza kutafutiwa fedha ya kuweza kuendelea na ujenzi wa mabweni hayo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Neema Mwandabila, swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Ujenzi wa *hostel* unahitaji miundombinu ya maji na shule nyingi hazina maji, kwa mfano Shule ya Ndugu iliyopo Mbozi. Ni nini mkakati wa Serikali kuhakikisha maji yanakuwepo kwenye shule zote za *hostel*? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, ni mkakati wa Serikali kuhakikisha shule zote zinazojengwa ambazo ni za bweni zinakuwa na maji. Ndiyo maana tunasisitiza *coordination* kati ya taasisi zote za Serikali katika maeneo husika. Pale ambapo shule inajengwa, Mkurugenzi wa Halmashauri afanye kazi kwa karibu na wenzetu wa RUWASA kwa ajili ya kuhakikisha miundombinu ya maji inafika karibu.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumuelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya alikotaja Mheshimiwa Neema Mwandabila kuhakikisha kwamba anawasiliana na wenzetu wa RUWASA kuvuta maji katika shule hii ambayo maji bado hayajafika.

**SPIKA:** Mheshimiwa George Natany Malima, Mbunge wa Mpwapwa sasa aulize swali lake.

Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Mheshimiwa Mbunge.

Na. 113

**Ujenzi wa Vituo vya Afya – Jimbo la Mpwapwa**

**MHE. GEORGE N. MALIMA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga vituo vya afya katika Kata za Mlembule, Godegode, Chunyu na Berege – Mpwapwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa George Natany Malima, Mbunge wa Jimbo la Mpwapwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua mahitaji ya vituo vya afya katika Kata za kimkakati kote nchini. Katika kipindi cha miaka mitano Serikali imetekeleza ujenzi wa vituo vipatavyo 2,406 vya kutolea huduma za afya ambavyo bado vina uhitaji wa baadhi ya miundombinu ikiwemo vifaa tiba na watumishi.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutenga kwa awamu fedha kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya kwenye maeneo ya kimkakati kote nchini ikiwemo Kata za Godegode, Chunyu na Berege katika Halmashauri ya Mpwapwa, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa George Malima, swali la nyongeza.

**MHE. GEORGE N. MALIMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Ujenzi wa Kituo cha Afya cha Kata ya Iwondo umefikia asilimia 80 lakini fedha za kumalizia asilimia 20 iliyobaki zimekwisha. Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza fedha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa kituo hicho ili wananchi wa kata hiyo waweze kupata huduma?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Kituo cha Afya cha Kata ya Matomondo kimekamilika na sasa kinatoa huduma lakini kuna upungufu mkubwa sana wa watumishi na hasa kada ya madaktari. Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza watumishi katika kituo hicho cha afya ili wananchi wa Kata ya Matomondo waweze kufurahia huduma ya afya? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Mpwapwa kwamba Serikali inajenga vituo hivi vya afya kwa awamu. Niwapongeza kwa kujenga kituo cha afya hiki cha Iwondo mpaka kufikia hatua ya asilimia 80 na bado asilimia 20 ya fedha kwa ajili ya ukamilishaji.

Mheshimiwa Spika, nitoe wito kwa Mkurugenzi wa Halmashauri kufanya mahesabu tufahamu hii asilimia 20 iliyobaki

ni sawa na shilingi ngapi ili tuweze kuona namna ya kupata fedha Serikali Kuu pia na namna ya kupata fedha kutoka kwenye mapato ya ndani kwa ajili ya kukamailisha ujenzi wa kituo hiki cha afya.

Mheshimiwa Spika, pili, kituo cha afya ambacho kinatoa huduma, Serikali hii ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt, Samia Suluhu Hassan katika kipindi cha miaka miwili na nusu imeajiri jumla ya watumishi wa sekta ya afya wapatao 17,000 ambao wamepangwa katika vituo mbalimbali kikiwepo kituo hiki. Zoezi hili ni endelevu na tutatoa kipaumbele kwa ajili ya kituo hiki cha afya cha Mpwapwa, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa George Mwenisongole, swali la nyongeza.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Kata ya Igamba katika Wilaya ya Mbozi ni moja ya kata ambazo zimeahidiwa kupelekewa shilingi milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya. Je, ni lini sasa hizo fedha zitaenda ili ujenzi uanze?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kata hii ya Igamba itapelekewa shilingi milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya kama ambavyo Serikali imeahidi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, swali la nyongeza.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Je, ni lini Serikali itajenga kituo cha afya katika Kata ya kimkakati ya Kandawale? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ujenzi wa vituo vya afya vya kimkakati katika Kata zetu zote nawahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba Serikali imefanya tathmini na kuainisha maeneo ambayo yana sifa ya kuwa na vituo vya afya vya kimkakati na tutakwenda kujenga vituo hivi vya afya kwa awamu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge nakuhakikishia kwamba itakapofikika awamu hiyo tutawapatia fedha kwa ajili ya kujenga kituo hicho cha afya, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Masache Kasaka, swali la nyongeza.

**MHE. MASACHE N. KASAKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kuniona. Katika Wilaya ya Chunya zipo Kata chache za kimkakati ambazo hazina vituo vya afya. Je, ni lini Serikali itatenga na kupeleka fedha kwa ajili ya kujenga vituo vya afya kwenye Kata za Luwalaje, Upendo na Kata ya Chokaa katika Kijiji cha Mapogoro? Ahsante.

**SPIKA:** Kata moja tu Mheshimiwa kwa sababu ni swali la nyongeza. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nampongeza Mheshimiwa Mbunge wa Chunya kwa kuwa na taarifa ya vituo vyake vya kimkakati kama walivyo Waheshimiwa Wabunge wengine. Wameshazileta Ofisi ya Rais, TAMISEMI Serikali inaendelea kutafuta fedha ili ujenzi kwa awamu katika maeneo haya ufanyike. Tutatoa kipaumbele katika Kata ambazo umezitaja, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. David Mathayo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID:** Mheshimiwa Spika, Kata za Suji, Vudee na Mshewa ni Kata za kimkakati; je, ni lini Serikali itajenga vituo vya afya katika Kata hizo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa Kata moja.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inatafuta fedha kwa ajili ya kuanza kujenga vituo vya afya hivi vya kimkakati katika maeneo ambayo ameyataja. Nitoe wito na kusisitiza kwamba ni wajibu wa halmashauri kupitia Wakurugenzi na Mabaraza ya Madiwani kuanza kutenga fedha kupitia mapato ya ndani kuanza ujenzi huu na Serikali Kuu itachangia kwa kadri fedha zitakavyokuwa zinapatikana, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Flatei Massay, swali la nyongeza.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Serikali ilileta shilingi milioni 500 ya kumalizia Kituo cha Afya cha Maretadu na Mheshimiwa Naibu Waziiri unajua. Sasa mkagawana kupeleka Hospitali ya Wilaya sasa kituo hakijaisha cham Maretadu Hospitali ya Wilaya haijaisha. Je, ni lini mnaleta fedha kumalizia kituo na hospitali hiyo?

**SPIKA:** Uliza swali moja kati ya hayo mawili.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mmepeleka fedha shilingi milioni 500 na mmechukua milioni 300. Je ni lini inapeleka fedha kwa ajili ya kumaliza kituo cha afya cha Maretadu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu DC, ambako fedha ya Serikali shilingi milioni 500 ilipelekwa kwa ajili ya kujenga kituo cha afya lakini kwa maamuzi ya Mkurugenzi na Baraza la Madiwani walikiuka utaratibu wakahamisha shilingi milioni 300 kutoka kituo cha afya wakapeleka kwenye mradi mwingine wa hospitali ya wilaya.

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia fursa hii kumuelekeza Mkurugenzi wa Mbulu Vijijini kuhakikisha shilingi milioni 300

waliyoihamisha bila kufuata utaratibu inarejeshwa kwenye kituo cha afya na kukamilisha kituo cha afya kwa haraka iwezekanavyo na sisi ofisi ya Rais, TAMISEMI tutafuatilia, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Catherine Magige, swali la nyongeza.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Je, ni lini Serikali itaona umuhimu wa kubadilisha Zahanati ya Reguruki iiliyoko Jimbo la Arumeru Mashariki kuwa kituo cha afya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Serikali imekuwa na utaratibu wa kupandisha hadhi zahanati ambazo zipo katika maeneo yanayokidhi vigezo vya kuwa vituo vya afya. Kwa hiyo, naomba nipokee hoja ya Mheshimiwa Mbunge kwa zahanati hii ya Reguruki ili tuweze kufanya tathmini na kuona ni kwa kiasi gani anakidhi vigezo vya kuwa kituo cha afya na Serikali ichukue hatua kwa ajili ya kupandisha hadhi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hassan Zidadu Kungu, swali la nyongeza.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya Kuuliza swali la nyongeza. Rais wa Awamu ya Tano wakati wa uhai wake alipokuwa katika ziara Wilaya ya Tunduru aliahidi ujenzi wa kituo cha afya katika Kata ya Namihungo. Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya Rais ya ujenzi wa kituo cha afya katika kituo cha Namihungo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

Mheshimiwa Spika, naomba nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge, ahadi za Viongozi wetu wakuu wa kitaifa ni kipaumbele katika utekelezaji wa miradi hiyo kupitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Nachukua hoja hii, tayari najua tumeshaanza kuiratibu na

tunatafuta fedha na mara fedha zikipatikana tutaleta shilingi milioni 500 kwa ajili ya kujenga kituo hiki cha afya, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Edward Olelekaita Kisau, swali la nyongeza.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kuwa mimi bado natafuta vituo vitatu vya tarafa, lini Serikali italeta fedha kwa ajili ya vituo vya tarafa?

**SPIKA:** Sasa Mheshimiwa Kisau umeamua kutaja vituo vitatu, mimi namruhusu kituo kimoja. Chagua kimoja kati ya hivyo vitatu kwa sababu ni swali la nyongeza. *(Kicheko)*

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Spika, unajua wengine wanataja za kata, mimi bado nipo juu sana, za tarafa kwa hiyo, nafikiri mnipe kipaumbele. Tulisema za tarafa tumalize halafu twende kwenye kata.

**SPIKA:** kwa hiyo tarafa tatu hazina kituo cha afya? hata kimoja?

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Spika, hazina hata kimoja.

**SPIKA:** haya umesikika. Mheshimiwa Naibu Waziri. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na nakushukuru, naomba tu kumuhakikishia Mheshimiwa Mbunge wa Kiteto kwamba, pamoja na yeye, bado kuna baadhi ya majimbo pia na wilaya zetu ambazo tarafa nzima haina kituo cha afya. Tunafanya mpango wa kuhakikisha kwamba tarafa zote ambazo zina idadi kubwa ya wananchi na kuwa na umbali mrefu kutoka kituo kingine zinapewa kipaumbele kwenye vituo vya afya vya kimkakati. Kwa hiyo nikuhakikishie kwamba tarafa ulizozitaja zitapewa kipaumbele kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Kassinge, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Serikali iliahidi kutuma wataalam kwenda kufanya tathmini na uchambuzi ili kijengwe kituo cha afya Kata ya Likawage Jimbo la Kilwa Kusini.

Je, ni lini wataalam hawa watakwenda kufanya tathmini hii ili kituo hicho kijengwe mara moja?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Suala hili lipo ndani ya uwezo wa wataalam wa Mkoa wa Lindi. Tuna Mganga Mkuu wa Mkoa wa Lindi na tuna Mganga Mkuu wa Wilaya ya Kilwa. Natoa maelekezo, ndani ya siku 14 wawe wamefanya tathmini ya vigezo kama tunahitaji kujenga kituo cha afya hapo lakini wawasilishe Ofisi ya Rais, TAMISEMI ili tufanye maamuzi kwa ajili ya kuanza kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi. Nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Condester Sichalwe, swali la nyongeza.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi. Kwa kuwa kata ya Ikuna ni miongoni mwa kata za kimkakati na ni kata ambayo ina wakazi wengi, na wananchi wameshaanza kujenga kituo cha afya kwa nguvu zao zaidi ya miaka miwili.

Je, ni lini Serikali itatupatia kiwango cha fedha ili tumalizie kituo hicho cha afya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, nawapongeza wananchi wa Kata hii ya Ikuna kwa kuanza kujenga kituo cha afya kwa nguvu zao. Tutakwenda kuchangia nguvu za wananchi kumalizia kituo hichi cha afya

baada ya kufanya tathmini ya kuona hatua waliyofika na kiasi gani cha fedha kinahitajika. Lakini pia nimuombe Mkurugenzi wa Halmashauri atenge fedha pia za mapato ya ndani wakati tunatafuta fedha za Serikali Kuu. Ahsante.

**SPIKA:** Waheshiniwa Wabunge, nawaona mmesimma wengi sana hapo. Mheshimiwa Tunza Malapo, swali la nyongeza.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, je, ni lini Serikali itajenga upya ama kukarabati jengo la wagonjwa wa nje *(OPD)* katika Kituo cha Afya Likombe kilichopo Manispaa ya Mtwara Mikindani? Jengo hilo limechakaa, na la zamani, halikidhi mahitaji ya sasa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba kutumia fursa hii kumuelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara Mikindani, kuwasilisha Ofisi ya Rais, TAMISEMI tathmini ya gharama zinazohitajika kwenye kufanya ukarabati lakini pia kama ni kufanya ujenzi mpya, ili tuweze kuona kama gharama hiyo ipo ndani ya uwezo wa mapato ya ndani ya Halmashauri. Tutatoa maelekezo ili waanze kutenga fedha mwaka wa fedha 2024/2025. Kama ipo nje ya uwezo wao, Ofisi ya Rais TAMISEMI, kwa maana ya Serikali Kuu, itaangalia namna ya kuwaunga mkono kupitia fedha ya Serikali Kuu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kassim Hassan Haji, Mbunge wa Mwanakwerekwe, sasa aulize swali lake.

Na. 114

**Marekebisho ya Sheria ya Mfuko wa Jimbo**

**MHE. KASSIM HASSAN HAJI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itafanya maboresho ya Sheria ya Mfuko wa Jimbo ili kuondoa kikwazo cha utekelezaji Zanzibar kwa kuwa Wabunge siyo Madiwani?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Haji Kassim, Mbunge wa Mwanakwerekwe kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Mfuko wa Jimbo Na. 16 ya mwaka 2009, uidhinishwaji wa vipaumbele na matumizi ya fedha hufanywa na Kamati ya Mfuko wa Jimbo yenye wajumbe saba, akiwemo Mbunge wa Jimbo husika ambaye ndiye Mwenyekiti wa Kamati. Aidha, Kamati ina jukumu la kupokea, kujadili vipaumbele vya miradi iliyowasilishwa na wananchi na kuidhinisha miradi itakayotekelezwa.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya jimbo inatekelezwa sambamba na Sheria ya Fedha, Sheria ya Manunuzi ya Umma pamoja na Miongozo mbalimbali ya Mipango, Bajeti na Matumizi ya fedha za Umma. Hivyo, utaratibu uliopo kisheria unamwezesha Mbunge wa Jimbo husika kutimiza wajibu wake wa kupokea maombi, kuweka vipaumbele na kuidhinisha fedha kwa ajili ya utekelezaji wa vipaumbele vilivyokubaliwa, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kassim Hassan Haji, swali la nyongeza.

**MHE. KASSIM HASSAN HAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa kodi inayokatwa katika matumizi ya mfuko huu ni kubwa sana, ni lini Serikali itaenda kuondoa kodi hiyo katika matumizi ya Mfuko wa Jimbo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, kwa kuwa Wakurugenzi wetu wengi ni wapya ambao wamechaguliwa katika kuendesha halmashauri zetu. Je, ni lini Serikali itakwenda kupeleka mafunzo

kuwawezesha Wakurugenzi hawa kujua thamani ya Mfuko wa Jimbo kwa Waheshimiwa Wabunge? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kassim Hassan Haji, Mbunge wa Mwanakwerekwe kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba tulipokee suala la kodi inayokatwa katika fedha za Mfuko wa Jimbo na hususan kwa upande wa Zanzibar. Suala hili ni la kiutaratibu, tutafanya utaratibu kuhusiana na Wizara ya Fedha lakini pia Wizara ya Muungano, Ofisi ya Rais TAMISEMI, kwa pamoja tuweze kuona njia nzuri zaidi ya kurekebisha changamoto hii ili tuweze kwenda vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la pili kuhusiana na Wakurugenzi wengi kuwa wapya. Ni kweli na tunahitaji kuona Wakurugenzi wetu wanaelewa vizuri wajibu wao wa kutekeleza Mfuko wa Jimbo. Nitumie fursa hii kwanza, kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tutafanya mafunzo kwa Wakurugenzi wote ili wajue wajibu wao katika kusimamia Mfuko wa Jimbo.

Mheshimiwa Spika, natoa msisitizo kwa Wakurugenzi wote kote nchini, kumekuwa na changamoto, Waheshimiwa Wabunge wanakaa na Kamati za Mfuko wa Jimbo, wanapitisha miradi lakini Wakurugenzi wanazuia fedha zisiende kutekeleza miradi ile.

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia fursa hii kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, kuelekeza kwamba Mkurugenzi yeyote atakayekiuka utaratibu baada ya Mwenyekiti wa mfuko huo kuidhinisha matumizi, tutachukua hatua kali za kinidhamu dhidi yake. Miradi hii itekelezwe kwa wakati baada ya Waheshimiwa Wabunge kupitisha miradi hiyo. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Naona Mheshimiwa Mbunge wa Kibamba amesimama ana swali la nyongeza.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona. Kwa kuwa fedha za Mfuko wa Jimbo zinategemea sana idadi ya watu kwenye majimbo yetu, na ni ukweli sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022 imekamilika na hivyo tunazo takwimu mpya kwenye majimbo yetu.

Je, katika mwaka wa fedha 2023/2024 fedha zitakazotolewa zitazingatia idadi ya watu kwenye majimbo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba fedha za Mfuko wa Jimbo zinategemea idadi ya wananchi katika jimbo husika, ukubwa wa kijiografia lakini pia na kasi ya umaskini katika eneo husika.

Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwanza Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kipindi cha mwaka wa fedha uliopita iliongeza fedha za Mfuko wa Jimbo. Waheshimiwa Wabunge wote ni mashahidi; iliongezeka na imeendelea kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa miradi hiyo. Suala la kuzingatia matokeo ya sensa ya mwaka jana ni muhimu na Serikali itaendelea kufanya kazi kwa sababu moja ya kigezo ni idadi ya watu katika maeneo hayo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, asante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge…

*(Hapa baadhi ya Wabunge walisimama kuashiria kutaka kupata nafasi kuuliza maswali)*

**SPIKA:** Samahani, wengine nimewaona baada kwa sababu nilishasema ili nikuone, uwe umesimama yule mwenye swali anaposimama. Nikikuona baada ya hapo inakuwa kama umefikiri baadaye kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Waziri, hii hoja ya Mfuko wa Jimbo Zanzibar, nadhani alichoomba Mheshimiwa Mbunge ni cha muhimu kwa sababu Mfuko wa Jimbo una majimbo pia Zanzibar. Mafunzo yanayotolewa kwa upande wa Wakurugenzi walioko Bara, kwenye hoja hiyo pia mtume wataalam kule ili wale Wakurugenzi wawe na uelewa sawa katika matumizi ya fedha hizi za Mfuko wa Jimbo. Changamoto za Waheshimiwa Wabunge kutoka upande wa Zanzibar nimezipata mara kadhaa kwa hivyo ni muhimu ikafanyiwa kazi. *(Makofi)*

Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Aida Joseph Khenan, Mbunge wa Nkasi Kaskazini, sasa aulize swali lake.

Na. 115

**Semina kwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya**

**MHE. AIDA J. KHENANI** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa semina elekezi kwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya mara kwa mara kuhusu utawala bora?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais Utumishi na Utawala Bora, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, Mbunge wa Nkasi Kaskazini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa mafunzo elekezi kwa viongozi wa ngazi mbalimbali katika kuwajengea uwezo wa kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia misingi ya utawala bora.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu huo, Serikali imeendelea kutoa semina elekezi kwa viongozi wanaoteuliwa kushika nyadhifa mbalimbali ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia Sera, Sheria, Kanuni na Taratibu zilizopo. Katika kipindi cha mwezi Februari hadi Agosti, 2023, Serikali ilitoa mafunzo elekezi kwa viongozi wa ngazi ya Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Makatibu Tawala wa Wilaya ambapo agenda moja wapo ilikuwa ni ya utawala bora.

**SPIKA:** Mheshimiwa Aida Khenani, swali la nyongeza.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kutokana na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakubaliana kwamba semina elekezi ni muhimu mara baada tu ya kuteuliwa. Nina swali moja tu la nyongeza.

Kwa kuwa ripoti ya Tume ya Haki Jinai iliyotolewa hivi karibuni, imezungumzia matumizi mabaya ya waliopewa mamlaka, Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa, namna wanavyotumia masaa 24 kuwaweka watu ndani bila kufuata taratibu.

Je, ni lini Serikali italeta Mswada hapa Bungeni ili tufanye marekebisho kuwaondolea hayo mamlaka wabaki kuwa wasimamizi wa shughuli za maendeleo na yabaki kwa Jeshi la Polisi pekeyake? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, ni ukweli kuwa kwamba sasa Serikali imekwisha toa tayari taarifa ya kijinai, na kwamba taarifa hiyo imekwisha anza kufanyiwa kazi na wananchi wanashirikishwa katika maeneo mbalilmbali ili kuweza kutoa maoni yao na baada ya hapo taratibu nyingine za mabadiliko ya sheria ziweze kufuatwa.

Mheshimiwa Spika, namuomba mheshimiwa Mbunge na Bunge lako liwe na Subira wakati mchakato wa kuendelea

kukusanya maoni ya watu yanaendelea kupatikana ili itakapokuwa tayari sasa tuweze kuleta; na kama kutakuwa na mapendekezo ya mabadiliko ya sheria na kama kutakuwa na miongozo yeyote ile sisi kama Serikali au nchi tuweze kuifanyia kazi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Janejelly Ntate, swali la nyongeza.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Spika, ahsante, je, ni lini Serikali itarejesha utaratibu wa mafunzo elekezi ya uongozi, utawala bora na uadilifu kwa watumishi ambao wamefikia ngazi ya Afisa Mkuu ili wanapopata nafasi za uteuzi waweze kutumika ipasavyo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Utumishi wa Umma na Sheria ya Utumishi wa Umma pia Ibara ya 4 hadi Ibara ya 8 inampa mamlaka Katibu Mkuu Kiongozi kuweza kuhakikisha kwamba utumishi wa umma unakuwa ulio bora na ambao unakwenda na weledi lakini pia ambao unaweza kuwahudumia wananchi.

Mheshimiwa Spika, nataka kumuhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako, kwamba Serikali imeendelea kufanya utaratibu wa kutoa mafunzo kwa watendaji wote au watumishi wote ambao wanakuwa katika ngazi za uteuzi ili kuweza kuwa katika viwango bora vya kutoa huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, nataka kumhakikishia kwamba hilo jambo au maombi ya Mheshimiwa Mbunge tutaendelea kuyafanyia kazi na tutaendelea kuhakikisha kwamba tunakuwa na utumishi ulio bora kama ambavyo sheria inamtaka Katibu Mkuu Kiongozi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Mbunge wa Urambo, sasa aulize swali lake.

Na. 116

**Uhitaji wa mawasiliano ya simu Wilaya ya Urambo**

**MHE. MARGARET S. SITTA** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itapeleka huduma ya mawasiliano ya simu katika maeneo ambayo orodha yake iliwasilishwa Wizarani – Urambo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia a Habari, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Mbunge wa Jimbo la Urambo kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imetekeleza ujenzi wa minara kumi katika kata 10 ambazo ni kati ya kata 18 za Wilaya ya Urambo, ambapo minara tisa imekamilika katika Kata za Imalamakoye, Kasisi, Songambele, Itundu, Ukondamoyo, Nsenda, Uyogo, Vumilia, Ugalla pamoja na Uyumbu.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuboresha upatikanaji wa huduma ya mawasiliano katika baadhi ya Vijiji vya Kata ya Kasisi na Kiloleni na tayari imekwisha wapata watoa huduma wa kufikisha huduma ya mawasiliano katika kata hizo. Kwa upande wa kata za Kapilula, Kiyungi, Mchikichini na Muungano, Serikali kupitia *UCSAF* itafanya tathmini ili kupata hali halisi ya changamoto ya mawasiliano katika maeneo hayo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, swali la nyongeza.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake. Maswali yangu ni kwamba;

a) Je, ni lini Serikali itafanya tathmini katika kata ambazo hazina mawasiliano ya uhakika ili changamoto ziondolewe nao wapate mawasiliano kama wenzao?

*b)* Je, ni lini Serikali itaachana na teknolojia ya *2G* ili nao waende kisasa *4G* na *5G*?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni dhamira ya Serikali kuhakikisha kwamba maeneo yote nchini yanapata huduma ya mawasiliano. Kwa upande wa kata ambazo, kama ambavyo nimejibu katika jibu la msingi, Serikali inatafuta fedha na fedha zikipatikana tutaenda kufanya tathmini ili kuhakikisha kwamba tunafikisha huduma ya mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, kipengele cha pili, kuhusu suala la kuondokana na huduma ya *2G*; tunapokuwa na *3G* ndani yake *2G* imo. Tunapokuwa na *4G* ndani yake *2G* imo, tunapokuwa na *5G* kwa sababu ile ni *specific* kwa ajili ya *voice* na hizi zingine ni kwa ajili ya *data*. Hizi zote zitakuwa zinaenda sambamba na kuhakikisha pamoja na kwamba kuna *advancement* ya teknolojia lakini hatuwezi kuachana na huduma ya sauti.

Mheshimiwa Spika, huduma ya sauti itaendelea kuwepo hivyo, hatutaweza kuachana kwa sasa kwa sababu ulimwenguni

kote huduma ya *2G* inaendelea kutumika na sisi kama nchi tutaendelea kuhakikisha kwamba kuna wananchi ambao watakuwa wanaendelea kutumia huduma hiyo basi tutahakikisha kwamba miundombinu ya huduma hiyo itaendelea kuwepo. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, sehemu ya pili ya swali la Mheshimiwa Mbunge, nadhani alitaka kujua hiyo huduma ambayo inatolewa sasa, ukiacha hiyo ya *voice* kama ulivyosema ya *2G*, hizo nyingine zitawafikia lini hao wananchi? Ndilo lililokuwa swali la Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, Serikali kuanzia mwaka 2021 tulitoa maelekezo, miundombinu yetu yote ya minara ya mawasiliano inayojengwa, lazima iwe na huduma ya *2G* na *3G*. Hakuna mnara kuanzia mwaka 2021 ambao umejengwa ukiwa na huduma ya *2G* pekeyake.

Mheshimiwa Spika, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge, katika jimbo lake la Urambo ambalo hata mimi nimepata kutembelea katika kata zake 12, katika kila mnara unaojengwa sasa hivi Urambo una huduma ya kutoa *internet*. Nakushukuru sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Aleksia Kamguna.

**MHE. ALEKSIA A. KAMGUNA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Katika Halmashauri ya Mlimba, Kata ya Uchinjile hakuna kabisa mawasiliano ya simu. Je, ni lini Serikali itapeleka mawasiliano ya simu katika kata hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, nimeshafika Mlimba na katika kata ambayo Mheshimiwa Mbunge ameitaja ni kwamba tayari

imeingizwa katika miradi 758. Zaidi ya hapo, Jimbo la Mlimba tumewapelekea minara saba ambapo tunaamini kwamba itakapojengwa basi utatuzi wa changamoto za mawasiliano utakuwa umefikia ukomo. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Midimu, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Je, ni lini Serikali itafikisha Mkongo wa Taifa Mkoa wa Simiyu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Esther Midimu, Mbunge wa Mkoa wa Simiyu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa katika mikoa 26 ya Tanzania Bara ni Mkoa wa Simiyu pekee ambao haukuwa umeunganishwa na Mkongo wa Taifa lakini Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ametafuta fedha zimeshapatikana na tayari Mradi wa Ujenzi wa Mkongo wa Taifa kutoka Shinyanga kupita Bariadi kuelekea Bunda umeshaanza.

**SPIKA:** Mheshimiwa Vita Kawawa, swali la nyongeza.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Je, ni lini sasa Serikali itaanza kupeleka mawasiliano ya simu katika Vijiji vya Mgema, Mtelamwai, Mtonya na Masuguru, Wilayani Namtumbo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Vita Kawawa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nafahamu kwamba kumekuwa na changamoto ya namna gani Serikali inaenda kutekeleza Mradi

wa Tanzania kidigitali hasa katika Miradi ya Minara 758 ambayo imesainiwa.

Mheshimiwa Spika, naomba niwatoe hofu Waheshimiwa Wabunge, tayari utekelezaji umeshaanza lakini ni kwamba kinachofanyika sasa hivi ni upatikanaji wa maeneo yale ambayo yanaenda kujengwa minara na baadaye vibali vipatikane kwa ajili ya kuhakikisha kwamba, utekelezaji huo unafanyika. Kwa hiyo nimwombe Mheshimiwa Mbunge asiwe na wasiwasi na nimtoe wasiwasi kabisa. Pindi miradi hiyo itakapoanza kujengwa kwa haraka na itakamilika kwa wakati bila kuwa na shida yoyote. Tumewapatia miezi 18 kuhakikisha kwamba wanakamilisha miradi yote, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Michael Mwakamo, swali la nyongeza.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa Serikali ilishatupa taarifa Wabunge juu ya uwepo wa minara hiyo 758; je, ni lini sasa Wabunge tutapata taarifa rasmi na kuzirudisha kwa wananchi kwamba kazi hiyo inaanza? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, tumeingia mikataba na mikataba ya utekelezaji wa miradi hii ni kuanzia miezi tisa mpaka miezi 20. Kwa sababu muda wa mkataba ndio ambao Serikali tunaosimamia, tunahakikisha kwamba ndani ya muda wa makubaliano watoa huduma wote, kulingana na idadi ya minara ambayo waliipata, miradi hiyo iwe imekamilika ndani ya muda wa mkataba, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa George Kakunda, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, kule Sikonge tunayo minara kama mitano hivi ambayo ina nguvu ndogo sana yaani *coverage* yake ni eneo dogo sana. Je, ni lini Serikali itaelekeza haya makampuni waboreshe *coverage* ya minara yao hasa kwenye Kijiji cha Ibumba?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kakunda kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa kuna timu ambayo iliundwa na Mheshimiwa Waziri na inazunguka kufanya tathmini ili kujiridhisha na changamoto zilizopo.

Mheshimiwa Spika, kuna minara ambayo ilijengwa miaka ya nyuma ambapo mahitaji yake ilikuwa watu labda 2,000 au 3,000. Sasa unakuta kwamba katika eneo fulani kuna ongezeko la wakazi 5,000 mpaka 6,000 kiasi kwamba inazidiwa. Kuna miradi mingine ambayo changamoto yake ni masafa, lakini kuna miradi mingine changamoto yake ni teknolojia iliyotumika. Kwa hiyo timu hii inapopita na kujiridhisha chanzo cha tatizo ni nini, ili Serikali ikachukue hatua stahiki kulingana na tatizo la eneo husika. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Kakunda eneo lake tayari alishanijulisha na tayari tumeshaliweka katika utekelezaji wa utafiti huo. Watakaporudi wataalam wetu tutajua kwamba tunaenda kuchukua hatua gani ili tutatue tatizo kulingana na hali halisi iliyopo katika eneo husika, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hamisi Taletale, swali la nyongeza.

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kuuliza swali dogo la nyongeza. Je, ni lini Serikali italeta mawasiliano katika Kata ya Gwata, Tununguo na Tomondo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hamisi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kata ya Gwata ipo katika utekelezaji na tusubiri Mheshimiwa Mbunge mradi huu ambapo ukiwa unaendelea kutekelezwa ndani ya kipindi cha mkataba,

tunaamini Kata ya Gwata itakuwa imefikishiwa huduma ya mawasiliano, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Mlaghila Jumbe, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Je, ni lini Serikali itaiondoa Wilaya ya Kyela kwenye adha ya mawasiliano yake kuingiliwa na Mtandao wa Malawi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ally Mlaghila Jumbe, Mbunge wa Kyela kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa tunafahamu kwamba mawasiliano ni uchumi, mawasiliano ni usalama na mawasiliano ni huduma ya msingi ya kila Mtanzania. Sasa wakati Serikali ikiendelea kutafuta fedha tunaona ni busara kuwaacha kwanza wananchi wetu waishi katika mazingira ambayo wanaweza kuwasiliana. Pindi fedha zitakapopatikana, ndipo sasa tutakapoenda kuweka miundombinu yetu na kuhakikisha kwamba sasa mitandao ya nchi jirani tunaiondoa ili waweze kutumia mitandao ya nchi yetu, ili waweze kuchangia uchumi ndani ya Taifa letu na vilevile wawe na usalama ambao unajitosheleza katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa, Serikali ina mkakati madhubuti wa kuhakikisha kwamba tunakuja na mradi maalum wa *borders and special zone* kuhakikisha kwamba changamoto hii inaisha ili Watanzania wawe na amani ndani ya nchi yao.

**SPIKA:** Mheshimiwa Boniphace Butondo, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Katika mikataba iliyosainiwa ya wakandarasi kwa ajili ya kushughulikia masuala ya minara, nina minara tisa katika Wilaya ya Kishapu, lakini hadi sasa minara

hiyo haijaanza kufanyiwa kazi; je, ni lini Serikali itaanza kutekeleza miradi hii?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Butondo Mbunge wa Kishapu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa, kwanza Mheshimiwa Butondo alikuwa na tatizo kubwa sana, akaleta na Serikali ikaipokea maombi yake na tukampelekea minara tisa9 kama ambavyo ametaja. Sasa kusaini mkataba ni jambo la kwanza. Jambo la pili, watoa huduma wanaenda ndani ya Jimbo la Mheshimiwa Butondo ili kutafuta eneo kwa ajili ya kujenga hiyo minara. Wakishapata eneo wanakuja kutafuta vibali kwa mfano kibali cha mazingira *(environmental impact assessment permit)*, kibali cha anga *(aviation permit)* vilevile wanatafuta kibali cha kutoka halmashauri kwa ajili ya ujenzi. Kwa hiyo mlolongo wa vibali hivi, kila sehemu ukikuta kwamba wanatoa kwa uharaka basi mkandarasi ataweza kuanza ujenzi kwa haraka, lakini kukiwa na *delay* katika baadhi ya maeneo, ndipo inatokea kwamba tunasaini mkataba lakini miezi mitano unakuta kwamba mradi haujaanza.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali imeshaliona hilo, tunawaomba wote ambao wanahusika katika mnyororo mzima wa utoaji wa vibali, watoe kwa wakati ili kuhakikisha kwamba miradi hii inakamilika kwa wakati kwa sababu Watanzania wanahitaji huduma ya mawasiliano ili washiriki katika uchumi wa kidigitali.  Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mhata, swali la nyongeza.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi kwenye Wilaya yangu ya Nanyumbu tulipatiwa minara tisa, lakini kuna kata ambayo ina changamoto kubwa haipo ndani ya minara hiyo tisa.

Je, Serikali haioni haja kuleta mnara mmoja kwenye Kata ya Likokona ambayo kuna changamoto ya mawasiliano?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mhata, Mbunge wa Nanyumbu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nafahamu kabisa kwamba, Kata ya Likokona ina changamoto hiyo, mimi pamoja na Mheshimiwa Mbunge tulishafika katika maeneo hayo, lakini Serikali ilipokea kata hiyo na katika miradi inayotarajiwa kuja katika ile minara 600, kata hiyo tumeiingiza. Kwa hiyo tumwombe Mheshimiwa Mbunge tuendelee kuiombea Serikali iweze kuendelea kupata fedha kwa ajili ya kuboresha huduma ya mawasiliano nchini, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Ujenzi Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo, Mbunge wa Mbagala, sasa aulize swali lake.

Na. 117

**Ujenzi wa mifereji eneo la Mikwambe katika barabara ya Kongowe – Kibada**

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani kujenga mifereji Barabara ya Kigamboni – Kongowe, Mtaa wa Mikwambe, Kata ya Toangoma - Mbagala?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Innocent Lugha Bashungwa, majibu.

**WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo, Mbunge wa Jimbo la Mbagala kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* Mkoa wa Dar es Salaam ipo kwenye hatua ya manunuzi ya kumpata Mkandarasi wa kufanya ukarabati wa mabega ya Barabara ya Kongowe – Kibada, yenye urefu wa kilometa moja. Ukarabati huo pia utahusisha Ujenzi wa mitaro kwenye baadhi ya maeneo, ikiwemo eneo la Mikwambe yenye urefu wa kilometa mbili, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Chaurembo, swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri. Naomba kuuliza, Serikali ina mpango gani wa dharura wa kuokoa wananchi wa Mikwambe hasa Mtaa wa Zahanati, Rushe, Chambaruba A na B ambao wanaathirika na kutokuwa na mifereji katika barabara hiyo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; ni upi mkakati wa Serikali wa kujenga mifereji katika barabara zote za lami zilizopo katika Jimbo la Mbagala?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Chaurembo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza na la pili Mheshimiwa Chaurembo anaulizia mkakati wa kuhakikisha barabara ambazo tunaweka lami hasa hasa kwenye majiji ni barabara ambazo ni kama barabara za mitaa. Mpango wetu ni upi katika kuhakikisha tunajega mifereji ama mitaro?

Mheshimiwa Spika, Wizara chini ya *TANROADS* tunayo *program* ya kuhakikisha barabara ambazo tunaweka lami, tunajenga na mitaro, lakini hata barabara ambazo ni za changarawe pia programu hiyo tunayo.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu Mamlaka ya Hali ya Hewa imetabiri mvua kubwa za *El-Nino*. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na nitumie nafasi hii kutoa maelekezo kwa Meneja Mkuu wa *TANROADS* kushirikiana na *TARURA* kuhakikisha barabara za *TANROADS* ambazo maji yanaenda kwenye barabara za *TARURA* wakae mara moja hasa hasa kwenye maeneo ya majiji na manispaa kujiandaa na kuhakikisha tunajitayarisha vyema kuhakikisha mvua za *El-Nino* zitakazonyesha basi mifereji na mitaro tutakuwa tumeitengeneza vizuri ili kuwaepushia wananchi maafa ambayo yanaweza yakatokea kwa mvua kubwa na mifereji kutokuwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, hili la Mheshimiwa Mbunge tumelichukua, lakini nimeona nitoe maelezo ya jumla hasa kwenye majiji na manispaa Mkurugenzi Mtendaji wa *TANROADS* ajipange na Mkurugenzi Mtendaji wa *TARURA* ili tuweze kulifanya kwa ufasaha, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said, Mbunge wa Magomeni, sasa aulize swali lake.

Na. 118

**Zuio la Jeshi la Polisi kwa wananchi wanaopata huduma vituo nje ya makazi yao**

**MHE. MWANAKHAMIS KASSIM SAID** aliuliza:-

Je, kwa nini Jeshi la Polisi haliondoi zuio la kuwahudumia wananchi wanaokwenda kupata huduma kwenye vituo nje ya maeneo yao?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Jumanne Sagini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said, Mbunge wa Magomeni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 7 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai Namba 20 kama ilivyofanyiwa marejeo mwaka 2022, kikisomwa pamoja na Kanuni za Jeshi la Polisi *(PGO)* Namba 309, mtu yeyote aliyetendewa au anayefahamu jinsi kosa lilivyotendeka au linavyotaka kutendeka anatakiwa kutoa taarifa kituo chochote cha Polisi kilicho karibu na taarifa hiyo itachukuliwa na kufanyiwa kazi. Hivyo, hakuna zuio lolote la kuwahudumia wananchi wanaohitaji huduma za polisi kwenye vituo vilivyo nje na maeneo yao, nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwanakhamisi Kassim Said, swali la nyongeza.

**MHE. MWANAKHAMISI KASSIM SAID:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Serikali. Kuna wananchi wanapata matatizo panapokuwa na kesi za jinai, lakini wanapokwenda baadhi ya vituo wanakuwa hawapati huduma hizi wanaambiwa pale hawahusiki, waende kituo kingine.

Je, Serikali iko tayari kukifuta kifungu hiki ili wananchi pale wanapopata matatizo wapate huduma? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi, hatuna kifungu chochote cha kisheria kinachozuia mwananchi aliyebaini uwepo wa kosa la jinai kuzuiwa kuripoti kwenye Kituo chochote cha Polisi.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kuelekeza kwamba ikiwa itatokea raia au mwananchi anapewa majibu hayo na askari wetu yeyote, atoe taarifa kwa Mkuu wa Kituo au Ofisa Upelelezi wa Wilaya au Mkuu wa Polisi wa Wilaya.

Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge lako tukufu nielekeze *IGP* atoe mwongozo kwa Makamanda wote wa Polisi wa Mikoa ili kama kuna udhaifu wa namna hii uelekezwe kwamba kuondolewe msingi wa kuzuia mwananchi kutoa taarifa kwenye Kituo chochote cha Polisi, nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Faharia Shomari Khamis, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 119

**Watuhumiwa wa nchi za nje wanaomiliki hati za kusafiria kama Watanzania**

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS** aliuliza:-

Je, lipi tamko la Serikali kwa watuhumiwa waliopo magereza ya nchi za nje wanaomiliki vitambulisho na hati za kusafiria za Tanzania?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fakharia Shomari Khamis, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Pasipoti na Hati za Kusafiria, Sura ya 42, pasipoti hutolewa kwa raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa madhumuni ya kusafiria nje ya nchi. Pale inapothibitika kuwa raia wa nchi za nje wanamiliki hati za kusafiria za Tanzania kinyume na matakwa ya sheria yetu ya pasipoti wanakuwa wametenda makosa na hivyo wanastahili kuchukuliwa hatua za kisheria.

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia fursa hii kumshauri Mheshimiwa Mbunge kama ana taarifa zitakazowezesha kupatikana kwa watuhumiwa hao azikabidhi kwa vyombo vyetu ili waweze kuchukuliwa hatua stahiki, nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Fakharia Shomari Khamis, swali la nyongeza.

**MHE. FAKHARIA SHOMARI KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nakubaliana na maelezo ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini napenda Watanzania wapatiwe elimu. Naomba kujua hiyo sheria inazunguza nini au inasema nini wakati kitendo kama hicho kikitokea ili Watanzania wote waelewe kwamba kuna sheria inazungumza hivi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa hicho kitendo sana huwa kinatokea nchi za nje na kule tuna balozi zetu. Je, balozi zetu zimepewa elimu gani kama litatokea tatizo kama hilo waweze kukabiliana nalo bila shida yoyote? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ikiwa aliyefanya kosa yuko Tanzania, sheria zinazopaswa kuchukuliwa ni pamoja na mhusika kufikishwa mahakamani kwa mujibu wa Sheria ya Pasipoti, Sheria ya Uhamiaji, Sura ya 54 iliyorejewa mwaka 2016. Baada ya kutiwa hatiani na kuadhibiwa hunyanganywa pasipoti ya Tanzania na kuifuta ili isije ikatumika tena. Jambo la tatu, hufukuzwa nchini kwa kupewa hati ya kufukuzwa nchini *(prohibit legal notice)* ili aondoke katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Maofisa wa Ubalozi wetu katika kila ubalozi tunaye Afisa Balozi ambaye ikitokea tutapata taarifa kama kuna Mtanzania kawekwa gerezani au kafungwa hufuatilia kumhoji ili kujua kama kweli ni Mtanzania na ikithibitika si Mtanzania, basi taarifa hutolewa kwenye nchi husika, lakini ikithibitika kwamba ni Mtanzania itabidi atumikie kifungo chake. Kitakachofanyika kama ni Mtanzania, atakuwa anakwenda

kumsalimia, kumwona kwenye vile vipindi vinavyoruhusiwa na mambo kama hayo, nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, Mbunge wa Mbulu Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 120

**Ujenzi wa Jengo la Mahakama ya Wilaya Mbulu**

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa jengo la Mahakama Wilayani Mbulu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Pauline Gekul, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru na pia ninamshukuru Mwenyezi Mungu, na naomba sasa kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria niweze kujibu swali la Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, Mbunge wa Mbulu Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mahakama ya Wilaya ya Mbulu kwa sasa inaendeshwa katika jengo ambalo ni chakavu na finyu sana kukidhi mahitaji. Aidha, jengo hilo pia lipo kwenye eneo la hifadhi ya barabara na hivyo linapaswa kuondolewa. Katika mpango wetu wa ujenzi wa Mahakama ya Wilaya ya Mbulu itajengwa katika mwaka wa fedha 2023/2024 na tayari mshauri elekezi ameshakamilisha usanifu na maandalizi ya zabuni kwa ajili ya kupata mkandarasi wa ujenzi. Ujenzi unatarajia kuanzia mwezi Septemba, 2023 na kukamilika kabla ya Juni, 2024.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, swali la nyongeza.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali na hatua hiyo ya kuanza ujenzi. Mimi nina swali moja tu.

Mheshimiwa Spika, katika Tarafa ya Nambisi kuna Mahakama chakavu katika Halmashauri ya Mji wa Mbulu. Je, utaratibu wa Serikali ukoje wa kukarabati majengo ya Mahakama katika Tarafa zetu nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru na nimshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa pongezi hizo.

Mheshimiwa Spika, mhimili wetu wa Mahakama una mpango wa miaka mitano wa kukarabati na kujenga majengo ya Mahakama kote nchini na katika mpango huu Mtendaji Mkuu wa Mahakama akishirikiana na Watendaji wa Mikoa wanafanya wanafanya utafiti katika Tarafa zote nchini zaidi ya Tarafa 500 na Kata zaidi ya 3,000 kuona ni wapi ambapo kuna mashauri mengi na umbali, tafiti hii tutakapokamilisha tutakuja sasa na *list* ya kwamba wapi tuanze.

Mheshimiwa Spika, ninafahamu kwamba hata Nambisi ambako Mheshimiwa Mbunge amepataja kuna uhitaji naomba avute subira tuweze kukamilisha tafiti hii halafu tutamwambia kama hapo tutakwenda kujenga. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali ya nyongeza mafupi. Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, swali la nyongeza.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, Mahakama ya Mwanzo ya Machame ilisimamishwa kwa kipindi kirefu kutokana na uchakavu wa majengo, lakini kwa kushirikiana na wadau tumejenga, tumefanya ukarabati wa Mahakama hiyo ya Mwanzo ya Machame na imekamilika na jengo liko pale.

Je, ni lini sasa mtapeleka Hakimu pale ili aweze kuanza kutoa huduma?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru na naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, Mbunge wa Hai kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Saashisha, amechangia katika Mfuko wake wa Jimbo kuhakikisha lile jengo la Mahakama pale Hai – Machame linakarabatiwa, lakini tatizo tulilonalo pale lile jengo bado lina *crack* nyingi, Mheshimiwa anafahamu hilo.

Mheshimiwa Spika, katika mpango wetu wa Mahakama tumetenga fedha kwenye Kata hiyo ya Machame tunakwenda kujenga eneo lingine. Ninamuhaidi Mheshimiwa Mbunge tutakwenda pale Hai – Machame tuone hilo eneo ambalo lina-*disputes* hilo ambalo jengo limechakaa na pale ambako tunataka kujenga tutafikia *consensus* wapi tujenge, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Almas Maige, swali la nyongeza.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kuniruhusu niulize swali la nyongeza. Wilaya ya Uyui ni mpya na hatuna Mahakama, tunatumia chumba kidogo sana; je, lini Serikali itajenga Mahakama ya Wilaya ya Uyui?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru na naomba nijibu swali la Mheshimiwa Maige, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mpango wetu wa kujenga Mahakama za Wilaya ni pamoja na kukarabati ambazo ni chakavu, naomba nipokee Mahakama hii ya Uyui nita-*check* na Mheshimiwa Mbunge tuone tuiweke kwenye mpango ili tuweze kukarabati pia.

**SPIKA:** Mheshimiwa Josephine Genzabuke, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi.

Tarafa ya Heru Juu iliyopo katika Halmashauri ya Mji wa Kasulu haina Mahakama, inafanyia kazi katika Ofisi ya Mtendaji. Je, ni lini Serikali itajenga Mahakama katika Tarafa ya Heru Juu? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru na naomba sasa nijibu swali la Mheshimiwa Genzabuke, Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba nimjulishe Mheshimiwa Mbunge kwamba katika mpango wetu wa kujenga Mahakama 60 kote nchini katika bajeti ya mwaka huu, ambayo mlitupitishia, Tarafa ya Heru Juu, Kata ya Heru Juu iko katika *list* hiyo Mheshimiwa Mbunge tunakwenda kujenga mwaka huu wa fedha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Oliver Semuguruka, swali la nyongeza.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniona.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa muda mrefu imekuwa na mpango wa kujenga Mahakama ya Mwanzo Kata ya Izigo, Wilaya ya Muleba, ningependa kujua utekelezaji wa ujenzi wa Mahakama hiyo umefikia wapi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru na naomba nijibu swali la Mheshimiwa Oliver Semuguruka, Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wetu wa Kagera katika Wilaya ya Muleba Kata hii ya Izigo, Tarafa ya Izigo iko kwenye mpango wa mwaka huu, tunakwenda kujenga mwaka huu Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa Mahakama ya Mwanzo ya Usanda katika Wilaya ya Shinyanga imechakaa. Je, ni lini Serikali itafanya ukarabati wa Mahakama hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Mnzava, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wetu wa Shinyanga tunakwenda kujenga katika mwaka huu wa fedha katika Tarafa ya Majengo, Kata ya Malunga naomba ni-*check* na Mheshimiwa Dkt. Mnzava ili tuone kwamba Mahakama hiyo ambayo imechakaa tuweze kuingiza kwenye mpango unaofuata wa Mahakama ya ujenzi. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tecla Mohamedi Ungele, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swa lake.

Na. 121

**Ujenzi wa Jengo Jipya la Mahakama ya Wilaya Nachingwea**

**MHE. TECLA M. UNGELE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga jengo jipya la Mahakama ya Wilaya Nachingwea?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri kabla haujajibu maswali.

Waheshimiwa Wabunge, Waheshimiwa Wabunge, Waheshimiwa Wabunge, sauti zenu ziko juu sana, mnajadili mambo ya muhimu yanayohusu Majimbo na mambo kama hayo, mnatafuta majibu kutoka kwa Waheshimiwa Mawaziri, tafadhali kama ni lazima mzunguze kwa nguvu sana milango ya kutoka nje iko Sita, mnaweza kutoka hapo mkajadiliana ndiyo mrejee. Kwa sababu wengine wanataka kuuliza maswali ya nyongeza lazima wamsikie Mheshimiwa Naibu Waziri anachojibu ni nini? Kwa hiyo, niwaombe sana sauti ziwe za chini wakati mkitafuta majibu ya hoja za wananchi kutoka kwa Serikali.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru na kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria naomba sasa nijibu swali la Mheshimiwa Tecla Mohamedi Ungele, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutekeleza mpango wa ujenzi na ukarabati wa majengo ya Mahakama katika ngazi mbalimbali ili kuboresha mazingira ya utoaji haki. Katika mpango huo Mahakama ya Wilaya ya Nachingwea imepangwa kujengwa katika mwaka huu wa fedha 2023/2024. Mshauri Elekezi ameshakamilisha usanifu na maandalizi ya gharama za mradi na taratibu za kupata Mkandarasi wa ujenzi zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, jengo linatarajiwa kukamilika ifikapo Juni, 2024.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tecla Ungele, swali la nyongeza.

**MHE. TECLA M. UNGELE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa juhudi kubwa za Serikali kwenda kutujengea Mahakama ya Wilaya kule Nachingwea. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, kuna upungufu mkubwa wa Watumishi katika Idara ya Mahakama Wilaya ya Nachingwea; je, Serikali ina mkakati gani wa kuongeza watumishi kwa ajili ya kuboresha ufanisi wa kazi? *(Makofi)*

Swali la pili, kwa kuwa Hakimu mmoja anahangaika kuhudumia Mahakama ya Mwanzo zaidi ya tano, lakini fedha za kuhudumia shughuli za Mahakama hazitoshi; je, Serikali ina mkakati gani kuongeza fedha kila mwezi kwa ajili ya shughuli za Mahakama? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ungele kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ninakiri ni kweli tuna upungufu wa watumishi katika Muhimili wetu wa Mahakama kama ambavyo upungufu huu upo katika Serikali kwa maeneo mbalimbali. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, amekuwa akituongezea watumishi katika Muhimili wetu wa Mahakama, na ninyi ni mashahidi ndugu zangu ni majuzi tu ametuteulia Majaji wa Mahakama ya Rufani, Mahakama Kuu na kadhalika, tunaendelea kuomba kupeleka vibali kwa ajili ya nyongeza ya watumishi.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Nachingwea ni kweli wana upungufu wa watumishi. *Primary Court (PC)* ambazo zina Mahakimu ni tatu, *Primary Court* ambazo zinahudumiwa na hao Mahakimu watatu ni watano. Mheshimiwa Mbunge nikuhaidi kwamba tutaendelea kuwasiliana ndani ya Serikali kuongeza Mahakimu katika Mahakama hizo ili huduma iweze kupatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili anazunguzia suala la nyongeza ya fedha, kwamba hawa watumishi wanapokuwa wanatoka maeneo hayo kuhudumia Mahakama zile ambazo inabidi waende, kwa kuwa Mahakimu hawajafika wanahitaji fedha kwa ajili ya kuhudimia.

Mheshimiwa Spika, nishukuru Bunge lako Tukufu, nimshukuru Mheshimiwa Rais kwamba mhimili wa Mahakama umekuwa ukiongezewa fedha. Mwaka huu ambao bajeti hii tunayoendelea nayo *OC* ya Mahakama ilipanda kutoka bilioni 60 mpaka bilioni 70, maana yake tunayo nyongeza ya zaidi ya bilioni 11. Kwa hiyo, tuwashukuru kwamba mmetuongezea na sisi tutaendelea kupeleka hizo fedha za *OC* ili Mahakimu hawa waweze kuhudumia maeneo ambako wanakwenda kuhudumia. Ahsante.*(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Amandus Chinguile, swali la nyongeza.

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Tarafa ya Ruponda katika Wilaya ya Nachingwea haina Jengo la Mahakama ya Mwanzo; je, ni lini Serikali itajenga Jengo la Mahakama ya Mwanzo kwenye Tarafa hii ya Ruponda iliyoko Makao Makuu ambayo yako kwenye Kata ya Ruponda? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naomba sasa nijibu swali Mheshimiwa Amandus Chingweli, Mbunge wa Nachingwea kama ifuatavyo:-

**SPIKA:** Ni Mheshimiwa Chinguile.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. *Sorry* kwa kukosea hilo jina.

Mheshimiwa Spika, Tarafa hii ya Ruponda ambako Mheshimiwa Mbunge ametamka, iko kwenye mpango wetu wa bajeti. Kwenye zile Mahakama 60 tunakwenda kujenga Mheshimiwa Mbunge, na tunafahamu ina umbali wa zaidi ya kilometa 14 kufuata huduma eneo lingine. Kwa hiyo, liko kwenye mpango tumeweka. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Suma Fyandomo, swali la nyongeza.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Spika, Wilayani Rungwe, Kata ya Kiwira ina Mahakama ya Mwanzo. Mahakama hiyo ni ya muda mrefu sana haijafanyiwa ukarabati, ukizingatia Mahakama hiyo inategemewa na Kata ya Ndanto, Isongole, Kinyala, Swaya, Kyimo na Kiwira yenyewe.

Je, ni lini Serikali itakwenda kufanya ukarabati wa Mahakama hiyo? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Suma, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, awali nilisema kwamba tuna mpango wa kukarabati majengo ya Mahakama kote nchini. Tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwamba ameridhia wenzetu wa *World Bank* wametupa zaidi ya dola milioni 90, zaidi ya bilioni 200 kuhakikisha tunaboresha miundombinu ya Mahakama kote nchini. Nikuhaidi Mheshimiwa Mbunge baada ya tafiti yetu kufanyika kwa Mtendaji Mkuu wa Mahakama akishirikiana na Watendaji wa Mikoa kuona maeneo ambapo pamechakaa zaidi tutakuja na mpango huu ili tuingize na hayo maeneo ambayo yamechakaa tuyaboreshe, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Charles Kajege, swali la nyongeza.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Majengo ya Mahakama ya Mwanzo katika Jimbo la Mwibara yamechakaa kabisa. Je, ni lini Serikali itajenga upya majengo hayo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimetangulia kusema kwamba fedha hizi ambazo tumezipata haziishi kujenga Mahakama za Mwanzo

ni pamoja na za Wilaya, lakini tunajenga pia *Integrated Justice Centers* kwenye Mikoa, kujenga Mahakama Jumuishi kuanzia Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya, Mkoa mpaka ya juu. Kwa hiyo, nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge katika mpango huu pia tutakufikia. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Regina Qwaray, swali la nyongeza.

**MHE. REGINA N. QWARAY:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Wananchi wa Tarafa ya Terati pamoja na Tarafa za jirani ikiwemo Mji mdogo wa Mererani wamekuwa wakitembea umbali mrefu kufuata huduma za Mahakama. Je, ni lini sasa Serikali itaanza ujenzi wa Mahakama ya Mwanzo katika eneo hilo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Regina Qwaray, Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wa Manyara na katika Wilaya ya Simanjiro tunakwenda kujenga Mahakama hiyo ya Terati, lakini siyo hapo tu pia tuna Mahakama ya Orkesumet, Mheshimiwa Regina umekuwa ukilifuatilia hili, tunaanza ujenzi mwaka huu. Ahsante.*(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali kutoka kwenu na majibu kutoka upande wa Serikali nitaleta matangazo niliyonayo hapa mbele halafu tutaendelea na ratiba yetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwanza tutaanza na tangazo la wageni; tutaanza na wageni waliopo Jukwaa la Spika, wageni 11 ambao ni wageni wangu kutoka Baraza la Waislamu Tanzania (BAKWATA) wakiongozwa na Sheikh Ally Ngeruko, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Sheikhe Ally Ngeruko ameongozana na viongozi wengine nao ni Mjumbe wa Baraza la ULAMAA na Naibu Kadhi Mkuu Tanzania, karibu sana. *(Makofi)*

Wageni wengine ambao ameongozana nao ni Sheikh Khamisi Kwangaya ambaye ni Katibu wa Kadhi Mkuu wa Tanzania, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Mudhihir Mchoye ambaye ni Mwenyekiti wa Sekretarieti, karibu sana; yupo pia Ndugu Mussa Hamis – Katibu wa Sekretarieti, karibu sana; yupo pia Muharami Pemba ambaye ni Mjumbe; yupo pia Faidhwa Yunusi huyu naye ni Mjumbe; yupo Ndugu Ramadhan Ally naye ni Mjumbe, yupo Ibrahim Tawfiq Mjumbe, yupo Ally Ally naye ni Mjumbe; yupo Shabani Hamis – Mjumbe; Fatuma Mayele – Mjumbe; Salum Mgodo – Mjumbe na yupo Ndugu Omary Jokoo naye ni Mjumbe; na Ndugu Ramadhani Magambo – Mjumbe, ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ujumbe huu ni kutoka BAKWATA lakini wanafanya kazi chini ya Kadhi Mkuu na kwa sasa wanafanya utafiti juu ya kukithiri kwa kuvunjika kwa ndoa na athari zake. Kwa hiyo, wanakusudia kuzunguka nchi nzima kwa ajili ya kukusanya maoni ili wajue nini cha kushauri wananchi katika hoja hii muhimu sana. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunawakaribisha sana Bungeni, karibuni sana na tunawatakia kila la kheri katika utafiti huu ambao mnaenda kuufanya, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Khamis Hamza Chilo ambaye ni Ndugu Machano Ali Machano, Mbunge wa Bunge la Afrika Mashariki kutoka Zanzibar, karibu sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao sasa wageni wa Wabunge mbalimbali ambao tunao leo hapa Bungeni; wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mheshimiwa Ridhiwani

Kikwete na hawa ni wapiga kura wake kutoka Chalinze, Mkoani Pwani, karibu sana. *(Makofi)*

Wapo wageni 46 wa Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Mhandisi Maryprisca Mahundi ambao ni Waandishi wa Habari kutoka Mkoa wa Mbeya, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 32 wa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mheshimiwa Omari Kipanga ambao ni Viongozi na Wajumbe wa CCM kutoka Jimbo la Mafia, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 63 wa Mheshimiwa Dkt. David Mathayo ambao ni Viongozi wa UVCCM kutoka Wilaya ya Same, Mkoa wa Kilimanjaro, karibuni sana *(Makofi)*

Tunao pia wageni 15 wa Mheshimiwa Stanslaus Mabula ambao ni Viongozi wa Kwaya ya *African Inland Church* Mkolani kutoka Nyamagana, Jijini Mwanza, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 60 wa Mheshimiwa Dkt. Florence Samizi ambao ni wanafunzi wa Shule ya Sekondari Ahwa kutoka Muhambwe Mkoa wa Kigoma, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 23 wa Mheshimiwa Priscus Tarimo hawa ni Wenyeviti Kata, Makatibu Kata na Wenezi Kata kutoka Moshi Mjini, Mkoa wa Kilimanjaro, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Regina Qwaray ambao ni ndugu zake kutoka Dar es Salaam. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Charles Kajege ambaye ni jamaa yake kutoka Bunda Mkoa wa Mara. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Masache Kasaka ambaye ni mpiga kura wake kutoka Chunya, Mkoani Mbeya. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Hussein Amar ambao ni wapiga kura wake kutoka Nyang'hwale, Mkoa wa Geita. *(Makofi)*

Tunao wageni saba wa Mheshimiwa Husna Sekiboko ambao ni wadau wa Elimu na Maendeleo Tanzania. *(Makofi)*

Tunao wageni watano wa Mheshimiwa Japhet Hasunga ambao ni wapiga kura wake kutoka Vwawa, Mkoani Songwe; na pia tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Abdallah Chaurembo ambao ni wapiga kura wake kutoka Mbagala, Jijini Dare es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Vilevile tunaye mgeni wa Mheshimiwa Francis Ndulane ambaye ni mdogo wake kutoka Kilwa, Mkoani Lindi. *(Makofi)*

Tunao wageni watano wa Mheshimiwa Abeid Ighondo ambao ni wapiga kura wake kutoka Singida Kaskazini. *(Makofi)*

Tunao wageni saba wa Mheshimiwa Neema Mwandabila ambao ni ndugu zake kutoka Mkoa wa Kigoma. *(Makofi)*

Tunao wageni sita wa Mheshimiwa Abdul Maalim ambao ni jamaa zake kutoka Shirika la Umeme Zanzibar, na pia tunao wageni 52 wa Mheshimiwa Esther Midimu ambao ni wanakwaya kutoka Boko, Jijini Dar es Salaam na wenyeji wao kutoka Dodoma Kati, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hawa ndio wageni tulionao asubuhi hii, lakini nimejulishwa wapo wageni wengine ambao wataingia baadaye. *(Makofi)*

Haya hapa nimeletewa orodha tayari ya wageni wengine ambao tuko nao hapa ndani na walikuwa hawajatangazwa. Hawa ni wageni ambao wapo Jukwaa la Spika pia.

Tunao wageni saba ambao ni wageni wangu, wanatoka *Riyadha Mosque and Islamic Center* wakiongozwa na Mbunge Mstaafu wa Bunge la Kenya, Mheshimiwa Abubakar Muhammad Badawi, karibuni sana Bungeni wageni wetu na karibuni sana nchini. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Abubakar Muhammad Badawi ameambatana na Sekretarieti ya *Riyadha*

*Mosque and Islamic Center* ambao ni Ndugu Hussein Mohamed Sayyid Ali; yupo pia Mohamed Abdulkadir Mohamed, yupo pia Hassan Abubakar Muhdhar; pia yupo Abdallah Abdulkadir Mohamed; yupo Japhary Salum Kininki; yupo Ahmed Munuve, yupo Ally Seif Kasembo; na Ndugu Ally Majid Ally, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni wengine ambao nimeongezewa orodha hapa ni wageni sita ambao pia ni wageni wangu kutoka *Tanzania Association of Radiographers (TARA)* wakiongozwa na Ndugu Joseph Ndumbaro, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni watano wa Waziri wa Fedha - Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba na hawa ni Ndugu Jenifa Omolo ambaye ni Naibu Katibu Mkuu Huduma za Hazina; yupo Dkt. Fredrick Mwakibinga, Kamishna wa Sera ya Ununuzi wa Umma; yupo pia Ndugu Eliakim Maswi ambaye ni Afisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Kudhibiti Ununuzi wa Umma; yupo pia Ndugu James Sando ambaye ni Katibu Mtendaji wa Mamlaka ya Rufaa ya Ununuzi wa Umma; na pia yupo Profesa Geraldine Rasheli ambaye ni Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Huduma za Ununuzi Serikalini, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia tunao wageni watatu kutoka Kanisa la Waadiventista Wasabato Jimbo la Kati Dodoma ambao ni Askofu Richard Kaniki ambaye ameongozana na mke wake Ndugu Wemael Kaniki pamoja na Mchungaji Kois Mollen, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema wageni wengine tutaendelea kuwatangaza watakapopata nafasi ya kuingia hapa ndani kwa sababu wageni ni wengi na hawakuweza wote kuingia kwa wakati mmoja. Kwa hiyo, tutawatangaza kadiri ya wanavyopata nafasi ya kuingia hapa ndani.

Tangazo lingine linatoka kwa Katibu wa Bunge, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kuwa Tume ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI *(TACAIDS)* kwa kushirikiana na Baraza la

Taifa la Watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI *(NACOPHA)* chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu imeandaa mdahalo wa kitaifa juu ya kuimarisha ushirikiano na ushiriki wa jamii kwenye mwitikio wa UKIMWI hapa nchini. Mdahalo huo utafanyika leo siku ya Alhamisi tarehe 7 Septemba, 2023, kuanzia saa 7.00 mchana katika Ukumbi wa Mkutano wa *Jakaya Kikwete Convention Center,* Dodoma na utaambatana na Maadhimisho ya miaka 20 ya *NACOPHA*.

Waheshimiwa Wabunge, mgeni rasmi katika mdahalo huo anatarajiwa kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge wote mnaalikwa kuhudhuria mdahalo huu muhimu.

Waheshimiwa Wabunge, hayo ndiyo matangazo tuliyonayo, tutaendelea na ratiba yetu.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Ununuzi wa Umma wa Mwaka 2023**

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Muswada unasomwa Mara ya Pili, hivyo nimwite Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, aje awasilishe hoja yake.

Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Ununuzi wa Umma wa mwaka 2023 pamoja na marekebisho yake sasa usomwe kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Mbunge wa Babati Vijijini, kwa kuujadili kwa kina muswada huu na kutoa ushauri kwa ajili ya kuuboresha.

Mheshimiwa Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako tukufu kwamba Muswada huu umezingatia kwa kiasi kikubwa ushauri na mapendekezo mazuri ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti na wadau mbalimbali ambao kwa nyakati tofauti walitoa ushauri wao. Aidha, nitoe shukurani zangu kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, wataalam wake pamoja wataalam wa Wizara ya Fedha kwa kuuandaa Muswada huu pamoja na marekebisho yake.

Mheshimiwa Spika, lengo la kutunga Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2023 ni kuweka masharti bora ya usimamizi wa ununuzi wa umma, ugavi na uondoshaji wa mali kwa njia ya zabuni. Kwa ujumla, sheria inayopendekezwa inakusudia kutatua changamoto zilizobainika katika utekelezaji wa masharti na utaratibu wa ununuzi na ugavi pamoja na uondoshaji wa mali kwa njia ya zabuni.

Mheshimiwa Spika, changamoto zilizopo hivi sasa ni pamoja na Sheria: -

(a) Kutotofautisha masharti ya ununuzi kati ya Taasisi za Umma zinazojiendesha kibiashara na zisizojiendesha kibiashara;

(b) Kutojumuisha masuala ya ugavi;

(c) Kutokuwa na sehemu mahususi inayohusu masuala ya usimamizi wa mikataba ya ununuzi;

(d) Kutoa mwanya wa ununuzi kutekelezwa nje ya mfumo wa ununuzi kwa njia ya kielektroniki;

(e) Kutobainisha masharti ya bei kikomo katika ununuzi wa umma;

(f) Kutokuwa na masharti kuhusu ukomo wa thamani ya mradi, taarifa za ukaguzi wa kazi zilizofanyika, kipindi cha uangalizi wa ubora wa kazi, sharti la kudhibiti viwango vya weledi na uzoefu wa kiutekelezaji wa miradi ya ujenzi kwa utaratibu wa *force account;*

(g) Kutokuwa na viwango vya ukomo na uidhinishaji wa zabuni; na

(h) Kuweka muda wa urefu wa hatua za utekelezaji wa ununuzi.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya kutungwa kwa sheria inayopendekezwa ni pamoja na haya yafuatayo: -

(a) Kuimarika kwa mazingira ya ununuzi na ugavi kwa taasisi na mashirika ya umma yanayojiendesha kibiashara;

(b) Kujumuisha katika mnyororo wa ugavi masuala ya ununuzi, ugavi na uondoshwaji wa mali kwa njia ya zabuni ili kupata thamani halisi ya fedha zinazotumika kupitia ununuzi na utekelezaji wa miradi ya Serikali;

(c) Kuimarika kwa usimamizi wa mikataba ya ununuzi;

(d) Kuongeza ufanisi katika mnyororo wa ugavi kupitia matumizi ya mfumo wa ununuzi kwa njia ya kielektroniki kwenye ununuzi na ugavi na uondoshwaji wa mali kwa njia ya zabuni;

(e) Kuweka masharti ya bei kikomo kwa baadhi ya bidhaa na huduma katika ununuzi wa umma na hivyo kudhibiti gharama;

(f) Kuongezeka kwa ufanisi katika utekelezaji wa miradi kwa utaratibu wa *force account;*

(g) Kupunguza urasimu katika uidhinishaji wa zabuni, hivyo kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa shughuli za mnyororo wa ugavi; na mwisho

(h) Kufuta Sheria ya Ununuzi wa Umma, Na. 7 ya mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya Muswada huu ni kwanza ni kufangamanisha masuala ya ununuzi na ugavi katika mnyororo wa usimamizi wa ugavi; pili, kuimarisha mazingira ya ununuzi na ugavi katika taasisi na mashirika ya umma yanayojiendesha kibiashara; na tatu, kupunguza muda katika hatua na michakato ya zabuni.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umegawanyika katika sehemu 12 kama ifuatavyo:- -

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kwanza kama ilivyorekebishwa kupitia Jedwali la Marekebisho inaweka masharti ya utangulizi ambayo ni jina la sheria, tarehe ya kuanza kutumika, matumizi ya sheria, tafsiri ya maneno mbalimbali yanayotumika katika sheria, wajibu wa kimataifa, misingi na viwango vya jumla vya ununuzi, ugavi na uondoshaji mali kwa njia ya zabuni.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Pili kama ilivyorekebishwa kwenye jedwali la marekebisho, inaainisha uwepo wa Kamishna wa Idara ya Sera ya Ununuzi wa Umma na majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tatu kama ilivyorekebishwa kupitia jedwali la marekebisho inaainisha masuala yafuatayo: -

(a) Kuendelea kuwepo kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma, malengo na majukumu yake;

(b) Nguvu ya kisheria Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma kufanya uchunguzi, kupata taarifa, kutoa mapendekezo kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali au Afisa Masuuli wa Taasisi ya Umma inayohusika na uchunguzi, kuwasilisha matokeo ya uchunguzi kwa mtu au watu wenye mamlaka ya kuchukua hatua za kinidhamu au

nyinginezo stahiki dhidi ya afisa au mtumishi na kuwasilisha taarifa maalumu kwa Waziri mwenye dhamana;

(c) Taarifa za uendeshaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma hazitachukuliwa kuwa batili kwa kigezo cha kutokuwepo kwa utaratibu ulioainishwa katika sheria;

(d) Majukumu ya Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma ikiwemo kuomba taarifa, nyaraka na kumbukumbu ya aina yoyote, kuhusu mchakato wa ununuzi na ugavi, kutoa wito, kufanya uchunguzi na kuanzisha ukaguzi kwenye shughuli zinazohusiana na ununuzi na ugavi;

(e) Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma kupendekeza kwenye chombo chenye mamlaka kuhusu kusitisha utoaji wa fedha au kuzitaka taasisi kurejesha fedha zilizopotea, kubadilishwa kwa Mkuu wa Kitengo cha Usimamizi wa Ununuzi, kuchukuliwa hatua za kinidhamu kwa Afisa Masuuli, Mkuu wa Kitengo cha Usimamizi wa Ununuzi, Mjumbe wa Kamati ya Tathmini au afisa mwingine yeyote anayehusika katika mchakato wa ununuzi na uhamisho wa muda wa majukumu ya ununuzi ya taasisi kwenda taasisi nyingine au Wakala;

(f) Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma; na

(g) Vyanzo vya mapato ya Mamlaka ambavyo vitajumuisha fedha zitakazotengwa na Bunge, mikopo au misaada, mapato yatokanayo na bidhaa au huduma zinazotolewa na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma, fedha nyingine zote zitakazopokelewa na Mamlaka kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yoyote yale.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Nne kama ilivyoainishwa katika jedwali la marekebisho inapendekeza kuweka masharti kuhusu mpangilio wa taasisi katika ununuzi na ugavi. Aidha, Sehemu hii, inaainisha ngazi mbalimbali za maamuzi katika hatua za ununuzi pamoja na kuainisha majukumu ya kila ngazi katika jukumu hilo.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tano kama ilivyorekebishwa kupitia Jedwali la Marekebisho, inapendekeza masharti kuhusu taratibu mbalimbali za ununuzi wa umma ikiwemo ununuzi katika taasisi zinazojiendesha kibiashara, wajibu wa taasisi za ununuzi, uidhinishaji wa mpango wa ununuzi wa mwaka, ununuzi wa kupitia mikataba maalum pamoja na nyingine.

Mheshimiwa Spika, vilevile sehemu hii ya tano inaweka masharti mbalimbali yanayohusu upendeleo katika zabuni kwa watu na makundi maalum ya kijamii au kampuni za ndani na bidhaa na huduma zilizotengenezwa au kuzalishwa ndani ya nchi. Lengo la masharti haya ni kuweka upendeleo ili kujenga uwezo kwa kampuni za ndani na wataalamu wa ndani ili kuwezesha ushiriki katika zabuni mbalimbali. Aidha, sehemu hii pia inaweka masharti ya kukubaliwa au kukataliwa kwa zabuni au hatua zilizochukuliwa kwa mzabuni aliyekiuka taratibu mbalimbali za ununuzi.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Sita kama ilivyorekebishwa katika jedwali la marekebisho, inaainisha masharti kuhusu njia ya michakato ya ununuzi wa umma. Sehemu hii inaweka masharti kwa taasisi za ununuzi kufanya shughuli za ununuzi, ugavi na uondoshaji mali kwa njia ya kielektroniki kwa kuzingatia bei kikomo, uchaguzi wa njia za ununuzi na matumizi ya rasilimali za ndani *(Force Account)*.

Mheshimiwa Spika, aidha, sehemu hii inaainisha masharti ya ununuzi wa dharura, ununuzi wa moja kwa moja kutoka kwa mzalishaji, wakala au mtoa huduma. Aidha, sehemu hii inaweka masharti kuhusu viwango vya ununuzi vilivyoidhinishwa, ununuzi wa vichwa na mabehewa vya treni, meli, ndege zilizotumika, zabuni shindani, ununuzi wa bidhaa za afya na masharti kuhusu mwaliko wa zabuni na matangazo.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Saba kama ilivyorekebishwa kupitia jedwali la marekebisho inaweka masharti ya usimamizi wa mikataba ya ununuzi. Sehemu hii inampa Afisa Masuuli wajibu wa jumla katika utekelezaji wa mkataba wa ununuzi ikiwemo kutoa jukumu kwa Afisa Masuuli kuteua timu, msimamizi, Meneja wa Mradi au Mshauri Elekezi atakayesimamia utekelezaji wa mkataba.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Nane kama ilivyorekebishwa kupitia jedwali la marekebisho inaweka masharti kuhusu usimamizi wa ugavi ikiwemo upokeaji wa bidhaa, vifaa ama mali zilizonunuliwa, uwekaji wa kumbukumbu, utunzaji na usambazaji wa bidhaa, vifaa na mali kwa ajili ya matumizi yaliyokusudiwa na taasisi za umma.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tisa ya Muswada kama ilivyorekebishwa kupitia Jedwali la Marekebisho inaainisha utaratibu utakaotumika katika ununuzi wakati wa utekelezaji wa miradi ya ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi kama ilivyorekebishwa kupitia jedwali, inafanya marekebisho inaainisha masuala yafuatayo: -

(a) Vitendo na mienendo mbalimbali inayokatazwa katika hatua za ununuzi ikiwemo rushwa, udanganyifu, na ulaji wa njama;

(b) Ulazima kwa wazabuni kuwasilisha taarifa ya maandishi kwa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) na Mamlaka ya Mapato Tanzania kuhusu malipo ya kamisheni ya kupata mkataba wa zabuni ya ununuzi;

(c) Vitendo vitakavyofanywa na Mkurugenzi, wafanyakazi au mawakala wa taasisi kuchukuliwa kuwa vimefanywa na taasisi nafsi hiyo; na

(d) Ufunguaji wa mashauri ya jinai dhidi ya mtu yeyote anayetekeleza majukumu ya ununuzi wa umma.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Moja kama ilivyorekebishwa kupitia jedwali la marekebisho, inaainisha masuala ya utatuzi wa migogoro kama ifuatavyo: -

(a) Kuendelea kuwepo kwa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma malengo na majukumu yake;

(b) Utaratibu wa uwasilishaji wa malalamiko au migogoro inayotokana na taratibu za rufani kwa Afisa Masuuli au Mamlaka ya Rufani;

(c) Usitishwaji wa michakato ya ununuzi; na

(d) Haki ya kuomba mapitio ya kimahakama kwa taasisi nunuzi au mzabuni ambaye hajaridhika na uamuzi wa Mamlaka ya Rufani.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Mbili kama ilivyorekebishwa kupitia jedwali la marekebisho inahusu masharti ya jumla kama ifuatavyo: -

(a) Masharti ya uzingatiwaji wa kanuni za maadili katika ununuzi wa umma pamoja na kinga dhidi uwajibikaji binafsi;

(b) Makosa mbalimbali yanayoweza kutendwa na wazabuni na watumishi wa umma wanaotekeleza majukumu ya ununuzi wa umma na ugavi pamoja na adhabu zake;

(c) Mamlaka ya Waziri kuandaa kanuni pamoja na kuipa Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma nguvu ya kisheria ya kutoa miongozo kuhusu masuala mbalimbali; na

(d) Kufuta Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 7 ya Mwaka 2011 na kuweka masharti ya mpito kuhusu matumizi ya baadhi ya vifungu vya sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, naomba taarifa yangu yote iingie katika kumbukumbu rasmi za Bunge na majedwali mengine tutayaleta ili yaweze kujadiliwa wakati wa kupitisha hoja.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, naomba Bunge lako liujadili Muswada huu pamoja na marekebisho yake na hatimaye mkubali kuupitisha kuwa sheria.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MAELEZO YA WAZIRI WA FEDHA, MHESHIMIWA MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MUSWADA WA SHERIA YA UNUNUZI WA UMMA WA MWAKA 2023 KUSOMWA KWA MARA YA PILI - KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

**UTANGULIZI**

1. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Ununuzi wa Umma wa Mwaka 2023 pamoja na marekebisho yake sasa **usomwe kwa mara ya pili.**

2. ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti chini ya Mwenyekiti wake **Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Mbunge wa Babati Vijijini** kwa kuujadili kwa kina Muswada huu na kutoa ushauri kwa ajili ya kuuboresha.

3. ***Mheshimiwa Spika*****,** napenda kulihakikishia Bunge lako tukufu kwamba, Muswada huu umezingatia kwa kiasi kikubwa ushauri na mapendekezo mazuri ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti na wadau mbalimbali ambao kwa nyakati tofauti walitoa ushauri wao. Aidha, nitoe shukran zangu kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, wataalam wake pamoja wataalam wa Wizara ya Fedha kwa kuandaa Muswada huu pamoja na marekebisho yake.

4. ***Mheshimiwa Spika*****,** lengo la kutunga Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2023 ni kuweka masharti bora ya usimamizi wa ununuzi wa umma, ugavi na uondoshaji wa mali kwa njia ya zabuni. Kwa ujumla, Sheria inayopendekezwa inakusudia kutatua changamoto zilizobainika katika utekelezaji wa masharti na

taratibu za ununuzi, ugavi na uondoshaji wa mali kwa njia ya zabuni.

5. ***Mheshimiwa Spika,*** changamoto zilizopo hivi sasa ni pamoja na Sheria:

a) kutotofautisha masharti ya ununuzi kati ya taasisi za umma zinazojiendesha kibiashara na zisizojiendesha kibiashara;

b) kutojumuisha masuala ya ugavi;

c) Kutokuwa na sehemu mahsusi inayohusu masuala ya usimamizi wa mikataba ya ununuzi;

d) kutoa mwanya wa ununuzi kutekelezwa nje ya mfumo wa ununuzi kwa njia ya kielektroniki;

e) kutokubainisha masharti ya bei kikomo katika ununuzi wa umma;

f) kutokuwa na masharti kuhusu ukomo wa thamani ya mradi, taarifa za ukaguzi wa kazi zilizofanyika, kipindi cha uangalizi wa ubora wa kazi, sharti la kudhibiti viwango vya weledi na uzoefu wa watekelezaji wa miradi ya ujenzi kwa utaratibu wa *force account* ;

g) kutokuweka viwango vya ukomo wa uidhinishaji wa zabuni; na

h) kuweka muda mrefu wa hatua za utekelezaji wa ununuzi.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** matokeo ya kutungwa kwa sheria inayopendekezwa ni pamoja na:

a) kuimarika kwa mazingira ya ununuzi na ugavi kwa taasisi na mashirika ya umma yanayojiendesha kibiashara;

b) kujumuisha katika mnyororo wa ugavi masuala ya ununuzi, ugavi na uondoshwaji wa mali kwa njia ya zabuni ili kupata

thamani halisi ya fedha zinazotumika kupitia ununuzi na utekelezaji wa miradi ya Serikali;

c) kuimarika kwa usimamizi wa mikataba ya ununuzi;

d) kuongeza ufanisi katika mnyororo wa ugavi kupitia matumizi ya mfumo wa ununuzi kwa njia ya kielektroniki kwenye ununuzi, ugavi na uondoshwaji wa mali kwa njia ya zabuni;

e) kuweka masharti ya bei kikomo kwa baadhi ya bidhaa na huduma katika ununuzi wa umma na hivyo kudhibiti gharama;

f) kuongezeka kwa ufanisi katika utekelezaji wa miradi kwa utaratibu wa *force account*;

g) kupunguza urasimu katika uidhinishaji wa zabuni hivyo kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa shughuli za mnyororo wa ugavi; na

h) kufuta Sheria ya Ununuzi wa Umma, Na. 7 ya mwaka 2011.

**MADHUMUNI YA MUSWADA**

7. ***Mheshimiwa Spika,*** Madhumuni ya Muswada huu ni: **Kwanza** kufangamanisha masuala ya ununuzi na ugavi katika mnyororo wa usimamizi wa ugavi; **Pili,** kuimarisha mazingira ya ununuzi na ugavi kwa taasisi na mashirika ya umma yanayojiendesha kibiashara, **Tatu;** kupunguza muda katika hatua na michakato ya zabuni.

***Mheshimiwa Spika,*** Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Kumi na Mbili kama ifuatavyo:-

***Mheshimiwa Spika,*** Sehemu ya Kwanza kama ilivyorekebishwa kupitia Jedwali la Marekebisho inaweka masharti ya utangulizi ambayo ni jina la Sheria, tarehe ya kuanza kutumika, matumizi ya sheria, tafsiri ya maneno mbalimbali yanayotumika katika sheria, wajibu wa kimataifa, misingi na viwango vya jumla vya ununuzi, ugavi na uondoshaji mali kwa njia ya zabuni.

***Mheshimiwa Spika,*** Sehemu ya Pili kama ilivyorekebishwa kupitia Jedwali la Marekebisho inaainisha uwepo wa Kamishna wa Idara ya Sera ya Ununuzi wa Umma na majukumu yake.

***Mheshimiwa Spika,*** Sehemu ya Tatu kama ilivyorekebishwa kupitia Jedwali la Marekebisho inaainisha masuala yafuatayo;-

(a) kuendelea kuwepo kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma, malengo na majukumu yake;

(b) nguvu ya kisheria Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma kufanya uchunguzi, kupata taarifa, kutoa mapendekezo kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali au Afisa Masuuli wa Taasisi ya umma inayohusika na uchunguzi na kuwasilisha matokeo ya uchunguzi kwa mtu au watu wenye mamlaka ya kuchukua hatua za kinidhamu au hatua nyingine stahiki dhidi ya afisa au mtumishi na kuwasilisha taarifa maalumu kwa Waziri;

(c) taratibu za uendeshaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma hazitachukuliwa kuwa batili kwa kigezo cha kutokuwepo kwa utaratibu ulioainishwa katika Sheria;

(d) majukumu ya Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma ikiwemo kuomba taarifa, nyaraka na kumbukumbu ya aina yoyote, kuhusu mchakato wa ununuzi na ugavi, kutoa wito, kufanya uchunguzi na kuanzisha ukaguzi kwenye shughuli zinazohusiana na ununuzi na ugavi;

(e) Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma kupendekeza kwenye chombo chenye mamlaka kuhusu: kusitisha utoaji wa fedha au kuzitaka taasisi kurejesha fedha zilizopotea, kubadilishwa kwa Mkuu wa Kitengo cha Usimamizi wa Ununuzi, kuchukuliwa hatua za kinidhamu kwa Afisa Masuuli, Mkuu wa Kitengo cha Usimamizi wa Ununuzi, Mjumbe wa kamati ya tathmini au afisa mwingine yoyote anayehusika katika mchakato wa ununuzi na uhamisho wa muda wa majukumu ya ununuzi ya taasisi kwenda taasisi nyingine au Wakala.

(f) Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma;

(g) vyanzo vya mapato ya Mamlaka ambavyo vitajumuisha fedha zitakazotengwa na Bunge, mikopo au misaada, mapato yatokanayo na bidhaa au huduma zinazotolewa na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma na fedha nyingine zozote zitakazopokelewa na Mamlaka kwa kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake;

(h) utunzaji wa vitabu vya hesabu, ukaguzi wa hesabu utakaofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali pamoja na uwasilishaji wa mpango kazi wa mwaka wa Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma kwenye Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka; na

(i) utaratibu wa uwasilishwaji wa taarifa ya mwaka ya tathmini ya utendaji kazi wa ununuzi wa Umma na thamani halisi ya fedha kwa Mheshimiwa Rais na uwasilishwaji wa taarifa ya mwaka ya shughuli za Mamlaka kwa Waziri.

***Mheshimiwa Spika,*** Sehemu ya Nne kama ilivyorekebishwa kupitia Jedwali la Marekebisho inapendekeza kuweka masharti kuhusu mpangilio wa kitaasisi katika ununuzi na ugavi. Aidha, Sehemu hii, inaainisha ngazi mbalimbali za maamuzi katika hatua za ununuzi pamoja na kuainisha majukumu ya kila ngazi kama ifuatavyo; Bodi za Zabuni, Afisa Masuuli, Kitengo cha Usimamizi wa Ununuzi, Idara Tumizi na Kamati ya Tathmini.

***Mheshimiwa Spika,*** Sehemu ya Tano kama ilivyorekebishwa kupitia Jedwali la Marekebisho inapendekeza masharti kuhusu taratibu mbalimbali za ununuzi wa umma ikiwemo; ununuzi katika taasisi zinazojiendesha kibiashara, wajibu wa taasisi nunuzi, uidhinishaji wa mpango wa ununuzi wa mwaka, ununuzi wa kupitia mikataba maalum. Aidha, sehemu hii inaainisha sifa za wazabuni, taratibu za uchambuzi wa sifa za awali, uhakiki wa sifa za wazabuni, upendeleo wa kitaifa, upendeleo wa kipekee kwa wazabuni wa ndani na ushiriki kwa Kampuni za ndani na wataalamu katika mikataba ya ushauri elekezi na matumizi ya

wataalamu wa ndani katika mikataba ya kazi za ujenzi na huduma zisizo za kitaalamu.

***Mheshimiwa Spika,*** vilevile sehemu hii ya tano inaweka masharti mbalimbali yanayoruhusu upendeleo katika zabuni kwa watu na Makundi Maalum ya kijamii au kampuni za ndani na bidhaa au huduma zilizotengenezwa au kuzalishwa ndani ya nchi. Lengo la masharti ya upendeleo ni kujenga uwezo kwa kampuni za ndani na wataalamu wa ndani ili kuziwezesha kushiriki katika zabuni mbalimbali. Aidha, sehemu hii pia inaweka masharti ya kukubaliwa au kukataliwa kwa zabuni na hatua zinazoweza kuchukuliwa kwa mzabuni anayekiuka taratibu mbalimbali za zabuni za ununuzi.

***Mheshimiwa Spika,*** Sehemu ya Sita kama ilivyorekebishwa kupitia Jedwali la Marekebisho inaainisha masharti kuhusu njia na michakato ya ununuzi wa umma. Sehemu hii inaweka masharti kwa taasisi nunuzi kufanya shughuli za ununuzi, ugavi na uondoshaji mali kwa njia ya kielektroniki kwa kuzingatia bei kikomo, uchaguzi wa njia za ununuzi na matumizi ya rasilimali za ndani (*Force Account)*.

***Mheshimiwa Spika,*** aidha, sehemu hii inaainisha masharti ya ununuzi wa dharura, ununuzi wa moja kwa moja kutoka kwa Mzalishaji, Wakala au Mtoa Huduma. Aidha, sehemu hii inaweka masharti kuhusu; viwango vya ununuzi vilivyoidhinishwa, ununuzi wa vichwa na mabehewa ya treni, meli au ndege zilizotumika, zabuni shindani, ununuzi wa bidhaa za afya; na masharti kuhusu mwaliko wa zabuni na matangazo.

***Mheshimiwa Spika,*** vilevile sehemu hii ya sita inaweka masharti ya utoaji wa nyaraka za zabuni yenye lengo la kuhakikisha uwazi katika mchakato wa ununuzi na kuondoa ucheleweshaji unaoweza kuepukika katika hatua mbalimbali za ununuzi. Taratibu za ununuzi zinazoelezewa katika sehemu hii ni pamoja na masharti kuhusu utoaji wa nyaraka za zabuni na maudhui yake, ufunguaji wa zabuni, tathmini ya zabuni, uidhinishaji na utoaji wa tuzo ya mkataba.

***Mheshimiwa Spika,*** Sehemu ya Saba kama ilivyorekebishwa kupitia Jedwali la Marekebisho inaweka masharti ya usimamizi wa mikataba ya ununuzi. Sehemu hii inampa afisa masuuli wajibu wa jumla katika utekelezaji wa mkataba wa ununuzi ikiwemo: kutoa jukumu kwa afisa masuuli kuteua timu, msimamizi, meneja wa mradi au mshauri elekezi atakayesimamia utekelezaji wa mkataba. Aidha, Sehemu hii inazipa wajibu idara tumizi kuhakikisha kuwa bidhaa zilizowasilishwa, kazi za ujenzi zilizofanyika au huduma zilizotolewa zimekidhi vigezo na masharti ya mkataba. Vilevile, Sehemu hii imeainisha taratibu za mabadiliko au marekebisho ya mkataba, ufungaji na uvunjaji wa mkataba.

***Mheshimiwa Spika,*** Sehemu ya Nane kama ilivyorekebishwa kupitia Jedwali la Marekebisho inaweka masharti kuhusu usimamizi wa ugavi ikiwemo upokeaji wa bidhaa, vifaa au mali zilizonunuliwa, uwekaji kumbukumbu, utunzaji na usambazaji wa bidhaa, vifaa na mali kwa ajili ya matumizi yaliyokusudiwa na taasisi za umma. Aidha, sehemu hii inaweka sharti kwa taasisi nunuzi kuzingatia miongozo inayotolewa na Mlipaji Mkuu wa Serikali chini ya Sheria ya Fedha za Umma, Sura 348 kuhusu usimamizi wa bidhaa, vifaa na mali.

***Mheshimiwa Spika,*** Sehemu ya Tisa ya Muswada kama ilivyorekebishwa kupitia Jedwali la Marekebisho inaainisha utaratibu utakaotumika katika ununuzi wakati wa utekelezaji wa miradi ya ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi.

***Mheshimiwa Spika,*** Sehemu ya Kumi kama ilivyorekebishwa kupitia Jedwali la Marekebisho inaainisha masuala yafuatayo:

a. vitendo na mienendo mbalimbali inayokatazwa katika hatua za ununuzi ikiwemo rushwa, udanganyifu, na ulaji wa njama;

b. ulazima kwa wazabuni kuwasilisha taarifa ya maandishi kwa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kuhusu malipo ya kamisheni ya kupata mkataba wa zabuni ya ununuzi;

c. vitendo vitakavyofanywa na Wakurugenzi, wafanyakazi au mawakala wa taasisi nafsi, kuchukuliwa kuwa vimefanywa na taasisi nafsi hiyo; na

d. ufunguaji wa mashauri ya jinai dhidi ya mtu yoyote anayetekeleza majukumu ya ununuzi wa umma.

***Mheshimiwa Spika,*** Sehemu ya Kumi na Moja kama ilivyorekebishwa kupitia Jedwali la Marekebisho inaainisha masuala ya utatuzi wa migogoro kama ifuatavyo;

a. kuendelea kuwepo kwa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma malengo na majukumu yake;

b. utaratibu wa uwasilishaji wa malalamiko au migogoro inayotokana na taratibu za ununuzi wa umma kwa Afisa Masuuli au Mamlaka ya Rufani;

c. usitishwaji wa michakato ya ununuzi; na

d. haki ya kuomba mapitio ya kimahakama kwa taasisi nunuzi au mzabuni ambaye hajaridhika na uamuzi wa Mamlaka ya Rufani.

***Mheshimiwa Spika,*** Sehemu ya Kumi na Mbili kama ilivyorekebishwa kupitia Jedwali la Marekebisho inahusu masharti ya jumla kama ifuatavyo:

a. masharti ya uzingatiwaji wa kanuni za maadili katika ununuzi wa umma pamoja na kinga dhidi uwajibikaji binafsi;

b. makosa mbalimbali yanayoweza kutendwa na wazabuni na watumishi wa umma wanaotekeleza majukumu ya ununuzi wa umma na ugavi pamoja na adhabu zake;

c. mamlaka ya Waziri kuandaa kanuni pamoja na kuipa Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma nguvu ya kisheria ya kutoa miongozo kuhusu masuala mbalimbali; na

d. kufuta Sheria ya Ununuzi wa Umma Namba 7 ya Mwaka 2011 na kuweka masharti ya mpito kuhusu matumizi ya baadhi ya vifungu vya sheria hiyo.

**HITIMISHO**

***Mheshimiwa Spika,*** baada ya maelezo haya naomba Bunge lako liujadili Muswada huu pamoja na marekebisho yake na hatimaye mkubali kuupitisha kuwa Sheria.

***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.

***MLNM***
***WF***

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Sasa nimwite Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, Mheshimiwa Daniel Baran Sillo aje awasilishe maoni ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MHE. DANIEL B. SILLO – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 naomba kutoa maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 5 ya mwaka 2023.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umebadilisha lugha ya Sheria ilivyo hivi sasa kutoka lugha ya Kiingereza kwenda lugha ya Kiswahili ili Sheria hii iweze kueleweka kwa urahisi kwa watumiaji. Manunuzi ya Umma yanatumia kiasi kikubwa cha fedha za Serikali na inakadiriwa takriban asilimia 70 ya Bajeti yote ya Serikali

hutumika kwenye ununuzi wa Umma na hivyo inapaswa kusimamiwa kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba Taarifa yetu ya Kamati iingie katika Kumbukumbu Rasmi za Bunge kama ilivyowasilishwa Mezani.

Mheshimiwa Spika, jinsi Kamati ilivyoshughulika na Muswada; Kamati ilianza uchambuzi wa muswada huu kwa kukutana na Serikali kupitia vifungu vya Sheria ya Ununuzi wa Umma Sura 410 vinavyofanyiwa marekebisho katika Muswada pamoja na maudhui yake. Aidha, kwa mujibu wa Kanuni ya 97(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 Kamati ilifanya mkutano na wadau tarehe 15 na 16 Agosti, 2023 ili kupokea mapendekezo na maoni kuhusu muswada huu. Aidha, kutokana na umuhimu wa sheria hii Kamati ilitoa mualiko kwa Waheshimiwa Wabunge kufika mbele ya Kamati ili kutoa maoni yao kuhusu muswada huu.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge waliofika mbele ya Kamati ni kama wafuatao; Mheshimiwa Salome Makamba, Mheshimiwa Jumanne Kidera Kishimba, Mheshimiwa Mhandisi Mwanaisha Ulenge na Mheshimiwa Anastazia James Wambura. Kamati iliupitia muswada huu kifungu kwa kifungu kwa madhumuni ya kujielimisha maudhui ya kila kifungu na kupendekeza marekebisho katika maeneo yanayohitaji marekebisho.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya majadiliano ya kina na Waziri wa Fedha, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Kamishna wa Sera ya Ununuzi pamoja na Wataalam kutoka Wizara ya Fedha na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Vilevile, Kamati ilikutana na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma, Wakala wa Ununuzi Serikalini *(GPSA)*, Mamlaka ya Rufani ya Ununuzi wa Umma pamoja na Bodi ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi.

Mheshimiwa Spika, wadau waliofika mbele ya Kamati kwa ajili ya kutoa maoni juu ya Muswada huu ni Shirika la Mawasiliano Tanzania *(TTCL)*, Kampuni ya Taifa ya Mbolea. Aidha, kampuni binafsi kama vile *Nyakwe Enterprises* na Umoja wa Watalaamu wa

Ununuzi na Ugavi pamoja na watu binafsi waliwasilisha maoni yao kwa njia ya barua pepe.

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya muswada; muswada huu unakusudia kufuta na kutunga upya Sheria ya Ununuzi wa Umma Sura 410 ya Mwaka 2011 kama ilivyorekebishwa mwaka 2013, 2014, 2015, 2016 na 2018 mtawalia. Muswada huu unalenga kufuta iliyokuwa Sheria ya Ununuzi wa Umma Sura 410 na kutunga upya ili kuweka masharti bora ya usimamizi wa ununuzi wa umma, ugavi na uondoshaji mali kwa njia ya zabuni.

Mheshimiwa Spika, mapungufu ya sheria ya sasa; marekebisho haya ni sehemu ya kutatua na kurekebisha changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa Sheria hii. Pia yanaenda kuokoa fedha za Serikali na kuhakikisha kuwa thamani halisi ya fedha inapatikana katika ununuzi wa umma. Changamoto za utekelezaji wa Sheria ya Ununuzi wa Umma zinazoenda kutatuliwa katika muswada huu:-

(i) Bei kubwa za bidhaa, huduma na kandarasi ikilinganishwa na bei ya soko;

(ii) Kukosekana kwa viwango vya ukomo wa uidhinishaji wa zabuni kati ya Bodi ya Zabuni na Afisa Masuuli;

(iii) Usimamizi hafifu wa masuala ya mnyororo wa ugavi;

(iv) Matumizi mabaya ya utaratibu wa rasilimali za ndani katika utekelezaji wa miradi kutokana na kukosekana kwa wataalamu na miongozo ya usimamizi;

(v) Usimamizi hafifu wa Mikataba ya Ununuzi;

(vi) Kutokufanya manunuzi kwa njia ya mfumo wa ununuzi wa kielektroniki;

(vii) Mzabuni kuongezewa muda wa ziada kama adhabu zaidi ya ule aliofungiwa nje ya nchi;

(viii) Sheria kutokuwa na utaratibu maalumu wa ununuzi kwa taasisi, mashirika na kampuni za umma zinazojiendesha na zisizojiendesha kibiashara;

(ix) Sheria kutojumuisha masuala ya ugavi na uondoshaji mali;

(x) Kutokuwepo kwa sehemu mahususi katika sheria inayohusu masuala ya usimamizi wa mikataba ya ununuzi na ugavi;

(xi) Kutokuwepo na sharti la bei kikomo katika ununuzi wa umma.

(xii) Muda mrefu katika utekelezaji wa michakato ya ununuzi.

Mheshimiwa Spika, sehemu mpya na ibara zinazofanyiwa marekebisho ya kiuandishi; sehemu mpya, muswada huu umeanzisha sehemu mpya mbili zinazohusu Usimamizi wa Mikataba pamoja na Usimamizi wa Ugavi ambazo ni sehemu ya saba na sehemu ya nane. Lengo la uanzishwaji wa sehemu hizi ni kuweka usimamizi mzuri wa mikataba pamoja na kujumuisha masuala ya Ugavi ikiwemo upokeaji wa bidhaa, vifaa au mali zilizonunuliwa. Uwekaji kumbukumbu, utunzaji na usambazaji. Sehemu hizi mpya zimeainisha taratibu za usimamizi wa mikataba na miongozo ya ugavi inayopaswa kuzingatiwa na taasisi nunuzi.

Mheshimiwa Spika, ibara zilizofanyiwa marekebisho ya kiuandishi; muswada huu umefanya marekebisho ya kiuandishi kwa takribani Ibara 29 kwa madhumuni ya kuleta maana iliyokusudiwa, kuondoa tafsiri sisisi na kuondoa mkanganyiko wakati wa utekelezaji wa Sheria hii.

Mheshimiwa Spika, marekebisho yaliyofanyika; marekebisho yaliyofanyika kupitia muswada huu yana lengo la kuondoa kasoro zilizojitokeza wakati wa utekelezji wa sheria hii kama zilivyoainishwa awali. Marekebisho yaliyopendekezwa kupitia ibara mbalimbali ili kuondoa kasoro hizo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 32 - viwango vya ukomo wa uidhinishaji wa Bodi ya Zabuni; muswada unapendekeza kuongeza vifungu vipya vidogo kwa lengo la kutenganisha mamlaka ya uidhinishaji wa ununuzi kati ya Bodi ya Zabuni na Afisa Masuuli kwa kuzingatia ukomo wa uidhinishaji. Lengo la marekebisho haya ni kupunguza muda wa mchakato wa manunuzi na gharama. Taratibu za ununuzi zinazohitaji idhini ya Bodi ya Zabuni na zinazohitaji idhini ya Afisa Masuuli zitaainishwa katika kanuni.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 38 - majukumu na Mamlaka ya Afisa Masuuli; Ibara hii inarekebishwa ili kumpa Afisa Masuuli mamlaka ya kuidhinisha masuala ya ununuzi, ugavi na uondoshaji mali kwa kuzingatia ukomo wa uidhinishaji. Lengo ni kuongeza uwajibikaji kwa Afisa Masuuli, kupunguza muda, gharama, na kuongeza ufanisi katika ununuzi wa umma.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 49 - ununuzi katika taasisi zinazojiendesha kibiashara; madhumuni ya kuongeza ibara hii mpya ni kuweka mazingira ya kutunga kanuni zinazohusu taratibu maalumu za ununuzi kwa mashirika na taasisi za umma zinazojiendesha kibiashara. Masharti ya ununuzi yaliyopo kwenye sheria hivi sasa hayatofautishi utaratibu wa ununuzi kati ya mashirika na taasisi zinazojiendesha na zisizojiendesha kibiashara.

Mheshimiwa Spika, kukosekana kwa utofauti huo kumesababisha mashirika yanayojiendesha kibiashara kuchukua muda mrefu katika kufanya manunuzi na hivyo kutokuwa shindani. Ibara hii inalenga kurahisisha utekelezaji wa ununuzi katika taasisi za umma na mashirika yanayojiendesha kibiashara ili kuleta ufanisi. Utaratibu utakaofuatwa na Taasisi hizi utaainishwa katika Kanuni za ununuzi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 71- kuondoa masharti ya mzabuni aliyefungiwa nje kupewa adhabu mara mbili; ibara hii imeondoa masharti ya mzabuni kuongezewa muda wa ziada kama adhabu zaidi ya ule aliofungiwa nje ya nchi. Sheria ilivyo hivi sasa mzabuni aliyefungiwa nje ya nchi huongezewa adhabu ya ziada nchini kwa kufungiwa kwa kipindi cha miaka 10 kwa

makosa ya udanganyifu au rushwa, au miaka 5 kwa makosa mengine.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 72 - ununuzi kwa njia ya kielektroniki; ibara hii inarekebishwa ili kuondoa mwanya kwa taasisi nunuzi kufanya ununuzi nje ya mfumo wa kielektroniki. Matumizi ya mfumo wa kielektroniki hivi sasa ni takriban asilimia 17.5 tu na asilimia 82.5 ya manunuzi hufanyika nje ya mfumo. Muswada unapendekeza kuondoa sharti linalotoa mwanya kwa taasisi nunuzi kufanya ununuzi nje ya mfumo wa kielektroniki. Maboresho haya yatazitaka taasisi nunuzi zote kufanya ununuzi ndani ya mfumo wa kielektroni, ili kuimarisha dhana ya uwazi, ushindani na ufanisi katika ununuzi na ugavi. Endapo mfumo haufanyi kazi, mamlaka itatoa notisi ya mwongozo kwa watumiaji wa mfumo na kwa umma.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 73 - bei kikomo; ibara hii inakusudia kuweka bei kikomo katika bidhaa, kazi za ujenzi na huduma ili kutatua changamoto ya bidhaa moja katika eneo moja kununuliwa kwa bei tofauti na taasisi za umma mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, muswada unapendekeza kuweka masharti kwa taasisi nunuzi kununua bidhaa, huduma na kazi za ujenzi kwa kuzingatia bei kikomo ambazo zitaandaliwa kwa kuzingatia bei ya soko. Lengo ni kupunguza gharama kwa kutatua changamoto ya bei kubwa zinazotokana na ununuzi ambao hauzingatii bei halisi ya soko. Hata hivyo, mtumishi wa umma atakayehusika na ununuzi wa bidhaa, huduma kazi za ujenzi kwa bei ya juu kuliko bei kikomo, atachukuliwa hatua za kinidhamu.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 75 - matumizi ya rasilimali za ndani; Sheria ya Ununuzi wa Umma inayofutwa ilikuwa imeruhusu matumizi ya rasilimali za ndani katika kutekeleza miradi ya ujenzi. Hata hivyo, utekelezaji wake umekuwa si wa kuridhisha kutokana na changamoto mbalimbali. Changamoto hizo ni kukosekana kwa wataalam wenye sifa katika taasisi nunuzi wa kusimamia miradi, usimamizi usioridhisha wa malighafi kwa ajili ya utekelezaji wa miradi, uandaaji wa gharama na makisio ya miradi yasiyo na

uhalisia, kukosekana kwa taarifa za utekelezaji wa miradi na udhibiti hafifu wa ubora wa miradi inayotekelezwa.

Mheshimiwa Spika, muswada unapendekeza kutatua changamoto hizo kwa kuweka masharti yafuatayo:-

(i) Kuzingatia ukomo wa thamani kwa miradi inayotumia njia hii ya ununuzi;

(ii) Kuwa na vifaa na wataalamu wenye weledi kwa ajili ya kusimamia miradi;

(iii) Uwepo wa uandaaji wa taarifa ya ukaguzi wa kazi zilizofanyika na;

(iv) Uwepo wa ushindani katika upatikanaji wa bidhaa na mafundi.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 92 hadi 97 - usimamizi wa mikataba; Serikali inakusudia kuanzisha ibara mpya mahususi kwa ajili ya usimamizi na utekelezaji wa mikataba ya ununuzi. Ibara hii inabainisha majukumu ya Afisa Masuuli na idara tumizi katika usimamizi wa mikataba na udhibiti wa gharama, thamani ya fedha, ubora na muda katika mikataba ya ununuzi. Mapendekezo haya yametokana na kuwa awali jukumu la usimamizi wa mikataba lilikuwa halifanyiki na hivyo kukosa wa kumuwajibisha pindi utekelezaji wa mkataba unapokuwa na changamoto.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 98 hadi 103 - usimamizi wa ugavi; muswada unapendekeza kuongeza sehemu mpya ya nane kuhusu usimamizi wa ugavi na uondoshaji mali. Ugavi ni miongoni mwa maeneo muhimu katika mnyororo wa usimamizi wa ununuzi unaopaswa kusimamiwa. Aidha, katika Sheria inayofutwa masuala ya ugavi yalikuwa hajajumuishwa na hivyo kusababisha kuwepo na usimamizi hafifu katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, marekebisho haya yanaenda kuongeza ufanisi katika matumizi ya fedha za umma kwa kuhakikisha kuwa

wakati wote Taasisi ya Umma ina hesabu halisi ya vifaa na mali zake ili kuzuia upotevu na uharibifu.

Mheshimiwa Spika, Kupunguza Muda wa Mchakato. Sheria inayopendekezwa imeweka masharti yatakayopunguza muda wa hatua za utekelezaji wa ununuzi wa Umma. Mfano:-

(i) Sheria hii imepunguza muda wa kutangaza nia ya kutoa tuzo kutoka siku thelathini hadi siku kumi na nne kama ilivyofanyiwa marekebisho kwenye ibara ya 68 (15);

(ii) Imeondoa hitaji la muda wa kusubiri malalamiko kutoka kwa wazabuni kwa ununuzi wa bidhaa mtambuka kutoka siku saba za kazi hadi siku siku tano kama ilivyofanyiwa marekebisho kwenye Ibara ya 68(4) pamoja na;

(iii) Imepunguza muda wa kushughulikia malalamiko ya zabuni kutoka siku saba hadi siku tano kama ilivyofanyiwa marekebisho kwenye Ibara ya 119(6).

Mheshimiwa Spika, Maeneo ya Muswada Yanayofanyiwa Marekebisho na Kamati. Kamati baada ya kuchambua Muswada huo na kupokea maoni ya wadau ilibaini maeneo ya ziada ambayo yalihitaji marekebisho ili kuleta tija iliyokusudiwa. Maeneo hayo ni kama yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 2 - matumizi; Serikali imeongeza kifungu kipya kidogo cha 5 katika ibara hii ili kuakisi marekebisho yaliyofanyika kwenye kifungu cha 2 cha marekebisho ya mwaka 2023 ya Sheria ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, Sura 103. Aidha, Kamati iliona umuhimu wa kifungu hiki kuboreshwa ili kuleta maana iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 3 – tafsiri; katika ibara hii Kamati iliishauri Serikali kutoa tafsiri ya maneno mbalimbali kama yalivyotumika kwenye Muswada kwa sababu zifuatazo:-

(i) Kutafsiri makosa kama yanavyotumika kwenye sheria mama;

(ii) Kufuta maneno na kuandika upya ili yalete maana iliyokusudiwa;

(iii) Kutafsiri maneno yaliyotumika ndani ya muswada bila kutafsiriwa;

(iv) Kufuta maneno yaliyokuwa na maana sawa.

Mheshimiwa Spika, marekebisho hayo ni kama yanavyoonekana kwenye Jedwali la marekebisho ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 6 na 7 – Kamishna wa Sera ya Ununuzi wa Umma; ibara hizi zilivyokuwa katika sheria inayofutwa zilikuwa zinatambua uwepo wa Idara ya Sera ya Ununuzi wa Umma pamoja na kubainisha majukumu ya Idara hiyo. Aidha, Kamati ilibaini majukumu yaliyobainishwa kwenye ibara ndogo ya 7(2) yanashabihiana na Majukumu ya Mamlaka ya Ununuzi wa Umma *(PPRA)* na Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi *(PSPTB)*.

Mheshimiwa Spika, vilevile Kamati iliona umuhimu wa ibara hii kuitambua Wizara ya Fedha badala ya idara kwa sababu idara hiyo ilivyo hivi sasa haijisemei yenyewe bali iko ndani ya muundo wa Wizara. Baada ya majadiliano ilikubalika ibara hizi kumtambua Kamishna wa Sera ya Ununuzi wa Umma na kufuta Ibara 7(2) na majukumu ya msingi ya Kamishna yahamishiwe katika Ibara ya 7(1) ili yasilete mgongano wa majukumu. Marekebisho hayo ni kama yanavyoonekana kwenye Jedwali la marekebisho ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 9 – malengo ya mamlaka; kati ya masuala ya msingi yaliyozingatiwa katika Muswada huu ni pamoja na wazabuni wa ndani kupewa kipaumbele katika zabuni za Serikali. Sheria inayofutwa ilikuwa inatoa fursa ya upendeleo kwa wazabuni wa ndani, hata hivyo, upendeleo huo haukuwa na taasisi inayofuatilia utekelezaji wake. Hivyo, kupitia Muswada huu Serikali imeongeza lengo la mamlaka kuhakikisha

kuwa taasisi nunuzi inazingatia utoaji wa kipaumbele kwa wazabuni na watoa huduma wa ndani katika zabuni za bidhaa, kazi za ujenzi na huduma. Marekebisho hayo ni kama yanavyoonekana katika jedwali la marekebisho ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 10 – Majukumu ya *PPRA;* aya (o) ya Ibara hii inaiwezesha *PPRA* kupata taarifa za bei kwa bidhaa na huduma mtambuka pekee kutoka kwa taasisi za umma zinazohusika na uandaaji wa bei hizo. Hata hivyo, kifungu hiki hakiruhusu Mamlaka kupata bei ya bidhaa za kazi za ujenzi na huduma ambayo siyo bidhaa na huduma mtambuka.

Mheshimiwa Spika, baada ya majadiliano baina ya Kamati na Serikali, Kamati ilipendekeza kuboresha kifungu hiki ili kuruhusu mamlaka kupata taarifa ya bei ya bidhaa, kazi za ujenzi na huduma zinazowekewa viwango kutoka kwa taasisi za umma husika kwa lengo la kuhakikisha kuwa bei zinaendana na bei za soko kwa wakati huo. Hatua hii itaiwezesha *PPRA* kupata taarifa za bei kwa bidhaa, kazi za ujenzi na huduma zinazowekewa viwango kutoka kwa taasisi za umma zinazohusika kuandaa bei hizo. Marekebisho hayo ni kama yanavyoonekana katika jedwali la marekebisho ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, aya mpya ya (p) imeanzisha utaratibu mpya wa kuwepo kwa bei kikomo. Lengo la utaratibu huu ni kuhakikisha kwamba bidhaa na huduma zinazonunuliwa na Serikali hazizidi bei ya soko. Kutokuwepo kwa bei kikomo katika sheria iliyopo hivi sasa kunasababisha bidhaa nyingi kununuliwa kwa bei ya juu ukilinganisha na bei ya soko kwa wakati huo.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko haya yanaenda kuipa jukumu Mamlaka ya Usimamizi wa Ununuzi wa Umma kuandaa bei kikomo kwa baadhi ya bidhaa, kazi za ujenzi na huduma ambazo zitazingatiwa wakati wa ununuzi. Hatua hii itasadia kuhakikisha kuwa ununuzi wa umma unaakisi bei ya soko kwa wakati huo na kuleta usawa na uwazi. Marekebisho hayo ni kama yanvyonekana katika jedwali la marekebisho ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 11 – wigo wa uchunguzi unaofanywa na mamlaka; ibara hii inampa mamlaka *PPRA*

kufanya uchunguzi katika masuala mbalimbali. Hata hivyo, *PPRA* haikuwa na jukumu kisheria la kufanya uchunguzi wa maombi ya uhalalisho wa ununuzi uliokwishafanyika kwa njia ya dharura kama ilivyoainishwa katika Ibara ya 76 ya Muswada huu. Aidha, ibara hii haikuwa imetoa fursa kwa Afisa Masuuli kuomba mamlaka kufanya uchunguzi au ukaguzi maalumu kuhusu suala lolote katika ununuzi au uondoshaji mali.

Mheshimiwa Spika, hivyo, marekebisho yanayopendekezwa yanaenda kumpa *PPRA* mamlaka ya kufanya uchunguzi wa maombi hayo na kushughulikia maombi ya Afisa Masuuli. Lengo la marekebisho hayo ni kuhakikisha kuwa masuala ya ununuzi na uondoshaji mali yanafuata taratibu zilizoainishwa katika sheria inayopendekezwa pamoja na kanuni zake zitakazotungwa. Marekebisho hayo ni kama yanavyoonekana katika jedwali la marekebisho ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 15 – Utaratibu wa Uchunguzi. Serikali inafuta na kuandika upya ibara hii kama inavyoonekana kwenye Muswada ili ilete maana iliyokusudiwa kama ilivyokuwa kwenye sheria inayofutwa. Marekebisho hayo ni kama yanvyonekana katika Jedwali la Marekebisho ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 20 – Usitishaji wa Michakato ya Ununuzi. Ibara hii ina lengo la kusitisha mchakato wote wa manunuzi pale inapobainika uwepo wa ukiukwaji wa sheria, kanuni na miongozo. Hata hivyo, baada ya majadiliano na Serikali, Kamati ilipendekeza kuongeza kifungu kidogo cha 2 ili kuondoa sharti la kusimamisha zabuni yote kwa bidhaa za afya endapo kuna bidhaa chache katika loti hazikukidhi vigezo.

Mheshimiwa Spika, kifungu hicho kitaweza kuendelea na manunuzi ya bidhaa za afya ambazo katika loti moja zitakuwa zimekidhi vigezo ili kupunguza muda wa manunuzi. Pendekezo hili linaakisi ukweli kwamba ununuzi wa dawa uhusisha dawa zaidi ya moja kwenye zabuni moja. Marekebisho hayo ni kama yanavyoonekana katika jedwali la marekebisho ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, vilevile katika ibara hii kifungu kidogo cha 1, Kamati ilipendekeza kiandikwe upya ili kuleta maana

iliyokusudiwa na kwa Kiswahili fasaha ili kuepusha tafsiri sisisi. Serikali ilizingatia mapendekezo ya Kamati kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 21 – hatua baada ya mapendekezo ya mamlaka; mapendekezo ya Serikali katika ibara hii hayakubainisha hatua atakazochukuliwa Mjumbe wa Bodi ya Zabuni endapo atajihusisha na vitendo vilivyo kinyume na sheria hii. Hivyo, Kamati ilipendekeza Mjumbe wa Bodi ya Zabuni kujumuishwa kati ya watu watakaochukuliwa hatua endapo watavunja sheria kwa kuwa ni mdau mkubwa kwenye maamuzi yote ya ununuzi yanayofanyika kupitia Bodi ya Zabuni. Hatua hii inaenda kudhibiti Wajumbe wa Bodi kutumia vibaya nafasi zao katika mchakato wa manunuzi. Marekebisho ya ibara hii ni kama yanavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 30 – taarifa ya mwaka ya tathmini ya utendaji kazi wa ununuzi wa umma na thamani halisi ya fedha; Kamati iliboresha ibara hii ili kuiwezesha taarifa ya mwaka inayoandaliwa na mamlaka kujumuisha shughuli za ugavi na uondoshaji mali. Lengo ni kuifanya Taarifa ya Mwaka itakayowasilishwa iweze kujihusisha na masuala ya ugavi. Serikali ilipokea mapendekezo hayo na marekebisho ni kama yanavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, pia katika Ibara ndogo ya 2, Kamati ilipendekeza kufuta takwa la taarifa hiyo kuwasilishwa Bungeni kwa sababu taarifa hiyo ni sehemu ya Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya kila mwaka inayowasilishwa Bungeni. Vilevile kwa kuwa taarifa hiyo ni ya kiutendaji, Kamati iliona hamna umuhimu wa kuwasilishwa Bungeni badala yake iishie katika ngazi ya Waziri mwenye dhamana ya ununuzi kwa ajili ya kufanyiwa kazi ili kurekebisha mapungufu yaliyobainishwa na mamlaka katika taarifa yake. Maboresho ya ibara hii ni kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 32 – Bodi za Zabuni; mapendekezo ya Serikali katika ibara hii hayakuzingatia umuhimu wa Kamati za Fedha na Uongozi katika masuala ya ununuzi, ugavi

na uondoshaji mali katika ngazi ya Serikali za Mitaa. Hivyo, Kamati ilipendekeza ibara hii iboreshwe na kurejesha utaratibu uliokuwepo awali kwa kuzingatia umuhimu wa kamati hizo. Maboresho ya ibara hii ni kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 38 – majukumu na mamlaka ya Afisa Masuuli; ibara ya 38(2) ilikuwa inamruhusu Afisa Masuuli kuomba ushauri wa kitaalamu au kiufundi kutoka nje ya nchi. Kamati inaona umuhimu wa Afisa Masuuli kuomba ushauri kwa taasisi ya umma ili kuepusha gharama zitakazotokana na kumtafuta mshauri binafsi pamoja na kuokoa muda. Vilevile, Afisa Masuuli ashauriane na Bodi ya Zabuni kabla ya kuomba mtu wa kutoa ushauri elekezi nje ya nchi. Serikali imezingatia marekebisho hayo kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, ibara hii pia inarejesha jukumu la Afisa Masuuli kuanzisha Bodi ya Zabuni na kuteua wajumbe wake kama ilivyokuwa katika Sheria inayopendekezwa kufutwa. Muswada unaopendekezwa ulikuwa umesahau kujumuisha jukumu hili kati ya majukumu mengine ya Afisa Masuuli. Marekebisho hayo ni kama yanavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 40 – majukumu ya Kitengo cha Usimamizi wa Ununuzi; ibara hii inarejesha jukumu la Kitengo cha Usimamizi wa Ununuzi la kuandaa taarifa za utendaji kazi wa kitengo kwa ajili ya bodi za zabuni kama ilivyokuwa katika sheria inayopendekezwa kufutwa. Muswada unaopendekezwa ulikuwa umesahau kujumuisha jukumu hili kati ya majukumu mengine ya kitengo. Marekebisho hayo ni kama yanavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 49 – ununuzi katika Taasisi zinazojiendesha kibiashara; ibara hii ni mpya katika Sheria ya Ununuzi inayopendekezwa, yenye lengo la kutofautisha masharti ya ununuzi kwa taasisi za umma zinazojiendesha kibiashara na zile zisizojiendesha kibiashara. Aidha, ibara hii ilikuwa haitambui sheria zinazoanzisha taasisi, kampuni na mashirika yanayojiendesha kibiashara. Hivyo Kamati ilipendekeza kuandikwa upya ili

kuzitambua sheria husika ili kuharakisha mchakato wa ununuzi kwa taasisi zinazojiendesha kibiashara. Marekebisho hayo ni kama yanavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 50(3) – wajibu wa Taasisi Nunuzi. Ibara hii inamtaka Mkaguzi wa Nje katika taarifa yake kuonyesha endapo ununuzi wa bidhaa, kazi za ujenzi au huduma umefanyika kwa kuzingatia Sheria ya Ununuzi wa Umma. Hata hivyo, jukumu hilo limeainishwa wazi katika Kifungu cha 26 cha Sheria ya Ukaguzi, Sura 418. Hivyo, Kamati ilipendekeza kufutwa kwa kifungu hiki ili kuepusha jukumu moja kutamkwa katika sheria mbili tofauti. Serikali iliridhia mapendekezo ya Kamati na marekebisho ni kama yanavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 60 iwe upendeleo kwa bidhaa za ndani. Ibara hii imefanyiwa marekebisho na Serikali ili kuweka masharti kwa taasisi nunuzi ili kutoa kipaumbele kwa bidhaa zinazotengenezwa, kuzalishwa au kuchimbwa nchini kabla ya kununua bidhaa hizo kutoka nje ya nchi. Aidha sharti hilo linazitaka taasisi nunuzi kubainisha takwa hili katika nyaraka za zabuni. Lengo la marekebisho haya ni kuendeleza watoa huduma pamoja na viwanda vya ndani katika matumizi ya rasilimali za ndani zilizopo nchini. Marekebisho hayo ni kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 61 inahusu kujenga uwezo kwa kampuni za ndani. Ibara hii haikubainisha ni mikataba ipi iliyokuwa inakusudiwa na vyombo vilivyokuwa vinarejewa ambavyo vinapaswa kushauriana na taasisi nunuzi katika kuitenga mikataba hiyo. Changamoto ambayo iliweza kujitokeza wakati wa utekelezaji wa sheria hii ni aina ya mikataba na vyombo vipi vinatakiwa kurejewa ili kujenga uwezo wa kampuni za ndani.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipendekeza kuboreshwa kwa Ibara hii ili kuondoa changamoto zinazoweza kujitokeza wakati wa utekelezaji wa masharti ya Ibara hii. Baada ya majadiliano na Serikali kukubaliana na mapendekezo ya Kamati ikafuta na kuandika upya Ibara Ndogo ya Kwanza na ya Pili ili kuleta maana

iliyokusudiwa. Marekebisho ni kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Ibara mpya ya 62 inahusu uingiaji wa ushirika au mikataba midogo na kampuni za ndani. Baada ya kufanya maboresho katika Ibara ya 61 iliyopo hivi sasa, Serikali imeongeza Ibara mpya ya 62 ili kuakisi maudhui ya Ibara ya 61. Ibara hii inaweka masharti kwa mzabuni wa kigeni aliyepewa tuzo ya mkataba kuingia ushirika kwa mikataba midogo na kampuni za ndani. Aidha, Ibara hiyo inaweka sharti kwa mzabuni wa kigeni aliyepata tuzo ya mkataba kubainisha ni asilimia ngapi ya mikataba midogo atashirikisha kampuni za ndani. Kifungu hiki kina lengo la kuziwezesha kampuni za ndani kushiriki katika zabuni ili kupata ujuzi pamoja na kubakiza fedha nchini, kuliko hivi sasa ambapo kampuni za kigeni zilizoshinda zabuni hazikulazimika kisheria kushirikisha kampuni za ndani. Marekebisho hayo ni kama yanavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 67 inahusu kukataliwa kwa wazabuni. Katika aya (d) ya Ibara hii Kifungu kilikuwa hakiruhusu taasisi nunuzi kukataa zabuni ambayo inahusisha gharama kubwa kuliko bei ya soko. Hivyo, Kamati ilipendekeza kuongeza neno bei ya soko katika aya hiyo ili kuleta maana iliyokusudiwa. Marekebisho hayo ni kama inayoonekana katika Jedwali la Marekebisho ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 71 inahusu kufungiwa kwa mzabuni. Katika ibara hii Kamati inapendekeza Kifungu hiki kuweka bayana muda wa kukata rufaa kwa mzabuni ambaye hajaridhishwa na uamuzi wa mamlaka. Lengo la mapendekezo ya Kamati ni kuleta usawa, kwa kuwa Muswada umeainisha muda wa kukata rufaa kwa afisa masuuli au muda wa sfisa masuuli kutoa uamuzi kwa walengwa wa mgogoro kwa mchakato wa ununuzi, ugavi, uondoshwaji mali na kinga za mikataba katika Ibara 119. Serikali ilizingatia pendekezo hilo na kupitia Jedwali la Marekebisho imependekeza siku 21 kuanzia siku mzabuni alipofahamu kuwepo kwa uamuzi huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 72 (1) inahusu ununuzi kwa njia ya Kielekroniki. Ibara hii haikuweka sharti la lazima la matumizi ya

mfumo wa kielektroniki katika ununuzi, ugavi na uondoshaji mali kwa taasisi nunuzi. Kamati iliona endapo Kifungu hiki kingebaki kama kilivyo kingeweza kutumika vibaya. Hivyo, Kamati ilipendekeza Kifungu hicho kuweka sharti la lazima kwa taasisi nunuzi kutumia mfumo kufanya shughuli za ununuzi, ugavi na uondoshaji mali kwa njia ya zabuni na kutoa taarifa kupitia mfumo huo.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kwamba, hivi sasa ni asilimia 17.5 tu ya manunuzi yote ya umma yanafanyika kwa njia ya kielektroniki. Kamati inaamini kwamba, hatua hii itaenda kuchochea matumizi ya mfumo na hivyo kupata thamani halisi ya fedha na kuongeza ufanisi, uwazi na usawa. Marekebisho hayo ni kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 76 inahusu ununuzi wa dharura. Mazingira yaliyowekwa kwenye Kifungu cha Kwanza aya (a) na (b) hayakuzingatia upekee wa ununuzi wa bidhaa za afya. Hivyo, Kamati ilipendekeza kwa Serikali kuanzisha aya mpya (c) ili kujumuisha ununuzi wa bidhaa za afya kwa upekee wake ili kuondoa changamoto inayojitokeza hivi sasa katika kuhalalisha ununuzi wa dawa kwa njia ya dharura. Serikali ilikubali mapendekezo ya Kamati na marekebisho ni kama yanavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 79 inahusu ununuzi wa vichwa vya mabehewa ya treni, ndege na meli zilizotumika. Katika Ibara hii Kamati ilipendekeza kuongeza Kifungu Kidogo cha Sita, kitakachoainisha sharti la kuweka sifa na vigezo vitakavyozingatiwa wakati wa ununuzi wa vichwa na mabehewa ya treni, ndege na meli zilizotumika kuainishwa katika kanuni. Lengo la hatua hii ni kuhakikisha kwamba vifaa vinavyonunuliwa vina ubora na viwango na vitatumika kwa muda mrefu. Marekebisho ni kama yanavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 81 inahusu ununuzi wa bidhaa za afya zinazookoa uhai; katika Ibara hii Kamati ilibaini kuwa utaratibu wa ununuzi wa bidhaa za afya zinazookoa uhai uliokuwa unapendekezwa ulikuwa unabagua bidhaa za afya

katika makundi mawili. Bidhaa zinazookoa uhai na bidhaa zisizookoa uhai. Vile vile, Ibara hii haikuweka wazi utaratibu wa ununuzi wa kawaida kwa dawa na vifaatiba.

Mheshimiwa Spika, baada ya Kamati kushauriana na Serikali, Serikali ilifuta na kuandika upya kwa kuongeza majukumu ya Bohari ya Dawa, pamoja na Wizara yenye dhamana na masuala ya afya katika kuandaa na kuidhinisha viwango vya bidhaa za afya kulingana na hadhi ya vituo vya kutolea huduma pamoja na jedwali la mahitaji na vigezo msawazo kwa kuzingatia viwango vya bidhaa.

Mheshimiwa Spika, Ibara ndogo zinazoongezwa zinaweka sharti kwa vituo vya kutolewa huduma za afya na Bohari ya Dawa kuzingatia vigezo vilivyowekwa chini ya sheria iliyopendekezwa. Lengo ni kuhakikisha kwamba kunakuwa na vigezo msawazo kulingana na hadhi ya maeneo ya kutolea huduma za afya. Pia Serikali ilibadilisha maneno ya pembeni *(marginal notes*) na sasa kusomeka Ununuzi wa bidhaa za afya. Marekebisho ni kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 90(3) inahusu majadiliano na Utoaji wa Tuzo ya Mikataba. Ibara hii jinsi ilivyokuwa imeandikwa ilikuwa imempa mamlaka Afisa Masuuli kusitisha majadiliano kwa zabuni zote bila kuzingatia ukomo wa uidhinishaji. Hivyo, Ibara hii imerekebishwa ili kuzingatia ukomo wa uidhinishaji, ambao kwa zabuni zilizoidhinishwa na Afisa Masuuli zitasitishwa na Afisa Masuuli. Aidha kwa zabuni zilizoidhinishwa na Bodi ya Zabuni Afisa Masuuli atasitisha zabuni hizo baada ya kushauriana na bodi na kuendelea na hatua inayofuata. Marekebisho hayo ni kama yanavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 94(1) inahusu mabadiliko na marekebisho. Katika Ibara hii Kamati ilipendekeza kuwa, mkataba baada ya kusainiwa unaweza kubadilishwa au kurekebishwa lakini mabadiliko hayo yasizidi asilimia 15 ya jumla ya bei ya mkataba wa awali badala ya asilimia 30 iliyokuwa imependekezwa. Vile vile Kamati ilipendekeza kuongeza aya ya pili katika Ibara ya 94, itakayoweka sharti la lazima kwa mkataba unaopendekezwa kuongezewa muda na Afisa Masuuli, kurejewa

na kufanyiwa upekuzi na Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Marekebisho ni Kama yanayoonekana katika Jedwali la Marekebisho ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 103 inahusu miongozo ya usimamizi wa bidhaa, vifaa na mali. Mapendekezo ya awali ya Ibara yaliyokuwa yanaonesha jukumu la usimamizi wa bidhaa, vifaa au mali halina sheria inayosimamia; kimsingi jukumu hili linasimamiwa na Sheria ya Fedha za Umma, na hivyo, marekebisho haya yamerejea masharti yaliyopo katika sheria inayohusika. Marekebisho ni kama yanayoonekana katika Jedwali la Marekebisho ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 119 inahusu utatuzi wa malalaliko au migogoro kwa Afisa Masuuli. Ibara hii inaweka utatuzi wa malalamiko au migogoro kwa Afisa Masuuli. Utaratibu uliokuwa unapendekezwa na Serikali ulibainisha siku tano. Vile vile Ibara hii inampa Afisa Masuuli mamlaka ya kuunda jopo kwa ajili ya kufanya uchunguzi. Kamati ilibaini endapo Afisa Masuuli atatakiwa kuunda jopo, atalazimika kutoa uamuzi ndani ya siku tano. Hivyo, ilipendekeza pale ambapo jopo linaundwa, maamuzi yatolewe ndani ya siku saba. Serikali ilipokea mapendekezo hayo, kama yanavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, marekebisho haya pia yanamtaka Afisa Masuuli, endapo ataunda jopo huru kuwataarifu wazabuni ndani ya siku moja baada ya kupokea malalamiko au mgogoro. Marekebisho hayo ni kama yanavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 123 inahusu kusitishwa kwa mchakato wa ununuzi. Ibara hii inaweka masharti ya kusitishwa mchakato wa ununuzi. Kamati imebaini kuwa masharti yanayowekwa katika Ibara hii yalikuwa hayatoi fursa kwa zabuni za bidhaa za afya, kusitishwa kwa baadhi ya bidhaa na si zabuni nzima. Aidha, Serikali imeongeza Ibara Ndogo ya Tatu ili kumpa Afisa Masuuli idhini ya kuomba kwa mamlaka kutokusitisha kwa mchakato wa ununuzi wa bidhaa za afya endapo malalamiko au mgogoro upo kwa Afisa Masuuli. Marekebisho hayo ni kama yanayoonekana katika Jedwali la Marekebisho ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, vilevile katika Ibara hii Kamati ilipendekeza kwamba, usitishwaji wa mchakato wa manunuzi kwa bidhaa za afya uzingatie loti au baadhi ya bidhaa za afya zilizopo katika zabuni moja ambazo hazikiukidhi vigezo na hivyo kuruhusu loti au baadhi ya bidhaa za afya zilizokidhi vigezo kuendelea na mchakato wa ununuzi. Serikali ilikubali mapendekezo ya Kamati na marekebisho ni kama yanavyoonekama katika Jedwali la Marekebisho ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 127(2) inahusu makosa. Katika Ibara hii Kamati ilikuwa na mapendekezo yafuatayo, ambayo Serikali iliyapokea na kuyafanyia marekebisho kama yanavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho ya Serikali. Kwa ajili ya kuongeza aya mpya ili kubainisha bayana kwa kuwa, itakuwa ni kosa kwa mtu yeyote atakaposhindwa kufanya shughuli za ununuzi, ugavi na uondoshwaji mali kwa kutumia mfumo wa kielektroniki wa ununuzi wa Umma. Hatua hii itasaidia kuleta uwajibikaji na matumizi sahihi ya mfumo.

Mheshimiwa Spika, pili, kuongeza aya mpya ili kuainisha bayana kuwa, ni kosa kwa mtu yeyote pamoja na Mjumbe wa Bodi, atakayekiuka masharti yanayohusiana na upendeleo wa ndani wa kitaifa bila sababu za msingi. Lengo ni kuhakikisha kuwa mtu wa Tanzania anashiriki kikamilifu katika zabuni za Serikali. Mapendekezo haya yanalenga kutambua makosa ya kutotumia mfumo na kutotoa upendeleo kwa kampuni za ndani, chini ya sheria hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mabadiliko ya jina refu la sheria. Pamoja na marekebisho mengine yaliyofanyika kupitia Muswada huu, Serikali imependekeza kubadili jina refu la sheria ili kujumuisha masuala ya ugavi na hivyo kusomeka Sheria ya Ununuzi wa Umma na Ugavi.

Mheshimiwa Spika, maoni na mapendekezo ya jumla; kutokuwa na Sera na Mkakati wa ununuzi na ugavi. Kamati ilibaini kwamba, pamoja na uwepo wa Sheria ya Ununuzi wa Umma tangu mwaka 2001 mpaka hivi sasa Taifa halina sera wala mkakati wa ununuzi wa umma ambavyo ni nyenzo muhimu katika kuhakikisha upatikanaji wa thamani halisi ya fedha. Uwepo wa

sera na mkakati wa ununuzi wa umma,utasaidia katika maeneo yafuatayo: -

1. Namna ya kupunguza gharama katika ununuzi wa Umma na ugavi.

2. Namna ya kushughulikia vihatarishi katika ununuzi na ugavi.

3. Kuwekamasharti ya ununuzi usioathiri mazingira.

4. Usimamizi wa ubora na

5. Usimamizi na upatikanaji wa watoa huduma.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri maboresho haya yanayofanyika katika Sekta ya Ununuzi, Ugavi na Uondoshaji Mali, kwenda sambamba na uandaaji wa sera na mkakati wa ununuzi na ugani. Hivyo, Kamati inaitaka Serikali kuanza mara moja mchakato wa uandaaji wa Mkakati wa Ununuzi na Ugavi.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa mfumo mpya wa ununuzi wa *NeST*; Kifungu cha 9 (1) aya (K) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura ya 410, kimeipa *(PPRA)* jukumu la kuanzisha, kutunza na kuhuisha mfumo wa nunuzi wa Umma wa kielektroniki. Kupitia Kifungu hiki, Serikali iliamua kujenga mfumo mpya ili kufikia malengo yafuatayo: -

1. Kupata ufumbuzi wa changamoto za Mfumo wa *TANePS*, ikiwa ni pamoja na kukidhi mahitaji ya Serikali.

2. Mfumo wenye uwezo wa kuongeza uwazi na uwajibikaji

3. Kuongeza uzingatiaji wa sheria, taratibu na miongozo ya ununuzi

4. Kupunguza mianya ya rushwa na kuleta thamani halisi ya fedha za umma.

5. Kuongeza wigo kwa watumiaji kwa makundi yote.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapenda kuipongeza Serikali kwa hatua hiyo muhimu. Hivyo Kamati inaishauri Serikali kukamilisha mfumo huu na kuutumia.

Mheshimiwa Spika, usimamizi wa mikataba na uandaaji wa mikataba msawazo. Pamoja na kwamba Muswada unapendekeza kuainisha sehemu mpya inayohusu usimamizi wa mikataba, bado kuna changamoto katika uandaaji wa mikataba msawazo. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuwepo na miongozo ya uandaaji wa mikataba msawazo, itakayotumika ili kuepusha gharama za ziada zinazoweza kujitokeza katika kufanya mabadiliko ya mikataba. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kwamba, taratibu za kisheria zinafuatwa wakati wa uvunjaji wa mikataba ya ununuzi ili kuiepusha Serikali kuingia hasara.

Mheshimiwa Spika, utungaji wa kanuni; Kamati inapendekeza, kabla ya kuanza kutumika sheria mpya, kanuni zitakazotungwa kupitia sheria hiyo ziwasilishwe kwenye Kamati. Lengo ni kuhakikisha kanuni hizo zimezingatia mapendekezo ya Kamati wakati wa majadiliano na Serikali. Vile vile, kuzichambua na kuona kama zinaakisi maboresho yaliyofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuwajengea uwezo wazabuni na wakandarasi wa ndani. Kamati inapendekeza wazabuni na wakandarasi wa ndani kujengewa uwezo kwa kuimarisha mifumo ya kifedha ili waweze kupata mitaji kwa ajili ya kutengeneza miradi nchini. Aidha, Serikali ihakikishe kwamba, wakandarasi na wazabuni wanakopesheka katika benki na uwekezaji kwa riba nafuu, pamoja na kuhakikisha kwamba malipo na madeni ya wakandarasi na wazabuni wa ndani yanapewa kipaumbele.

Mheshimwa Spika, mahitaji ya rasilimali watu na fedha kwa ajili ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Muswada huu unapendekeza katika maeneo mbalimbali, kuongeza majukumu kwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kufanya upekuzi wa mikataba ya ununuzi pamoja na marekebisho ya mikataba. Kamati imebaini kwamba, kwa mujibu wa Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Sura ya 268, Wanasheria wote wa Serikali wanawajibika kwa ofisi hii. Hivyo pindi inapotokea kuna ongezeko la majukumu yasiyoendana na

rasilimali zilizopo kwenye ofisi hii, basi wanasheria wengine wana waazima kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, ili ofisi hii itimize majukumu yake kikamilifu, lazima itengewe fedha za kutosha kwa ajili ya matumizi ya kawaida na mafunzo kwa ya watumishi wake. Ongezeko hili kibajeti litasaidia kuwaongezea uwezo wanasheria, ndani na nje ya nchi, pamoja na nyanja za uandaaji wa mikataba, usimamizi wake pamoja na mashauriano ya kitaifa na kimataifa. Vile vile, sheria hii ya utekelezaji wa majukumu ya ofisi hii utamruhusu Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuondoa ushauri wa kitaalamu kutoka kwa mtu au taasisi yoyote ya umma ya ndani ya nchi. Endapo utaalamu huo haupatikani nchini anaweza kuomba nje nchi.

Mheshimiwa Spika, hatua hii itaiepusha Serikali kwa hasara inayotokana na mikataba mibovu na usimamizi hafifu wa mikataba.

Mheshimiwa Spika, naomba kuhitimisha. Napenda kukushukuru kwa miongozo yako wakati wa utendaji kazi wa Kamati. Aidha napenda kumshukuru Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb) na Naibu Spika, kwa kuendelea kukusaidia wewe kuliongoza vyema Bunge lako Tukufu. Vile vile, namshukuru Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb) na Waziri wa Fedha, pamoja na Mheshimiwa Hamad Hassan Chande (Mb) na Naibu Waziri wa Fedha kwa ushirikiano wao waliotoa kwa Kamati wakati wote wa kuchambua Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Jaji Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi, Naibu Makatibu Wakuu wa Wizara ya Fedha, Ndg. Jenifa Omolo na Ndg. Elijah Mwandumbya, Kamishina wa Sera ya Ununuzi Dkt. Frederick Mwakibinga, Mtendaji Mkuu wa *PPRA* Ndg. Eliakim Maswi na watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati kwa kipindi chote cha kuchambua Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia inawashukuru wadau wote kwa maoni yao kuhusu Muswada huu. Naomba kuwapongeza

Wajumbe wa Kamati, wakiongozwa na Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua (Mb) na Makamu Mwenyekiti wa Kamati kwa umahiri na ushirikiano wao katika kuchambua Muswada huu na kuweza kuboresha hadi kufikia hatua hii. Naomba majina ya Wajumbe yaingie katika kumbukumbu Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee namshukuru pia Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa J. Mwihambi *ndc*, kwa kuiwezesha Kamati kuendelea na majukumu yake kikamilifu. Hali kadhalika napenda kushukuru Sekretarieti ya Kamati ya Bajeti ikiongozwa na Mkurugenzi wa Idara ya Bajeti, Ndg. Michael Kadebe akishirikiana na Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Emmanuel Rhobi, Makatibu wa Kamati Ndg. Lilian Masabala, Ndg. Wilfred Akas, Ndg. Jenifer Maurice na Ndg. Trifina Karaguza. Ndg. Ludovick Ringia, Mwanasheria wa Ofisi ya Bunge, kwa kuipatia Kamati ushauri wa kitaalamu na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MAONI YA KAMATI KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA UNUNUZI WA UMMA WA MWAKA 2023 *[THE PUBLIC PROCUREMENT (AMENDMENT) BILL, 2023]* – KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

**1.0. UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 99(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 naomba kutoa maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 5 ya Mwaka 2023 *(The Public Procurement (Amendment) Bill 2023)*. Muswada huu umebadilisha lugha ya Sheria ilivyo hivi sasa kutoka lugha ya Kiingereza kwenda lugha ya Kiswahili ili Sheria hiyo ieleweke kwa urahisi kwa watumiaji. Manunuzi ya Umma yanatumia kiasi kikubwa cha fedha za Serikali. Inakadiriwa kwamba takriban **asilimia 70** ya Bajeti yote ya Serikali hutumika kwenye ununuzi wa Umma na hivyo inapaswa kusimamiwa kikamilifu.

**1.1. Jinsi Kamati ilivyoshughulikia Muswada Mheshimiwa Spika,** Kamati ilianza uchambuzi wa Muswada huu kwa kukutana na Serikali ili kupitia kifungu vya Sheria ya Ununuzi wa Umma Sura 410 vinavyofanyiwa marekebisho katika Muswada pamoja na maudhui yake. Aidha, kwa mujibu wa Kanuni ya 97 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023. Kamati ilifanya Mkutano na Wadau (Public Hearing) tarehe 15 na 16 Agosti, 2023 ili kupokea mapendekezo na maoni kuhusu Muswada huu. Aidha, kutokana na umuhimu wa Sheria hii Kamati ilitoa mualiko kwa Waheshimiwa Wabunge kufika mbele ya Kamati ili kutoa maoni yao kuhusu Muswada huu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati iliupitia muswada huu kifungu kwa kifungu kwa madhumuni ya kujielimisha maudhui ya kila kifungu na kupendekeza marekebisho katika maeneo ambayo yalihitaji maboresho. Kamati ilifanya majadiliano ya kina na Waziri wa Fedha, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Kamishna wa Sera ya Ununuzi pamoja na Wataalam kutoka Wizara ya Fedha na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Vilevile, Kamati ilikutana na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA), Wakala wa Ununuzi Serikalini (GPSA), Mamlaka ya Rufani ya ununuzi wa Umma (PPAA) na Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB).

**Mheshimiwa Spika,** Wadau waliofika mbele ya Kamati kwa ajili ya kutoa maoni juu ya Muswada huu ni: Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL), Kampuni ya Taifa ya Mbolea (TFC). Aidha, kampuni binafsi kama vile Nyakwe Enterprises Ltd (NEL) na Umoja wa Watalaamu wa Ununuzi na Ugavi (Association of Procurement and Supplies Professionals - APSP) pamoja na watu binafsi waliwasilisha maoni yao kwa njia ya barua pepe.

**2.0. MADHUMUNI YA MUSWADA**

**Mheshimiwa Spika,** Muswada huu unakusudia kufuta na kutunga upya Sheria ya Ununuzi wa Umma Sura 410 ya Mwaka 2011 kama ilivyorekebishwa mwaka 2013, 2014, 2015, 2016 na 2018 mtawalia. Muswada huu unalenga kufuta iliyokuwa Sheria ya Ununuzi wa Umma Sura 410 na kutunga upya ili kuweka masharti bora ya usimamizi wa ununuzi wa umma, ugavi na uondoshaji mali kwa njia ya zabuni.

**2.1. Mapungufu ya Sheria ya sasa.**

**Mheshimiwa Spika,** Marekebisho haya ni sehemu ya kutatua na kurekebisha changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa Sheria hii, pia yanaenda kuokoa fedha za Serikali na kuhakikisha kuwa thamani halisi ya fedha inapatikana katika ununuzi wa Umma. Changamoto za utekelezaji wa Sheria ya Ununuzi wa Umma zinazoenda kutatuliwa kupitia Muswada huu ni:-

i. Bei kubwa za Bidhaa, Huduma na Kandarasi ikilinganishwa na bei ya soko;

ii. Kukosekana kwa viwango vya ukomo wa uidhinishaji wa zabuni kati ya Bodi za Zabuni na Afisa Masuuli;

iii. Usimamizi hafifu wa masuala ya mnyororo wa Ugavi;

iv. Matumizi mabaya ya utaratibu wa Rasilimali za Ndani (Force Account) katika utekelezaji wa Miradi kutokana na kukosekana kwa wataalamu na miongozo ya usimamizi;

v. Usimamizi hafifu wa Mikataba ya Ununuzi;

vi. Kutokufanya manunuzi kwa njia ya mfumo wa ununuzi wa Kielektroniki;

vii. Mzabuni kuongezewa muda wa ziada kama adhabu zaidi ya ule aliofungiwa nje ya Nchi;

viii. Sheria kutokuwa na utaratibu maalumu wa ununuzi kwa Taasisi, Mashirika na Kampuni za Umma zinazojiendesha na zisizojiendesha kibiashara;

ix. Sheria kutojumuisha masuala ya ugavi (supply) na uondoshaji mali;

x. Kutokuwepo kwa sehemu mahususi katika Sheria inayohusu masuala ya usimamizi wa mikataba ya ununuzi na Ugavi;

xi. Kutokuwepo kwa sharti la bei kikomo katika ununuzi wa umma; na

xii. Muda mrefu katika utekelezaji wa michakato ya ununuzi.

## 2.2. Sehemu Mpya na Ibara zilizofanyiwa Marekebisho ya Kiuandishi

### 2.2.1. Sehemu Mpya

**Mheshimiwa Spika**, Muswada huu umeanzisha sehemu mpya mbili zinazohusu Usimamizi wa Mikataba pamoja na usimamizi wa Ugavi ambazo ni sehemu ya saba na sehemu ya nane. Lengo la uanzishwaji wa sehemu hizi ni kuweka usimamizi mzuri wa Mikataba pamoja na kujumuisha masuala ya Ugavi ikiwemo upokeaji wa bidhaa, vifaa au mali zilizonunuliwa, uwekezaji kumbukumbu, utunzaji na usambazaji. Sehemu hizi mpya zimeainisha taratibu za usimamizi wa mikataba na miongozo ya ugavi inayopaswa kuzingatiwa na taasisi nunuzi.

### 2.2.2. Ibara zilizofanyiwa Marekebisho ya Kiuandishi

**Mheshimiwa Spika**, Muswada huu umefanya marekebisho ya kiuandishi kwa takribani Ibara 29 kwa madhumuni ya kuleta maana iliyokusudiwa, kuondoa tafsiri sisisi (word to word translation) na kuondoa mkanganyiko wakati wa utekelezaji wa Sheria hii.

## 2.3. Marekebisho yaliyofanyika

**Mheshimiwa Spika,** Marekebisho yaliyofanyika kupitia muswada huu yana lengo la kuondoa kasoro zilizojitokeza wakati wa utekelezji wa Sheria hii kama zilivyobainishwa awali. Marekebisho yaliyopendekezwa kupitia ibara mbalimbali ili kuondoa kasoro hizo ni kama ifuatavyo:-

### 2.3.1. Ibara ya 32: Viwango vya ukomo wa uidhinishaji wa Bodi ya Zabuni.

**Mheshimiwa Spika**, Muswada unapendekeza kuongeza vifungu vipya vidogo kwa lengo la kutenganisha mamlaka ya uidhinishaji wa ununuzi kati ya Bodi ya Zabuni na Afisa Masuuli kwa kuzingatia ukomo wa uidhinishaji. Lengo la marekebisho haya ni kupunguza muda wa mchakato wa manunuzi na gharama. Taratibu za ununuzi zinazohitaji idhini ya Bodi ya Zabuni na zinazohitaji idhini ya Afisa masuuli zitaainishwa katika Kanuni.

**2.3.2. Ibara ya 38: Majukumu na mamlaka ya Afisa Masuuli**

**Mheshimiwa Spika,** Ibara hii inarekebishwa ili kumpa Afisa Masuuli mamlaka ya kuidhinisha masuala ya ununuzi, ugavi na uondoshaji mali kwa kuzingatia ukomo wa uidhinishaji. Lengo ni kuongeza uwajibikaji kwa Afisa Masuuli, kupunguza muda, gharama, na kuongeza ufanisi katika ununuzi wa umma.

**2.3.3. Ibara ya 49: Ununuzi katika Taasisi zinazojiendesha kibiashara**

**Mheshimiwa Spika,** madhumuni ya kuongeza Ibara hii mpya ni kuweka mazingira ya kutunga Kanuni zinazohusu taratibu maalumu za ununuzi kwa Mashirika na Taasisi za Umma zinazojiendesha kibiashara. Masharti ya ununuzi yaliyopo kwenye Sheria hivi sasa hayatofautishi utaratibu wa ununuzi kati ya Mashirika na Taasisi zinazojiendesha na zisizojiendesha kibiashara.

**Mheshimiwa Spika,** kukosekana kwa utofauti huo kumesababisha Mashirika yanayojiendesha kibiashara kuchukua muda mrefu katika kufanya manunuzi na hivyo kutokuwa shindani. Ibara hii inalenga kurahisisha utekelezaji wa ununuzi katika Taasisi za Umma na Mashirika yanayojiendesha kibiashara ili kuleta ufanisi. Utaratibu utakaofuatwa na Taasisi hizi utaainishwa katika Kanuni za ununuzi wa Umma.

**2.3.4. Ibara ya 71**: **Kuondoa masharti ya mzabuni aliyefungiwa nje kupewa adhabu mara mbili Mheshimiwa Spika,** Ibara hii imeondoa masharti ya mzabuni kuongezewa muda wa ziada kama adhabu zaidi ya ule aliofungiwa nje ya Nchi. Sheria ilivyo hivi sasa mzabuni aliyefungiwa nje ya nchi huongezewa adhabu ya ziada nchini kwa kufungiwa kwa kipindi cha miaka 10 kwa makosa ya udanganyifu au rushwa, au miaka 5 kwa makosa mengine.

**2.3.5. Ibara ya 72**: **Ununuzi kwa Njia ya Kielektroniki**

**Mheshimiwa Spika,** Ibara hii inarekebishwa ili kuondoa mwanya kwa Taasisi nunuzi kufanya ununuzi nje ya mfumo wa kielektroniki. Matumizi ya mfumo wa kielektroniki hivi sasa ni takriban **asilimia 17.5** tu na **asilimia 82.5** ya manunuzi hufanyika nje ya mfumo. Muswada unapendekeza kuondoa sharti linalotoa mwanya kwa Taasisi nunuzi kufanya ununuzi nje ya mfumo wa kielektroniki.

Maboresho haya yanazitaka Taasisi nunuzi zote kufanya ununuzi ndani ya mfumo wa kielektroni, ili kuimarisha dhana ya uwazi, ushindani na ufanisi katika ununuzi na ugavi. Endapo mfumo haufanyi kazi, Mamlaka itatoa notisi ya mwongozo kwa watumiaji wa mfumo na kwa Umma.

**2.3.6. Ibara ya 73: Bei Kikomo**

**Mheshimiwa Spika,** Ibara hii inakusudia kuweka bei kikomo katika bidhaa, kazi za ujenzi na huduma ili kutatua changamoto ya bidhaa moja katika eneo moja kununuliwa kwa bei tofauti na Taasisi za Umma mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika,** Muswada unapendekeza kuweka masharti kwa Taasisi nunuzi kununua bidhaa, huduma na kazi za ujenzi kwa kuzingatia bei kikomo ambazo zitaandaliwa kwa kuzingatia bei ya soko. Lengo ni kupunguza gharama kwa kutatua changamoto ya bei kubwa zinazotokana na ununuzi ambao hauzingatii bei halisi ya soko. Hata hivyo, Mtumishi wa Umma atakayehusika na ununuzi wa bidhaa, huduma  kazi za ujenzi kwa bei ya juu kuliko bei kikomo, atachukuliwa hatua za kinidhamu.

**2.3.7. Ibara ya 75: Matumizi ya Rasilimali za Ndani**

**Mheshimiwa Spika,** Sheria ya Ununuzi wa Umma inayofutwa ilikuwa imeruhusu matumizi ya rasilimali za ndani katika kutekeleza miradi ya ujenzi. Hata hivyo, utekelezaji wake umekuwa si wa kuridhisha kutokana na changamoto mbalimbali. Changamoto hizo ni kukosekana kwa wataalamu wenye sifa katika Taasisi nunuzi wa kusimamia miradi, usimamizi mbovu wa malighafi kwa ajili ya utekelezaji wa miradi, uandaaji wa gharama na makisio ya miradi yasiyo na uhalisia, kukosekana kwa taarifa za utekelezaji wa miradi na udhibiti hafifu wa ubora wa miradi inayotekelezwa.

**Mheshimiwa Spika,** Muswada unapendekeza kutatua changamoto hizo kwa kuweka masharti yafuatayo;

i) Kuzingatia ukomo wa thamani kwa miradi inayotumia njia hii ya ununuzi;

ii) Kuwa na vifaa na wataalamu wenye weledi kwa ajili ya kusimamia miradi;

iii) Uwepo wa uandaaji wa taarifa ya ukaguzi wa kazi zilizofanyika; na

iv) Uwepo wa ushindani katika upatikanaji wa bidhaa na mafundi.

**2.3.8. Ibara ya 92 – 97**: **Usimamizi wa Mikataba**
**Mheshimiwa Spika,** Serikali inakusudia kuanzisha ibara mpya mahususi kwa ajili ya usimamizi na utekelezaji wa mikataba ya ununuzi. Ibara hii inabainisha majukumu ya Afisa Masuuli na Idara tumizi katika usimamizi wa mikataba, na udhibiti wa gharama, thamani ya fedha, ubora na muda katika mikataba ya ununuzi. Mapendekezo haya yametokana na kuwa awali jukumu la usimamizi wa mikataba lilikuwa halifanyiki na hivyo kukosa wa kumuwajibisha pindi utekelezaji wa mkataba unapokuwa na changamoto.

**2.3.9. Ibara ya 98 – 103**: **Usimamizi wa Ugavi**
**Mheshimiwa Spika,** Muswada unapendekeza kuongeza sehemu mpya ya nane kuhusu usimamizi wa ugavi na uondoshaji mali. Ugavi ni miongoni mwa maeneo muhimu katika mnyororo wa usimamizi wa ununuzi unaopaswa kusimamiwa. Aidha, katika Sheria inayofutwa masuala ya ugavi yalikuwa hajajumuishwa na hivyo kusababisha kuwepo na usimamizi hafifu katika eneo hili.

**Mheshimiwa Spika,** marekebisho haya yanaenda kuongeza ufanisi katika matumizi ya fedha za umma kwa kuhakikisha kuwa wakati wote Taasisi ya Umma ina hesabu halisi ya vifaa na mali zake ili kuzuia upotevu na uharibifu.

**2.3.10. Kupunguza Muda wa Mchakato**
**Mheshimiwa Spika,** Sheria inayopendekezwa imeweka masharti yatakayopunguza muda wa hatua za utekelezaji wa ununuzi wa Umma.
Mfano:-

i. Sheria hii imepunguza muda wa kutangaza nia ya kutoa tuzo kutoka siku thelathini(30) hadi siku kumi na nne (14) kama ilivyofanyiwa marekebisho kwenye ibara ya 68 (15);

ii. Imeondoa hitaji la muda wa kusubiri malalamiko kutoka kwa wazabuni kwa ununuzi wa bidhaa mtambuka kutoka siku saba za kazi hadi siku siku tano kama ilivyofanyiwa marekebisho kwenye Ibara ya 68(4); pamoja na

iii. Imepunguza muda wa kushughulikia malalamiko ya zabuni kutoka siku saba hadi siku tano kama ilivyofanyiwa marekebisho kwenye Ibara ya 119(6).

**3.0. MAENEO YA MUSWADA YALIYOFANYIWA MAREKEBISHO NA KAMATI**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati baada ya kuchambua muswada huo na kupokea maoni ya wadau ilibaini maeneo ya ziada ambayo yalihitaji marekebisho ili kuleta tija iliyokusudiwa. Maeneo hayo ni kama yafuatayo: -

**3.1. Ibara ya 2 – Matumizi**

**Mheshimiwa Spika,** Serikali imeongeza kifungu kipya kidogo cha 5 katika Ibara hii ili kuakisi marekebisho yaliyofanyika kwenye kifungu cha 2 cha Marekebisho ya mwaka 2023 ya Sheria ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, Sura 103. Aidha, Kamati iliona umuhimu wa kifungu hiki kuboreshwa ili kuleta maana iliyokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,** kifungu kidogo cha 5 kinaruhusu mikataba iliyoridhiwa na Baraza la Mawaziri kutofuata taratibu za ununuzi na uondoshaji mali kupitia sheria hii. Hata hivyo, Kamati ilibaini kwamba kifungu hicho hakikutofautisha mikataba ya miradi ya kimkakati na mikataba ya miradi ya kawaida, hivyo kingeweza kutumika vibaya. Baada ya majadiliano baina ya Kamati na Serikali, muafaka ulifikiwa kwamba kifungu hiki kilenge miradi ya kimkakati pekee**.**

**Mheshimiwa Spika**, Marekebisho haya yatafanya kifungu hiki kurandana na Sheria ya PPP pamoja na kuzuia kifungu hiki kutumika vibaya na kudhibiti matumizi ya fedha za umma katika

ununuzi wa huduma na bidhaa. Serikali ilikubali mapendekezo ya Kamati na marekebisho ni kama yanavyoonekana katika jedwali la marekebisho ya Serikali.

**3.2. Ibara ya 3 – Tafsiri**

**Mheshimiwa Spika,** katika ibara hii Kamati iliishauri Serikali kutoa tafsiri ya maneno mbalimbali kama yalivyotumika kwenye Muswada kwa sababu zifuatazo;

i. Kutafsiri makosa kama yanavyotumika kwenye Sheria Mama;

ii. Kufuta maneno na kuandika upya ili yalete maana iliyokusudiwa;

iii. Kutafsiri maneno yaliyotumika ndani ya Muswada bila kutafsiriwa; na

iv. Kufuta maneno yaliyokuwa na maana sawa.

Marekebisho hayo ni kama yanavyoonekana kwenye Jedwali la marekebisho ya Serikali.

**3.3. Ibara ya 6 na 7 – Kamishna wa Sera ya Ununuzi wa Umma**

**Mheshimiwa Spika,** Ibara hizi zilivyokuwa katika Sheria inayofutwa zilikuwa zinatambua uwepo wa Idara ya Sera ya Ununuzi wa Umma pamoja na kubainisha majukumu ya Idara hiyo. Aidha, Kamati ilibaini majukumu yaliyobainishwa kwenye ibara ndogo ya 7(2) yanashabihiana na Majukumu ya Mamlaka ya Ununuzi wa Umma (PPRA) na Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB). Vilevile, Kamati iliona umuhimu wa Ibara hii kuitambua Wizara ya Fedha badala ya Idara kwa sababu idara hiyo sio kwamba inajisimamia yenyewe bali iko ndani ya Muundo wa Wizara. Baada ya majadiliano ilikubalika Ibara hizi kumtambua Kamishna wa Sera ya Ununuzi wa Umma na kufuta Ibara 7(2) na majukumu ya msingi ya Kamishna yahamishiwe katika ibara ya 7(1) ili yasilete mgongano wa majukumu. Marekebisho hayo ni kama yanavyoonekana kwenye Jedwali la marekebisho ya Serikali.

**3.4. Ibara ya 9 – Malengo ya Mamlaka**
**Mheshimiwa Spika,** kati ya masuala ya msingi yaliyozingatiwa katika muswada huu ni pamoja na wazabuni wa ndani kupewa kipaumbele katika zabuni za Serikali. Sheria inayofutwa ilikuwa inatoa fursa ya upendeleo kwa wazabuni wa ndani, hata hivyo, upendeleo huo haukuwa na taasisi inayofuatilia utekelezaji wake. Hivyo, kupitia muswada huu Serikali imeongeza lengo kwa Mamlaka kuhakikisha kuwa taasisi nunuzi inazingatia utoaji wa kipaumbele kwa wazabuni na watoa huduma wa ndani katika zabuni za bidhaa, kazi za ujenzi na huduma. Marekebisho hayo ni kama yanavyoonekana katika jedwali la marekebisho ya Serikali.

**3.5. Ibara ya 10 – Majukumu ya PPRA**
a) **Mheshimiwa Spika,** aya (o) ya Ibara hii inaiwezesha PPRA kupata taarifa za bei kwa bidhaa na huduma mtambuka pekee kutoka kwa Taasisi za umma zinazohusika na uandaaji wa bei hizo. Hata hivyo, kifungu hiki hakiruhusu Mamlaka kupata bei ya bidhaa za kazi za ujenzi na huduma ambazo siyo bidhaa na huduma mtambuka.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya majadiliano baina ya Kamati na Serikali, Kamati ilipendekeza kuboresha kifungu hiki ili kuruhusu Mamlaka kupata taarifa ya bei ya bidhaa, kazi za ujenzi na huduma zilizowekewa viwango kutoka kwa Taasisi za umma husika kwa lengo la kuhakikisha kuwa bei zinaendana na bei za soko kwa wakati huo. Hatua hii itaiwezesha PPRA kupata taarifa za bei kwa bidhaa, kazi za ujenzi na huduma zilizowekewa viwango kutoka kwa Taasisi za umma zinazohusika kuandaa bei hizo. Marekebisho hayo ni kama yanavyoonekana katika jedwali la marekebisho ya Serikali.

b) **Mheshimiwa Spika,** aya mpya ya (p) imeanzisha utaratibu mpya wa kuwepo kwa bei kikomo. Lengo la utaratibu huu ni kuhakikisha kwamba bidhaa na Huduma zinazonunuliwa na Serikali hazizidi bei ya soko. Kutokuwepo kwa bei kikomo katika sheria iliyopo hivi sasa kunasababisha bidhaa nyingi kununuliwa kwa bei ya juu ukilinganisha na bei ya soko kwa wakati huo.

**Mheshimiwa Spika,** mabadiliko haya yanaenda kuipa jukumu Mamlaka ya Usimamizi wa Ununuzi wa Umma (PPRA) kuandaa

bei kikomo kwa baadhi ya bidhaa, kazi za ujenzi na huduma ambayo itazingatiwa wakati wa ununuzi. Hatua hii itasadia kuhakikisha kuwa ununuzi wa Umma unaakisi bei ya soko kwa wakati huo na kuleta usawa na uwazi. Marekebisho hayo ni kama yanvyonekana katika jedwali la marekebisho ya Serikali.

**3.6. Ibara ya 11 – Wigo wa Uchunguzi Unaofanywa na Mamlaka**

**Mheshimiwa Spika,** Ibara hii inampa mamlaka PPRA kufanya uchunguzi katika masuala mbalimbali. Hata hivyo, PPRA haikuwa na jukumu kisheria la kufanya uchunguzi wa maombi ya uhalalisho wa ununuzi uliokwishafanyika kwa njia ya dharura kama ilivyoainishwa katika Ibara ya 76 ya muswada huu. Aidha, Ibara hii haikuwa imetoa fursa kwa Afisa Masuuli kuomba Mamlaka kufanya uchunguzi au ukaguzi maalumu kuhusu suala lolote katika ununuzi au uondoshaji mali. Hivyo, marekebisho yanayopendekezwa yanaenda kumpa PPRA mamlaka ya kufanya uchunguzi wa maombi hayo na kushughulikia maombi ya Afisa Masuuli. Lengo la marekebisho hayo ni kuhakikisha kuwa masuala ya ununuzi na uondoshaji mali yalifuata taratibu zilizoainishwa katika Sheria inayopendekezwa pamoja na Kanuni zake zitakazotungwa. Marekebisho hayo ni kama yanavyoonekana katika jedwali la marekebisho ya Serikali.

**3.7. Ibara ya 15 – Utaratibu wa Uchunguzi**

**Mheshimiwa Spika,** Serikali inafuta na kuandika upya Ibara hii kama inavyoonekana kwenye Muswada ili ilete maana iliyokusudiwa kama ilivyokuwa kwenye Sheria inayofutwa. Marekebisho hayo ni kama yanvyonekana katika jedwali la marekebisho ya Serikali.

**3.8. Ibara ya 20 – Usitishaji wa Michakato ya Ununuzi Mheshimiwa Spika,** Ibara hii ina lengo la kusitisha mchakato wote wa manunuzi pale inapobainika uwepo wa ukiukwaji wa sheria, kanuni na miongozo. Hata hivyo, baada ya majadiliano na Serikali, Kamati ilipendekeza kuongeza kifungu kidogo cha 2 ili kuondoa sharti la kusimamisha zabuni yote kwa bidhaa za afya endapo kuna bidhaa chache katika loti hazikukidhi vigezo. Kifungu hicho kitaweza kuendelea na manunuzi ya bidhaa za Afya ambazo katika loti moja zitakuwa zimekidhi vigezo ili kupunguza muda wa manunuzi. Pendekezo hili linaakisi ukweli

kwamba ununuzi wa dawa uhusisha dawa zaidi ya moja kwenye zabuni moja. Marekebisho hayo ni kama yanavyoonekana katika jedwali la marekebisho ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** vilevile, katika Ibara hii kifungu kidogo cha 1, Kamati ilipendekeza kiandikwe upya ili kuleta maana iliyokusudiwa na kwa Kiswahili fasaha ili kuepusha tafsiri sisisi. Serikali ilizingatia mapendekezo ya Kamati kama inavyoonekana katika jedwali la marekebisho ya Serikali.

**3.9. Ibara ya 21 – Hatua baada ya Mapendekezo ya Mamlaka**

**Mheshimiwa Spika,** mapendekezo ya Serikali katika Ibara hii hayakubainisha hatua atakazochukuliwa Mjumbe wa Bodi ya Zabuni endapo amejihusisha na vitendo vilivyo kinyume na Sheria hii. Hivyo, Kamati ilipendekeza Mjumbe wa Bodi ya Zabuni kujumuishwa kati ya watu watakaochukuliwa hatua endapo watavunja sheria kwa kuwa ni mdau mkubwa kwenye maamuzi yote ya ununuzi yanayofanyika kupitia Bodi za Zabuni. Hatua hii inaenda kudhibiti Wajumbe wa Bodi kutumia vibaya nafasi zao katika mchakato wa manunuzi. Marekebisho ya ibara hii ni kama yanavyoonekana katika jedwali la marekebisho ya Serikali.

**3.10. Ibara ya 30 – Taarifa ya Mwaka ya Tathmini ya Utendaji Kazi wa Ununuzi wa Umma na Thamani Halisi ya Fedha**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati iliboresha Ibara hii ili kuiwezesha taarifa ya mwaka inayoandaliwa na Mamlaka kujumuisha shughuli za ugavi na uondoshaji mali. Lengo ni kuifanya Taarifa ya Mwaka itakayowasilishwa iweze kuhusisha masuala ya Ugavi. Serikali ilipokea mapendekezo hayo na marekebisho ni kama yanavyoonekana katika jedwali la marekebisho ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, pia katika Ibara ndogo ya 2, Kamati ilipendekeza kufuta takwa la Taarifa hiyo kuwasilishwa Bungeni kwa sababu taarifa hiyo ni sehemu ya Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya kila mwaka inayowasilishwa Bungeni. Vilevile, kwa kuwa Taarifa hiyo ni ya kiutendaji, Kamati iliona hamna umuhimu wa kuwasilishwa Bungeni badala yake iishie katika ngazi ya Waziri mwenye dhamana ya ununuzi kwa ajili ya kufanyiwa kazi ili kurekebisha mapungufu yaliyobainishwa na Mamlaka katika Taarifa yake.

Maboresho ya Ibara hii ni kama inavyoonekana katika jedwali la marekebisho ya Serikali.

**3.11. Ibara ya 32 – Bodi za Zabuni**

**Mheshimiwa Spika,** mapendekezo ya Serikali katika Ibara hii hayakuzingatia umuhimu wa Kamati za Fedha na Uongozi katika masuala ya ununuzi, ugavi na uondoshaji mali katika ngazi ya Serikali za Mitaa. Hivyo, Kamati ilipendekeza Ibara hii iboreshwe na kurejesha utaratibu uliokuwepo awali kwa kuzingatia umuhimu wa Kamati hizo. Maboresho ya Ibara hii ni kama inavyoonekana katika jedwali la marekebisho ya Serikali.

**3.12. Ibara ya 38 – Majukumu na Mamlaka ya Afisa Masuuli**

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 38(2) ilikuwa inamruhusu Afisa Masuuli kuomba ushauri wa kitaalamu au kiufundi kutoka nje ya nchi. Kamati inaona umuhimu wa Afisa Masuuli kuomba ushauri kwa Taasisi ya Umma ili kuepusha gharama zitakazotokana na kumtafuta mshauri binafsi pamoja na kuokoa muda. Vilevile, Afisa Masuuli ashauriane na Bodi ya Zabuni kabla ya kuomba mtu wa kutoa ushauri elekezi nje ya nchi. Serikali imezingatia marekebisho hayo kama inavyoonekana katika jedwali la marekebisho ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara hii pia inarejesha jukumu la Afisa Masuuli kuanzisha bodi ya zabuni na kuteua wajumbe wake kama ilivyokuwa katika Sheria inayopendekezwa kufutwa. Muswada uliokuwa unapendekezwa ulikuwa umesahau kujumuisha jukumu hili kati ya majukumu mengine ya Afisa Masuuli. Marekebisho hayo ni kama yanavyoonekana katika jedwali la marekebisho ya Serikali.

**3.13. Ibara ya 40 – Majukumu ya Kitengo cha Usimamizi wa Ununuzi**

**Mheshimiwa Spika,** Ibara hii inarejesha jukumu la kitengo cha usimamizi wa ununuzi la kuandaa taarifa za utendaji kazi wa kitengo kwa ajili ya bodi za zabuni kama ilivyokuwa katika Sheria inayopendekezwa kufutwa. Muswada uliokuwa unapendekezwa ulikuwa umesahau kujumuisha jukumu hili kati ya majukumu

mengine ya kitengo. Marekebisho hayo ni kama yanavyoonekana katika jedwali la marekebisho ya Serikali.

**3.14. Ibara ya 49 – Ununuzi katika Taasisi zinazojiendesha kibiashara**

**Mheshimiwa Spika,** Ibara hii ni mpya katika Sheria ya Ununuzi inayopendekezwa, yenye lengo la kutofautisha masharti ya ununuzi kwa Taasisi za umma zinazojiendesha kibiashara na zile zisizojiendesha kibiashara. Aidha, Ibara hii ilikuwa haitambui sheria zilizoanzisha Taasisi, Kampuni na Mashirika yanayojiendesha kibiashara. Hivyo, Kamati ilipendekeza kuandikwa upya ili kuzitambua sheria husika ili kuharakisha mchakato wa ununuzi kwa Taasisi zinazojiendesha kibiashara. Marekebisho hayo ni kama yanavyoonekana katika jedwali la marekebisho ya Serikali.

**3.15. Ibara ya 50 (3) – Wajibu wa Taasisi Nunuzi**

**Mheshimiwa Spika,** Ibara hii inamtaka Mkaguzi wa nje katika taarifa yake kuonyesha endapo ununuzi wa bidhaa, kazi za ujenzi au huduma umefanyika kwa kuzingatia Sheria ya Ununuzi wa Umma. Hata hivyo, jukumu hili limeainishwa wazi katika Kifungu cha 26 cha Sheria ya Ukaguzi Sura 418. Hivyo, Kamati ilipendekeza kufutwa kwa kifungu hiki ili kuepusha jukumu moja kutamkwa katika Sheria mbili tofauti. Serikali iliridhia mapendekezo ya Kamati na marekebisho ni kama yanavyoonekana katika jedwali la marekebisho ya Serikali.

**3.16. Ibara ya 60 – Upendeleo kwa Bidhaa za Ndani**

**Mheshimiwa Spika,** ibara hii imefanyiwa marekebisho na Serikali ili kuweka sharti kwa taasisi nunuzi kutoa kipaumbele kwa bidhaa zilizotengenezwa, kuzalishwa au kuchimbwa nchini kabla ya kununua bidhaa hizo kutoka nje ya nchi. Aidha, sharti hilo linazitaka taasisi nunuzi kubainisha takwa hili katika nyaraka za zabuni. Lengo la marekebisho haya ni kuendeleza watoa huduma pamoja na viwanda vya ndani katika matumizi ya rasilimali za ndani zilizopo nchini. Marekebisho hayo ni kama yanavyoonekana katika jedwali la marekebisho ya Serikali.

**3.17. Ibara ya 61- Kujenga Uwezo wa Kampuni za Ndani**
**Mheshimiwa Spika,** Ibara hii, haikubainisha ni mikataba ipi iliyokuwa inakusudiwa na vyombo vilivyokuwa vinarejewa ambavyo vinapaswa kushauriana na Taasisi nunuzi katika kutenga mikataba hiyo. Changamoto ambayo ingeweza kujitokeza wakati wa utekelezaji wa Sheria ni aina ya mikataba na vyombo vipi vinatakiwa kurejewa ili kujenga uwezo wa kampuni za ndani.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipendekeza kuboreshwa kwa ibara hii ili kuondoa changamoto zinazoweza kujitokeza wakati wa utekelezaji wa masharti ya ibara hii. Baada ya majadiliano Serikali ilikubaliana na mapendekezo ya Kamati na ikafuta na kuandika upya ibara ndogo ya (1) na (2) ili kuleta maana iliyokusudiwa. Marekebisho ni kama yanavyoonekana katika jedwali la marekebisho ya
Serikali.

**3.18. Ibara Mpya ya 62 - Uingiaji wa Ushirika au Mikataba Midogo na Kampuni za Ndani**
**Mheshimiwa Spika,** baada ya kufanya maboresho katika ibara ya 61 iliyopo hivi sasa, Serikali imeongeza ibara mpya ya 62 ili kuakisi maudhui ya ibara ya 61. Ibara hii inaweka masharti kwa mzabuni wa kigeni aliyepewa tuzo ya Mkataba kuingia ushirika wa mikataba midogo (Sub-contract) na kampuni za ndani. Aidha, ibara hiyo inaweka sharti kwa mzabuni wa kigeni aliepata tuzo ya mkataba kubainisha ni asilimia ngapi ya mikataba midogo atashirikisha kampuni za ndani. Kifungu hiki kina lengo la kuziwezesha kampuni za ndani kushiriki katika zabuni ili kupata ujuzi pamoja na kubakiza fedha nchini kuliko hivi sasa ambapo kampuni za kigeni zilizoshinda zabuni hazikulazimika kisheria kushirikisha kampuni za ndani. Marekebisho hayo ni kama yanavyoonekana katika jedwali la marekebisho ya Serikali.

**3.19. Ibara ya 67 – Kukataliwa kwa Wazabuni**
**Mheshimiwa Spika,** katika aya (d) ya ibara hii, kifungu kilikuwa hakiiruhusu Taasisi nunuzi kukataa zabuni ambayo inahusisha gharama kubwa kuliko bei ya soko. Hivyo, Kamati ilipendekeza kuongeza neno bei ya soko katika aya hiyo ili kuleta maana

iliyokusudiwa. Marekebisho hayo ni kama yanavyoonekana katika jedwali la marekebisho ya
Serikali.

**3.20. Ibara ya 71 – Kufungiwa Kwa Mzabuni**
**Mheshimiwa Spika,** katika Ibara hii Kamati ilipendekeza kifungu hiki kuweka bayana muda wa kukata rufaa kwa mzabuni ambaye hajaridhishwa na uamuzi wa Mamlaka. Lengo la mapendekezo ya Kamati ni kuleta usawa kwa kuwa Muswada umeainisha muda wa kukata rufaa kwa Afisa Masuuli au muda wa Afisa Masuuli kutoa uamuzi wa malalamiko au mgogoro wa mchakato wa ununuzi, ugavi, uondoshaji mali na tuzo za mikataba katika Ibara ya 119. Serikali ilizingatia pendekezo hilo na kupitia jedwali la marekebisho imependekeza siku ishirini na moja (21) kuanzia siku mzabuni alipofahamu kuwepo kwa uamuzi huo.

**3.21. Ibara ya 72 (1)- Ununuzi kwa Njia ya Kielektroniki**
**Mheshimiwa Spika,** Ibara hii haikuweka sharti la lazima la matumizi ya mfumo wa kielektroniki katika Ununuzi, ugavi na uondoshaji mali kwa Taasisi nunuzi. Kamati iliona endapo kifungu hiki kingebaki kama kilivyo kingeweza kutumika vibaya. Hivyo, Kamati ilipendekeza kifungu hiki kuweka sharti la lazima kwa Taasisi nunuzi kutumia mfumo kufanya shughuli za ununuzi, ugavi na uondoshaji mali kwa njia ya zabuni na kutoa taarifa kupitia Mfumo huo.

**Mheshimiwa Spika,** ikumbukwe kwamba hivi sasa ni **asilimia 17.5** tu ya manunuzi yote ya Umma yanafanyika kwa njia ya Kieletroniki. Kamati inaamini kwamba hatua hii itaenda kuchochea matumizi ya mfumo na hivyo kupata thamani halisi ya fedha na kuongeza ufanisi, uwazi na usawa. Marekebisho hayo ni kama yanavyoonekana katika jedwali la marekebisho ya Serikali.

**3.22. Ibara ya 76 – Ununuzi wa Dharura**
**Mheshimiwa Spika,** mazingira yaliyowekwa kwenye kifungu cha 2 aya (a) na (b) hayakuzingatia upekee wa ununuzi wa bidhaa za afya. Hivyo, Kamati ilipendekeza kwa Serikali kuanzisha aya mpya (c) ili kujumuisha ununuzi wa bidhaa za afya kwa upekee

wake ili kuondoa changamoto inayojitokeza hivi sasa katika kuhalalisha ununuzi wa dawa kwa njia ya dharura. Serikali ilikubali mapendekezo ya Kamati na marekebisho ni kama yanavyoonekana katika jedwali la marekebisho ya Serikali.

**3.23. Ibara ya 79 - Ununuzi wa Vichwa vya Mabehewa ya Treni, Ndege na Meli zilizotumika**

**Mheshimiwa Spika,** katika Ibara hii Kamati ilipendekeza kuongeza kifungu kipya cha (6) kitakachoainisha sharti la kuweka sifa na vigezo vitakavyo zingatiwa wakati wa ununuzi wa vichwa na mabehewa ya treni, ndege na meli zilizotumika kuainishwa katika kanuni. Lengo la hatua hii ni kuhakikisha kwamba vifaa vilivyotumika vinavyonunuliwa vina ubora na viwango na vitatumika kwa muda mrefu. Marekebisho ni kama yanavyoonekana katika jedwali la marekebisho ya Serikali.

**3.24. Ibara ya 81 – Ununuzi wa Bidhaa za Afya Zinazookoa Uhai**

**Mheshimiwa Spika,** katika Ibara hii Kamati ilibaini kuwa utaratibu wa ununuzi wa bidhaa za afya zinazookoa uhai uliokuwa unapendekezwa ulikuwa unabagua bidhaa za afya katika makundi mawili, bidhaa zinazookoa uhai na bidhaa zisizookoa uhai. Vilevile, Ibara hii haikuweka wazi utaratibu wa ununuzi wa kawaida wa dawa na vifaa tiba.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya Kamati kushauriana na Serikali, Serikali ilifuta na kuandika upya kwa kuongeza majukumu ya Bohari ya dawa pamoja na Wizara yenye dhamana ya masuala ya afya katika kuandaa na kuidhinisha viwango vya bidhaa za afya kulingana na hadhi ya vituo vya kutolea huduma pamoja na jedwali la mahitaji na vigezo msawazo kwa kuzingatia viwango vya bidhaa.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ndogo zilizoongezwa zinaweka sharti kwa vituo vya kutolea huduma za afya na bohari ya dawa kuzingatia vigezo vilivyowekwa chini ya sheria inayopendekezwa. Lengo ni kuhakikisha kwamba kunakuwa na vigezo msawazo kulingana na hadhi ya maeneo ya kutolea huduma za afya. Pia, Serikali ilibadilisha maneno ya pembeni (Marginal notes) na sasa kusomeka **Ununuzi wa bidhaa za Afya**. Marekebisho ni kama yanavyoonekana katika jedwali la marekebisho ya Serikali.

**3.25. Ibara ya 90 (3) – Majadiliano na Utoaji wa Tuzo ya Mikataba**
**Mheshimiwa Spika,** Ibara hii jinsi ilivyokuwa imeandikwa ilikuwa imempa mamlaka Afisa Masuuli kusitisha majadiliano kwa zabuni zote bila ya kuzingatia ukomo wa uidhinishaji. Hivyo, ibara hii imerekebishwa ili kuzingatia ukomo wa uidhinishaji ambapo kwa zabuni zilizoidhinishwa na Afisa Masuuli zitasitishwa na Afisa Masuuli. Aidha, kwa zabuni zilizoidhinishwa na Bodi za Zabuni, Afisa Masuuli atasitisha zabuni hizo baada ya kushauriana na Bodi na kuendelea na hatua inayofuata. Marekebisho hayo ni kama yanavyoonekana katika jedwali la marekebisho ya Serikali.

**3.26. Ibara ya 94 (1) – Mabadiliko na Marekebisho**
**Mheshimiwa Spika,** katika Ibara hii Kamati ilipendekeza mkataba baada ya kusainiwa unaweza kubadilishwa au kurekebishwa lakini mabadiliko hayo yasizidi **asilimia 15** ya jumla ya bei ya mkataba wa awali badala ya **asilimia 30** iliyokuwa imependekezwa. Vilevile, Kamati ilipendekeza kuongeza aya ya 2 katika Ibara ya 94 itakayoweka sharti la lazima kwa mkataba unaopendekezwa kuongezewa muda na Afisa Masuuli, kurejewa na kufanyiwa upekuzi na Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Marekebisho ni kama yanavyoonekana katika jedwali la marekebisho ya Serikali.

**3.27. Ibara ya 103 – Miongozo ya Usimamizi wa Bidhaa, Vifaa au Mali**
**Mheshimiwa Spika,** Mapendekezo ya awali ya Ibara yalikuwa yanaonyesha jukumu la usimamizi wa bidhaa, vifaa au mali halina Sheria inayoisimamia lakini kimsingi jukumu hili linasimaiwa na Sheria ya Fedha za Umma. Hivyo, marekebisho hayo yamerejea masharti yalipo katika Sheria husika. Marekebisho ni kama yanavyoonekana katika jedwali la marekebisho ya Serikali.

**3.28. Ibara ya 119 – Utatuzi wa Malalamiko au Migogoro kwa Maafisa Masuuli**
**Mheshimiwa Spika,** Ibara hii inaweka utatuzi wa malalamiko au migogoro kwa Afisa Masuuli. Utaratibu uliokuwa umependekezwa na Serikali ulibainisha siku 5, vilevile ibara hii inampa mamlaka Afisa Masuuli kuunda jopo kwa ajili ya kufanya uchunguzi. Kamati ilibaini endapo Afisa Masuuli atatakiwa

kuunda jopo atalazimika kutoa uamuzi ndani ya siku 5. Hivyo, ilipendekeza pale ambapo jopo linaundwa maamuzi yatolewe ndani ya siku 7. Serikali imepokea mapendekezo hayo kama inavyoonekana katika jedwali la marekebisho ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** marekebisho haya pia yanamtaka Afisa Masuuli endapo ataunda jopo huru kuwataarifu wazabuni ndani ya siku moja baada ya kupokea malalamiko au mgogoro. Marekebisho hayo ni kama yanavyoonekana katika jedwali la marekebisho ya Serikali.

**3.29. Ibara ya 123 – Kusitishwa kwa Mchakato wa Ununuzi**
**Mheshimiwa Spika,** ibara hii inaweka masharti ya kusitisha mchakato wa ununuzi. Kamati imebaini kwamba masharti yaliyowekwa katika ibara hii yalikuwa hayatoi fursa kwa zabuni za bidhaa za afya kusitishwa kwa baadhi ya bidhaa na si zabuni nzima. Aidha, Serikali imeongeza Ibara ndogo ya 3 ili kumpa Afisa Masuuli idhini ya kuomba kwa Mamlaka kutokusitishwa kwa Mchakato wa ununuzi wa bidhaa za afya endapo malalamiko au mgogoro upo kwa Afisa Masuuli. Marekebisho hayo ni kama yanavyoonekana katika jedwali la marekebisho ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** vilevile katika Ibara hii Kamati ilipendekeza kwamba usitishwaji wa mchakato wa manunuzi ya bidhaa za afya uzingatie loti au baadhi ya bidhaa za afya zilizoko katika zabuni moja ambazo hazikukidhi vigezo na hivyo kuruhusu loti au baadhi ya bidhaa za afya zilizokidhi vigezo kuendelea na mchakato wa manunuzi. Serikali ilikubali mapendekezo ya Kamati na marekebisho ni kama yanavyoonekana kwenye jedwali la marekebisho ya Serikali.

**3.30. Ibara ya 127 (2) - Makosa**
**Mheshimiwa Spika,** katika Ibara hii, Kamati ilikuwa na mapendekezo yafuatayo ambayo Serikali iliyapokea na kuyafanyia marekebisho kama inavyoonekana katika jedwali la marekebisho ya
Serikali.

a) Kuongeza aya mpya ili kuainisha bayana kuwa itakuwa ni kosa kwa mtu yoyote atakayeshindwa kufanya shughuli za

ununuzi, ugavi na uondoshaji mali kwa kutumia mfumo wa kielektroniki wa ununuzi wa umma. Hatua hii itasaidia kuleta uwajibikaji na matumizi sahihi ya mfumo.

b) Kuongeza aya mpya ili kuainisha bayana kuwa ni kosa kwa mtu yoyote pamoja na mjumbe wa bodi atakaekiuka masharti yanayohusiana na upendeleo wa ndani wa kitaifa bila sababu za msingi. Lengo ni kuhakikisha kuwa Watanzania wanashiriki kikamilifu katika zabuni za Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** mapendekezo haya yanalenga kutambua makosa ya kutokutumia mfumo na kutokutoa upendeleo kwa kampuni za ndani chini ya
Sheria hii.

**3.31. Mabadiliko ya Jina Refu la Sheria**

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na marekebisho mengine yaliyofanyika kupitia Muswada huu Serikali imependekeza kubadilisha jina refu la Sheria ili kujumuisha masuala ya ugavi, na hivyo kusomeka "Sheria ya ununuzi wa umma na ugavi."

**4.0. MAONI NA MAPENDEKEZO YA JUMLA**

**4.1. Kutokuwa na Sera na Mkakati wa Ununuzi na Ugavi**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini kwamba pamoja na uwepo wa Sheria ya Ununuzi wa Umma tangu mwaka 2001 mpaka hivi sasa Taifa halina Sera wala Mkakati wa ununuzi wa Umma ambao ni nyenzo muhimu katika kuhakikisha upatikanaji wa thamani halisi ya fedha. Uwepo wa Sera na Mkakati wa Ununuzi wa Umma utasaidia katika maeneo yafuatayo:-

a) Namna ya kupunguza gharama katika ununuzi wa umma na ugavi.

b) Namna ya kushughulikia vihatarishi katika ununuzi na ugavi.

c) Kuweka masharti ya ununuzi usioathiri mazingira (Green Procurement);

d) Usimamizi wa ubora.

e) Usimamizi na upatikanaji wa watoa huduma.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri maboresho haya yanayofanyika katika Sekta ya Ununuzi, Ugavi na Uondoshaji mali kwenda sambamba na uandaaji wa Sera na Mkakati wa Ununuzi na Ugavi. Hivyo, Kamati inaitaka Serikali kuanza mchakato wa uandaaji wa Mkakati wa Ununuzi na Ugavi.

**4.2. Ujenzi wa Mfumo Mpya wa Ununuzi wa NeST**

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 9 (1) aya (k) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma Sura 410 kimeipa PPRA jukumu la kuanzisha, kutunza na kuhuisha mfumo wa ununuzi wa umma wa kielektroniki. Kupitia kifungu hiki Serikali iliamua kujenga mfumo mpya ili kufikia malengo yafuatayo;

a) Kupata ufumbuzi wa changamoto za mfumo wa TANePS ikiwa ni pamoja na kukidhi mahitaji ya Serikali.

b) Mfumo wenye uwezo wa kuongeza uwazi na uwajibikaji.

c) Kuongeza uzingatiaji wa sheria, taratibu na miongozo ya ununuzi.

d) Kupunguza mianya ya rushwa na kuleta thamani halisi ya fedha za umma.

e) Kuongeza wigo wa watumiaji kwa makundi yote.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inapenda kuipongeza Serikali kwa hatua hii muhimu. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kukamilisha mfumo huu na kuutumia.

**4.3. Usimamizi wa Mikataba na Uandaaji wa Mikataba Msawazo**

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kwamba Muswada unapendekeza kuainisha sehemu mpya inayohusu usimamizi wa mikataba, bado kuna changamoto katika uandaaji wa mikataba msawazo (Standard Contract). Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuwepo na miongozo ya uandaaji wa mikataba msawazo itakayotumika ili kuepusha gharama za ziada zinazoweza kujitokeza katika kufanya mabadiliko ya mikataba.

Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba taratibu za kisheria zinafuatwa wakati wa uvunjaji wa mikataba ya ununuzi ili kuiepusha Serikali kuingia hasara.

**4.4. Utungaji wa Kanuni**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inapendekeza kabla ya kuanza kutumika kwa Sheria mpya kanuni zitakazotungwa kupitia Sheria hiyo, ziwasilishwe kwenye Kamati. Lengo ni kuhakikisha kanuni hizo zimezingatia mapendekezo ya Kamati wakati wa majadiliano na Serikali. Vilevile, kuzichambua na kuona kama zinaakisi maboresho yaliyofanyika.

**4.5. Kuwajengea Uwezo Wazabuni na Wakandarasi wa ndani**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inapendekeza wazabuni na Wakandarasi wa ndani kujengewa uwezo kwa kuimarisha mifumo ya kifedha ili waweze kupata mitaji kwa ajili ya kutekeleza miradi nchini. Aidha, Serikali ihakikishe kwamba Wakandarasi na Wazabuni wanakopesheka katika mabenki ya uwekezaji kwa riba nafuu pamoja na kuhakikisha kwamba malipo na madeni ya Wakandarasi na Wazabuni wa ndani yanapewa kipaumbele.

**5.0. HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika,** napenda kukushukuru kwa miongozo yako wakati wa utendaji kazi wa Kamati. Aidha, napenda kumshukuru Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mb Naibu Spika, kwa kuendelea kukusaidia kuliongoza vyema Bunge lako Tukufu. Vilevile, namshukuru Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, Mb Waziri wa Fedha pamoja na Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, Mb Naibu Waziri wa Fedha kwa ushirikiano wao walioutoa kwa Kamati wakati wote wa kuchambua Muswada huu. Napenda kumshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Jaji Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi, Manaibu Katibu Wakuu Wizara ya Fedha Ndg. Jenifa Omolo na Ndg. Elijah Mwandumbya, Kamishna wa Sera ya Ununuzi Dkt. Frederick Mwakibinga, Mtendaji Mkuu wa PPRA Ndg. Eliakim Maswi na watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati kipindi chote cha kuchambua Muswada huu. Kamati pia inawashukuru wadau wote kwa maoni yao kuhusu Muswada huu.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwapongeza Wajumbe wa Kamati wakiongozwa na Mhe. Omari Mohamed Kigua, Mb Makamu Mwenyekiti wa Kamati kwa umahiri na ushirikiano wao katika kuchambua Muswada huu na kuweza kuuboresha hadi kufikia hatua hii. Naomba kuwatambua
Wajumbe hao kama ifuatavyo :-

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Daniel Baran Sillo, Mb | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Omari Mohamed Kigua, Mb | M/Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, Mb | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Mariam Madalu Nyoka, Mb | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Dkt. Charles Stephen Kimei, Mb | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Josephat Sinkamba Kandege, Mb | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Leah Jeremiah Komanya, Mb | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Juma Hamad Omar, Mb | Mjumbe |
| 9. | Mhe. Subira Khamis Mgalu, Mb | Mjumbe |
| 10. | Mhe. Shally Josepha Raymond, Mb | Mjumbe |
| 11. | Mhe. Stella Alex Ikupa, Mb Mjumbe | |
| 12. | Mhe. Jonas William Mbunda, Mb | Mjumbe |
| 13. | Mhe. Zainab Athumani Katimba, Mb | Mjumbe |
| 14. | Mhe. Kwagilwa Reuben Nhamanilo, Mb | Mjumbe |
| 15. | Mhe. Bahati Khamis Kombo, Mb | Mjumbe |
| 16. | Mhe. Vedastus Manyinyi Mathayo, Mb | Mjumbe |
| 17. | Mhe. Omar Ali Omar, Mb | Mjumbe |
| 18. | Mhe. Zaytun Seif Swai,Mb | Mjumbe |
| 19. | Mhe. Oran Manase Njeza, Mb | Mjumbe |
| 20. | Mhe. Rashid Abdallah Rashid, Mb | Mjumbe |
| 21. | Mhe. Joseph Zacharius Kamonga, Mb | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya kipekee nimshukuru pia Katibu wa Bunge Bi. Nenelwa J. Mwihambi, *ndc* kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Aidha, napenda kuishukuru Sekretarieti ya Kamati ya Bajeti ikiongozwa na Mkurugenzi wa Idara ya Bajeti Ndg. Michael Kadebe akishirikiana na Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Emmanuel Rhobi, Makatibu wa Kamati Ndg. Lilian Masabala, Ndg. Wilfred Akasi, Ndg. Jenifer Maurice na Ndg. Trifina Karaguza, Ndg. Ludovick Ringia, Mwanasheria wa Ofisi ya Bunge kwa kuipatia Kamati ushauri wa kitaalamu na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Daniel Baran Sillo,
**MWENYEKITI KAMATI YA BUNGE YA BAJETI**
07 Septemba, 2023

**SPIKA:** Ahsante sana Mwenyekiti. Waheshimiwa Wabunge, Mwenyekiti amewasilisha maoni ya Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Muswada huu ambapo uliwasilishwa hapa na kusomwa mara ya pili na Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Sasa ninayo orodha hapa ya Wabunge ambao wameomba kuchangia kwenye Muswada huu. Tutaanza na Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, Mheshimiwa Kwagilwa Reuben Nhamanilo ajiandae.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nashukuru kupata nafasi ya kwanza kuchangia kwenye mjadala huu unaohusu Muswada wa Ununuzi wa Umma, Ugavi na Uondoshaji Mali za Umma wa Mwaka 2023, ambao naamini utaenda kupita na kufuta ile sheria ambayo tunatumia sasa hivi ya *Public Procurement Act No. 7* ya mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kuipongeza Serikali kwa dhati; Serikali hii inayoongozwa na Mama yetu Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jinsi ambavyo imekuwa sikivu na kuona kwamba kulikuwa na malalamiko mengi na mapungufu mengi yaliyojitokeza katika utekelezaji wa sheria hii ambayo sasa wamependekeza kufuta. Wote tunafahamu na tunajua mijadala iliyoendelea hapa Bungeni; Bunge limekuwa likijadili upotevu wa fedha kwa namna nyingi, na tuliishia kusema kwamba, pengine hatupati thamani ya fedha kabisa kwa kutumia mchakato uliokuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tunaona malalamiko mengi na kero nyingi ambazo analeta Mheshimiwa *CAG*. Dhana nyingi zinatokana na mchakato wa sheria ya ununuzi. Kwa hiyo, naamini kwamba baada ya sheria hii kupita, ambapo tunamshukuru sana

Mheshimiwa Rais kwa kukubali ije kwa haraka, na naamini kwamba imekuja kwa wakati muafaka. Sasa tutaenda kupata thamani ya fedha ambapo ni asilimia 70 ya bajeti tunayopitisha au takribani asilimi 14 ya pato la Taifa inapitia kwenye ununuzi. Kwa hiyo naamini tukipata thamani hiyo ya fedha, basi tutaona miradi inatekelezwa kwa tija na manunuzi yanafanyika kwa tija na hivyo, kuwaletea wananchi manufaa yale ambayo yanatarajiwa na bajeti na mapitio ya Bunge hapa.

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba, cha kwanza kabisa ambacho kimetushangaza ni kwamba utekelezaji wa sheria unafanyika lakini hakuna sera. Mimi nafikiri kwamba Serikali izingatie kwamba, kabla haijatengeneza Muswada au sheria tupitie kwanza kwenye mchakato wa sera ili tujue kitu gani tunaenda kukihalalisha kiwe ni sheria. Kwa hilo mimi naamini kwamba tutafuatana na Kamati kama alivyoeleza Mheshimiwa Mwenyekiti wetu. Tunaiomba Serikali sasa iende kutengeneza sera ambayo itajulikana wazi na iwe na mkakati wake wa kuitekeleza hiyo sera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama alivyosema Mwenyekiti wetu, Kamati ilipitia na kuchambua kwa kina sana huu Muswada. Tulipata muda wa kutosha kabisa kuchambua lakini pia kukutana na wadau na wametupatia maoni yao. Baada ya kupata maoni yale tukaweza kutoa mapendekezo kwa Serikali; na nashukuru sana Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba na timu yake kwa kukubali kuingiza mengi ya yale mapendekezo ambayo tulipendekeza. Ndiyo sababu sisi wanakamati tunaunga mkono hii hoja kwa nguvu zote, kwa asilimia 100, na tunawaomba Wabunge wenzetu wakubali hii ipite. Hakuna kitu ambacho kinapita ambacho ni *full,* kwamba hakina mapungufu lakini naamini kwamba hii sheria ni kati ya sheria ambazo zimefanyiwa kazi kwa kina sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijasema mawili au matatu ambayo mimi ninafikiri kila mmoja anapaswa aelewe sheria hii inaleta kitu gani nizungumzie suala la upendeleo kwa wazawa au upendeleo kwa kampuni zinazosajiliwa hapa nchini na upendeleo kwa manunuzi yanayozalishwa hapa nchini, pamoja na wakandarasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naamini kwamba njia pekee ya kupeleka fedha kwa wananchi, tunasema kwamba Serikali inasaidia wananchi wapate fedha, njia pekee ni hiyo ya kutoa upendeleo, kwa sababu sisi ndiyo tunalipa kodi, sisi wananchi ndiyo tunalipa kodi na tozo ambazo ndiyo zinaingia kwenye Mfuko wa Serikali, ndiyo zinatakiwa zitumike hapa ndani na zizunguke hapa ndani. Sasa mzunguko huo hautakamilika endapo sehemu kubwa ya miradi inayotekelezwa, sehemu kubwa ya manunuzi tunayofanya tunatoa nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hiyo hela ambayo tunaitoa mifukoni kwa watu tunaenda kuirudisha na watu wa nje wanafaidika kwenye viwanda vyao, sisi tunabaki hapa tunazubaa tu. Kwa hiyo, naomba kabisa kwamba kama kweli uadilifu utakuwepo na hii sheria nia yake ni kuingiza uadilifu, kulazimisha watu wawajibike kwenye mchakato huu, ina maana kwamba pengine tutakwenda kushuhudia kwamba sehemu kubwa ya manunuzi yatakayokuwa yanapita kwenye zabuni, basi yatakwenda kwa wananchi ambao watanufaika.

Mheshimiwa Spika, nasema hivi siyo kwamba ni kitaifa tu, lakini hata kwenye vitongoji tunavyotoka. Tunapotekeleza miradi ya maendeleo au manunuzi tukafanya kwenye maeneo yale ya vijiji vyetu, kwenye majimbo yetu yakafanyika mlemle kama *local* hata *force account* lakini kwa namna hiyo kwamba manunuzi yafanyike pale ili wale watu washiriki kwenye utekelezaji wa ule mradi, ndipo watakuwa na *ownership* na umiliki wa ule mradi na kuutunza na kuhakikisha kwamba ule mradi unaendelea kuwepo, kwa sababu wameshiriki kwenye utekelezaji, wamefaidi kwa kupata kipato kutokana na mradi ule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kufanya hivyo, wataupenda na mara nyingi inakuwa ni kitu kizuri sana na niseme hata kwa watu binafsi tu. Tunashangaa kwa mfano *Tour Operators*, *Tour Operator* anapandisha watu katika Mlima Kilimanjaro wageni, watalii, anatoka na nguvu kazi kutoka mjini, anatoka nao wengi kutoka Mjini Arusha, kutoka Moshi wanakuja kupanda mlima, wanafika pale wanakuta vijana wamekaa usiku kucha, hawajapata kazi, kipato chochote na wengine wanazungumza tusaidiane basi tuwe wapagazi tuweze kupandisha hawa watu mlimani.

Mheshimiwa Spika, huwa anakuja na watu wake kiasi kwamba anavunja moyo sana wale watu ambao wapo kwenye lile eneo na wale watu waliopo kwenye lile eneo hamna kipato kingine, hakuna *source* nyingine ya *income*. Wanabakia sasa kusema ili tupate kazi hizi, basi na sisi tukimbilie mijini, tukiwa kule mijini tunajulikana, tutaanza kujikuta na vikundi vya mjini, basi na sisi tutapata hizo kazi za *Tour Operator* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, naomba sana hata sekta binafsi tuhakikishe kwamba kule tunapoenda kujenga, hata kama umepata ukandarasi, umeupata mjini kwa sababu ya vifaa ulivyonavyo, lakini uhakikishe unaenda kwenye lile eneo, kwenye kile kijiji, unachukua nguvu kazi pale. Unaweza ukawa na wataalam wa kusaidia kutoka mjini lakini sehemu kubwa ya nguvu kazi itoke kwenye maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, niseme machache kwamba kusema kweli kama tulivyosema, nitasema vitu vitatu ambavyo vinanifurahisha sana kwenye Muswada huu. Kwanza ni kuomba kuongeza uwazi na usawa kwenye zabuni kwa kulazimisha kwamba ni lazima sasa ununuzi wote wa Taasisi Nunuzi, ufanyike kupitia mchakato huu wa mifumo ya eletroniki. Ninachojua kwamba kitu kinachosababisha watu kuanza kuombana hongo, rushwa ni kwa sababu wanakutana uso kwa uso.

Mheshimiwa Spika, kama hawakutani uso kwa uso kama mabenki tunasema hawakutani, wanachakata hata mikopo bila ya kukutana na wateja wale. Kwa sababu ukishaweza kuzuia kile kinapunguza sehemu kubwa ya ushawishi wa kutoa rushwa. Sasa kama unapitisha kwenye mfumo moja kwa moja na jawabu linatoka kwenye mfumo basi itakuwa kwamba siyo rahisi kuwe na *intervention* ambayo binadamu atanufaika nayo. Kwa hiyo nafikiri hilo ni moja.

Mheshimiwa Spika, pia naamini kwamba imekataliwa kabisa usinunue bila kupitia hiyo mifumo, lakini naamini kwamba pia kwa sababu ununuzi unachukua muda mrefu sana. Kwa mfano, kuna barabara zinatangazwa, baada ya muda mrefu, unasikia kwamba bado, mpaka mwisho wa mwaka ndiyo unakuta

mkandarasi amepatikana, lakini bajeti tulikuwa tumetenga toka Julai. Kwa hiyo, naamini kwamba *issue* hiyo ni kitu cha msingi sana, naamini Muswada huu umepunguza siku kama alivyoeleza Mheshimiwa Mwenyekiti wetu na naamini hilo linaweza kufanyika.

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ambacho kinasaidia ni kwamba ununuzi wa dharura utakuwepo tu kwa namna moja au nyingine, lakini huu Muswada unalazimisha kwamba iwe ni cha kidharura kwelikweli. Baada ya kufanya huo ununuzi wa dharura, lazima uripoti kwa Mdhibiti, kwa Mkurugenzi wa Mamlaka ambaye naye atakuja kutathmini kama ulifuata kanuni zitakazokuwepo kwenye Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, naamini kwamba ununuzi wa holela hatuwezi kuukwepa kwa sababu kuna mambo ya majanga na kadhalika nayo lazima yawe *accommodated*, lakini uzuri wa Muswada wake, umekwenda zaidi kwa kusema kabisa kwamba ni mazingira yapi yanaweza kusababisha ununuzi wa dharura.

Mheshimiwa Spika, pia kwenye Muswada huu kuna jambo moja ambalo litasaidia sana hasa kwenye manunuzi wa vifaa vya tiba pamoja na madawa. Ununuzi moja kwa moja kutoka kwa wazalishaji au mawakala wao. Hii tunaondoa yule mtu kati *(middle man)* ambayo maana yake kwamba, tunapunguza gharama, tozo za *middle man* zinaondoka. Kwa hiyo, pia hicho ni kitu ambacho nashukuru kwamba thamani ya fedha inakwenda kupatikana. Kingine ambacho pia wote tufahamu, Mkurugenzi Mkuu wa mamlaka hii ya ununuzi na Ugavi atakuwa anafanya *continuous follow up* ya mienendo ya ununuzi kwenye Taasisi za Umma na mwishoni anatakiwa atengeneze ripoti yake ambayo itafika mpaka kwa Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwanzoni sisi kwenye Kamati tulikuwa na wazo kwamba pengine hiyo ripoti pia ije hapa Bungeni, lakini kwa ushawishi wa Mheshimiwa Dkt. Nchemba, tumeamua kukubaliana naye kwamba, basi pengine Mheshimiwa Rais, atakapopokea hii ripoti, basi impendeze kuirudisha kwa Waziri anayehusika ili aweze kwenda kuifanyia kazi, lakini pia tunajua kwamba masuala mengi pia yatakuwa yametufikia kupitia kwenye ripoti ya CAG ambayo na yenyewe inakuja Bungeni. Kwa hiyo, tukasema tusi-*duplicate*.

Hili wazo nafikiri siyo baya sana, lakini liwe kama tulivyokubaliana na Serikali.

Mheshimiwa Spika, nataka kusema kwamba *issue* ya Bei Kikomo ambayo ningependa sana iwe inaitwa Bei Elekezi kwa sababu huwezi kuwa *exactly*. Kutakuwa na upungufu wa asilimia 10 au *plus minus ten percent,* ni kitu ambacho kisitusumbue sana. Naamini kwamba bei za ukomo hizi zitajitokeza baada ya muda na kutokana na hiyo kanzidata ambayo Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka atatengeneza, basi ataanza kuona *evolution* ikoje, Kilimanjaro au Mwanza au wapi, bei za kujenga darasa zitakuwa shilingi ngapi? Anatoa sasa hiyo bei, lakini isiwe bei ambayo ni *cut stone* ambayo huwezi kushuka *plus minus*, yaani ningependa sana sana labda pengine hilo la bei elekezi lifahamike vizuri…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa, kengele ya pili imegonga.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, jambo lingine zuri…

**SPIKA:** Mheshimiwa kengele ya pili ilishagonga.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, kumbe muda ulishakwisha, nilifikiri napata, basi…

Mheshimiwa Spika, naomba niunge mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, atafuatiwa na Mheshimiwa Kwagilwa Reuben Nhamanilo na Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha, ajiandae.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Nianze kwa kuwapongeza sana wezetu wa Serikali, kwa kuona haja ya kuboresha Sheria hii ya Ununuzi wa Umma. Kwa sababu sheria ya mwanzo ilikuwa na mapungufu makubwa na tukijua kwamba asilimia 70 ya bajeti ya nchi yetu inaenda eneo la ununuzi wa umma. Kwa hiyo, kutokana na mapungufu ya sheria ya mwanzo ilikuwa inatoa mwanya kwa

Serikali kupoteza fedha nyingi sana. Mara zote tumekuwa tukishuhudia ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali *(CAG)* ikionesha ukiukwaji mkubwa wa taratibu za manunuzi, upotevu wa fedha nyingi. Kwa hiyo sasa ile sheria ni ishara kwamba ilikuwa imeshashindwa kusimamia eneo hili la ununuzi wa umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia huu Muswada wa sasa una ibara zipatazo 131 ambazo zote ukizisoma, unaona sasa zinakwenda kusimamia vizuri eneo hili la ununuzi na ugavi. Kama ambavyo taarifa ya upande wa Serikali na Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti wameeleza ni kwamba sheria ya mwanzo ilikuwa haijasema mambo mengi sana kuhusiana na eneo la Ugavi. Hii ya sasa hivi ukiangalia utaona inakuja kuongeza uwezo wa sheria kusimamia sehemu ya ugavi na hata kwenye *short title* unaona pale eneo la ugavi limeweza kuongezwa. Kwa hiyo, ni jambo la kuipongeza sana Serikali kwa kuboresha sheria hii.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia utaona kifungu cha 64 cha sheria ya mwanzo, kilikuwa tu kimetoa tafsiri ya matumizi ya ile *force account*. Kule halmashauri kuna miradi mingi ambayo ilikuwa inatekelezwa kwa *force account*, sasa tumeona changamoto nyingi sana ambazo zilikuwa zinajitokeza kwenye *force account*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna miradi mingine ilikuwa miradi mikubwa sana ambayo Serikali ilikuwa inatoa fedha kadri ya upatikanaji. Unakuta mradi wa Shilingi Bilioni sita, Shilingi Bilioni tano unawekwa kwenye *force account* na Serikali inatoa fedha kadri inavyokusanya, lakini kumbe miradi ile mikubwa akipewa Mkandarasi anafanya kwa fedha yake. Kwa hiyo, mradi unakamilika kwa wakati, wananchi wanaendelea kupata huduma wakati Serikali inaendelea kufanya malipo. Ile ya kusubiri Serikali mpaka ipeleke fedha ilikuwa inaleta changamoto nyingi.

Mheshimiwa Spika, hata uwezo wa baadhi ya wataalam wetu kusimamia hii miradi ulikuwa upo chini sana. Kwa hiyo, unakuta kuna halmashauri nyingine zilikuwa hazina wale watu wa kuandaa ule mchanganuo wa gharama za ujenzi, wakadiriaji majenzi, hamna wahandisi. Kwa hiyo, unakuta mradi mkubwa

wanapewa watu ambao uwezo wao kitaaluma upo chini, lakini kwa sheria hii utaona hapa inamwelekeza Waziri mwenye dhamana kuja na kanuni ambazo zitatoa mwongozo sasa, kwamba ni miradi ipi iweze kutekelezwa kwa hii *force account* na miradi ipi iweze kwenda kwa wakandarasi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nafikiri hii itaongeza sana ufanisi katika kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo. Ukiangalia hata kule vijijini ambapo miradi ya madarasa ipo, vituo vya afya na zahanati, wapo vilevile mafundi wale wenyeji kule ambao nao walikuwa wanaweza wakapata kipato kupitia hii *force account*. Serikali imeweka utaratibu wa kutambua wale wenye ujuzi na kuwapa vyeti. Kwa hiyo wakitambuliwa wale mafundi ambao ni wazoefu wanafanya kazi, kwa sababu nayo ni namna ya kupeleka ajira kwa wananchi, kwa hiyo fedha ndogondogo zitakuwa zinabaki kwa wananchi katika maeneo yaleyale.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba hili pia Serikali liende sambamba na kutambua ujuzi na uwezo wa mafundi wale waliokuwa vijijini na kuwa na utaratibu maalum wa kuwapa mafunzo na ujuzi zaidi ili waweze kutekeleza hii miradi ya kutumia rasilimali za ndani, ambayo inajulikana kama *force account*.

Mheshimiwa Spika, tukiangalia ibara ya 75 ya muswada tunaona imeenda kuboresha kile kifungu cha 64 cha sheria ya mwanzo, imeweka utaratibu mzuri na mwongozo mzuri ambao utakwenda kuwarahisishia Maafisa Masuuli, kwanza kufuata hizi *procedures* ule utaratibu wa kutangaza zile kazi kuwapata watu wa kufanya kazi na hata usimamizi wake. Kwa sababu sheria imeeleza mambo mazuri.

Mheshimiwa Spika, vile vile ukisoma ibara ya 75, ibara ndogo ya nne inasema; "Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha kwanza, fundi maana yake ni fundi ujenzi ambaye ana ujuzi wa kitaaluma katika fani ya ujenzi ingawa hajasajiliwa na chombo kinachohusika na usajili wa wataalam wa ujenzi au ambaye hana ujuzi na maneno mengine yanaendelea."

Kwa hiyo, vitu kama hivi vitaenda kutengeneza ajira kwa wananchi wanaozunguka hiyo miradi.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni ibara ya 63 ya Muswada ambao sasa unakuja kuwa sheria iwapo tutapitisha. Eneo hili linazungumzia kwamba kila Afisa Masuuli, aweze kutenga fedha kwa ajili ya vikundi vya akinamama, vijana na watu wenye ulemavu. Kwa hiyo, eneo hili sasa kama kutakuwa na utekelezaji mzuri wa eneo hili la ibara ya 63, tunaona kwamba tutakwenda kutengeneza ajira kwenye jamii wakati miradi yetu vilevile tunaendelea kuitekeleza.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tutakuwa tu tunasimamia ubora wa kazi, lakini sio fedha zote zitakwenda maeneo mengine na watu wetu wanaweza kupata ajira. Nitatoa mfano watu wa *TARURA* kule jimboni kwangu wana vikundi vya akinamama zaidi ya 15 na vikundi vya vijana vilevile na tayari wameweza kuwapa mafunzo, kazi ndogo ndogo za ukandarasi, kama kufyeka *line* ya *TANESCO*. Vikundi hivi vidogo vidogo wanaweza siyo kazi zote zinahitaji uandisi au ujuzi wa hali ya juu sana. Kufyeka barabara kwenye kazi za *TANROADS*, siyo lazima wakandarasi wakubwa. Kwa hiyo, vikundi vya vijana wanaweza wakapewa hizo zabuni wakasimamia na wakafanya kazi. Kwa hiyo, sheria hii imekuja kuweka vizuri sana eneo hilo na ndiyo sababu na mimi pia naunga mkono hoja hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia lengo la hii sheria ni zuri sana. Kwa hiyo, imekuja kuboresha sasa kasoro ambazo zilikuwepo kwenye ile Sheria ya Ununuzi ya mwanzo na vilevile kuna eneo linazungumzia matumizi ya mifumo, tuliona takwimu zinaonyesha kwamba sheria mpya ilisababisha kutokana na kuwa *loose* ni asilimia 18 tu ya kazi ndiyo ilitumika kwa kufuata mifumo, lakini asilimia kubwa zilikuwa zinafanyika *manually*. Kwa hiyo, sasa hili linakwenda pia kuhakikisha kwamba mifumo inayotumika katika ununuzi wa umma inaboreshwa na inasomana na mifumo mingine.

Mheshimiwa Spika, hii itaongeza sana ufanisi katika miradi, lakini vile vile itaongeza uwazi kwa sababu, mwananchi yeyote anaweza kuingia tu kwenye mfumo akapata taarifa. Vilevile

itaokoa muda ambao mtu anautumia katika kuandaa nyaraka za zabuni, kuomba hizo kazi na *tender* mbalimbali. Kwa hiyo, muda utakuwa mchache, lakini hata gharama ile ya kuandaa makabrasha ambayo ni ya gharama kubwa kidogo ilikuwa inaweza ikaleta changamoto.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya mifumo nina imani yatakwenda kusimamiwa vizuri kwa sababu ni takwa la kisheria. Tutaondokana na ile hali ya kufanya mambo *manually*. Kwa hiyo, niipongeze sana Serikali kwa hatua hiyo na nasema kwamba naunga mkono sana.

Mheshimiwa Spika, vilevile ukiangalia hii sheria inakwenda kwenye eneo la ugavi, Serikali inakuwa na mali ambazo ni chakavu kama magari na bidhaa mbalimbali. Kwa hiyo, sasa namna ya kuziondoa zile kuzipeleka ilikuwa na urasimu sana, kwa sababu mwongozo wa kisheria haukukaa vizuri. Kwa hiyo sasa hili, inakwenda kurekebisha hiyo hali na kuhakikisha kwamba kunakuwa na ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache, nitamke kwamba naunga mkono hoja na niwashawishi Wabunge wote tuweze kuiunga mkono sheria hii ili iweze kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa majukumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Kwagilwa Reuben Nhamanilo, atafuatiwa na Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha na Mheshimiwa Halima James Mdee, ajiandae.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nipate kuchangia Sheria ya Ununuzi ya Umma ya mwaka 2023. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa dhamira na nia ya dhati ya kuhakikisha fedha za Watanzania zinapokwenda kwenye manunuzi zinatumika kwa usahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sheria hii ya Ununuzi, Bunge lako limeipigia kelele kwa miaka mingi sana. Sheria hii ya Ununuzi, ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa hesabu ya Serikali, imekuwa ikitoa msisitizo jinsi ambavyo ilivyo na madhaifu. Hakuwepo mtu miaka yote wa kusikiliza na kulibeba jambo hili kwa udhati kama ambavyo Mheshimiwa Rais, amefanya sasa. Kkwa hiyo ni vyema Watanzania wakafahamu aina ya Rais tuliyenaye na dhamira aliyonayo kwa maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye maeneo haya 12 ya sheria hii tunayoiandika upya, nitachangia maeneo mawili, eneo la pili na eneo la saba. Eneo la pili linaweka Idara ya Sera ya Ununuzi wa Umma. Amezungumza Mheshimiwa Kimei, kutangulia kusema kwamba tunaanzisha idara hii lakini bahati mbaya iliyopo ni kwamba hatuna Sera ya Taifa ya Ununuzi wa Umma. Kwa sababu ya umuhimu wenyewe wa jambo lenyewe, ndiyo maana tumefikia hapa kwamba ni lazima tuwe na sheria, wakati wenzetu wa Serikali wakiandaa sera.

Mheshimiwa Spika, utaratibu ulipaswa uwe ianze sera, tutunge sheria halafu ndiyo mambo mengine ya mikakati na kanuni yaendelee. Nitumie nafasi hii kuiomba Serikali kufanya haraka iwezekanavyo kukamilisha mchakato wa utungaji wa sera ya manunuzi ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uwepo wa sera utatusaidia kuwa na maelekezo mahususi kwenye mambo ya manunuzi yanayogusa uadilifu, ufanisi, ushirikishwaji, mikakati ya kukuza makampuni yetu ya wazawa wa ndani kwenye manunuzi. Vilevile, matumizi ya rasilimali zetu za ndani yanapokuja manunuzi kwenye uzalishaji pamoja na mambo ya utawala bora na kuondoa migongano ya kimaslahi kwenye manunuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri pekee tuliyonayo ni kwamba wenzetu wa Wizara ya Fedha pamoja na kutokuwepo na sera wamejaribu sana kuyagusa maneno haya niliyoyataja. Mambo ya uadillifu, mambo ya ufanisi, yote tumeyagusa kwenye sheria hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ambalo ningependa nichangie ni ile sehemu ya saba ya Muswada tulionao mezani, ambayo ni usimamizi wa mikataba. Eneo hili kwa kiasi kikubwa linazungumzia wajibu wa kusimamia utekelezaji wa mikataba. Sasa kwa sababu jambo hili linahusisha sekta kubwa kwa nafasi kubwa, linahusisha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mambo ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali tusingeweza kuyaandika kwenye Sheria hii ni vema sasa wakati tukiangalia wajibu na usimamiaji wa utekelezaji wa mikataba ni vema kuona umuhimu wa kuiwezesha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa sababu sheria ya manunuzi haikamiliki bila kuwa na mikataba. Kwa hiyo, lazima kuiboresha sana Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuiwezesha kibajeti, kusomesha vijana wetu, wataalam. Vilevile, kuisimamia kwa ukaribu kama Bunge.

Mheshimiwa Spika, nitatoa mifano ambayo Sheria za Manunuzi zinatupeleka kwenye mikataba ambayo mikataba hiyo tukishindwa kuifuata au Ofisi ya Mwanasheria Mkuu isipopewa nafasi ya kuisimamia, mikataba hiyo inaingizia hasara Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitatoa mifano ya mikataba mitano maarufu kwenye nchi yetu . Mkataba wa kwanza ambao ulitokana Sheria ya Manunuzi iliyopita ulikuwa kati ya *Heritage Rukwa Tanzania Limited* wakiwashtaki *TPDC* pamoja na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kukiuka mkataba wa uwekezaji jambo ambalo lilisababisha maamuzi yake Serikali ilitakiwa kulipa dola milioni 72.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana nasisitiza kuiboresha na kuiwezesha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, kama tunataka Sheria hii tunayoitunga ikafanye kazi hii kwa usahihi na hizi asilimia 70 za mapato yetu yote na makusanyo tunayopeleka kwenye manunuzi zikasimamie vizuri, lazima ofisi hii tuiwezeshe kibajeti iwe na wataalam wa kutosha. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo, nitumie fursa hii kuipongeza Ofisi ya Mwanasheria Mkuu pamoja na kwamba

wapo watu wanabeza Wanasheria wetu huko nje, wapo watu wanaobeza Ofisi hii ya Mwanasheria Mkuu, ninataka niwaambie kwenye kesi hii Ofisi yetu ya Mwanasheria Mkuu ilisimama na kushiriki kesi pamoja na majadiliano na kuokoa kiasi chote hiki cha fedha ambacho ilikuwa tukilipe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mfano wa mkataba wa pili, ambao ulisababisha nchi yetu kushitakiwa, ili tuone umuhimu kwamba Sheria hii ya Manunuzi haikamiliki bila mikataba na sehemu pekee ya kuisimiamia mikataba ni Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Shauri Namba *ICSID* kesi Namba *ARB1733* kati ya *Eco Energy* akiishitaki Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kosa lipi, kwa kosa la kukiuka mkataba wa kulinda uwekezaji, angalieni hiki Waheshimiwa Wabunge pamoja na Watanzania wanaonisikiliza hapa kukiuka mikataba. Unajua kuna watu wanafika mahala wanaona tu kunaweza tu kukawa na mkataba na mtu akaamua tu akalala akaamka amekiuka, *it is not that way!* Haiwi hivyo, mikataba ina taratibu zake siyo habari tu ya kuamka, mtu ametoa tamko kwamba futa mkataba.

Mheshimiwa Spika, kesi kati ya *Eco Energy* na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kukiuka mkataba wa kulinda uwekezaji, kampuni moja ya Uswisi, baada ya mashtakiano Serikali ilikuwa inadaiwa, ilitakiwa ilipwe dola milioni 166 zote hizi ni fedha, ndio maana nasema Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, kama kweli haya manunuzi na sheria tunayotunga tunataka ifanye kazi lazima tuisimamie na kuiwezesha iweze kusimamia haya mambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, dola milioni 166 na hapa naipongeza tena Ofisi ya Mwansheria Mkuu wa Serikali kwa mara ya pili kwa kupambana sana na kuhakikisha tumeokoa dola karibia milioni 37 kwenye hili shauri. Yote hii iliyotupeleka ni Sheria ile ya Manunuzi ya zamani. Ndiyo maana nikasema Rais, pekee Mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ameliona hili ni tatizo na ameamua kuleta Muswada hapa wa kuandika upya Sheria hii ya Manunuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mkataba wa tatu uliovunjwa na ambao ulituingiza kwenye matatizo, mkataba wenye shauri namba *ICC*

kesi Namba *22261/TO* hii ni ya *Symbion Power Limited* wakiwashtaki *TANESCO,* kwa nini wamevunja mkataba wa uwekezaji wa umeme hii ni *power purchase agreement*. Madai ya dola milioni 355. Sikilizeni niwaambie haya mambo yalikuwepo toka zamani, Bunge limepiga kelele toka zamani, ripoti ya *CAG* imeandika toka zamani na sisi tumeonge hapa toka zamani hizo, lakini sheria ilibaki vilevile, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, mwenye kuona uchungu wa mambo haya ameleta Muswada wa Sheria hapa iandikwe upya, halafu anatokeaje Mtanzania anakuwa na mashaka na Rais huyu?

Mheshimiwa Spika, kwenye usimamizi wa rasilimali za nchi yetu, ataokeaje mtu anakuwa na mashaka na Rais huyu. Kesi ile Ofisi ya Mwanasheria Mkuu niipongeze tena, wamepambana natukaokoa katika dola ambazo tulitakiwa tulipe milioni 355, tumeokoa dola millioni 202, *so these people are doing their job, last time* walikuja hapa wanomba milioni 300 tu tuwaongeze, lakini haikuwezekana *this is very sad*. Mheshimiwa Waziri wa Fedha tunaomba sana kwenye *Mid - Year Budget Review* ya Mwezi wa 12 pamoja na mambo mengine yatakayoletwa Bungeni, Serikali mlete namna ya kuiwezesha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, kitengo kinachosimamia mikataba, ikafanye kazi ya Watazania.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mfano wa mkataba wa nne, shauri Namba *ICC Arbitration Award 15947/VRO* hii ni kati ya *Dowans Holding*, haya kampuni yote ninayoyataja ni maarufu, mnayajua vizuri na sarakasi zote. *Dowans Holding SA Tanzania Limited,* wote hawa kwa pamoja wanaishitaki *TANESCO*. Shauri ambalo iliamuliwa tulipe dola millioni 77. Ofisi yetu ya Mwansheria Mkuu, wamepambana kwenye hizo tumekoa dola milioni 25, lakini mashtaka haya yote mnayoyaona Mheshimiwa Rais , amefika mahala akona hakuna namna zaidi ya kuandika sheria upya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kesi na mfano wa mwisho, *Mohamed Abdulmohsin Al-kharafi and Sons, General Trading, General Contructing and Industrial Stucture WLL,* watu wa Kuwait, walishitaki Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na Wizara ya Kazi lakini na Wakala wa Barabrara Tanzania na tulihukumiwa kulipa dola milioni 30.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, ahsante sana, kengele ya pili imeshagonga.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha, atafuatiwa na Mheshimiwa Halima James Mdee, Mheshimiwa Mhandisi Mwanaisha Ng'azi Ulenge, ajiandae.

**MHE. SHAMSI VUAI NAHODHA:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kutumia nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kutoa mchango wangu. Mimi ni Mjumbe wa Kamati yako ya Bajeti, tumeupitia Muswada ulio mbele yetu kadri ya uwezo wetu, hata hivyo nina maoni katika maeneo machache.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu inatumia zaidi ya asilimia sabini ya fedha za bajeti katika masuala ya manunuzi na ugavi, kusema kweli hiki ni kiwango kikubwa sana cha fedha, kwa mantiki hiyo basi Waheshimiwa Wabunge tunao wajibu wa kutunga sheria iliyo madhubuti ili tuweze kuthibiti vitendo mbalimbali vya rushwa na ukosefu wa maadili.

Mheshimiwa Spika, suala la kuwa na sheria nzuri ni jambo moja na suala la kuwa na sheria inayotekelezeka ni jambo jingine. Ili tuweze kuisimamia sheria hii ipasavyo ninapendekeza Serikali ifanye mambo manne. Jambo la kwanza, Serikali inapaswa kuteua watendaji walio makini na wenye weledi, wenye ujuzi wa kusimamia na kuongoza sekta wanazozisimamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile tunahitaji kuwa na watendaji na viongozi wenye hekima, wenye, busara na wenye ujasiri wa kufanya maamuzi magumu. Kwa nini ninayasema haya, nasema haya kwa sababu upo utamaduni ambao tumeuzoea ambao siyo mzuri sisi Watanzania, anapotokea mtendaji au kiongozi akapitisha mradi kwa haraka anatuhumiwa rushwa, anaposhindwa kutekeleza kwa wakati pia tunamtuhumu rushwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa usipokuwa makini unashindwa kujua ufanye kipi kati ya haya mawili. Ucheleweshe ili usituhumiwe rushwa au utekeleze kwa haraka utuhumiwe rushwa. Sasa kwa maoni yangu tunahitaji watu walio makini na ujasiri ili wafanye maamuzi yenye maslahi mkubwa na Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, nimezungumzia suala la kuwa na watendaji wenye weledi , napendekeza tuwapeleke watendaji , viongozi wanoongoza mashirika hasa ya kibiashara, tuwapeleke nchi za nje wakajifunze uongozi, wakajifunze utamaduni wa kusimamia na kuendesha mashirika haya kibiashara. Nalisema hili kwa sababu mwaka 1978, aliyekuwa Rais wa China wakati ule marehemu Deng Xiaoping aliwapeleka vijana wa Kichina Marekani wapatao laki moja.

Mheshimiwa Spika, matokeo yake leo tunayaona, China leo wana makampuni yenye uwezo mkubwa sana, wana mashirika ya Serikali yenye uwezo mkubwa sana na wakati hizi kampuni hizi za ujenzi tunazoziona zinakuja katika nchi yetu, kutekeleza *tender* mbalimbali haya ni makampuni ya Serikali, ninatamani na nchi yangu ifikie huko.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu ninaishauri Serikali ianzishe Mfuko Maalumu wa Wawekezaji na Wazalishaji wa Ndani. Hivi sasa tuna mifuko midogo midogo ipatayo 30 Serikalini, ambayo ukiuliza utaambiwa yote inatoa misaada na fedha kwa ajili ya uwekezaji na wajasiriamali wadogo wadogo. Kwa maoni yangu nafikiri hali ya kusimamia miradi mingi kiasi hiki, usimamizi wake unakuwa mgumu sana. Kwa hiyo, napendekeza Serikali iunganishe Mifuko hii yote midogo midogo ili tuwe na mfuko moja imara wenye uwezo wa kutoa misaada na fedha kwa wawekezaji wa Tanzania na vijana ambao wana mawazo mazuri ya kibiashara ili watekeleze miradi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la nne, nashauri wawekezaji wa ndani waunganne ili tuwe na kampuni moja yenye nguvu. Kwa nini ninasema hili? Ukiangalia makapuni yanayokuja kuwekeza katika nchi yetu, wanao uwezo mkubwa sana wa mtaji, wana uwezo mkubwa sana wa teknolojia, kwa kusema kweli kama wawekezaji wa ndani kama hawakuungana pamoja hawawezi

kushindana na makampuni yenye uwezo mkubwa kiasi hiki. Wakati mwingine makumpuni haya yanapata msaada mkubwa sana kutoka Serikali zao. Kwa hiyo, njia pekee ni kuungana tu, kama Waswahili wasemavyo umoja ni nguvu utengano ni udhaifu.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, tusipofanya hivyo tutaendelea tu kulalamika kwamba Watanzania wawekezaji wa ndani hawapewi msaada unaostahiki na baada ya mwaka moja nina hakika, tutarudi hapa kusema Sheria hii mpya ya Manunuzi ina kasoro ina udhaifu, kumbe tatizo si sheria, tatizo ni weledi, tatizo ni maadili, tatizo ni utashi wa kusimamia yale tunayoyapanga, ndiyo maana nasema sheria nzuri tunaipitisha lakini tuende zaidi kuliko sheria ilivyo, vinginevyo tutaendelea tu kulalamika kwamba sheria haitekelezwi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja na nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimwa Halima James Mdee, atafuatiwa na Mheshimiwa Mhandisi Mwanaisha Ng'anzi Ulenge, Mheshimiwa Erick James Shigongo, ajiandae.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru.

Mheshimiwa Spika, Sheria hii tukipitisha leo maana yake tunaachana na Sheria ya Ununuzi wa Umma Namba 7 ya mwaka 2011, kama ilivyorekebishwa mwaka 2016 na Kanuni zake za mwaka 2013, kama zilivyorekebishwa mwaka 2016. Nimeanza haya na ukiongezea pale ambapo Mheshimwa Nahodha amemalizia kwa kuonesha kwamba kulikuwa na sheria ambayo tunayo sasa, hii sheria haikuwa mbaya yote ndiyo maana mara ya mwisho tumeifanyia marekebisho 2016 ambayo ni kama miaka Saba hivi iliyopita.

Mheshimwa Spika, changamoto kubwa tuliyonayo ni kuwa na watu wenye weledi, watu wenye uzalendo, watu wanopenda Taifa lao, kutekeleza wajibu waliopewa kuutekeleza kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nini ninasema hivi? Nashukuru wachangiaji wote waliopita wameelezea changamoto ambazo tumetoka nazo. Ukisoma ripoti zote za Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali za mwaka huu, ama miaka miwili ama mitatu iliyopita, nitatoa mfano wa mwaka huu ambao chimbuko lake ni matokeo ya tulikotoka.

Mheshimiwa Spika, kuna eneo maalumu linalohusu usimamizi wa manunuzi na mikataba. Kwa Serikali za Mitaa peke yake, eneo hili lina gharama ya shilingi bilioni 100.4. Serikali za Mitaa peke yake. Kwa mujibu wa Bajeti ya Serikali za Mitaa zenyewe mtanielewa, kama kwenye shilingi bilioni 600 au 700, shilingi bilioni 100 inahusu eneo la manunuzi, *challenge* ni kubwa. Ripoti ya Mashirika ya Umma iliyotoka sasa hivi, eneo la mikataba na manunuzi ni shilingi bilioni 600. Ukija Serikali Kuu ambayo ndiyo tunaiita baba lao, eneo la mikataba na manunuzi ni shilingi trilioni 8.12. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nini nimesema hivi? Katika hii shilingi trilioni nane, shilingi trilioni 3.4 ni madeni ya wazabuni. Sasa tuje kwenye kanuni tulizonazo tuone zinasema nini? Kanuni ya 44.1 ya Kanuni ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2013, inaeleza, "kwa madhumuni ya kusaidia ukuaji wa makampuni ya ndani na kuwezesha makampuni hayo kutimiza wajibu wao kimkataba, taasisi zinapofanya ununuzi, zitahakikisha kuwa malipo yanafanyika kwa wakati kwa wazabuni." Hii ni Kanuni ya mwaka 2013 ambayo ipo sasa, lakini tunapozungumzia madeni ya wazabuni wanaotoa huduma nchi hii, ni *crisis* kwa miaka nenda miaka rudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nakubaliana na Mheshimiwa Nahodha kwamba tatizo kubwa siyo sheria zetu, tatizo kubwa watekelezaji wa sheria waliopewa jukumu la kufanya hizi sheria ziende kwenye utekelezaji ukoje? Taratibu za zabuni; mikataba ikifanyika; kazi zikifanywa; nani anatakiwa aidhinishe malipo; malipo yanaidhinishwa kwa wakati; hili ndilo tatizo.

Mheshimiwa Spika, tukisema hapa kwamba eti huu ndiyo msahafu utaondoa matatizo na wakati tuna *mentality* ya watumishi wale wale, wenye akili zile zile, wasiotaka kubadilika,

wasiochukuliwa hatua na mamlaka zinazotakiwa ziwachukulie hatua, tutakuja tena. Amesema Mheshimiwa Nahodha, tutakuja tena. Natoa rejea kwa *senior*, tutakuja miaka mitatu ijayo, tutasema eti tubadilishe sheria. Kwa hiyo, *we should change, we must change our mentality*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama tunadhani watu wetu wanahitaji kusaidiwa, wana upungufu, tuwasaidie, tuwajengee uwezo. Kama tunadhani watu wetu wanafanya hujuma za makusudi kwa Serikali na kwa Taifa, tuchukue hatua. Kinyume na hapo, *we are just wasting* muda wa Bunge, tutakuja tutabadilisha tena na tunapoteza rasilimali za Umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, ukubwa wa hili eneo kwa bajeti ya nchi, tuchukulie mfano bajeti za miaka miwili; 2021/2022 katika shilingi trilioni 37, shilingi trilioni 23 zilikuwa za matumizi ya kawaida. Tunaposema matumizi ya kawaida, maana yake unalipa deni la Taifa, unalipa mishahara na matumizi mengine *(other chargers)*. Kwenye mwaka 2021/2022, shilingi trilioni 14.9 zilienda kwenye maendeleo, mwaka 2022/2023, shilingi trilioni 15.06 zilienda kwenye maendeleo.

Mheshimiwa Spika, tunavyozungumzia shughuli za maendeleo, tafsiri yake ni kwamba, tunazungumzia miradi mbalimbali ya ujenzi ama miradi mingine yoyote ile inayohusu manunuzi. Kwa hiyo, tunavyozungumzia asilimia 36 ya bajeti, ninazungumzia kipengele cha maendeleo. Kama huku kwenye matumizi ya kawaida hii asilimia 60 na kitu, ina manunuzi, hilo ni jambo lingine. Mimi nazungumzia *specifically* fedha ambazo zimetengwa kwa ajili ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, hatuwezi kuchukulia shilingi trilioni 15 kimzaha mzaha. Ndiyo maana nakubaliana kabisa na Muswada kama ulivyoletwa awali. Ulisema, Taarifa ya Mwaka ya Tathmini ya Utendaji Kazi wa Ununuzi wa Umma na Thamani Halisi ya Fedha, ikisema kwamba taarifa ikishawasilishwa kwa Rais italetwa Bungeni. Dhumuni ya hili ilikuwa ni nini? Kwa sababu *PPRA* ina majukumu mengi, inafanya chunguzi kubwa. Chunguzi za shilingi trilioni karibu 16. Mwanasheria Mkuu na timu yake kwa busara kubwa wakasema, Rais akishakabidhiwa hiyo ripoti tarehe 30

Machi, mchakato ufanyike kwa Waziri mwenye dhamana kuileta taarifa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, taarifa ikiletwa Bungeni ni Taarifa ya Umma. Wabunge wanajua, tunaweza tukaijadili, tukajua shida ni nini, turekebishe tunachokijua. Namshukuru Mheshimiwa Dkt. Kimei kafunguka, hakujua mimi nilikuwa na*m-note*. Mheshimiwa Waziri umeenda kushawishi Kamati ya Bunge, eti hii ngoma isiletwe kwa sababu ipo kwenye sehemu ya taarifa ya CAG, wakati mnajua Taarifa ya *CAG* inajumuisha mambo mengi! Kwa hili akalizungumza kwa ufupisho, *(in summary form),* Lakini ikiletwa hiyo taarifa yote, tutajua hizi shilingi trilioni karibia 16 ambazo tunapeleka kwenye manunuzi zimeendaje?

Mheshimiwa Spika, licha ya kwamba Kamati ya Bajeti ni Kamati yangu, imenikuza sana, lakini katika hili nitaomba nilete mabadiliko ili nikubaliane na *spirit* ya Serikali. Serikali imesema inataka kuwa wazi, inataka kuonekana, inataka kujinyumbulisha. Sasa tunataka hii *spirit* ya Serikali isiwe iliingia bahati mbaya kwa mkono huu, walivyoona kama vipi, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu alitumwa ama alijituma mwenyewe? Ninaamini kwa sababu *spirit* ilikuwa ni njema, na kwa sababu *CAG* hataainisha mambo kwa mapana yake, na sheria hii imeipa mamlaka makubwa sana *PPRA* ili iweze kufanya udadavuzi wa mambo, nitaleta marekebisho kesho ili hiki kipengele kiweze kurudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naona kengele imelia, nimalizie mambo mawili; hili la mabehewa, kifungu cha 79(1). Ununuzi wa vichwa na mabehewa ya treni ya ndege mitumba. Sawa, inawezekana *spirit* ya ununuzi wa vitu vipya tumeiona ina faida na hasara zake, lakini mashaka yangu, unapozungumiza ndege mtumba, unapozungumzia mabehewa mitumba, tafsiri yake ni kwamba, na hapa bahati mbaya sana tunasema hivi vitu kwa mapana yake vitaelezwa kwenye kanuni ambazo Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana amepewa jukumu la kwenda kuziandaa.

Mheshimiwa Spika, juzi tulikuwa na Kamati hapa ya Kanuni ya Bunge, imelalamika kwa namna gani Bunge linapokwa mamlaka yake kwenye mambo muhimu. Nilikuwa naangalia gharama ya *Airbus* ikiwa mpya, karibia shilingi bilioni 500. Tufanye

mtumba basi kwa ndege moja, labda tufanye shilingi bilioni 200. Uamuzi mmoja wa namna hii una kishindo kikubwa kuliko maamuzi 1,000 ya Serikali zetu za Mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haiwezekani Bunge hili likaruhusu Waziri apewe mamlaka makubwa namna hiyo. Tumejenga reli ya *SGR* kwa mikopo, kwa *trillions of money,* halafu tunaruhusu mtu aje mwenyewe kivyake vyake kwa kanuni zake akatuelekeze namna ya kununua mitumba. Hapana. Tukubaliane mitumba itakuwaje humu humu ili tukishajua mitumba itakuwaje, tumwambie akatekeleze mitumba yetu. Sio tumruhusu yeye akajichimbie kule, ukizingatia taarifa iliyoelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, naenda pamoja na kifungu cha 128. Maeneo 28 ya sheria hii muhimu amepewa Waziri akatunge kanuni. Haiwezekani. *Otherwise* tukubaliane kwamba akitunga hizo kanuni zake, alete kwenye Kamati ya Bunge ya Bajeti *plus* Kamati ya Bunge ya Sheria Ndogo, kabla hazijafanya chochote. Kama ndiyo tumeamua maeneo 28 muhimu ya sheria hii muhimu tumpe Mheshimiwa rafiki yangu, kaka yangu Dkt. Mwigulu akatungie kanuni, kwa mambo nyeti, tusifanye chochote paka ziende Kamati ya Bajeti na Kamati ya Sheriia Ndogo, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Kimei naona umesimama.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, nampa taarifa kwamba kama ilivyosomwa kwenye Taarifa yetu ya Kamati, hizo kanuni tumependekeza ziletwe kwenye Kamati tuzipitie tena tuone kama zimekidhi matakwa yetu. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Taarifa ya Kamati kweli ninayo na mimi hapa, nimepaona. Ukurasa wa 40, inasema kwamba kanuni ziletwe hapa ndani. Nilikusudia kutoa huo ufafanuzi baadaye kuliko kuutoa sasa wakati michango inaendelea. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Mhandisi Mwanaisha Ng'anzi Ulenge, atafuatiwa na Mheshimiwa….

Ah, naona muda wetu utakuwa hauruhusu, wengine watachangia mchana. Mheshimiwa Mhandisi Mwanaisha Ng'anzi Ulenge atafuatiwa na Mheshimiwa Zainab Athman Katimba.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi ya kuchangia. Awali ya yote, niendelee kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mahali hapa kwa ajili ya kuchangia Muswada huu wa Sheria ya Manunuzi ya Umma.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Kamati, imefanya kazi nzuri na kubwa ya kuchambua Muswada huu. Vilevile naipongeza Serikali kwa dhamira yake nzuri na njema ya kuhakikisha manunuzi ya umma yanaleta thamani kwenye jamii na kuhakikisha miradi hiyo inadumu kwa muda unaotakiwa.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze na Ibara ya 75 ya Matumizi ya Rasilimali za Ndani. Kama ambavyo Mheshimiwa Waziri ameelezea, kwamba lengo la kupitia upya sheria hii ni ili kuhakikisha changamoto zilizojitokeza zinakwenda kuboreshwa kwa kupitia sheria hiii mpya ya mwaka 2023.

Mheshimiwa Spika, moja ya kitu ambacho ninaona kabisa kitakwenda kukinza utekelezaji wa sheria hii ni pamoja na kutokufanya *analysis* ya kina kwenye miradi iliyojengwa kwa rasilimali za ndani kwa maana ya *force account*. Hiii ni changamoto kubwa ambayo inapoteza fedha nyingi za umma na *analysis* ya kina kabla ya kuja na sheria hii, haijafanyika.

Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwa sababu gani? Kama kungekuwa kumefanyika tathmini ya kina kuona kiasi gani fedha za umma hazijatumika ipasavyo kwa kutumia *force account,* tusingeruhusu kwenye sheria hii kikomo cha thamani kuwekwa kwenye kanuni. Ilitakiwa sheria iende moja kwa moja izungumze kiwango cha fedha kitakachotumika kwenye *force account*.

Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwa sababu, hata katika sheria iliyopita ilikuwa ni hivyo hivyo, lakini miradi mikubwa mingi imetekelezwa na *force account*. Naomba nitoe mfano hai. Hospitali ya Uhuru, Chamwino imejengwa kwa *force account* na mpaka leo hospitali ile mradi unashindwa kufungwa kwa sababu ya changamoto ambazo zimejitokeza. Ukienda kwenye jengo lile, pale *reception* tu ukifika unaweza ukaiona thamani ya fedha jinsi ilivyofinyangwa katika mradi ule. Yote ni kwa sababu tunaamua kuifinyanga Sheria hii ya Manunuzi ya Umma na kuamua kuweka vipengele vya thamani ya fedha ambavyo vitaweza kutajwa moja kwa moja kumpa mtu fulani mamlaka pekee ya kuweza kuainisha thamani ya fedha. Hii haitaweza kurudisha thamani ya fedha za umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sipingi kabisa matumizi ya *force account* katika nchi yetu, lakini ni ukweli usiopingika, ni lazima tukubaliane na sheria ilivyoelekeza. Naomba niisome Ibara ya 75 sehemu ya pili inasema: "Matumizi ya rasilimali za ndani yatakuwa halali endapo kazi za ujenzi ni ndogo, zimetawanyika na zipo katika maeneo yasiyofikika kwa urahisi kiasi kwamba makandarasi wenye sifa hawawezi kushiriki na kufanya kazi kwa bei nafuu." Je, Uhuru *Hospital*, eneo lile halifikiki? Je, mradi ule ni mdogo? Ni wazi tuliamua kuifinyanga sheria.

Mheshimiwa Spika, vilevile imezungumza kwamba, "*force account* itatumika iwapo Taasisi Nunuzi ina wafanyakazi wenye sifa na vifaa vya kusimamia na kutekeleza kazi za ujenzi zinazohitajika." Leo ni nani asiyefahamu kwenye mamlaka za Serikali za Mitaa hakuna idadi ya waandisi wa kutosha? Hakuna mafundi mchundo wa kutosha? Ni nani hajui? Ni miradi mingi inatekelezwa kule kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kutumia *force account*. Tunaifinyanga sheria.

Mheshimiwa Spika, vile vile, sheria imezungumza wazi kwamba, "matengenezo au ujenzi iwe ni shughuli za kawaida za kila siku za taasisi nunuzi." Angalia ukubwa wa Tawala za Mikoa, angalia ukubwa wa kazi za Serikali za Mitaa. TAMISEMI ina majukumu mengi makubwa, mazito kwa Taifa hili, lakini mnakwenda kuchanganya majukumu yale ambayo kiukweli yanakwenda kusababisha upotevu wa fedha za Serikali.

Wataalamu hawapo, wakati huo huo majukumu ya TAMISEMI ni mengi, lakini bado mnakwenda kutumia nguvu nyingi kwenda kufanya vitu ambavyo vingeweza kufanywa na watu wengine.

Mheshimiwa Spika, vilevile inazungumza kwamba Ibara ya 75(2) kazi za ujenzi zinatakiwa kuelekezwa bila kuvuruga utekelezaji wa shughuli za taasisi zinazoendelea. Sisi ni mashahidi walimu wanaacha kufundisha, madaktari wanaacha kufanya kazi zao za kitaalamu walizoajiriwa nazo wanakwenda kufanya kazi za *force account*, wanakwenda kusimamia miradi. Hakika tunaifinyanga sheria hii. Ni lazima tutengeneze kwenye sheria hii ukomo wa wazi bila kumpa mamlaka mtu mwingine kwa kuhakikisha sheria hii inaenda kutekelezwa ipaswavyo.

Mheshimiwa Spika, naomba kusema kwamba changamoto kubwa ya *force account* ni pale ambapo yule *local* fundi amekabidhi kazi halafu kunatokea upungufu. Zile *defects* ambazo zinakwenda kurekebishwa, zinakwenda kurekebishwa kwa kwa *liability* ya nani, wakati wewe taasisi nunuzi ambaye ni *Local Government* umenunua *material* mwenyewe, umekwenda kusimamia kazi mwenyewe? *Local* fundi unambana vipi kwamba upungufu uliotokea unatokana na yeye? Huku ni kuleta *contradiction* na mambo haya yanapoteza fedha nyingi za umma.

Mheshimiwa Spika, vilevile changamoto nyingine kubwa ya *force account* ni *quality assurance*. Hakuna *test* zinazofanyika katika kudhibiti ubora. Kwa sababu inahitaji *adequate supervision* ya kutosha kwenye miradi ile. Lakini walimu wana kazi zao za kufundisha, madaktari wana kazi zao nyingine na wahandisi na mafundi mchundo ni wachache. Je, hizo *test* zinafanyika vipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jamani naomba niwaambie, tunakokwenda Taifa hili litakosa wataalam makini wa kuweza kufanya kazi za ujenzi nchini. Kwa nini ninasema hivi? Ili mhandisi aweze ku-*qualify* vizuri ni lazima atoke chuoni, baada ya kupita kwenye *practical industrial training*, aende akakae na mkandarasi mwenye miradi mizuri kwa muda kadhaa ili awe *competent*. Ili

asajiriwe kama *Professional Engineer* halafu ndiyo aende akatekeleze miradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama miradi mikubwa inapelekwa kwenye *force account*, hakuna *training* kule. Hakuna chochote kinachoweza kufanyika kumjenga mhandisi *graduate* aliyetoka shuleni. Tunalipeleka wapi Taifa hili katika taaluma hii ya uhandisi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuache kufanya mzaha katika mambo ya msingi. Lazima kuna bodi iliyopewa mamlaka. Iliyotengenezwa kwa ajili ya wakandarasi nchini. Bodi ile ina sajiri, inaajiri na inatumia fedha za umma lakini wakati huo mnazuia *private sector* ku-*excel.* Kwa sababu ya kutokuwa na imani katika ubora wa kazi nyingine ambazo zinafanyika.

Mheshimiwa Spika, kuna watu wanaamini kwamba, miradi inayofanywa na wakandarasi ina gharama kubwa zaidi kuliko *force account*. Sasa tafiti zilizofanywa na Baraza la Ujenzi Tanzania *(National Construction Council)* wakishirikiana na Bodi ya Uhandisi, Bodi ya *Quantity Surveyor* na *Architect* na Bodi ya Wakandarasi nchini; inaonyesha kwamba miradi mingi iliyotekelezwa kwa *force account* imeshindwa kumalizika kwa wakati kwa sababu ya upungufu wa fedha. Makadirio yaliyofanyika hayakukidhi haja ya mradi. Kwa hiyo, miradi mingi imeshindwa kufungika kwa wakati. Hiyo ni kwa mujibu wa tafiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile tukubaliane, hii Ibara ya 75 inazungumzia suala zima la *size* ya mradi. Kwamba mradi ukiwa mdogo, ni wapi imekuwa *well defined* kwamba mradi mdogo ni wa *size* ipi? Yaani unaposema huu mradi ni mdogo au mradi huu ni mkubwa, ni kitu gani kinaelezea ukubwa wa mradi au udogo wa mradi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mradi unaweza ukawa mdogo lakini ile *complexity nature* ya mradi wenyewe, ukasababisha usifanywe *under force account*. Kwa hiyo, tunaposema *size* ya mradi ni lazima tu-*clarify well*, tu-*evaluate well size* ya mradi huu. *Otherwise*, tunaendelea kufinyanga fedha za Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, ni muda mrefu ninasikitika, nchi hii tumewahi kupita kwenye kufanya kazi kwa *force account* lakini baadaye *analysis* zikafanyika, zikaonekana tutoke huko tufanye *under contract basis*. Ajabu tumerudi tena kupoteza fedha nyingi za umma kwenye miradi isiyokamilika kwa wakatim kwenye miradi isiyofikia viwango vinanyofanyika hali inaumiza, inasikitisha.. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hakika sheria hii ikatekelezwe ipasavyo na *size* ya mradi inayotumika kwenye *force account* iwekwe wazi kwenye sheria hii. Asipewe mtu mamlaka ya kwenda kutengeneza kanuni ili kuhakikisha tunakwenda kutumia fedha za umma kama ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naona unaniangalia. Ninakushukuru. Ninaomba niunge mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kuna baadhi ya Wabunge nilikuwa nimewataja hapa lakini kwa sababu ya muda wetu watachangia jioni tutakaporejea hapa; yuko Mheshimiwa Zainab Athman Katimba, Mheshimiwa Eric James Shigongo, Mheshimiwa Elibariki Immanuel Kingu na wengine tutawataja kwa kadri muda utakavyokwenda.

Ufafanuzi kidogo halafu tangazo la wageni walioingia baada ya tangazo la wageni lililopita.

Kwanza ni hii hoja ya kanuni, kanuni kuletwa Bungeni kabla hazijaanza kutumia. Lilisemwa jana na Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria Ndogo, alisema kwamba wakati mwingine kanuni zinatengenezwa kwa namna ambayo ni kama inapoka madaraka ya Bunge. Kwa hiyo, Kamati iliona ni muhimu; aidha ni Kamati ama ni baada ya michango ya Waheshimiwa Wabunge, ndiyo akatoa yale maelezo aliyoyasema ambayo hayana tofauti sana na kile ambacho kimeletwa leo na Kamati yetu ya Bunge ya Bajeti.

Kamati yetu ya Bunge ya Bajeti kwenye taarifa yake inasema kwenye ukurasa wa 40, Kamati inapendekeza kabla ya

kuanza kutumika kwa sheria mpya, kanuni zitakazotungwa kupitia sheria hiyo ziwasilishwe kwenye kamati. Lengo ni kuhakikisha kanuni hizo zimezingatia mapendekezo ya Kamati wakati wa Majadiliano na Serikali.

Vilevile kuzichambua na kuona kama zinaakisi maboresho yaliyofanyika. Waheshimiwa Wabunge, kwanza kazi ya uchambuzi wa kanuni na sheria ndogo zote ni Kamati yetu ya Sheria Ndogo. *(Makofi)*

La pili, Bunge likishakasimu madaraka kwa chombo fulani, kwa Waziri, yaani kwa chombo chochote ambacho sheria yetu imesema kanuni zitatungwa na Waziri ama na chombo chochote ni kwamba tumekasimu hayo madaraka. Sasa hatuwezi sisi tena tukaingia kuwa watungaji wa kanuni, ndiyo utaratibu ulivyo. *(Makofi)*

Hatuwezi sisi tena tukaanza kutunga wenyewe kanuni na sheria ndogo. Wale tuliowakasimu ndiyo wanaokwenda kutengeneza. Tunachofanya sisi kupitia Kamati yetu ya Sheria Ndogo ni kujiridhisha kama wale ambao tumekasimu madaraka yetu kwao, wanafanya kulingana na yale madaraka waliyopewa kwa mujibu wa sheria tulizozitunga.

Maana yake ni nini, sheria kama hii, kama tunaona kuna mahali ambapo tunapaswa tuseme sisi na tusikasimu madaraka hayo, tunapaswa kufanya hivyo. Tukishatunga sisi sheria, hatuwezi tena wenyewe tuliokasimu kufanya hiyo kazi. *(Makofi)*

Maana yake ni kwamba Waheshimiwa Wabunge tunapotunga sheria, chochote tunachoona hakipaswi kukasimiwa madaraka kwa mtu mwingine ya kutunga kanuni ama sheria ndogo, tusiruhusu. Tukisharuhusu hakuna mahali ambapo kama Spika nitaanza kuwaambia walete kanuni tuzipitie kabla hazijaanza kufanya kazi Tutakuwa tunatunga wenyewe tena. Kwa hiyo, hatujakasimu hayo madaraka. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tutumie muda wetu vizuri ule wa kutunga sheria. Tujiridhishe yale tunayokasimu, ndiyo tunayotaka kukasimu na yale

ambayo tunaona haya hatuwezi kukasimu basi tuyatungie sheria badala ya kupeleka kwenye kanuni. *(Makofi)*

Huo ndiyo utaratibu wa kikatiba na kisheria wa namna ya utungaji wa sheria. Baada ya kusema hilo, Waheshimiwa Wabunge, jambo moja lingine ambalo nilitaka kuzungumza ni la Serikali. Kwa sababu, limezungumzwa sana ili jambo la mafuta na changamoto tunazozipitia. Nitumie fursa hii, pamoja na kwamba nilishampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na ambaye pia ni Waziri wa Nishati na kumtakia kheri katika majukumu yake. *(Makofi)*

Hili jambo wameshaanza kulifanyia kazi, lakini nafikiri ni wakati muafaka. Kwa sababu kabla ya kuweka mfumo wa ununuzi wa mafuta kwa pamoja, tulikuwa na mfumo mwingine. Tuliziona changamoto zake na tulipoenda kwenye huu mfumo, pia una changamoto zake.

Ninafikiri ni wakati muafaka kwa Serikali kufanya tathmini maalum kwa ajili ya huu mfumo mpya wa uagizaji mafuta. Kwa sababu, haiwezekani mafuta yawe yanakuwepo wiki mbili, wiki mbili zingine lazima tuanze kutafutana, halafu bei ikitangatwa tu mafuta yanaanza kuwepo. Sasa kama huu mfumo unatupelekea kwenye changamoto nyingi zaidi kuliko ule wa kwanza, basi tuangalie namna ya kuboresha ule uliokuwepo zamani. *(Makofi)*

Kama pia huu uliopo kuna mianya pengine tumeiachia, basi nafikiri ikifanywa hiyo tathmini itatuelekeza hiyo mianya iko wapi ili tuizibe. Tusifike mahali ambapo tunaanza kuona foleni, halafu ghafla foleni zinaondoka bei mpya zikishatangazwa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nafikiri tunaweza kufika hiyo sehemu nzuri, Serikali ikifanya hiyo tathmini itasaidia upande wenu kwa namna ya utendaji. Pia, itatusaidia na sisi Wabunge kuona wapi ambapo tunaweza kusaidia kwenye kiisimamia Serikali. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo, Waheshimiwa Wabunge, matangazo ya wageni walioingia baada ya wale waliopata nafasi asubuhi kutoka humu Bungeni.

Tutaanza na wageni walioko Jukwaa la Spika, na hawa ni wageni wangu ambao kwa ujumla wake ni wageni kutoka Jukwaa la Wahariri Tanzania *(TEF)*. Wale ambao wamekaa Jukwaa la Spika ni Kamati ya Utendaji ya Jukwaa la Wahariri Tanzania wakiongozwa na Mwenyekiti wa jukwaa hilo Ndugu Deodatus Balile, karibuni sana viongozi wetu, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo sasa na wajumbe wengine wa Jukwaa hili la Wahariri Tanzania ambao hawakupata nafasi kwenye Jukwaa la Spika, nao wote wasimame kwa pamoja, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tunao wageni saba wa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini, Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 32 wa Mheshimiwa Yahya Mhata ambao ni Madiwani na Wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Wilaya ya Nanyumbu, Mkoa wa Mtwara, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni 112 wa Mheshimiwa Lucy Mayenga, hawa ni Wenyeviti na Makatibu wa Umoja wa Wanawake Tanzania, Wilaya ya Kahama, Mkoa wa Shinyanga, karibuni sana Bungeni. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni saba wa Mheshimiwa Michael Mwakamo, ambao ni Watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha, Mkoa wa Pwani, karibuni sana. *(Makofi)*

Pia tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Dkt. John Pallangyo ambao ni Viongozi wa Chama cha Mapindizi kutoka Usa River Wilaya ya Meru, Jijini Arusha, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu muda wetu umekwenda, Mheshimiwa Sophia Mwakagenda nitampa nafasi Mwongozo wake nitausikiliza tutakaporejea jioni leo.

Baada ya kusema hayo, ninasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni leo. *(Makofi)*

*(Saa 7.14 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Ununuzi wa Umma wa Mwaka 2023

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano, Mheshimiwa Eric James Shigongo, atafuatiwa na Mheshimiwa Elibariki Immanuel Kingu, Mheshimiwa Zainab Athman Katimba ajiandae.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Spika, naomba kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi ya kipekee mchana huu wa leo kuwa mzungumzaji wa kwanza kwenye mjadala huu wa Sheria ya Ununuzi.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Kamati kwa kazi nzuri ambayo wameifanya ya kupitia sheria hii na kufanya mabadiliko ya muhimu kabisa ambayo mimi nimeyaona.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu sana nimekuwa nikilalamika kuhusiana na Sheria ya Ununuzi, kwamba sheria hii

imetumika sana kuwafanya Watanzania washindwe kuwa na kasi ya kukua kiuchumi. Nilikuwa na mjadala mrefu sana na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, baadaye nikapata mjadala mrefu sana na Mkurugenzi wa Sheria wa Bunge, baadaye nikapata nafasi ya kukutana na watu wa *PPRA* kujadiliana kuhusu sheria hii.

Mheshimiwa Spika, najua waliokuwepo kwenye Kamati ya Viwanda na Biashara watakumbuka kwamba nimewahi kuzungumzia huko nyuma ya kwamba iko sababu ya kuzipitia baadhi ya sheria zetu ili ziweze kutengeneza mazingira ya Watanzania kushikilia uchumi wa nchi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Taifa hili ni tajiri sana, nimeshazungumza na leo nasema na kesho nitasema na wiki ijayo nitasema, Taifa hili ni tajiri sana; kwa historia ndogo tu; Pato la Taifa letu ndani ya miaka miwili ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan limeongezeka kwa takribani dola za Kimarekani bilioni 20, ndani ya miaka miwili. Hii ni ishara ya kwamba Taifa hili likitumika vizuri hakika hakuna sababu ya Watanzania kuendelea kuwa maskini, lakini tunazo changamoto kubwa sana za sheria zetu.

Mheshimiwa Spika, sheria zetu mara nyingi zimefanya ukuaji wetu uwe kidogo kidogo au utajiri wetu usionekane kwenye maisha yetu. Nchi tajiri lakini watu wake wanakuwa maskini na hii ni kwa sababu ya sheria ambazo tumezitunga. Sasa najisikia mwenye bahati sana leo kupata nafasi ya kushiriki kutunga upya Sheria hii ya Ununuzi. Kwa utajiri tulionao hatutakiwi kuwa jinsi tulivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa naelewa nia ya Rais wetu ambayo ni kuona nchi hii tunapiga hatua kwa kasi, kuona Watanzania vijana wa nchi hii wanafanikiwa kushikilia uchumi wa nchi, ndiyo nia ya Rais wetu. Hili lengo haliwezi likatimia kama hatujapitia sheria kama hii ya ununuzi. Kuna msemo unasema *no one gets rich until the government decides* (hakuna mtu anaweza kutajirika mpaka Serikali yake iamue) kwa kutengeneza mazingira ya mtu kufanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimewahi kuzungumza nyuma na ninarudia tena, miaka 15 iliyopita hapakuwa na bilionea hata mmoja kwenye *list* ya mabilionea duniani, na katika *list* ya mamilionea 500 wa dunia hapakuwa na Mchina hata mmoja, lakini Rais wa China aliamua miaka 10 iliyopita kwamba nataka niweke watu wangu kwenye hiyo *list*. Leo ninavyozungumza nusu ya ile *list* ni Wachina kwa sababu nchi iliamua kuwafanya watu wake watajirike.

Mheshimiwa Spika, ongelea *Huawei, WeChat, Oppo,* kampuni zote za Kichina ambazo zimefanya vizuri kwa sababu nchi iliamua. Sasa kazi yetu kama Bunge ni kutunga sheria ili Serikali iendeshwe kwa sheria hizo. Nataka niseme kwa nia moja thabiti ya kwamba lazima kama Bunge na kama nchi tuamue kwamba tunataka vijana wetu wafanikiwe na washikilie uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Spika, vijana wetu wamechoka kutazama, wanakuja watu hapa kutoka nchi mbalimbali, sheria zetu zinaruhusu, wanafanya biashara na baada ya miaka mitano wakishakuwa mabilionea wanaenda kwenye mitandao wanaanza ku-*brag* kwamba *I came to your country, I earn a lot of money,* nawafahamu watu, ni marafiki zangu kabisa, ametoka nje amekuja Tanzania ame-*tender* vitabu vya shule ya sekondari halafu baadae ananipigia simu ananiambia nimekushinda kwenye ile *tender,* ananicheka, kwa sababu ya sheria zetu.

Mheshimiwa Spika, tumesaini mkataba hapa wa *African Continental Free Trade,* mkataba mzuri tu wa kufanya Afrika iwe soko moja. Mimi nilikuwepo na rafiki yangu Mheshimiwa Mkumbo alikuwepo, tukapitisha ile sheria lakini unajua ya kwamba kwa sheria hii tusipowalinda watu wetu, tutaenda kuua viwanda vyetu. Hivi tunajua kwamba tusipowalinda watu wetu kwa sheria hii tuliyosaini sisi wenyewe tunaenda kuua biashara za watoto wetu. Nilikuwepo kwenye Kamati na Mheshimiwa Mkumbo shahidi, nilisema napitisha sheria hii lakini naomba watu wetu walindwe. Atakumbuka na hata leo narudia, kwa sheria hii tuliyosaini kama hatuwezi kuwa-*protect* watu wetu tutaua biashara za watu wetu na tutawatia umaskini watu wetu. Ni sheria nzuri tu, lakini hakuna nchi isiyowalinda watu wao, haipo. Nakumbuka niliwahi

kuzungumza mtu mmoja akaniambia *protection is over,* kwamba mambo ya kulinda watu yalishapita, hapana, kila nchi inalinda watu wake na inasaidia watu wake waweze kukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumetunga Sheria ya Uwekezaji nzuri tu, nilikuwepo kwenye Kamati ya Viwanda, tumetunga sheria nzuri kabisa na tunawapa wawekezaji *incentives* nyingi waje nyumbani wawekeze. Sipingi *foreign direct investment* hata kidogo, sikatai. Nataka mitaji ije waanzishe biashara watu ili wetu waajiriwe, lakini bado naomba tuwalinde watu wetu kwa sheria zetu. Tusipofanya hivyo tutalaumiwa, watu watafilisika, biashara zitakufa kwa sababu tunawa-*expose* watu wetu kwenye ushindani ambao hawawezi kuuhimili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wanakuja tunawapa *incentives, good,* hamna shida, watu wao tunawapa *incentives* bado wanatudanganya, wanafanya *transfer pricing,* wanatudanyanya mambo mengi wana-*declare loss, they don't pay tax most of them,* huo ndio ukweli. Lakini tunafanya ili kuwasaidia akina Taletale? Tunafanya ili kumsaidia Taletale aweze kukua na kuweza kushindana na hawa wageni wanaokuja? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ununuzi hii ya mwaka 2011 na marekebisho yake yote 12, 13, 14 mpaka 18; naipongeza Kamati ya Bajeti na nimezungumza sana nao mmoja mmoja, nimefanya kazi nzuri, nimeona *preference,* ni upendeleo umewekwa mle. Lakini mimi sina amani na Ibara ya 57. Hii naomba niiseme Ibara ya 57 sina amani nayo kabisa na kama kuna kitu cha kukijadili kwa kirefu leo ni Ibara ya 57.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 57, naomba kwa idhini yako noisome, inasema; "Endapo rasilimali fedha zimetolewa na taasisi ya umma ya Kitanzania pekee, kila ununuzi wa kazi za ujenzi bidhaa na huduma zenye thamani isiyozidi ukomo ulioainishwa kwenye kanuni utatengwa kwa ajili ya watu wa kampuni za ndani." Imetamka hivyo kwamba kitakuwepo kiwango cha fedha kilichotengwa kwa ajili ya kampuni za ndani. Sasa ukienda kwenye kanuni kwa sheria hii tunayobadilisha kiwango kilichowekwa ni bilioni tano. Kampuni ikiwa na bilioni tano inakuwa hiyo *tender* ni *national tender,* ikifika bilioni sita inakuwa

*international tender*, ina maana niki-*tender tender* ya bilioni 10 lazima nitakutana na mchina, nitakutana na mhindi; sasa nitamshindaje kwenye *tender?* Nawezaje kumshinda mtu amekuja hapa na mkopo wa asilimia mbili ilhali mimi nina asilimia 18 za CRDB, inawezekanaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huyu mtu akienda kufanya biashara nje ya nchi anapewa *incentives* ya *20 percent* na nchi yake kwa sababu anakwenda kufanya biashara nje ya nchi. Mimi naweza *tender* nikamshinda huyu, matokeo yake akinishinda bei yake itakuwa ndogo kuliko mimi. Nataka sheria hii imsaidie Mtanzania kushinda kwenye biashara hizi.

Mheshimiwa Spika, mimi niwaombe Waheshimiwa Wabunge, Watanzania wanatutazama, wamechoka kuona utajiri wa nchi yao unaenda nje, wamechoka, wamechoka; tunapitisha bajeti hapa ya trilioni arobaini na kitu wanataka kujua fedha ngapi zinabaki nyumbani? *(Makofi)*

Mheshimwa Spika, tunao uwezo wa kutengeneza mabilionea 10 kila mwaka kwenye taifa hili, tunaweza sisi, kwa mnong'ono wa Taifa, taifa linong'one tu, kwamba biashara fulani bwana tutawapa wakina Kingu, basi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi siwezi kwenda India leo nikapewa kazi ya kuchapa vitabu, ni uongo, hata kama nime-*tender* kuna namna fulani watafanya kazi iende kwa watu wao. Sheria hii hasa kipengele hiki nataka kitamke, kwenye sheria na si kwenye kanuni, kitamke kwamba *limit* iwe angalau bilioni 50 angalau tutoke tano mpaka bilioni 50, hiyo hiyo *national tender,* baada ya hapo twende *international* hapo sawa, baada ya muda tutakua, na sisi tutawafata Wachina huko huko juu kwenye bilioni 60 kwenda juu.

Mheshimiwa Spika, hili si jambo la ajabu, Kenya jirani yetu sheria yake ya ununuzi inatamka kwamba *unit* ya *national tender* ni shilingi za Kenya milioni 500 ambazo ni sawasawa na bilioni 10 za Kitanzania. Wiki iliyopita wamepeleka tena muswada Bungeni wanaipandisha kutoka milioni 500 mpaka bilioni tano ambayo ni sawasawa na bilioni 100 za Kitanzania. Hao ni jirani zetu tu hapo

wamepandisha mpaka bilioni 100 za Kitanzania, hiyo kazi haifanywi na mgeni, wanafanya Wakenya wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ombi langu na ninaomba mnisikilize na Waheshimiwa Wabunge mniunge mkono, hii *limit* ihame kwenye bilioni tano iende angalau kwenye bilioni 50 angalau; hata 100 twende ili tuweze kuwalinda watu wetu waweze kutajirika.

Mheshimiwa Spika, umaskini ni kitu kibaya, hawa watoto wanamaliza vyuo vikuu wanakaa hapa hawana cha kufanya wanauza njugu, halafu anakuja Mchina anauza karanga Kariakoo, hawapendi, tunawafanya wanakuwa na chuki na wageni, tunasababisha *xenophobia* bila sababu ya msingi, tuwape nafasi vijana wetu ili wakue kwa kubadilisha hicho kipengele kwenye sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema haka kakipengele kasipo badilika leo moto utawaka…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge kengele ya pili ilishagonga.

**MHE. ERIC J. SHIGINGO:** Mheshimiwa Spika kwa haya machache naomba kuunga mkono hoja, ahsante kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Elibariki Immanuel Kingu, atafuatiwa na Mheshimiwa Zainab Athman Katimba, mtoa hoja ajiandae.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nakwenda kuzungumza eneo moja na kwa kweli kwa dhati ya moyo wangu niungane na mchangiaji wa mchana pamoja na kaka yangu Shigongo, kwanza kwa kuishukuru sana Serikali na kumpongeza Rais wetu kwa dhamira hii njema ya kuleta mabadiliko katika kuwasaidi Watanzania katika

masuala ya uwekezaji na biashara. Kaka yangu Shigongo alikuwa anazungumza hapa nilikuwa namsikiliza kwa makini sana, amezungumza kwa uchungu sana.

Mheshimiwa Spika, ukisoma Ibara ya 61 inasema; "Baada ya kushaurina na vyombo husika vilivyoanzishwa kisheria, taasisi nunuzi itatenga mikataba itakayotumika kwa lengo la kujenga uwezo wa makampuni ya ndani."

Mheshimiwa Spika, kifungu hiki ukikisoma na ukaendelea mbele kuna mahali zile *sub-article* inasema kwamba; *"A Minister may,"* kwamba Waziri anaweza kutunga kanuni.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe ushauri, kwa alichokuwa anakisema kaka yangu Eric Shigongo nataka nikupe ushahidi, tuna kampuni nyingi sana za Kitanzania zenye uwezo wa kutoa huduma na kazi ambazo ni za msingi na zina uwezo wa kufanywa na kampuni za Kitanzania. Lakini kwa bahati mbaya sana nikiri kwa moyo wangu kuwa baadhi ya wataalam wetu, *technocrats* walioko Serikalini na sizungumzii *technocrats* wote, baadhi ya *technocrats* wetu hawajali maslahi mapana ya kampuni za Kitanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano unaweza ukasema umetangaza kazi, kwa mfano *South Africa* wenzetu kwa hiki hiki kifungu cha 61, wametunga sheria inaitwa *Black Women Procurement Act*. *Black Women Procurement Act* imetoa msisitizo kwa nchi ya *South Africa* mgeni anakuja amepata *contract, sub-contract* inafanywa na mzawa na sheria hii inamlazimisha mgeni huyu kwa miaka miwili anayofanya kazi na mzawa anafanya *technological transfer* mpaka miaka minne inakwisha makampuni yanapata uwezo wa kujitegemea.

Mheshimiwa Spika, nitoe rai, niiombe sana Serikali tusiishie kutunga sheria, tusimamie na kuhakikisha utekelezaji wake unafanyika kule Serikalini kwa wale wanaokwenda kutekeleza kwa sababu inatia uchungu sana Watanzania wanakwenda kwenye *tender* hawashindi, wanafanya hiki lakini hawashindi. Kampuni zote za kigeni zinakuwa zinashinda ilhali kuna vijana wa

Kitanzania wana uwezo wa kutengeneza vitu *local* na vikauzika kwa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tutabaki kwenye Taifa hili kuwasindikiza wageni mpaka lini katika vitu ambavyo wazawa watoto wa Kitanzania wanaweza? Tanayo kampuni hapa zina uwezo wa kutengeneza mifumo ya kisasa, lakini ni nani anawapa nafasi? Tunazo kampuni zina utaalam wa hali ya juu katika fani zote za *IT,* lakini ni nani anawasikiliza? *Any way.*

Mheshimiwa Spika, mimi kwa leo nimesema hilo; naomba kwa kipekee sana nitumie nafasi hii, na utanisamehe sana haliendani na mada hii; nitumie nafasi hii kwa dhati ya moyo wangu kulishukuru sana Bunge la Kenya. Wiki mbili zilizopita Bunge la Kenya lilipeleka taarifa ya utekelezaji wa Wana-*IPU* (Wajumbe wa Bunge la Dunia wa Kenya).

Mheshimiwa Spika, katika Bunge la Kenya, Wakenya majirani zetu wamejipambanua, wamekusemea vizuri sana Mheshimiwa Spika kwenye Bunge lao. Kuna Mbunge ametoa hoja, akalieleza Bunge la Kenya namna ya uwezo alionao Spika wa Tanzania, ndani ya Bunge la Kenya. Hivi ninavyozungumza Kenya Bunge limefanya *adoption* ndani ya Bunge ya kuku-*endorse* wewe kama mgombea wa Bunge la *IPU*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siishii kulipongeza Bunge la Kenya peke yake, ninayapongeza Mabunge yote ya Afrika Mashariki ambayo yalikutana yakaku-*endorse* wewe kama mgombea wa kiti cha Urais wa Bunge la Dunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kama hiyo haitoshi sitapata nafasi nyingine baada ya Bunge hili, tunakwenda kwenye Uchaguzi wa Kiti cha Urais wa Bunge la Dunia.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kwa niaba ya Wabunge wenzangu ambao walituamini kutupeleka kwenye Bunge la *IPU,* kupongeza sana Mabunge yote ya *SADC*. Tulipokutana Arusha kikao kile nchi zote za *SADC* kwa sauti moja zilinyoosha mikono zikaku-*endorse* Dkt. Tulia Ackson kuwa

Mgombea wa Kiti cha Bunge la Dunia hapo mwezi wa 10, Angola. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kama hiyo haitoshi nitumie nafasi hii kuishukuru sana taasisi yetu muhimu na chombo muhimu cha maamuzi cha Afrika *(African Union.)* Katika kikao cha *African Union* kilichokaa Nairobi kimekupitisha na kuku-*endorse* wewe kama mgombea peke yake wa nafasi ya kiti cha dunia katika Bunge la Dunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nisipoyasema maneno haya, tutamaliza Bunge hili hatutakuwa na nafasi ya kuonesha uzalendo uliyooneshwa na Mataifa ya Kiafrika. Nataka nitumie nafasi hii pia kumshukuru sana aliyekuwa Waziri wetu wa Mambo ya Nje, Mheshimiwa Stergomena Tax na Mheshimiwa Rais wetu Mama Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Spika, diplomasia ya Mheshimiwa Dkt Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo tunafanya kampeni nje, tumeona heshima ya Taifa letu imekuwa kubwa, tumeona mapokeo ya Taifa letu yamekuwa makubwa na *In Shaa Allah* naamini Spika wangu mwezi Oktoba utakwenda kushinda kiti cha Urais wa Dunia na kulileta Taifa letu heshima jambo ambalo litaendelea kuifanya Tanzania ing'are katika medani za Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. Naomba Wabunge tuendelee kumwombea Spika wetu. Kwa muda mfupi nimekuwa naye karibu, dada yetu huyu ni mtu mnyenyekevu sana, Spika huyu ni mtu mtulivu sana, Spika huyu ni mtu mwenye maono makubwa sana na ndio maana dunia iko tayari kumuunga mkono katika uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunazo nchi kadhaa bado zimekataa kujitoa kwa sababu *Africa Union* wamesema kwamba wanakwenda na huyu, lakini *In Shaa Allah* kwa neema za Mwenyezi Mungu endeleeni kutuombea tupate ujasiri wa kuendelea kumsemea Mheshimiwa Dkt. Tulia tuweze kuleta *trophy* nyumbani kwa ajili ya heshima ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema haya, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Zainab Athman Katimba na mtoa hoja ajiandae.

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kupata fursa hii ili niweze kuchangia hoja iliyopo mezani ya Muswada wa Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2023. Ni dhahiri kwamba 70% ya Bajeti ya Serikali inaenda kwenye manunuzi na ni dhahiri katika kipindi hiki cha hivi karibuni sisi sote tumekuwa mashahidi, ni kiwango gani cha fedha nyingi zinatafutwa na Mheshimiwa Rais wetu Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan, lakini ni kwa kiasi gani kuna fedha nyingi sana za walipa kodi ambazo zinahitaji zionekane katika maendeleo ya nchi hii. Ni dhahiri ili fedha hizi ziweze kuonesha tija, tunahitaji kuhakikisha kwamba kunakuwa na thamani halisi ya pesa, yaani thamani halisi ya pesa inapatikana *(value for money)*.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umekuja katika kipindi hiki muafaka, kwa nini? Kwa sababu Sheria ile ya mwanzo ilikuwa ina dosari mbalimbali ambazo sasa tunatarajia kwamba Muswada huu au marekebisho haya ya Sheria hii yatakuja kutatua changamoto hizo na kuondoa ule upotevu wa fedha nyingi ambazo zilikuwa zinatokana na changamoto au mapungufu kwenye manunuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukianza kwanza kwenye Ibara ya 72 ya Muswada huu ambayo inatoa sharti la kwamba manunuzi yote yatakuwa yanafanyika kwa njia ya kieletroniki. Ibara hii ni Ibara muhimu sana kwa sababu kwa muda mrefu tumekuwa tunasema tunataka kuondoa ushiriki wa mkono wa binadamu moja kwa moja kwenye masuala ya manunuzi au moja kwa moja kwenye masuala ya fedha. Kwa hiyo, sasa kutumia mifumo ya TEHAMA, kutumia mifumo ya kieletroniki ni namna nzuri zaidi ya kuondoa mianya ya upotevu wa fedha katika manunuzi.

Mheshimiwa Spika, changamoto moja tu ninayoiona kwenye Ibara hii ni kwamba Ibara ndogo ya (2) ya Ibara hii ya 72 kwenye Muswada inasema; "Endapo mfumo haufanyi kazi,

Mamlaka itatoa *notice* ya mwongozo kwa watumiaji wa mfumo na kwa umma."

Mheshimiwa Spika, sasa swali langu hapa kwa nini mfumo haufanyi kazi? Kwa sababu hapa tumeona tumeanza kutumia Bunge mtandao, tunaona kwenye mabenki tunatumia mitandao, tunaona kwenye masuala ya *aviation, ticketing* kwenye masuala ya ndege tunatumia mtandao na hatujawahi kutengeneza mbadala wa hiyo mitandao. Sasa kifungu hiki kisije kikawa ni mwanya wa kuacha kutumia mifumo ya kieletroniki na ikawa ni sehemu ya kutengenezea huo mwongozo wa kufanya manunuzi nje ya mfumo wa kieletroniki.

Mheshimiwa Spika, nadhani msingi hapa ni kwamba, tukazanie mifumo ya kieletroniki ni lazima ifanye kazi. Kwa hiyo naiomba sana Serikali katika Kifungu hiki, sasa kwa sababu tayari kimeshaandikwa hivi, lakini kisije kikatumika kama kichaka cha kutengeneza manunuzi nje ya mfumo ambao wa kieletroniki. Kwa sababu Ibara hii ya 72 inaweka sharti kwamba manunuzi yote yatafanyika kwa njia ya eletroniki, tubakie huko, tujielekee huko, tuweke nguvu ili mifumo iweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, ukienda kwenye Ibara ya 63 ya Muswada huu, ambayo inazungumzia upendeleo kwa makundi maalum ya kijamii. Ibara hii ni nzuri sana kwa sababu inatoa sharti la kwamba taasisi nunuzi zitatenga kiwango fulani cha manunuzi yake kila mwaka wa fedha kwa ajili ya upendeleo pekee kwa ajili ya makundi haya maalum. Kifungu hii cha Sheria kilikuwepo kwenye sheria ile ya zamani ya *PPRA* na hata kutungiwa Kanuni, kulikuwa kuna Kanuni 30(c) ambayo ilitoa sharti la kwamba Maafisa Masuuli wote wa taasisi za umma, watenge 30% ya manunuzi ya taasisi zao kwa ajili ya kuziwezesha au kwa ajili ya kutoa manunuzi haya kwenye makundi maalum.

Mheshimiwa Spika, Kanuni hiyo ikasisitiza pia, taasisi yoyote inayoshindwa kutenga 30% ya fedha hizi za manunuzi na kuziweka kwa ajili ya makundi haya maalum, itatoa maelezo kwamba ni kwa nini imeshindwa kusimamia sharti hili la kutenga 30% ya manunuzi yake kuyatenga kwa ajili mahususi kwa ajili ya makundi maalum. Pia Kanuni hiyo ikaenda mbele kutaka kwamba Maafisa

Masuuli wote ambao wameshindwa kutekeleza takwa hili la kikanuni la kutenga 30% ya manunuzi yao wazitenge mahususi kwa ajili ya makundi maalum, watachukuliwa hatua za kinidhamu.

Mheshimiwa Spika, sasa mpaka leo hii Sheria hiyo ambayo tumekuwa nazo tunaitumia ya manunuzi, nataka kufahamu hivi ni Maafisa Masuuli wangapi wametoa maelezo ya kwa nini hawajatenga hizo fedha kwa ajili ya makundi haya maalum na kwa nini na wangapi katika hawa Maafisa Masuuli wamechukuliwa hatua? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, msingi wa kuuliza maswali hayo ni kwa sababu tunakiona hiki Kifungu kwenye Muswada huu, tunaona kwenye Ibara 63 inaweka huo upendeleo kwa makundi maalum ya kijamii na hiki Kifungu kimeboreshwa kwa sababu sasa katika kutunga Kanuni kwenye Kifungu hiki Waziri atashauriana na Wizara zinazohusiana na masuala ya makundi maalum, lakini tunajuaje kama itaenda kutekelezeka? Kwa sababu tumekuwa tuna Sheria, tumekuwa tuna Kanuni, tumekuwa na miongozo ambayo haijazingatiwa, haijatekelezwa na hamna hatua yoyote iliyochukuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo tunarudi tena Bungeni tunafanya marekebisho ya Sheria, sasa nataka kufahamu hapa tunatokaje, kwa sababu hizi ni ajira za Watanzania, tunataka tutengeneze ajira kwa ajili ya wananchi wetu na maeneo ya kupata mitaji, kupata kazi za kufanya za kupata ajira ni kwenye maeneo ya upendeleo kama haya. Sasa tunapokuwa hatusimamii utekelezaji tunatokaje? *(Makofi)*

Mhehimiwa Spika, naomba sana, nina imani kubwa na Mheshimiwa Waziri, nina imani kubwa na Serikali, naomba sana twende tukatekeleze Ibara hii, kifungu hiki cha 63 kwenye hii Sheria ya Ununuzi wa Umma tunapitisha lakini tunataka utekelezaji. Zile changamoto za kutokutekelezwa kwa Sheria na Kanuni tulizoziona nyuma, hatupendi kuziona katika kipindi hiki. Tunaamini tunaanza upya, lengo ni kutengeneza mazingira mazuri katika Sheria zetu na sheria zisimamiwe, kwa sababu nchi hii

inaenda kwa utawala wa sheria. Kwa hiyo sheria zizingatiwe na zitekelezwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukienda kwenye Ibara ya 21 ya Muswada huu inazungumzia adhabu au mapendekezo ya hatua za kinidhamu, inatoa hatua zinazoweza kuchukuliwa na mamlaka pale kunapokuwa na ukiukwaji, mamlaka kwa maana ya *PPRA,* kunapokuwa na ukiukwaji wa sheria hii, kanuni na miongozo yake. Sasa kwenye Ibara hii ya 21 ambayo naomba niinukuu, inasomeka hivi; "Endapo kuna ukiukwaji wa mara kwa mara au ukiukwaji mkubwa wa Sheria hii, Kanuni au miongozo iliyotolewa chini ya Sheria hii, mamlaka itapendekeza kwa chombo chenye mamlaka:

(a) kusitishwa utoaji wa fedha kwa taasisi kadha wa kadha."

Mheshimiwa Spika, sasa changamoto yangu kwenye Ibara hii ni unaposema endapo kuna ukiukwaji wa mara kwa mara au ukiukwaji mkubwa wa sheria hii kanuni au miongozo tafsiri yake inaenda vipi, kwa sababu kama tunafanya marekebisho, nafahamu kuna kifungu kama hichi kilikuwepo kwenye sheria hii ya zamani, lakini sasa kama tunataka kutengeneza na kuziba mianya ya upotevu wa fedha nyingi ambazo zinatokea kwenye manunuzi kwa,nini tunakuwa tuna Kifungu ambacho kinaruhusu ukiukwaji wa mara kwa mara. Sasa mara kwa mara ni mara ngapi? Je, ni mara moja, mara mbili, mara tatu au mara tano au hata mara kumi, mara kwa mara? Au ukiukwaji mkubwa wa sheria, sababu sheria kimsingi inabidi isimamiwe sasa ukiukwaji upi ni mkubwa na upi ni mdogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napendekeza kifungu hiki kiweze kuboreshwa ili kuondoa mianya au kichaka cha wale watakaotuingiza sisi Watanzania kwenye hasara, wamepewa dhamana na maamuzi yao yakasababishia Taifa hili hasara, basi wasiwe wana kichaka cha kupotea kwa misingi ya kwamba hawajafanya uvunjifu wa sheria wa mara kwa mara au hawajafanya uvunjifu wa sheria mkubwa. Kwa hiyo naomba sana kwenye kifungu hiki, naamini Serikali watakuwa wana maelezo

mazuri kwa sababu nia yetu ni njema, ni kufanya maboresho ya sheria ambayo yatalinufaisha Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine la kusisitiza ni Ibara ya 61 ambayo inazungumzia, inaweka masharti au inazungumzia kuhusu kujenga uwezo wa kampuni za ndani, kwamba hapa Ibara hii ya 61 kifungu hiki kinazungumzia kuhusiana na kuhakikisha kwamba kunakuwa kuna mazingira ya kuwajengea uwezo au kujengea uwezo kampuni za ndani ili ziweze ziweze kushiriki vizuri katika mikataba mbalimbali ya manunuzi. Tumemsikia Mheshimiwa Eric Shigongo amezungumzia masuala ya kutengeneza mazingira mazuri kwa ajili ya wazawa ili na sisi wazawa, Watanzania hii ndiyo sehemu ya kupata ajira. Watanzania wapate fursa ya kupata mikataba na kufanya kazi za manunuzi ili waweze kujipatia kipato na tuondokane na umaskini kwa wananchi, kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sana kwenye Ibara hii ambayo itakuwa ni kifungu 61 cha hii sheria mpya kuwe na msisistizo mkubwa, tujielekeze zaidi katika kuwajengea uwezo wazawa wetu, kwa sababu huko nyuma hata sababu mojawapo ya kutokutenga fedha hizi 30% za manunuzi, hawa Maafisa Masuuli utakuta sababu zao wanasema kwamba makampuni hayana uwezo wa kuja kushiriki kwenye tenda, hayana uwezo ya kupata mikataba hii na kuweza kutoa huduma hii.

Kwa hiyo, naiomba sana Serikali ijengee uwezo makampuni ya ndani, muswada huu umeonesha maeneo mengi ya upendeleo wa kipekee kwa wazawa. Kwa hiyo katika utekelezaji tunahitaji sana kuona ni namna gani wazawa wanapata manufaa ya sheria hii nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina imani kubwa na Serikali, nina imani kubwa na Mheshimiwa Waziri na timu yake yote, kwa hiyo nina imani mchango wangu pamoja na michango ya Waheshimiwa Wabunge wengine ambayo inalenga kuwasaidia Watanzania na kuondoa mianya ya upotevu wa fedha kwenye manunuzi, Serikali itapokea ushauri na yale yote tuliyosema na kuyafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, uje uhitimishe hoja yako.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ili niweze kuhitimisha hoja ambayo niliwasilisha leo asubuhi. Awali ya yote niwapongeze sana Waheshimiwa Wabunge kwa hoja walizozitoa na niwahakikishie kwamba kwenye hoja hii hakuna pande mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye hoja hii Serikali pamoja na Wabunge tunaongea lugha moja. Kuanzia tulivyoenda kwenye Kamati tuliwaambia *position* ya Serikali kwamba tunataka tutunge sheria itakayotibu matatizo yanayoikabili nchi hii kwenye masuala ya manunuzi.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo Wabunge wametoka kuchangia na nikimnukuu Mheshimiwa Reuben Kwagilwa, Mbunge wa Handeni, jambo hili Mheshimiwa Rais aliahidi kwanzia kwenye hotuba yake kwamba atafanyia marekebisho sheria zozote zile ambazo zinatukwamisha kuweza kupiga hatua, kwenye hotuba ya Bajeti ya Serikali ya mwaka huu tulitoa ahadi hiyo kwamba tutarekebisha Sheria ya Manunuzi, tutarekebisha Sheria ya Ubia Kati ya Sekta Binafsi na Sekta ya Umma. Sheria ya Sekta Binafsi na Sekta ya Umma ilishapitishwa na Bunge na ilishasainiwa na leo hii tukaileta hii kama ambavyo Mheshimiwa Rais aliahidi katika baadhi ya hotuba zake na ambavyo tulileta katika Bajeti Kuu ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yale ambayo Waheshimiwa Wabunge wamesema, naomba nitoe ufafanuzi moja baada ya lingine. Kama ambavyo nimesema hii si sheria ambayo tuna ubishani nayo kwa sababu lengo ni kuwawezesha Watanzania na lengo ni kuwezesha shughuli hizi za masuala ya manunuzi zifanyike kwa ufanisi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikianza na hoja aliyoitoa Mheshimiwa Eric Shigongo, ameweka kwenye pendekezo lake na ameongea

kwa hisia kuguswa kwake kuhusu suala la wazawa. Hii ni *concern* ya Serikali kuhakikisha kwamba wazawa, wananchi wa Tanzania wanawezeshwa, wanapata fursa na lengo la sheria hii ilikuwa kuweka masharti hayo ambayo yatawawezesha Watanzania waweze kupata fursa hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Serikali inakubaliana na hilo wazo la kupeleka kiwango cha tenda, zile zabuni ambazo zitakuwa za ndani ya nchi ambazo ni *local* sio *international tender* kufika hiyo bilioni 50. Sisi tulikuwa tumeweka bilioni 30, Mheshimiwa Shigongo amependekeza tuiongeze zaidi ifike bilioni 50 na sisi kama Serikali hatuna tatizo na kupeleka kiwango cha zabuni za ndani ya nchi kufika bilioni 50. Tunataka tuwajengee uwezo wazawa na tunataka tuwajengee Watanzania waweze kushiriki katika shughuli hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeongea hata ndani ya Kamati ambacho tulikuwa tumekibishania kwa sehemu ndogo ilikuwa ni kuhusu iandikwe wapi. Sisi tukasema kwa majira haya ambayo mabadiliko yanabadilika sana, yanaenda kwa kasi sana. Mabadiliko ya *exchange rate* pamoja na yale mengine, tulisema Waheshimiwa Wabunge waridhie kiwango kile, tuweke kwenye sheria, mkakati huu wa kuwawezesha wazawa, kiwango kile cha bilioni 50 kiwekwe kwenye kanuni. Tulisema kiwekwe kwenye kanuni kwa sababu kwa mabadiliko haya ya *exchange rate,* lakini pia na kukua kwa uchumi tunaweza tukakaa baada ya mwaka mmoja, watu wenye bilioni 50 wakawa wameshakuwa wengi, tukataka tuweke bilioni 100, ama tuweke bilioni 150, tukasema hii isitutake tuitishe Bunge zima kuweza kuibadilisha hiyo.

Mheshimiwa Spika, tunaweka bilioni 50 na inakaa kwenye Kanuni, tunaendelea kusonga mbele kwa sababu uchumi unakua na masuala ya kifedha yanabadilika. Tunaungana na Mheshimiwa Shigongo, tunaungana na Kamati ya Bajeti pamoja na Wabunge wengine kuweka *international tender* iwe kuanzia bilioni 50 kwenda juu na bilioni 50 yenyewe na 50 kuja chini ziwe ni *local tendering*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama Serikali tumeenda hatua zaidi kwenye lile jambo ambalo Mheshimiwa Shigongo ameliongea kwa uchungu sana, Serikali tumeenda hatua zaidi. Mheshimiwa Rais mara zote amesema anataka kutengeneza mabilionea wa Tanzania, Watanzania na wenyewe waheshimike kwenye nchi yao, wajengewe uwezo, sasa hatua nyingine ambayo tumeiweka mtaona kwenye sheria yenyewe ile ambayo tunapendekeza. Tunapendekeza kampuni ya Kitanzania yenye uwezo, ikieleza kwamba kwenye kazi kubwa ambayo inataka kufanya, kama itapata wabia, au mshirika wa makampuni makubwa kutoka nje na wao Watanzania waruhusiwe kupewa kazi kama ambavyo wageni wamekuwa wakipewa kazi na kuruhusiwa kuwashirikisha Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii ni hatua kubwa ambayo itaenda kujenga uwezo kwa makampuni ya Watanzania na hata siku nyingine yaweze kwenda kushindana nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuweka kwenye sheria moja kwa moja kwamba makampuni ya Kitanzania hayatakiwi kupata kazi kubwa ni sheria ambayo inawakandamiza Watanzania na ni sheria ambayo inawapimia Watanzania kwamba wao wanatakiwa wawe wadogo tu na isitokee siku wakakua. Ni sheria ambayo tunawafanya wale wenzetu wa mataifa mengine waendelee kuwa wakubwa na sisi Watanzania tuendelee kuwa wadogo. Sasa kwenye sheria hii tumeleta pendekezo ambalo linasema, kampuni ya Kitanzania ikitaka kutekeleza mradi mkubwa iweke sharti la kuwaleta wale wakubwa ambao watatekeleza nao na wakionesha hiyo *capacity* kwamba tutashirikiana na hawa wakubwa na wenyewe waruhusiwe kuweza kupata mradi mkubwa waweze kushirikiana nao.

Mheshimiwa Spika, kwenye upande wa benki tumeweza kufanya hivyo. Tukitaka kufanya *syndication* ya kutafuta fedha nyingi, tunaruhusu benki ya Kitanzania hapa kuwa *lead arranger*, yeye ndiye anakuwa kiongozi halafu anatafuta benki zingine wamsaidie kuhamasisha kupata hizo fedha.

Mheshimiwa Spika, tumesema uwezo utaendelea kuamua lakini tusiweke sheria ambayo inawazima Watanzania wao

waendelee kuwa vibarua, *sub contract* bila kujali kwamba kuna siku na sisi tunataka hawa wawe wakubwa waweze kufanana na wale wengine. Tunaamini tutapiga hatua.

Mheshimiwa Spika, tumeona tufanye hivi kwa sababu gani? Mara nyingi imekuwa ikitokea, haya makampuni makubwa tunayoyaamini, tena wasikie, kuna maeneo wanakuwa hawawatendei haki Watanzania. Tunasaini mikataba tena kwa dola na tunaweka kwamba kila ifikapo tarehe 31 fedha zao za *certificate* ziwe zimelipwa, halafu wakishalipwa wanapeleka fedha makwao, hawawalipi *subcontractors* wa ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nimesikia malalamiko baadhi ya maeneo, *certificate* zinalipwa kwa wakati lakini ukienda kwenye utekelezaji inatokea makampuni ya ndani yanawadai wao, sasa tutengeneze utaratibu na kampuni ya ndani ikipata hiyo kazi iwapimie wao kwa kufanya kazi na faida ibaki ndani ya nchi.

Mheshimiwa Spika, tumeenda hatua nyingine kubwa zaidi. Tumependekeza tuzo ziruhusiwe kwa kampuni za ndani na kwa zile kampuni ambazo ziko ndani ya nchi, ambazo zinawekeza ndani ya nchi. Makampuni ya kigeni ambayo yanapata kazi ndani ya nchi na yanawekeza ndani ya nchi yaweze kupata upendeleo.

Mheshimiwa Spika, imekuwa ikitokea hasa kwenye hii miradi mikubwa mikubwa, watu wanatekeleza mradi wanapata fedha nyingi lakini wanawekeza nchi ya Jirani pale. Wanachukulia fedha kwetu wanawekeza nchi nyingine pale, sasa kwa sababu fursa za uwekezaji kwenye nchi yatu hazijajaa, tunapendekeza kampuni ile ambayo inawekeza ndani ya nchi na ile ambayo inaweka *commitment* kwamba ikipata mradi itawekeza ndani ya nchi, itapewa kipaumbele ili tuweze kuongeza uwekezaji ndani ya nchi. Haya ni mambo ambayo katika nchi za wenzetu yanawezekana.

Mheshimiwa Spika, nirudi kwenye jambo lingine moja. Mheshimiwa Halima Mdee aliongea kwamba Serikali tuliweka pendekezo la Sheria ya *PPRA* kuja ndani ya Bunge na baadae tukalitoa. Ndiyo, tuliahidi wakati tunasoma na matamanio yetu

yalikuwa hivyo, tulitamani Sheria ya *PPRA*, tulitaka taarifa ya *PPRA*, Taarifa ya Mkaguzi wa Ndani, Taarifa ya TAKUKURU, Taarifa ya *EWURA*.

Mheshimiwa Spika, tulitaka taarifa za taasisi hizi ziende kwenye Bunge lakini tumeshauriwa kisheria na bahati nzuri Mheshimiwa Mdee ni Mwanasheria. Tumeshauriwa kisheria kwamba taarifa ya Mkaguzi wa Hesabu za Serikali iko Kikatiba. Ukienda kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 143 inataja kwamba kutakuwa na Mkaguzi Mkuu na Mdhibiti wa Hesabu za Serikali na baadae ikataja majukumu yake, ukienda Ibara ya 43(3) inasema Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kila mtumishi wa Serikali anayeruhusiwa na Mkaguzi Mkuu wa Serikali ataruhusiwa kukagua vitabu, akaelezea vitabu atakavyokagua na majukumu mengine yote yakaelezewa.

Mheshimiwa Spika, lakini kipengele cha (4) cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kinasema; Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali atawasilisha kwa Rais kila taarifa atakayotoa kwa mujibu wa masharti ya Ibara ndogo ya (2) ya Ibara hii na baada ya kupokea taarifa hiyo, Rais atawaagiza watu wanao husika wawasilishe taarifa hiyo kwenye kikao cha kwanza cha Bunge kinachofanyika baada ya Rais kupokea taarifa ya *CAG*, hili ni takwa la Kikatiba.

Mheshimiwa Spika, tulipoona kuna taarifa ambayo ipo Kikatiba na inapitia taarifa hizi zingine zote, Taarifa ya TAKUKURU, Taarifa ya Mkaguzi wa Ndani, Taarifa ya *PPRA*, Taarifa ya *PPA*, tukasema hili la kikatiba libaki kama Katiba inavyoelekeza.

Mheshimiwa Spika, taarifa hizi zingine za *PPRA*, TAKUKURU na Taasisi zingine zote zimewekewa utaratibu wake wa kuingia Bungeni kwa sababu zile ni taarifa za kazi. Taarifa za kazi za mashirika yote ya umma zina Kamati zake ambazo zinazisimamia na zinakagua utendaji wake, na taarifa zile zinaingia Bungeni kwa kutumia mgongo ule wa Kamati inayosimamia majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, hivyo ndivyo ilivyo hata kwa taarifa zingine kwa taasisi zingine zilizosalia, kwa hiyo hata hii ya *PPRA* itaendelea kukabidhiwa kwa Rais, itakabidhiwa kwa sekta

inayohusika, itaenda kwenye Kamati inayosimamia majukumu ya *PPRA* na Kamati hiyo italeta taarifa hiyo Bungeni ili iweze kusimamiwa kama vile ambavyo sheria zingine zinasema.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hatuna haja ya kuvutana kwenye hili kwa sababu ni taratibu za kisheria ambazo tumezitunga. Hivyo hivyo na hili ambalo umeshalifafanua, sihitaji kufafanua bahati nzuri wewe ni Mwanasheria, Mwalimu na umewafundisha wanafunzi wengi humu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivyo, hata hili la kutunga kanuni na majukumu yaliyopo kwenye sekta hizi yapo kikatiba na yapo kisheria. Mheshimiwa Halima wakati anaongea alikuwa anasemea rafiki yangu, wakati mwingine urafiki ndiyo unatuponza inaonekana hivi viapo tulivyonavyo ni vidogo, majukumu haya tuliyonayo yapo Kikatiba.

Mheshimiwa Spika, kumeanza kuzuka utaratibu hivi wa mtaani mtaani na baadhi ya maeneo ya watu kut kuamini. Unaweza usimheshimu yeye kama mtu lakini heshimu jambo alilopewa na Katiba na unatakiwa uamini kwamba viongozi wote walioko Serikalini ni Watanzania, hakuna mtanzania na nusu kwa sababu hayupo Serikalini na yule aliyepo Serikalini ni nusu mtanzania kwamba anaweza akajali maslahi ya Tanzania nusu nusu. Mheshimiwa Halima angekuwepo ningemwambia, tumeibeba Tanzania mioyoni na wengine tumeibeba shingoni hapa. Tunajali maslahi ya Watanzania na hiki anachofanya Mheshimiwa Rais ni kwa ajili ya kuongeza ufanisi na kuongeza ustawi wa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wewe utaona kasi ya kubadilisha hizi sheria ambazo zinalenga kukuza sekta binafsi, sheria zote hizi zinazolenga kukukuza sekta binafsi, zinalenga kuwaongezea Watanzania utajiri. Hii siyo sheria ya usimamizi, hii ni sheria inayolenga kuwawezesha Watanzania washiriki katika keki ya Taifa. Kwa maana hiyo ni sheria yenye malengo mazuri kwa Watanzania, Vivyo hivyo na zile zingine ambazo tumezitoa.

Mheshimiwa Spika, lilikuwepo jambo lingine kuhusu mchango alioutoa Mheshimiwa Mpina. Alisema kwenye *force*

*account* tuongeze wigo. Sisi tulikuwa tumependekeza milioni 50, yeye anapendekeza ifike milioni mia moja.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema…

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, samahani, Mheshimiwa Mpina ameleta mchango kwa maandishi? Maana hapa sijamsikia akichangia na sina mchango wake hapa mbele.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, nilipokea pendekezo, sijui kama limeingia ama halijaingia.

**SPIKA:** Hapana. Kama ni *schedule of amendments* utapata nafasi ya kuzungumza tutakapoanza kushughulika na *amendments*, kwa sababu hapo umesema mchango wa Mheshimiwa Mpina na Mheshimiwa Mpina hajachangia, labda kama ameleta mchango kwa maandishi.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, ninakubaliana na mapendekezo yako kwa sababu sisi kama Serikali tulikuwa tunajiandaa na sheria ambazo zinatakiwa zije, ndiyo maana nimechangia na ya Mheshimiwa Mpina. Tunakubaliana na maelekezo yako.

Mheshimiwa Spika, pendekezo lingine ambalo lilitolewa na Mheshimiwa Reuben kuhusu kuleta sheria. Ndani ya Serikali tutajiratibu sera ya masuala ya manunuzi na tutaileta, hilo halina pingamizi. Kama nilivyosema, maoni yote ya Wabunge yanayoboresha ufanisi unaowafanya Watanzania wafurahie matunda ya uhuru wa nchi yao, wafurahie keki ya Taifa lao ni jambo ambalo Serikali hatupingani nalo na hatutachelewa hata sekunde moja kuweza kutekeleza masuala ya aina hiyo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kimei pamoja na Mwenyekiti wamechangia na yale yaliyotolewa na Kamati, tumekubaliana mengi kwenye Kamati kasoro yale machache, kama lile ambalo umelitolea ufafanuzi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo haya ya kutunga Kanuni, Kanuni hizi zinatungwa kwa kuzingatia sheria ambazo zinakuwa

zimeshawekwa, ambazo ndio muhimili unaotoa mwongozo kwenye upande wa zile Kanuni.

Mheshimiwa Spika, kwenye maeneo mengine ambayo tumepokea kutoka kwa Mheshimiwa Zainabu Katimba pamoja na Mheshimiwa Elibariki Kingu, tumeyapokea na tutakapoenda kupitia sheria, vipengele kwa vipengele, ni maoni makini nani maoni ya Wanasheria na yanaendana na mapendekezo ambayo ndani ya Serikali tulikubaliana nayo.

Mheshimiwa Spika, kuna Mheshimiwa Mbunge alisema jambo moja la kuwekea sheria masuala yanayohusu madeni. Mheshimiwa Halima amesema kwamba TAMISEMI kuna bilioni mia moja, Mashirika kuna bilioni mia moja, Serikali Kuu kuna trilioni 83 pamoja na yale yanayohusisha mifumo tunaendelea nayo. Utekelezaji wa masuala ya mifumo tunaendelea nayo, kama nilivyosema Mheshimiwa Rais anachukua hatua za kutatua tatizo moja baada ya lingine. Kulikuwepo na matatizo ambayo yalikuwa yanatusababishia malimbikizo mengi ya madeni, na malimbikizo mengi yalikuwa yanatokana na *mismatch* ya mapato pamoja na matumizi tunayopeleka.

Mheshimiwa Spika, haya yalikuwa yanatokea kwa sababu kuna vitu vingi vilikuwa vinajitokeza wakati tunaendelea kutekeleza bajeti. Mheshimiwa Rais kwa kuona hilo akairejesha Tume ya Mipango ambapo vitu vingi vitakavyokuwa vinatekelezwa vitakuwa vimepata kwanza ridhaa kutoka katika Tume ya Mipango. Maana yake vitu vitatekelezwa ambavyo viko kwenye mipango, vitatuondolea hiyo *imbalance* ambayo Waheshimiwa Wabunge wameiongelea hapa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Serikali ilishachukua hatua kwenye hilo na wala halihitaji Sheria ya Manunuzi kuweza kudhibiti masuala hayo ya upande wa madeni. Tunaamini tunakokwenda kutakuwa na huo mpango wa muda mrefu, kutakuwa na mipango ile ambayo ni ya muda mfupi, kutakuwa na ile mipango ya miaka mitano, na kwa sababu Tume ipo na hiyo ndiyo itakuwa inafanya kazi zake na Waziri makini Mheshimiwa Mkumbo yupo hapa, haya yataenda kutuondoa kwenye utaratibu ambao

ulikuwa unazalisha hii *mismatch* ya matumizi pamoja na mapato ambayo ilikuwa inasababisha haya madeni.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kutoa rai kwa Waheshimiwa Wabunge kwamba Serikali tumeleta sheria hii kwa nia njema ya kuhakikisha kwamba yale ambayo tumekuwa tukiyalalamikia kwa muda mrefu yapate suluhu. Hicho ndicho ambacho Mheshimiwa Rais amekuwa akikiona, siyo tu kwa sheria hii, mtakumbuka tumesharekebisha sheria nyingi, tumerekebisha Sheria ya Uwekezaji, Sheria ya Mawasiliano, Masuala ya Manunuzi, tumerekebisha hii ya Tume, Sheria ya Msajili wa Hazina, zote hizo zikiwa zinalenga kutengeneza mazingira wezeshi ya kumwezesha Mtanzania aweze kuwa na ustawi unaostahili na kunufaika na rasilimali zilizopo.

Mheshimiwa Spika, kwa sheria hii ilivyokuwa kuna mambo ambayo ilikuwa inakosea na ndiyo maana tumeileta hapa, hata kwenye mchango haijajionesha sana lakini kwenye hotuba yetu tumeiandika. Tumeweka ukomo katika manunuzi, hii ilikuwa inatumiwa vibaya, ule uwazi uliokuwepo ulikuwa unatumiwa vibaya, kwamba bidhaa ikienda tu kununuliwa na Serikali ghafla bei zake zinapenda ukienda kwenye soko bei ziko chini. Tukasema tukiweka tu bei elekezi ama bei kikomo au bei ya chini, bado haitoshi. Tukaongeza na ile bei kikomo, bei elekezi na tukaongeza bei ya chini kwa sababu kuna mazingira yalikuwa yanajitokeza katika sheria iliyokuwepo ya manunuzi kwamba, mtu anashindania kwa bei ya chini na akipewa zabuni, ile kwamba amepewa kwa kushindania bei ya chini lakini ukienda kwenye bei ya soko, gharama yake inakuwa ni mara tatu ya bei ya soko.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, anakuwa ameshinda kwa bei ya chini lakini ukienda kwenye thamani ya fedha, *value for money* anakuwa yupo mara nne, mara tatu au yuko mara tano na ukienda kwa baadhi ya Watanzania wasio waaminifu wanaweka njama tu. Wanakaa kwenye Halmshauri wanakuwepo watu wasio waaminifu watatu au wanne wanashirikiana na mmoja asiye mwaminifu ambaye yuko kwenye manunuzi wanakubaliana kwamba, wewe kwenye sekta ya afya uje tu kunitengenezea mimi kushinda, wewe kwenye sekta ya elimu mimi nitakuja nikutengenezee wewe kushinda.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kwenye afya yote yeye anakuja, kama thamani ya bei ya mradi kwenye soko ni kama bilioni 20 yeye anaweka bilioni 80 halafu yule aliyeletwa tu wa kuharibu soko anaweka bilioni 120, kwa hiyo tunampatia wa bilioni 80 tena kwa kufuata taratibu zote za manunuzi, huku tukisema huyu ndiye kashinda na ameteuliwa kwa sababu ndiye aliyeweka zabuni kwa bei ya chini. Bei ya chini bilioni 80 lakini bei halisi ilitakiwa iwe bilioni 20. Tumesema Hapana! Tumwezeshe Afisa Masuuli muungwana, mzalendo akiona bei halisi ni bilioni 20 hata kama wa chini alikuwa amefikia bilioni 80 aseme bado hii haina thamani ya fedha katika *project* hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ilivyokuwa sasa, kama ameshinda kwa bilioni 80 hata kama *project* ile ni bilioni 15 akikataa ataonekana aliyetaka kumpa hajashinda kwa hiyo ameamua kuifuta. Itaonekana ameifuta kwa sababu kuna mtu alikuwa anamtafuta na ameshindwa na huyo aliyeweka bilioni 80. Tumesema hapana, tunataka manunuzi yaangalie thamani ya fedha, yasiangalie tu huyu kashindania bei ya chini bali yaangalie thamani, *value for money*, ili yeyote atakayetoa zabuni akampa aliyeshinda lakini ikienda kwenye soko ikaonekana amempa ya juu sana, naye awe kwenye hatia kwa sababu yamekuwa yakitokea haya ambayo hayalindi thamani ya fedha ya mlipa kodi wa Tanzania katika miradi hiyo. Kwa hiyo, hili na lenyewe tumeliweka na mengine mengi ambayo yanahusiana na kuboresha shughuli hizi.

Mheshimiwa Spika, pale kwenye bilioni 50 ambayo tulisema hatupingani na Waheshimiwa Wabunge tumeongeza. Tukasema tukiweka asilimia na Mheshimiwa Katimba ameiongelea kwenye upande wa makundi maalum, tunaendelea na lenyewe kulitafakari. Tuliweka asilimia hata kwenye sheria iliyopita, tukasema asilimia 30 iende kwenye makundi maalum, lakini kwa kuwa tu tumeweka asilimia iende kwenye makundi maalum ikawa kama tumeandika barua kwa yeyote anayehusika ambayo haijibiwi kwa sababu haina mtu wa kukujibu.

Mheshimiwa Spika, kila mtu anapopata fungu lake la kutekeleza miradi anaendelea kutekeleza tu, ukienda mwisho wa mwaka haipatikani ile asilimia 30 iliyoenda kwenye makundi maalum. Hivyo, tukasema hata wazawa tukiweka asilimia itakuwa

inaenda hivyo hivyo inapita. Tukasema tutaje kiwango ili yeyote anayefanya manunuzi akikuta kiwango kile ajue hii inaenda huku, sasa tunaendelea kuangalia kuhusu ufatiliaji wa masuala ya makundi maalum kama alivyolisemea Mheshimiwa Katimba ili tuwe na utaratibu wa kuweza kuona kwamba hiki tulikiweka kwenye sheria na katika mwaka wa fedha ambao umefanyika utaratibu wake umetumika.

Kwa hiyo, tumesema tutaiweka kwenye kanuni ili kuweza kuweka *enforcement* ambayo itawawezesha Maafisa Masuuli na Kamati zetu za manunuzi ziweze kuzingatia kile kinachokwenda kwenye makundi maalum.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hoja ni nyingi, tumepokea na tumesema hatubishani. Mengine tutakwenda tunarekebisha kadiri tutakavyokuwa tunapitisha kipengele kwa kipengele.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Mheshimiwa Waziri, ahsante sana.

Baada ya hoja kuungwa mkono tunaendelea na utaratibu wetu. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria ya Ununuzi wa Umma wa Mwaka 2023**

Ibara ya 1

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaanza kifungu cha kwanza sijui Jedwali la Marekebisho lililoletwa na Serikali ilikuwaje. Safari hii haya marekebisho naona yamekuja na jambo ambalo sio rahisi kulifanyia kazi katika ngazi hii.

Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali uko hapa, hii sehemu ya kwanza kabla ya ibara ya kwanza mmeandika kwa ujumla kwamba A mnafanya haya marekebisho. Sasa haya marekebisho A kama Bunge tunalihoji vipi bila kuwa na vifungu? Kwa sababu mmeandika jumla (a) mpaka (h) sijui hivi hii Kiswahili inaitwa (ha) au inaitwa nini?

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni (ha).

**MWENYEKITI:** Ni (ha); sasa mmeanza kifungu (a) mpaka (ha) mnasema haya marekebisho popote maneno yanapotokea haya marekebisho tutayaingiza au tutayaweka wapi ili tulihoji Bunge? Maana vifungu vyake hatuna na sisi tunahoji kwa vifungu.

Sehemu pekee ambayo huwa tunaweza kuingiza ni yale marekebisho ya namba, kwamba namba hii sasa itasomeka hivi, sasa itasomeka hivi Sasa, maneno haya yamekusanywa yote kwa pamoja. Je, nayahoji vipi kwa Bunge? Kwa sababu hii (A) iliyoandikwa kwenye jedwali haipo popote kwamba itaingia kwa namna hii kwenye marekebisho.

Hebu nipate ufafanuzi kidogo, la sivyo, marekebisbo haya itabidi yawe sehemu ya yale marekebisho yanayotarajiwa kuletwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, nikusikilize. Inanipa ugumu kujua nalihoji vipi Bunge? Karibu.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tulimaanisha yawe popote yanaposomeka lakini pia ni sehemu ya marekebisho yaliyoletwa na Serikali.

**MWENYEKITI:** Sasa ili nilihoji popote yanaposomeka, hiki kifungu nitakiweka wapi? Sijui kama naeleweka? Yaani mimi nitakiweka wapi hiki? Kwa sababu ili nilihoji Bunge kwamba popote maneno haya yanapotokea, halafu hicho kifungu tutakuwa nacho wapi? Sijui kama nimeeleweka?

Mheshimiwa Waziri, naona kama unataka kutoa ufafanuzi.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema Mwanasheria Mkuu, kwa namna tulivyoweka hizi ni *footnotes*, yaani kwenye vifungu kuna maneno yaliyokuwa yanajirudia rudia yakiwa na lugha ambayo Kiswahili chake hakijanyooka. Kwa mfano; sehemu ambayo kwenye kifungu utakapokuta inasomeka "bodi ya zabuni" sisi tunasema popote utakapokuta inasomeka bodi ya zabuni pasomeke "Bodi za Zabuni."

**MWENYEKITI:** Sasa, hii *footnotes* Waheshimiwa Wabunge nawahoji kwenye kifungu kipi?

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kila kifungu ambapo imejitokeza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, nitakapofika kwenye hicho kifungu nitapajuaje?

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hizi ni *footnotes* na kama ambavyo ungeangalia maana yake tungekuwa tunalirudia moja baada ya lingine kila linapojitokeza kisha tuseme hapa sasa tuweke hii. Tuliona Muswada huu ungekuwa una maneno mengi yaliyojirudia. Kwa hiyo, tulifanya kama ile *computer work, select and replace*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, lakini si ndivyo tunavyotunga sheria? Palipo na *comma* toa *comma* weka nukta.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio, kwa sababu haya yanajirudia kwa mfano kadri imejirudia kila wakati, maalum imejirudia, mamlaka ya kudhibiti ununuzi wa umma inapojirudia tumeweka mamlaka ya udhibiti wa ununuzi wa umma.

**MWENYEKITI:** Sawa Mheshimiwa Waziri, mimi nimekuelewa lakini uzoefu niliopata ni kwamba Bunge halijawahi kutunga sheria yenye *footnotes*. Huu ndio uzoefu niliopewa na Ofisi ya Bunge. Sasa ninyi kama mna uzoefu wa ziada…

Naona Mwanasheria Mkuu wa Serikali unataka kusimama.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda neno hilo *footnotes*…

**MWENYEKITI:** Mimi nimelitumia kwa sura hiyo, sio kwa maana ya lile neno *footnote* halisi. Nimemaanisha kwamba hatujawahi kutunga sheria ambayo haya maneno tukayaweka mahali halafu hatuna pa kuyahojia. Sijui kama ndio Kiswahili halisi?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo letu lilikuwa ni kuepuka kurudia rudia kwa maana ya kwamba itakapokuja wakati wa kuandika baada ya kupitishwa kwa ujumla wake kama yamekubalika na hayajajengewa hoja ya kupingwa, basi itakuwa imerahisisha lile zoezi ambalo litakuja kutumika wakati wa kuandaa muswada wa kwenda kutiwa saini.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, napata wakati mgumu kidogo. Sasa kwa sababu tusingependa kufika mahali ambapo Bunge litatunga sheria ambayo pengine haieleweki, kwa sababu mabadiliko yaliyopo hapa juu yanayopendekezwa huko kwamba yanajitokeza kwenye sheria ni maneno ambayo hayazuii sheria kuwa sheria.

Waheshimiwa Wabunge, sijui kama naeleweka? Yaani haya maneno ambayo yamependekezwa kwamba yarekebishwe sio maneno ambayo yanatuzuia kuitunga sheria hii na kuwa sheria. Ni mabadiliko ambayo yanaweza yakafanywa kwa sababu ni ya kiuandishi. Maneno haya ni kama "kadri"

iandikwe "kadiri" ambayo sio kama ndio Kiswahili siku hizi. Mimi najua kadri ni kadri. Sasa kumbe sijui wametangaza ni kadiri. Neno "maalum" liandikwe "maalumu." Kwa hiyo maneno kama hayo hayazuii sheria kutungwa ama kuwa sheria hata tukitunga.

Kwa hiyo, ili tuendelee na utamaduni tuliouzoea ambao huwa tunahoji kifungu kimoja baada ya kingine, tusilete athari hii ya kujikuta kwamba haya maneno hatuna mahali tutakuwa nayo kwamba marekebisho yalifanyika kwa namna hii.

Sehemu hii ya kwanza iliyopendezwa ambayo imependekezwa kama (A) na humu haiingii kama (A), hii ni ya kutuonesha kwamba twende wapi. Hii sehemu kwa kuwa hatujatafuta vifungu hivi na hatuwezi kuvitafuta sasa, kama tungeweza tungetafuta. Kwa nini? Kwa sababu Serikali imekwishaleta na tunavyo hapa, lakini kwa sababu hatuwezi kutafuta kifungu kimoja kimoja, tutakwenda moja kwa moja kwenye vifungu, vile ambavyo tutakuwa tumepitisha marekebisho ya Serikali na mmehojiwa hivyo, vitakuwa vimepita pamoja na marekebisho ya Serikali na vile ambavyo marekebisho yake yamekusanywa kwa pamoja hapa juu, tutavipitisha kama haya marekebisho ya Serikali hayajakubaliwa na Bunge. Serikali itayaleta haya kwa utaratibu wetu wa kawaida katika Bunge lijalo. Nadhani nimeeleweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, umeeleweka na upo utaratibu wa kutumia *revision* kwa *power* za *CPD*, lakini ulichokisema ni sahihi.

**MWENYEKITI:** Kwa haya yaliyopo hapa yalete tu. Mheshimiwa Waziri si tumeelewana? Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo tutakwenda kwa sura hiyo, kwa wale wenye nakala hii ya maerekebisho ya ile sehemu (A), sasa tunakwenda sehemu (B).

Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

Ibara ya 1
Ibara ya 2
Ibara ya 3

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 4
Ibara ya 5

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 6
Ibara ya 7

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 8

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 9

*(Ibara ilizotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 10

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mpina.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ibara ya 10 ya muswada baada ya aya ya pili kwenye majukumu yale *PPRA*, nimependekeza kuongeza kufanya tathmini ya zabuni iliyotolewa kwa kampuni ya ndani na kampuni ya nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na shabaha ya kuongeza jukumu hili hapa kwenye majukumu haya ya mamlaka ni kutuwezesha kupata takwimu za kutosha na kuweza kujua namna ambavyo kazi zinavyotolewa kati ya makampuni ya ndani na makampuni ya nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukizingatia kwa muda mrefu tumekuwa tukipigwa sana, bajeti yetu kubwa imekuwa ikitumika kulipa watu wa Nje kuliko watu wa ndani. Kwa hiyo, naomba pendekezo hili liridhiwe na Serikali ili ituwezeshe kupata hizi takwimu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kipengele hiki kwa upande wa Serikali tulipendekeza ibaki kama ilivyo. Hili hatukuwa tumeliafiki kwa sababu zipo taratibu ambazo zinafanya ufuatiliaji huu wote. Suala hili limezingatiwa kwa maana ya kipengele cha 10 kipengele kidogo cha muswada ambacho *PPRA* imepewa jukumu la ufuatiliaji wa utoaji wa tuzo na utekelezaji wa mikataba kwa kuzingatia vigezo vilivyopo. Kwa hiyo, lipo na *PPRA* wanafanya ufuatiliaji huo hatua kwa hatua na hicho ndicho ambacho kimekuwa kikifanyika mpaka hivi sasa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mpina, ufafanuzi huo wa Waziri? Lakini ukiwa unafafanua au ukipewa nafasi ya pili umesema kufanya tathmini ya zabuni zilizotolewa kwa kampuni za ndani na kampuni za nje. Unakususdia kuorodhesha? Kwa sababu ukisema kufanya tathmini unazungumzia tathmini ya kitu gani? Ya ubora, ukubwa, fedha zilizoingia huko au tathmini ya kitu gani?

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini ninayoizungumzia hapa ni kuhusu idadi ya zabuni zilizotolewa na thamani ya fedha zilizotolewa.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, ulikususdia orodha? Yaani kuorodhesha...

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *actually* ni orodha ambayo inazalisha idadi, halafu itazalisha thamani na

kwa muda mrefu takwimu hizi huwa hatuzipati, na kama *PPRA* wangekuwa wanalifanya jukumu hili, takwimu hizi tungekuwa tunazipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna madhara yoyote kwa Mheshimiwa Waziri kuridhia hili kwa sababu ni kuongeza jukumu ili tupate uwazi katika taarifa zao wanazozitoa.

**MWENYEKITI:** Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri kusudio analolisema Mheshimiwa Mpina, akisoma ibara ya 30 ile taarifa inayotolewa kwa mwaka lengo lake kubwa ni kuonesha tathmini ya utendaji wa kazi za ununuzi wa umma na thamani halisi ya fedha itakayojumuisha.

Kwa hiyo, kwa lengo la kupata nini kimefanyika kwa mwaka mzima na kwa kila aina ya tenda, itakuwa ikifanyika na taasisi inayofanya manunuzi na taarifa yake kujumuishwa kwenye taarifa ya mwaka.

**MWENYEKITI:** Sawa, Mheshimiwa Mpina, hapo kwenye 10(b) hiyo hoja yako haiwezi kuingia hapo? Kwa sababu 10(b) naona majukumu ya mamlaka na wewe ndiyo unasema iongezeke; kufuatilia na kutoa taarifa juu ya utendaji kazi wa mifumo ya usimamizi. Si ndiyo mambo hayo ama?

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla taarifa itatolewa kwa namna manunuzi yalivyofanyika, lakini ule uwiano wa manunuzi yaliyofanyika ndani ya nchi kwa makampuni ya ndani na manunuzi yaliyofanyika kwa makampuni ya nje hakuna *room* hiyo, kwa sababu, itatolewa tu kwa ujumla kwamba manunuzi yetu kwa mwaka huu yalikuwa hivi, tuliajiri makampuni kadhaa na hivyo kwa mtumiaji wa taarifa huwezi kujua kama unataka kujua, kwa sababu kama Waheshimiwa Wabunge ni lazima tupate takwimu hizi ili tuweze kujua namna ya kuishauri Serikali yetu.

**MWENYEKITI:** Hebu tusaidie. Si unayo hii sheria?

**MHE. LIUHAGA J. MPINA.** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio ninayo.

**MWENYEKITI:** Hebu nenda kwenye hicho kifungu alichokitaja Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali Kifungu cha 30(a); "tathimini ya shughuli za taasisi nunuzi kuhusiana na uzingatiaji wa sheria."

Sasa kwa kuwa sheria imeshaweka kwamba yale manunuzi ambayo..., aah, yaani leo Kiswahili kinanipiga chenga kwenye huu muswada. Manunuzi yale ambayo yanayofanywa na makampuni ya ndani na huku, hii tathmini ya shughuli za taasisi nunuzi yaani za ndani na nje, ndio hoja ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwamba hii 30 inataka taarifa ya *PPRA* iwe na taarifa hizi. Ama kwako ni tofauti? Ukizisoma hivi kwa pamoja hauoni kama inashika na hiii ya kwako.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiisoma hii kwamba tathmini ya shughuli za taasisi nunuzi kuhusiana na uzingatiaji wa sheria. Huu ni uzingatiaji wa sheria tu.

**MWENYEKITI:** Ambao ni pamoja na hiyo inayoonesha kwamba hawa wa ndani wanafika mpaka hapa na hawa wa nje wanafika mpaka hapa.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ule ukomo tutakapokwenda kwenye 57 ambayo Mheshimiwa Waziri anazungumzia kwamba amekubaliana na bilioni 50, lakini bado wazawa hawakatazwi kuchukua *tender* ya zaidi ya bilioni 50. Kwa hiyo, hauwezi kupata ile takwimu unayoitaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili ni rahisi tu. Nilikuwa namshawishi tu Mheshimiwa Waziri kwamba akubali kuweka kwa sababu haipunguzi chochote, ni kuongeza majukumu ambayo yamenyooka na hayana kona.

**MWENYEKITI:** sasa, nadhani hoja ya Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni kwamba hakiwezi kuwa kinajirudia hicho hicho kwenye sheria. Ukiweka sehemu moja ndio hiyo hiyo inakaba kila mahali. Haya kama haujaielewa hoja yako

nilifanye Bunge lifanye maamuzi. Mheshimiwa Mpina, umeelewa ama niipeleke hoja iamuliwe na Bunge?

**MHE. LUIHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ufafanuzi huo naomba tu kwamba tukubaliane tuendelee. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Shukrani.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 11

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 12
Ibara ya 13
Ibara ya 14

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 15

*(Ibara iliyotajwa hapo juu Ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 16
Ibara ya 17
Ibara ya 18
Ibara ya 19

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 20
*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 21

**SPIKA:** Kifungu cha 21 kufuta maneno; "mara kwa mara na ukiukwaji" aah Mbunge alichangia, na badala yake kuweka maneno "unaojirudia."

Mwanasheria Mkuu wa Serikali hii "inayojirudia" maana yake hata mara moja siyo?

**MWANSHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio kiwango cha kuanza kwa Afisa Masuuli kuchukua hatua kwa mujibu wa mamlaka aliyopewa.

**SPIKA:** Sawa, nafikiri Waheshimiwa Wabunge tunapopitisha sheria kama hizi na tumeambiwa taarifa italetwa, tutaitazama huko mbele utekelezaji wake maana mtu asije akasema hii kujirudia ni mara moja. Ninavyoelewa neno "kujirudia" ni mara moja ukisema "kujirudiarudia" ndio mara nyingi.

Kwa hiyo, na sisi tunaamini ndio tutakuwa na uelewa mmoja maana wakati mwingine kuna maneno yakitumika yanaleta zile tafsiri zinazotupeleka mbali. Kwa hiyo, nafikiri na ninyi mtaendela kutafakari maana ndio tunatunga sheria kwa kiswahili inatupa kidogo mtihani.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 22
Ibara ya 23

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 24

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 25
Ibara ya 26
Ibara ya 27
Ibara ya 28
Ibara ya 29

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 30

**MWENYEKITI:** Kifungu cha 30 marekebisho ya Serikali na Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina. Mheshimiwa Mpina.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ibara hiyo ya 30 ina marekebisho matatu (a), (b) na (c) lakini ile (a) inafanana na ile Ibara ya 10. Kwa hiyo, hiyo (a), naiondoa; na ya (b) ilikuwa ni mpangilio tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ile (c), ndio ambayo nataka kuitolea ufafanuzi hapa kwamba Mheshimiwa Waziri hapa amezungumza kwamba taarifa ya *PPRA* inapowasilishwa kwa utaratibu huo inayowasilishwa sasa hivi haiwezi ikalisaidia Bunge hili. Taarifa hii ni taarifa kubwa, taarifa inayoangalia *conscience* ya manunuzi nchi nzima na matumizi ya fedha haiwezi kukabidhiwa kwa Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Fedha ni mkaguliwa sasa mkaguliwa hawezi kukabidhiwa hii taarifa ya fedha na yeye aifanyie kazi. Kwa hiyo, ndio maana nikapendekeza kwamba hii taarifa sasa wakati tunaandaa Katiba kipindi kile kwenye *umbrella* ya *CAG* haya mambo ya *PPRA* hayakuwepo lakini tulipofika katikati tukagundua kwamba *CAG* hawezi ku-*cover* mambo ya *compliance* ya kimanunuzi ndio tukaanzisha *PPRA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, pendekezo langu hapa sasa kwamba mwanzo ilivyokuwa imependekezwa kwenye mapendekezo ya Muswada uliopo kwa sasa kwamba Rais aweza iende tu kwamba Rais atakabidhi taarifa hii kwa Waziri wa Fedha na Waziri wa Fedha ataiwasilisha Bungeni na baadae iende

kwenye *relevant committee* kujadiliwa kama inavyojadiliwa Taarifa ya *CAG*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishauri kwamba tuanzishe sasa Kamati inayoitwa Kamati ya Manunuzi na Mikataba kwa ajili ya kushughulika na mambo haya na nimuombe Waziri akubaliane tu ili tuweze kudhibiti matumizi yanayofanyika ovyo katika Taifa letu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mpina ameijenga hoja vizuri na mwanzo ndivyo tulivyokuwa tunaiangalia lakini tumepata ushauri ndani ya Serikali wa wataalamu wa sekta zote ambazo zinashughulika na masuala ya manunuzi zinazoshughulika na masuala ya Rufani za Manunuzi na masuala ya kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona kwamba *CAG* anafanya kazi za ukaguzi zote hizi ambazo Mheshimiwa Mpina amezisema zote zinafanyika ndani ya *CAG* na ambacho Bunge hata katika bajeti iliyopita ambacho ndio tulichoona ni cha msingi sana imeongeza zaidi nguvu kwa *CAG* ili kuweza kufanya hizi shughuli zote zinazohusiana na manunuzi zinazohusiana na *value for money* zote zinakuwa *covered* mle.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa ya *PPRA* ni taarifa ya kazi, ile Taarifa ya *CAG* ni taarifa ya *audit*. Kwa hiyo, tuliona kwa kweli taarifa ambayo inalisaidia Bunge na ndio jicho la Bunge ni Taarifa ya *CAG* na hizi zingine zitaingia kama taarifa za kazi kama za Taasisi zingine ambazo zinaingia kama taarifa za kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshawishi Mheshimiwa Mpina akubaliane na utaratibu huu uliopo wa Taarifa ya *CAG* kuwa ndio taarifa inayoingia Bungeni kama Katiba inavyoelekeza. Lakini pia akubaliane na Bunge ndio limekuwa ndio kiu ya mara zote kumuongezea nguvu *CAG* atakagua vyote hivi vinavyohusiana na manunuzi na atakagua vyote vinavyohusiana na *value for money* na taarifa ile itakuja ikiwa *comprehensive*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshawishi Mheshimiwa Mpina na nilishawishi Bunge likubaliane na hilo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mpina.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya Waziri hii Taarifa ya *CAG* huwa anachukua *summary* tu ya Taarifa ya *PPRA*. Ni *summary* tu na hata sasa hivi tukiweka vitabu vya *CAG* hapa anasema yeye mwenyewe kwamba mambo aliyoyachukua kutoka kwa *PPRA*. Lakini la pili mamba yanayofanywa na *PPRA* si yote yanayofanywa na *CAG* huyu nanazungumza suala la *compliance* ya manunuzi na uzingatiaji wa taratibu za manunuzi na *value for money* ndio kazi ya *PPRA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namshawishi na nalishawishi Bunge lako likubaliane kwamba tuweke msingi wa kusimamia rasilimali za Watanzania kwa kuhakikisha kwamba Taarifa ya *PPRA* inapata nafasi ya kutosha inaingia Bungeni inaenda kwenye Kamati tunaijadili vya kutosha tukija hapa tunafanya maamuzi kwa ajili ya Watanzania. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge Taarifa ya Kamati inasema kwamba Kamati ya Bunge ya Bajeti ndio iliyoishauri Serikali. Taarifa ya Kamati inasema pia katika Ibara ndogo ya 2 Kamati ilipendekeza kufuta takwa la taarifa hiyo kuwasilishwa Bungeni kwa sababu taarifa hiyo ni sehemu ya Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya kila mwaka inayowasilishwa Bungeni. *(Makofi)*

Vilevile kwa kuwa taarifa hiyo ni ya kiutendaji Kamati iliona hamna umuhimu wa kuwasilishwa Bungeni badala yake iishie katika ngazi ya Waziri mwenye dhamana ya ununuzi kwa ajili ya kufanyiwa kazi ili kurekebisha mapungufu yaliyobainishwa na mamlaka katika taarifa yake. Maboresho ya Ibara hii ni kama yanavyoonekana kwenye jedwali la marekebisho ya Serikali. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge maana Mheshimiwa Mpina analishawishi Bunge sasa Bunge Taarifa ya Kamati hii hapa. *(Makofi)*

Haya Mheshimiwa Mpina ameshasema lakini sasa kwa sababu kama nilivyosema tunaendelea kujifunza, Mheshimiwa Mpina umeelewa Taarifa ya Kamati ama unataka hoja yako niitoe kwa Bunge iamue?

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba uitoe kwa Bunge kwa sababu…

**MWENYEKITI:** Hiyo imeshaeleweka kwa sababu umeshapewa nafasi ya pili tayari.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, basi Bunge liamue.

**MWENYEKITI:** Haya ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge kwanza unatoa hoja samahani, unatoa hoja hii sehemu ya pili halafu nione inaungwa mkono ama haiungwi mkono.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa mwenyekiti, naomba nitoe hoja kwamba sasa naomba Bunge liniunge mkono.

**MWENYEKITI:** Ahsante umeshaeleweka. Haya hoja haijaungwa mkono kasimama yule kule amesimama aanh! Wawili ndio mmesimama na wewe ni watatu. Kwa hiyo, hoja haijaungwa mkono, hoja inaungwa mkono na watu kumi.

Waheshimiwa Wabunge, kifungu cha 30 pia kina marekebisho ya Serikali, Mheshimiwa AG marekebisho ya Serikali uko nayo na kile kifungu chenyewe mlichokuwa mmeleta uko nayo. Hiki kifungu cha pili baada ya ile hoja ya Bunge kwamba hii taarifa isije Bungeni bado kina maana ya kuwepo hapa na Sheria isiwe *superflux* hiki kifungu cha pili?

Kwa sababu unasema kuna mahali mnasema tufute maneno kuwasilisha taarifa hiyo Bungeni katika kikao cha Bunge kitakachofuata baada ya Rais kupokea taarifa hiyo. Halafu mnasema haya yakishafutwa na badala yake kuweka maneno kufanyia kazi taarifa hiyo yaani kifungu hiki kinataka kusema hivi. Mara baada ya kupokea taarifa chini ya kifungu kidogo cha

kwanza Rais anaweza kumwelekeza Waziri kuifanyia kazi taarifa hiyo yaani ndio kifungu kitakuwa kinasema hivyo.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana ya yote ambayo hata Mheshimiwa Waziri aliyaeleza kifungu cha pili marekebisho haya yanafanywa maana yake taarifa hiyo kwa maana ya Serikali kama kuna mambo ya kufanyiwa kazi yafanyiwe kazi mara moja kwa utaratibu wa kiserikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili, ambayo nafikiri hata Kamati haikupenda kufika huko, taarifa yoyote inapobaki kwenye *mandate* ya Wizara maana yake ile Kamati ya Bunge iliyona dhamana na wizara ile inaweza ikahitaji taarifa ya utekelezaji na kuchukua hatua zinazopaswa. Hata kama ingetenganishwa na ile dhana ya Taarifa ya *CAG*.

**MWENYEKITI:** Yaani namaanisha hivi ukisoma hii 30(1)(2) baada ya hayo marekebisho kina maana yoyote? Yaani bado ya hiki kifungu kidogo cha pili kinakuwa na maana kwamba yaani hapa mwanzoni umesema atapelekewa Mheshimiwa Rais si ndio? Hapa chini unasema mara baada ya kupokea taarifa hiyo yaani kama vile tunamtungia Sheria Rais kwa Waziri. Sijui kama nimeeleweka Mheshimiwa *AG*? Yaani hiki kifungu cha pili kinasema Rais akipokea ampelekee Waziri kwa ajili ya utekelezaji ndio maana yake, Mheshimiwa Waziri naona unataka kusema jambo.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilivyomuelewa *AG* na nilivyokuelewa kwamba baada ya maoni ya Kamati tuende na utaratibu wa maoni ya Kamati na *flow* ile itakuwa inafuata taratibu za kawaida.

**MWENYEKITI:** Ni sawa kifungu hiki bado kinahitajika? ndio hoja yangu. Yaani hiki cha kwanza ni kama kimeshajitosheleza.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio kimejitosheleza.

**MWENYEKITI:** Sasa hiki cha pili tunakihitaji cha nini? yaani kwamba tunamwagiza Rais amwambie Waziri aifanyie kazi hii taarifa*, is it obvious*?

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hakina ulazima baada ya huu ufafanuzi tulikiweka kwa sababu ilikuwepo jambo ambalo tulikuwa tumeandaa mwanzoni kabla ya makubaliano na Kamati. Kwa hiyo, tuende na hiki unachoelekeza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa AG imeeleweka kweli?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana tukichukua ile 30(1)(c) nafikiri tunaweza tukaachana na hiyo Ibara ndogo ya (2) kwa sababu ilikuwa ni *necessary repetition* ambayo haipunguzi lolote.

**MWENYEKITI:** Kwa sababu kama ingekuwa Rais anampa Waziri ili alete Bungeni kifungu kiko sawasawa lakini kama Rais hampi Waziri ili alete Bungeni, Rais kumpelekea Waziri hatuwezi kutungia Sheria yaani inakuwa imekaa kiaina fulani hivi.

Kifungu cha 30 pamoja na marekebisho ya Serikali mliyokuwa mmeyasema kabla ya kusema haya maneno maana kuna na mengine ambayo mmebadilisha hapo. Hiki kifungu cha pili hakina maana yoyote kwenye kusoma. Yaani kusoma hiki kifungu ili kilete maana kinabaki kile cha kwanza na cha pili hakina maana. Sijui kama mmesoma wote Wabunge, si mnazo kwenye jamii? Ndio tunatunga Sheria hapa maana usiseme mimi sijui nilikuwa sijaona pale, haya kifungu kidogo cha 2 kinaondoka Waheshimiwa. Marekebisho yanayohusu kifungu kidogo cha 1, yanaafikiwa.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 31

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 32
Ibara ya 33
Ibara ya 34

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 35

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 36

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge hoja hii saa hizi tuko kutunga Sheria siyo hoja tena maana naona hamuitiki mmenyemaza kama vile… hizi sauti lazima zisikike kwenye Taarifa Rasmi za Bunge kwamba mliitika ndio. Kwa hiyo, nisiwe nasikika tu mwenyewe halafu ikaonekana Mheshimiwa Spika alipitisha peke yake Sheria Bungeni.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 37

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 38

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 39

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 40
Ibara ya 41

*(Ibara zilizotajwa Hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 42
Ibara ya 43
Ibara ya 44

*(Ibara zilizotajwa hapo Juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 45

*(Ibara iliyotajwa Hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 46
Ibara ya 47
Ibara ya 48

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 49
Ibara ya 50

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 51

*(Ibara iliyotajwa hapo juu Ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 52

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 53
Ibara ya 54
Ibara ya 55

*(Ibara Zilizotajwa Hapo Juu Zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 56

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 57

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Eric Shigongo.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sifa moja kubwa ya Serikali ya Awamu ya Sita ni usikivu kwa wananchi wake. Serikali imesikia na nimesikia maelezo ya Mheshimiwa Waziri ingawa lengo hasa la kutaka jambo hili liandikwe kwenye Sheria ilikuwa ni kuepuka kuwa pengine na Waziri huo mbele ambaye hatakuwa mzalendo na mwaminifu kama ilivyo kwa Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu kitu kikiwa kwenye kanuni Mheshimiwa Waziri anakuwa na *description* ya kutunga kanuni lakini Sheria huwezi kuigusa. Leo hii tuna Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, namwamini sana Mheshimiwa Dkt. Mwigulu na kwa *commitment* aliyoifanya hapa ndani Watanzania wanamsikia ambayo naamini huko nje kuna furaha kubwa sana kwa uamuzi aliousema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu nitoe hoja hiyo na nikubaliane na mambo aliyoyasema ya kwamba bilioni 50 zitatumika lakini nilikuwa na ombi Bunge lilete hapa Bungeni Sheria ile ya Uwezeshaji Wazawa Kiuchumi ya Mwaka 2005 ili tuifanyie marekebisho ili tuweze kueleza kila kitu wazawa wanatakiwa kufanya nini ndani ya sheria ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipotunga sheria ile kwa maelekezo ya Bunge lako tukufu…

**MWENYEKITI:** Sasa ngoja Mheshimiwa, ombi lile la jumla limeeleweka kwa sababu kwenye ngazi hii tuko kwenye kutunga Sheria kwa sasa ukianza kueleza ile sheria tena kidogo tutakuwa tuna changanya mambo. Labda kama bado uko hapa, kama ni kuhusu ile Sheria ombi la jumla umeshaleta kwamba ile Sheria inahitaji marekebisho.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme tu kwamba nimekubaliana na bilioni 50 alizozitamka na Watanzania wamemsikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kulikuwa na marekebisho mawili hapo, kulikuwa na A, pamoja na B, kama unaona B, ilikuwa ninaomba kuondoa kabisa Ibara ndogo ya 4 ambayo nikiisoma naiona ni kama uchochoro wa kufanya kilekile ambacho tumekibadilisha kwenye ile Ibara ya 1.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niisome, inasema "endapo Taasisi Nunuzi haijapokea *offer* zinazokidhi vigezo kutoka kwa watu au kampuni za ndani ununuzi uliotengwa utaondolewa na ikiwa vigezo bado viko halali *offer* mpya zitatangazwa kwa mara nyingine kwa misingi isiyo na upendeleo".

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini ni kwamba sasa itatangazwa kwa mara ya pili bila huu upendeleo ambao tumeweka kwenye Ibara ya 1. Sasa nilikuwa naomba hiki kipengele kama tumekubaliana kwenye bilioni 50 hiki kipengele namba nne tukiondoe sioni sababu ya kuwepo ili tutimize kabisa azma yetu ya kuwatetea wazawa, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shigongo hii ikishawekwa shilingi bilioni 50 na umekubali kwamba hii shilingi bilioni 50 kifungu cha kwanza kinaweza kubaki kilivyo na hii shilingi bilioni 50 ikawekwa kwenye kanuni kama alivyosema Mheshimiwa Waziri. Hoja yako ya kuondoa hii namba nne bado inakuwepo kama kile kiwango kikipandishwa mpaka shilingi bilioni 50?

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja inatakiwa iendelee kuwepo.

**MWENYEKITI:** Hebu nieleweshe mimi hapa, maana jamani tupo kwenye…

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikufafanulie…

**MWENYEKITI:** Ngoja kwanza ili uelewe kitu gani sijaelewa.

Ukisema hii iondoke shilingi bilioni 50 sio parefu sana lakini ni parefu, ikatokea kwamba hivyo vigezo vimeshindikana, hiki kifungu kina shida gani? Kama wakishapandisha kwamba 50 kama wapo wanaoweza wazawa si watapata? Ni pale ambapo sasa hii ni shilingi bilioni 50 halafu bado imeshindikana, ndipo kifungu hiki kitaisaidia Serikali kwamba iendelee na hiyo kazi, maana la si hivyo kazi itasimama. Ama hata kama imeshindikana bado iwe?

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba na hicho kipengele cha pili nikiondoe.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nadhani mmeelewa hoja ya Mheshimiwa Shigongo. Kwa sababu hiki kifungu cha nne ni muhimu kiwepo hapa kwa sababu mwanzo kilitangazwa watu wameshindwa, sasa ukisema utaendelea tena hivyo hivyo tena sasa Serikali itasimama na sisi tunataka kule majimboni mambo yafanyike, na hivyo itakuwa mtihani.

Kwa hiyo, hoja yake ameiondoa; kwa maana ya kwamba Mheshimiwa Waziri alishajibu kwamba ataenda kuifanyia kazi kwenye kanuni, kwa hiyo, hivi kilivyo hapa ni sawa kwake yeye. Sasa kifungu hiki pia kina marekebisho kutoka kwa Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipendekeza kwamba katika hii Ibara ya 57 kwamba kwanza yale maneno ya kanuni yaondolewe na ninafurahi kwamba imekubalika kwanza kuweka fedha badala ya kusema kanuni. Lakini nilipendekeza ziwe bilioni 100, wazawa wapewe *room* kubwa, wigo mkubwa wa kuomba *tender* kubwa ndani ya nchi yao. Fedha hizi ni za kwetu na hivyo hatuna sababu hata ya kurembaremba kuanza na shilingi bilioni 50, twende kwenye shilingi bilioni 100 ili tutoe nafasi kubwa zaidi kwa Watanzania, tumeshapigwa mno muda mrefu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri ufafanuzi.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kile alichokisema Mheshimiwa Shigongo na ambacho amekuja kurudia Mheshimiwa Mpina, kile alichosema Mheshimiwa Shigongo kilikuwa kinahusisha kuhusu kutangaza kwa kampuni za ndani zipate fursa ya kufanya hiyo kwa shilingi bilioni 50 na kwa shilingi bilioni 60 iende kwa *international tendering,* tumeona hiyo tuikubaliane nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hii ambayo amesema Mheshimiwa Mpina tumeitafutia dirisha lingine lile kwamba kwa kadiri kazi zinavyokuwa kubwa nadhani yatakuwepo kwenye marekebisho mengine, tumewapa fursa Watanzania kuwa kiongozi kwenye mradi. Hili ni jambo kubwa sana, kubwa mno. Ni kubwa hata kuliko hiyo shilingi bilioni 100. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani hapa tu ni Watanzania kujiamini, maeneo mengi ilikuwa inatokea Mtanzania akipewa hata kibali cha kuagiza sukari anaenda kukiuza kwa watu wengine. Watanzania wajiamini, akipewa kazi aifanye ili kujenga *capacity*.

Kwa hiyo, tuna jambo tumeliweka ambalo ni kubwa, kimsingi tumekubaliana na maoni ya Waheshimiwa Wabunge yote haya ya kuwafanya Watanzania wa-*enjoy steak,* wawe viongozi kwenye shughuli za uchumi ndani ya nchi yao. Kwa maana hiyo hii tuliyoweka shilingi bilioni 50 ni kwa ajili ya

*tendering,* lakini kwenye ushiriki tumeshaongeza, tumeongeza hata inayozidi na hiyo shilingi bilioni 100.

Kwa hiyo, niwashawishi Waheshimiwa Wabunge kwa hii *setup* tuliyoiweka bado ina-*cover* maoni hayo yote ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mpina.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri anasema kwamba ameshaweka mahali, sasa mahali ni kwenye Ibara gani ya muswada huu? Kwa sababu nchi hii ni ya kwetu sisi, rasilimali hizi ni za kwetu, bajeti tunazozipangia kuwa-*award* watu kwenye zabuni na kwenye shughuli nyingine zote ni fedha za Watanzania. Kuna uoga gani wa kuwapa shilingi bilioni 100? Wakishindwa si tutaenda hii *option* ya pili? Kwani kuna tatizo gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalishawishi Bunge lako likubali kutoa hiyo *favour* kwa Watanzania waweze kufikia ule wigo wa shilingi bilioni 100.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mpina toa hoja yako Serikali ilishatoa ufafanuzi.

Aah! haya umeuliza swali anataka kukujibu kabla hujatoa hoja.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kusema kiko wapi, nni kwamba hatujakifikia tu, vile vipengele vya upendeleo tumeviweka kwenye Ibara ya 61 tutakapofika, kwa hiyo tunasema tunasema Watanzania wataruhusiwa kuomba kazi, aoneshe tu *line up* nyuma kampuni kubwa ambazo atakuwa nazo. Kwa hiyo, hilo nadhani ni jambo ambalo linawapa fursa kubwa zaidi Watanzania kuliko hata hii shilingi bilioni 100.

**MWENYEKITI:** Haya, Mheshimiwa Mpina kifungu cha 61 kinaeleza hapo moja, mbili, tatu, kuna maelezo hapo anayoyasema Mheshimiwa Waziri. Soma hiyo namba mbili hapo inayosema; “Endapo kampuni binafsi hazina uwezo wa

kutekeleza mikataba kampuni hizo zinaweza kuanzisha ushirika kwa lengo la kuimarisha uwezo wake;" na namba tatu; "Waziri anaweza kutengenze kanuni zitakazoainisha taratibu za kujenga uwezo kwa kampuni za ndani chini ya kifungu hiki."

Haya umeshaelewa ama unataka kutoa hoja?

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshaelewa, *actually* haihusiana na hapa, lakini nachotaka kusema hiyo Ibara hiyo ya 90 haihusiani na hiki tunachokizungumza hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nataka niseme hivi, kwa sababu Serikali wamekubali walau kuanzia na hiyo shilingi bilioni 50 sisi tutaendelea kadiri tutakavyoona kushauri tena kupandisha hivi viwango, lakini kwa sasa hivi kwa maana ya hatua hii ya kuongeza mpaka shilingi bilioni 50 tunaipongeza Serikali, tuanzie hapo lakini tuendelee kupandisha viwango vyetu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Shukrani, Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 58
Ibara ya 59
Ibara ya 60
Ibara ya 61

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inafanya marekebisho kwa kuongeza kifungu kipya cha 62 na hivyo basi marekebisho haya yatafanyika kwa kubadili mpangilio wa kifungu cha 62 hadi 130 kuwa kifungu cha 63 hadi 131 mtawalia.

**MWENYEKITI:** Katibu vihoji vifungu vinavyofuata kimoja kimoja halafu haya maelezo tutayahoji mwisho ya kubadilisha mpangilio.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

Ibara ya 62

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 63
Ibara ya 64
Ibara ya 65
Ibara ya 66

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 67

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 68

**MWENYEKITI:** Kifungu cha 68, Mheshimiwa Mpina.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba hicho kifungu cha 68 kama nilivyopendekeza hapa kwamba baada ya Ibara ndogo ya 15 iongezeke Ibara nyingine ya 16 ambayo italazimisha mikataba walau yenye thamani ya kuanzia shilingi bilioni 50 inapokuwa *tender* imetangazwa na mkandarasi amepatikana au mzabuni amepatikana, ukiondoa zile za halmashauri ziletwe hapa kupitia Kamati zetu kwa ajili ya uhakiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shabaha yake tumepigwa mno, mikataba mibovu tumeimba kila leo, lakini bado Serikali inaingiwa. Kwa hiyo, ili ku-*cure* hili ni muhimu sana tukaanzia *oversight function* ya Bunge hili mapema wakati mkataba tu

unapongiwa ili kujiridhisha na vigezo pamoja na vipengele vilivyomo humu kwenye mkataba, kwamba vina uzingatiaji wa namna gani, na kwamba *value for money* imezingatiwa kiasi gani, ili kuliepusha Taifa hili kila siku kuingia kwenye mikataba mibovu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niombe Mheshimiwa Mpina asi-*overgeneralize,* hii kauli ameirudia sana ya tumepigwa mno, tumepigwa mno, tumepigwa mno. Maeneo katika nchi yetu ambayo ubadhirifu umetokea hatua zimechukuliwa, huo ndio utaratibu wa *good governance* kwamba jambo linatokea sheria inachukua hatua yake. Tuki-*overgeneralize* nadhani tutakuwa hatuitendei haki nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, sasa kwenye hili analolisemea la mikataba ya angalau shilingi bilioni 50, kwenye trilioni 30 naa, hata ukichukulia shilingi trilioni 30 tu kuna shilingi bilioni 50 nyingi sana. Kusema hizo zote ziletwe Bungeni ndipo kazi ianze tunaenda kuigandisha hii nchi kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani tunatakiwa tujenge utaratibu wa kuviamini vyombo vyetu pamoja na taasisi zetu. Utaratibu mzuri kwenye nchi yoyote ili kuweza kupiga hatua ni kufanya kazi kitaasisi. Lakini tukisema kwamba taasisi zingine zote zime-*flock* isipokuwa tu mikataba yote iletwe Bungeni, tutaligeuza Bunge lifanye kazi za Serikali.

Sasa mimi kwa maoni yangu Bunge likishaituma kazi Serikali, ikishaipitishia Bajeti, likaituma kazi na *oversight committee*s zikaenda, tuendelee kufanya utaratibu ule wa kiufuatiliaji na maeneo ambayo yataonekana hayakufanyiwa vizuri hatua za kisheria zifanyike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, utaratibu wa kusema mikataba yote inayozidi shilingi bilioni 50 iletwe Bungeni kabla ya kusainiwa, tutafanya shughuli za maendeleo zitasimame, yaani tutakuwa tu na kisima hapo, mradi wa visima unafika shilingi bilioni 50 hazisainiwi mpaka zije hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uzoefu uliopo kuna wakati tu tulisema *exemption* za kwenye miradi zisainiwe na Waziri, miradi yote ya maji ilisimama, tukarudi hapa kubadilisha kwamba zibaki kwa Kamishna wa Mamlaka ya Mapato ambaye anakasimisha kwa mameneja walioko katika maeneo husika ya miradi wapitie miradi na kuruhusu shughuli ziendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi nimuombe Mheshimiwa Mpina akubaliane na utaratibu ambao unatumika wa kuhakikisha kwamba Bunge linaipa kazi Serikali, Serikali inafanyakazi yake na Bunge linaisimamia Serikali. Tukilipeleka Bunge kwenye kusaini mikataba nadhani litakuwa limewahisha shughuli kabla ya ile ambayo inatakiwa ifanye ya msingi ya kuisimamia Serikali. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mpina naona umesimama.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza sijasema kwamba mikataba hiyo iletwe hapo kabla haijasainiwa. Ni mikataba iletwe hapa Bungeni kupitiwa Kamati Maalum ya Manunuzi na Mikataba baada ya kusainiwa kwa ajili ya uhakiki na la pili, …

**MWENYEKITI:** La pili una maanisha nini Mheshimiwa?

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahh, sio la pili, katika muendelezo wa kufafanua hiki ambacho ninachokieleza kusisitiza hoja yangu.

**MWENYEKITI:** Hoja yako imeeleweka Mheshimiwa na sasa kama Mwenyekiti, maana niliacha Serikali itoe ufafanuzi, lakini hoja kwa sababu inahusu Bunge kufanya kazi fulani.

Waheshimiwa Wabunge, tukitaka kufanya hii kazi sijui tutaisimamia Serikali kwa ngazi gani, kwa sababu maana yake tutakuwa sehemu ya ufanyaji wa ile kazi, sasa baadaye mambo yasipokuwa mazuri Serikali itasema lakini mkataba ninyi si ndio mliohakiki. Sasa sisi hapo tunahusikaje? Kwa hiyo, nani atakuwa anamuuliza mwenzie? Acha hapa inapotajwa bilioni, hata

mkataba wa trilioni kuuleta hapa Bungeni ni Serikali iwe inafanya huko likitokea jambo ndio sisi tuisimamie Serikali. Lakini kwamba ituletee ili sisi tuhakiki, kidogo itatupa mkanganyiko wa namna ya kufanya yale majukumu yetu ya Kikatiba. Sasa pamoja na hayo, nilimuona Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti amesimama.

**MHE. DANIEL B. SILLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, umeyasema vizuri sana. Nilikuwa nasema tu kwamba maudhui makubwa ya kubadilisha Sheria ya Ununuzi ni kwa ajili kupunguza michakato ya ununuzi na Serikali kufanya kazi yake. Sasa jukumu la Bunge ni kuishauri na kuisimamia Serikali, tukianza kuwa sehemu ya mikataba inayoingiwa na Serikali, pale ambapo inatekelezwa vibaya maana yake itakuwa imetungwa na Bunge.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba Serikali ifanye kazi yake na sisi kama Bunge tufanye kazi yetu ya kuisimamia Serikali, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mpina, umenielewa?

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, unaniruhusu kufafanua au kusemaje yaani? *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Yaani hiki kifungu unataka tukiweke...

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, unachokizungumza mimi nakuelewa vizuri, lakini hata mikataba yenyewe ya *natural resource* tulikuwa hatuileti hapa Bungeni, lakini ilipofika…

**MWENYEKITI:** Ngoja, hata ile mikataba si kwamba hatuileti hapa Bungeni, wewe kama Mbunge nenda huko ukishaona kuna mkataba mahali hautekelezwi sawasawa ambao tayari Serikali ilishaingia ndipo useme ili Bunge lichukue maamuzi, yaani sisi ndio Bunge lenyewe, hakuna Bunge lingine, na wewe ndiwe Mbunge.

Kwa hiyo, kama kuna shida mahali ni sisi tunaita tu huo mkataba, lakini kwamba sisi tuwe sehemu ya ule mkataba tutakuwa hii sheria tunatunga kwa ajili ya kuchukua sasa madaraka ya Serikali ambayo kwa kweli hatuna mpango wa

kuchukua. Serikali ifanye kazi yake na sisi tufanye ya kwetu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, hoja yako nafikiri ni hiyo ya kwamba unataka ile mikataba kama ukiwa na jambo hivi, ile unaruhusiwa kabisa sheria si zipo Mheshimiwa, ila hapo pa kusema kabla hapa ndipo kidogo itakuwa mtihani, tutakuwa na sisi tumeingia kwenye utekelezaji wa shughuli za Serikali, jambo ambalo si kazi ya Bunge. Lakini kwenye kuisimamia Serikali mikataba iliyoingia hiyo tunaweza kufanya.

Sasa kifungu chako unachopendekeza hapa kinalipeleka Bunge kwenda kuanza kufanyakazi za Serikali. Nimeeleweka au bado?

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, …

**MWENYEKITI:** Kama sijaeleweka toa hoja kwa Bunge, Bunge liamue ili twende…

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifupi sana…

**MWENYEKITI:** Wewe hoja yako ilishaeleweka na mimi umesema umenielewa, lakini hujaridhika. Toa hoja Bunge liamue halafu tusonge mbele, vifungu bado vingi na wewe mwenyewe pekee yako una marekebisho mengi tu.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia maelezo yako, hili jambo litahitaji *engagement* zaidi, kwa hiyo, katika hatua hii mimi nakubaliana na hicho ulichokielekeza na kitafanya *engagement* zaidi ili tuelewane hapa ninachozungumza ni nini.

**MWENYEKITI:** Sawa, shukrani. Waheshimiwa Wabunge.

Ibara ya 68

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 69
Ibara ya 70

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 71
Ibara ya 72
Ibara ya 73

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 74

**MWENYEKITI:** Kifungu cha 74, Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimependekeza hapo kwenye kile kipengele cha kwanza, kufuta maneno; "kwa kuzingatia taratibu zilizoainishwa kwenye kanuni," maana yale maneno yalivyowekwa pale ni kama yanaiua kabisa sheria yenyewe. Kwa hiyo, mambo ya kuzingatia kwenye kanuni yaondoke, sheria isimame kama ilivyopendekezwa. Maneno mengine yabaki, lakini hayo maneno tu yaondoke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini (b) yake ninapendekeza kwamba katika hii hatua ya kipengele cha 74 wanapokuwa wamefanya hizo hatua za kuchagua njia ya manunuzi, na wameamua kutumia *single source,* na kwa sababu *single source* eneo hili Waziri anasema narudia sana. Tumeumizwa sana kwa sababu tuna mfano wa fedha kupigwa kwenye maeneo haya.

Sasa watu wasiende kwenye *single source,* hata kama vile vipengele vilivyoainisha kwamba ili ukidhi matakwa ya *single source* ni moja, mbili, tatu, hata kama taasisi nunuzi imekubaliana na hilo, lakini wapate *approval* ya mamlaka ili sasa tuweke jicho lingine na tusiruhusu huu utumiaji holela wa njia ya *single source* ambao umekuwa ukituletea hasara kubwa sana kama Taifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali tunakubaliana na kile kipengele cha kwanza alichokisema Mheshimiwa Mpina kinachosema kufuta "uzingatiaji" tukiangalia pendekezo alalilotoa hatuna tatizo nalo, linalosema; "kuhusu kufuta maneno kuzingatia taratibu zilizoainishwa katika kanuni" kwa sababu imeshawekwa kwenye sheria. Lakini kile kipengele cha pili tulikuwa tunapendekeza kibaki vilevile kile kinachohusisha masuala ya namna ya kununua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna taratibu ambazo zimebainishwa ndani ya nchi ambazo tunazitumia. Ukiondoa kabisa kipengele cha aina hiyo, kuna maeneo ambayo yanaweza yakakwamisha utekelezaji wa baadhi ya majukumu ya muhimu ambayo yanakuwa na ulazima. Kwa sababu hiki tunachokifanya ni kutunga sheria, ni kama kwenye kipengele kile ambacho tulisema tutoe fursa inapotokea njia mojawapo haijatumika. Ni vizuri tukaendelea kuibakizia Serikali mwanya mwingine kufuatana na umuhimu wa jambo lenyewe ambalo linatakiwa kufanyika.

**MWENYEKITI:** Hebu hiyo sehemu ya kwanza Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, yakifutwa haya maneno kifungu bado kinakuwa kiko sawa? Yaani tukiishia maneno: "Taasisi Nunuzi inaweza kuzuia mwaliko wa zabuni."

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapana; ni muhimu lazima ziwepo kanuni kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri kwa sababu ndiyo zitasaidia zile Kamati pamoja na mamlaka husika katika ngazi zote za mchakato.

**MWENYEKITI:** Hebu nieleweshe mimi, Mheshimiwa Waziri anasema hii sehemu ya kwanza ya mapendekezo yaliyotolewa na Mheshimiwa Mpina kwenye (a) katika Ibara ya 74 (a) kwa kufuta maneno: "Kwa kuzingatia taratibu zilizoainishwa katika kanuni" haina shida yakifutwa, kifungu kitakuwa kiko sawa?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hakitakuwa sawa.

**MWENYEKITI:** Haya, Mheshimiwa Mpina ufafanuzi huo umeshatolewa, kama hujaridhika unatoa hoja, Bunge liamue.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwa sababu sijaridhika na ufafanuzi wowote uliotolewa.

**MWENYEKITI:** Haya, hoja haijaungwa mkono, huyo aliyekuwa amesimama kumbe anaondoka zake. *(Kicheko)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge zima pamoja na marekebisho yake)*

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

Ibara ya 75

**MWENYEKITI:** Kifungu cha 75 Mheshimiwa Luhaga Mpina.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tulivyo Wabunge wengi wamezungumza hapa suala la *task force* kwa nguvu kubwa sana na lilivyotupa matatizo makubwa. Sasa badala ya kusema Waziri tumpe mamlaka hapa yeye akatunge kanuni kule tuweke kabisa hapa kwamba, walau miradi pamoja na masharti yaliyotolewa ya kwamba ili uweze ku-*qualify* kuingia kwenye *task force* lazima ufuate utaratibu huu na huu na huu kama ulivyoainishwa kwenye sheria sina tatizo nao, lakini tuweke kiwango cha mwisho kwamba miradi walau tu yenye ukomo wa shilingi milioni 50 na kushuka chini, hiyo ndiyo inaweza ikaingia kwenye suala la *force account*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi ni huo kwamba, miradi mingi imekuwa ikiishia njiani, miradi mingi imekuwa ikileta usumbufu mkubwa, miradi mingi imekuwa ikiwasumbua sana Walimu wetu na Madaktari kugeuka kuwa wanunuzi badala ya kutibu wagonjwa na badala ya kufundisha Watoto. Kwa hiyo napendekeza kwamba, inapotokea kwamba tunahitaji *force account,* basi mradi huo usizidi shilingi milioni 50. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namwelewa Mheshimiwa Mpina, lakini sisi hapa sote ni Wabunge na tuna majimbo yetu. Wananchi wetu kule chini wanafurahia sana na wenyewe kupata hizi fursa kuliko utaratibu tu wa kubakiza shughuli zote kubwa kubwa pale kwenye maeneo yetu zifanywe na zabuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitumia hii lugha nisamehewe tu; kuna maeneo mengine unaweza ukakuta watumishi siyo waaminifu, mkishasema zote zifanyike kwa kuleta makampuni, mnaweza mkakuta wilaya nzima ama mkoa mzima wanaofanya hizo kazi wanatoka alikotoka Afisa Manunuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa shilingi milioni 50 sasa hivi ni kizahanati kidogo sana, ukienda kwenye hizi ramani mpya zinazotumika sasa hivi, zahanati tu imeshazidi hapo kwenye shilingi milioni 50. Kwa hiyo sasa tutakuwa tumebakiza wale watu wetu pale *force account* labda wajenge matundu ya vyoo, wajenge kitu gani kingine kidogo kidogo?

**MWENYEKITI:** Haya, ahsante sana.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani jambo la msingi hapa, zile kamati zetu zinazosimamia masuala haya ziwe imara. Sisi tumeweka angalau iwe shilingi milioni 100, lakini najua hata hiyo kwa sababu ni kanuni, tunakokwenda tutabadilisha tu, kwa sababu hii ndiyo kujengea watu hasa uwezo na wale ambao wanaopewa hizo kazi, wanaofanya hizo kazi na wenyewe wanapata mkate, tunapunguza watu kufanya vitendo vingine vya kihalifu, wafanye hizo shughuli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimshawishi Mheshimiwa Mpina akubaliane kwamba taasisi zetu zinazofanya *force account* waimarishe zile kamati, ili asilazimike yule kama ni mtumishi aliyepewa majukumu mengine yeye kugeuka ndiyo afanye zile kazi, kwa sababu kimsingi zinakuwa kamati ambazo zinafanya majukumu hayo. Kwa hiyo nimwombe akubaliane na pendekezo la Serikali na sisi tutakubaliana na maoni yake, Waziri wa TAMISEMI yupo watazingatia kuweza kutengeneza njia nzuri

zaidi ya kusimamia ili ufanisi uwepo, lakini pia kazi zingine za majukumu ya kila siku ziwepo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri umesema hapo shilingi milioni 100, iko kwenye sheria au unakusudia kuweka shilingi milioni 100 kwenye kanuni au iko hapa?

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nasema sisi kwa sababu haya yataenda kuandikwa kwenye kanuni, sisi tunakusudia isiwe tu milioni 50, kwa kuwa milioni 50 bado ni ndogo kwa sababu majengo tunayojenga yameshakuwa makubwa. Ukitaka kuona Mheshimiwa Rais alipoleta fedha za UVIKO, furaha ilitapakaa kila eneo kwa sababu kila eneo watu walipata kazi.

**MWENYEKITI:** Nilitaka tu kujua hiyo kwa sababu kama unaenda kuweka 100 huko kwenye *force account* hoja yako ya mwanzo inakuwa tena, leo Kiswahili jamani, inakuwa tena *defeated.* Zahanati inajengwa kwa shilingi milioni 250, kituo cha afya shilingi milioni zaidi ya 500, sasa ukisema *force account* shilingi milioni 100 ndiyo matundu ya vyoo.

Kwa hiyo pamoja na hizo kanuni, nafikiri hoja kubwa ni usimamizi, hoja kubwa ni usimamizi, lakini kwa maana ya *force account* kama wanaweza kufanya kazi nzuri wajenge tu. Ndiyo, katafuteni namna nyingine, lakini hiyo unayosema shilingi milioni 100 kwa kweli utarudi pale pale, utakuwa husongi mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mbunge umesimama sijajua ni kanuni ipi? Au kwa vile nilimwita Mheshimiwa Mwenyekiti kule? Haya Mheshimiwa Mbunge unasemaje?

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Najaribu tu ku-*interfere* kidogo japo mimi siyo mtoa hoja, lakini kama Mbunge uzoefu unatuonyesha katika maeneo yetu zikiwemo hospitali za wilaya ambazo zinajengwa kwa mabilioni, zile fedha zinapokuja zinagawanywa tu kwa mafundi kidogo kidogo, hata kama ni shilingi milioni 500 wanagawiwa mafundi watatu au wanne, hata kama ni shilingi bilioni moja ni kwa *style* hiyo. Maana yake ni namna tu ya urahisi wa kusimamia, ukisema

unaenda kuweka kwenye kanuni kiwango cha fedha tunaenda kudhoofisha miradi ambayo inakwenda kwenye halmashauri zetu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, nadhani Mbunge aliona wewe ulivyotaja ile kidogo itafanya watu wa pale jimboni kwake wasipate kazi na nadhani kila Mbunge anataka watu wa jimboni kwake wapate kazi. *(Makofi)*

Hoja kubwa ni usimamizi, kwenye fedha ukataje kule kwenye zile za kuwapa wale wageni zifike ngapi, lakini huku kwingine huku wewe weka tu mazingira mazuri kwenye hizo kanuni ili usimamizi uwe mzuri.

Haya, Mheshimiwa Mpina hii hoja umeshaitoa? Haijaamuliwa eh? Ama umeelewa?

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, umeshatoa maelekezo, kwa hiyo sasa napata wakati mgumu kusema chochote.

**MWENYEKITI:** Afadhali.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 76

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 77

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mpina.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hicho kifungu cha 77 naomba kufuta Ibara ndogo ya pili na kuandika maneno yafuatayo kwamba; "Bidhaa za Huduma zitakazonunuliwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (i) zitakuwa

ni zile tu ambazo zinapatikana kwa muuza au mtoa huduma mmoja pekee."

Mheshimiwa Mwenyekiti, shabaha ni hiyo kwamba, pamoja na vipengele vingine vyote vilivyowekwa ni muhimu sana kuhakikisha kwamba unapotaka kwenda kwa mnunuzi mmoja; je, kweli hiyo bidhaa unayoenda kununua kwa mnunuzi mmoja haitolewi na kampuni jingine? Haitolewi na kiwanda kingine? Ili tusije tukatoa mwanya hapa wa watu kufanya upendeleo na watakapofanya upendeleo maana yake watata uwekezaji, lakini pia watatupeleka kwenye thamani kubwa ambazo hazimo kwenye utaratibu. Kwa hiyo nashawishi Bunge lako na wewe mwenyewe na Waziri akubali kwamba hiki kifungu tukiongeze ili kuweza kuleta thamani zaidi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja anayoitoa Mheshimiwa Mpina kwa nadharia inawezekana, lakini katika *practice scenarios* ziko nyingi. Yeye anasema kwamba Serikali iende kununua huduma kwa mnunuzi moja kwa moja endapo tu mnunuzi huyo yuko peke yake, mazingira yalishabadilika, lakini tulichokuwa tunasema, kama jambo linajulikana lile pale liko (a) na lina mazingira yale mengine ambayo yana-*meet requirement* za kununua moja kwa moja kwa mnunuzi, kwa nini tutengeneze mizozo mingine ambayo na yenyewe inaweza ikaleta tu matatizo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kwa sababu Sheria hii inatoa tunatunga sheria tukienda tukai-*zero in* kwa namna ile tutakuwa tunaleta *quarrels* ambazo katika *practice* mara kwa mara zitakuwa zinashindikana. Hivyo, hii ilivyowekwa hivi ndiyo ina-*fit best practice*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano tuna jambo ambalo linajulikana bidhaa (a) inajulikana ubora wake, hata sasa kuna matumizi haya ambayo huwa tunafanya. Naweza nikatolea mfano, tunajua magari labda yanatumika ya *TOYOTA* na *TOYOTA* tunapajua; ndiyo watu wa magari wengine pia wapo lakini kama unajua pa kununulia kwa nini utafute nanii nyingine ambayo

itachelewesha tu shughuli hiyo. Sasa nimetumia tu *perspective* moja ile, naenda kununua maji yanajulikana pa kununulia, kwamba tununue tu maji kwa mtoa huduma (a) kama maji yako ya aina moja tu? Dunia hiyo tumeshaivuka, lakini hii tunafanya katika kurahisisha utendaji wa shughuli kitu ambacho kina ukomo, kinajulikana na kina *fit value for money.*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mpina, ufafanuzi wa Serikali huo.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokisema hapa ni kwamba, kwanza Waziri anaenda kutengeneza kanuni za kuzungumza jambo gani? Kwa sababu unaposema unamruhusu mtu aende akanunue moja kwa moja; anaenda kununua moja kwa moja kwa sababu gani wakati unajua kabisa Sheria ya Manunuzi inahitaji ushindani? Hapo unatoaje *room* ya kununua moja kwa moja na unasema tena unaenda kutengeneza kanuni, kwani kuna shida gani? Nasema hivi kwa sababu Sheria ya Manunuzi yenyewe kipengele hiki muda wote inasisitiza kwamba unapo-*opt* kwenda kwa mtu mmoja lazima u-*declare* kwamba *okay* hiyo huduma ninayoenda kuipata kwa huyo mtu mmoja ni yeye peke yake, vinginevyo nenda kwenye ushindani, kwa nini unataka kwenda kwenye manunuzi ya mtu mmoja na unajua kabisa manunuzi ni ushindani na ndiyo *base* ya manunuzi?

**MWENYEKITI:** Hebu nieleweshe mimi, ushindani utakuwa unashindana na nani wakati nia yako ni kwenda kwa yule mzalishaji au sijaelewa vizuri?

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti…

**MWENYEKITI:** Ngoja, ununuzi wa moja kwa moja kutoka kwa Mzalishaji, Wakala au Mtoa Huduma; twende vizuri ili niwe nimekuelewa, kama hawa wote wanazalisha kalamu, sawa na unataka ukanunue kule zinakotengenezwa kalamu, ni nani unayemshindanisha maana unataka kwenda wewe moja kwa moja kule kwa muuza kalamu na yako makampuni matatu yanatengeneza kalamu?

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndicho ninachokisema kwamba, kama una kampuni tatu zinazotengeneza na ume-*approve* wewe mwenyewe kwa *TBS* kwamba zote zina viwango vinavyokubalika, kwa nini useme huyu ndiyo a-*supply?* Unachotakiwa kwenda pale ni kwenda kwa njia ya ushindani, lakini hii ya moja kwa moja ikupeleke tu kwa mtu kama kwa mfano labda mtu anazalisha bidhaa hiyo yeye yuko peke yake na mna-*declare* kwamba huyo mtu yuko peke yake hapo ndiyo unaweza ukaenda moja kwa moja, lakini ukisema kwamba una wazalishaji watatu, halafu wewe unamchagua mmoja, hiyo siyo manunuzi tena na utakuwa umekiuka Sheria ya Manunuzi.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, humu ndani huwa nasisitiza sana utulivu mkiwa mnachangia sababu ni hizi; maneno mengi yaliyoko kwenye hii Sheria ni sisi tulisema humu ndani. Tulisema kuhusu *MSD* kwenda huko wanakotengeneza dawa kwa nini nyie hamuendi? Tulisema humu Bungeni, tukasema humu Bungeni kwa nini hamuendi pale, kwa nini hamuendi pale kwa kuamini kwamba kule zinakotengenezwa, hawa wananunua bei rahisi halafu wanakuja kuleta ushindani wa bei ya juu.

Sasa sisi wenyewe sahizi tena tunasema usiende kule tena yaani tusitengeneze mazingira ya wewe Kwenda, kama wako watatu; eeh! Sasa hapo tena hata hii Sheria sijui tutaitengeneza ifanane vipi ili ndiyo iweze sasa kushughulikia hoja zetu zote tunazozisema hapa, kwa sababu kifungu hiki kinafungua mwanya kwamba Waziri akitengeneza kanuni za vile vitu ambavyo sasa itaonekana vinahitaji kwenda kwa mtu mmoja kama ni dawa *panadol* hata kama Kenya, Uganda na wapi wanatengeneza kama imeonekana huko kwamba jamani twendeni Kenya ndiyo ziko bora nenda Kenya huko moja kwa moja kiwandani na ndiyo bei yake. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, haya maneno tulisema wenyewe, sasa tunaenda tunarejea nyuma. Ninachotaka kusema hapa ni kwamba hiki kifungu cha 77 siyo kifungu pekee kwenye Sheria hii, vifungu vingi vimetaja kuhusu ushindani huku, ushindani hapa, ushindani pale, ushindani hapa. Hiki kinatoa mwanya kwamba

ikitokea kuna uwezekano wa kwenda moja kwa moja kununua *cement* kule, sasa jamani si uende huko kiwandani?

Mheshimiwa Mpina sijaelewa, lakini nililiweka hili ili tujue kwamba mambo haya mengi tumesababisha sisi, tena nakumbuka hiyo hoja hasa kuhusu *MSD*. Ndiyo maana huwa inabidi usikilize na wenzio wakiwa wanachangia humu ndani ili iwe... *(Makofi)*

Mheshimiwa Mpina toa hoja Bunge liamue.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja Bunge hili liamue kuhusu hii ibara.

**MWENYEKITI:** Hoja haijaungwa mkono.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 78

**MWENYEKITI:** Kifungu cha 78 Mheshimiwa Mpina.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 78 nimependekeza kufutwa kwa ibara ndogo ya (3) ambayo iknasema: "*Bila kujali kifungu kidogo cha kwanza, Waziri anaweza kutengeneza kanuni za ununuzi wa bidhaa fulani kwa matumizi ya Serikali bila viwango vya manunuzi vilivyoidhinishwa*".

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa viwango vya manunuzi vilivyoidhinishwa vimeidhinishwa na sheria hii, halafu Waziri anapewa mamlaka ya kwenda kutunga kanuni ambayo mpaka hata inai-*undermine* hata Sheria yenyewe. Waziri hana mamlaka ya kutunga Sheria inayokinzana na Sheria mama na Bunge lisiingie kutunga sheria mbaya kama hivi ikubali kufuta kile kipengele cha tatu katika hicho kifungu cha 78 ili kuifanya Sheria iwe na uhai.

**MWENYEKITI:** Mwanasheria Mkuu wa Serikali, hebu fafanua hii 78(3).

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuielewa hii 78(3) nafikiri ni vizuri kusoma Ibara yote kwa pamoja, kwa sababu kwa mfano, Ibara ndogo ya pili, inaeleza kwamba vile viwango vipo vinavyotolewa na vyombo husika vya Serikali. Sasa ibara ndogo ya (3) inahusika na vile ambavyo havikufanyiwa tathmini na vyombo vya Serikali na ndivyo ambavyo sasa inakuwa dhamana ya Mheshimiwa Waziri.

**MWENYEKITI:** Sasa ukishasoma hii (1) na (2), hii (3) hapa inakuwa inafungua mlango wa kazi gani? Ukishasoma hicho kifungu kidogo cha (1) na cha (2), hiki cha (3) ni kwa ajili ya kazi gani? Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mantiki ya pendekezo hili tumesema tunaenda kuanzisha utaratibu wa kuweka bei kikomo, bei ambazo bidhaa ambazo bei zake zinajulikana kwa hiyo taasisi husika itaonesha kwamba maji ya kunywa bei yake huwa ni hii, tofali bei yake huwa ni hii, mfuko wa *cement* bei yake huwa ni hii; tumesema tutaweka bei kikomo za aina hiyo. Hata hivyo, katika Maisha, katika hali halisi katika *practice,* siyo bei zote zitakazoingia kwenye kikomo, siyo bei zote ambazo taasisi husika ama Serikali zitaingia kwenye hiyo orodha ya bei kikomo. Kwa hiyo tunasema zile bidhaa zingine ambazo hazitakuwa zimeingia na zenyewe zitahitaji zitungiwe kanuni.

**MWENYEKITI:** Kama hilo ndiyo lengo, mbona hii tatu kama haisomeki kwa hicho unachosema! Hiki kinasema, "Bila kujali kifungu kidogo cha (1), Waziri anaweza kutengeneza kanuni za ununuzi wa bidhaa fulani kwa matumizi ya Serikali bila viwango vya ununuzi vilivyoidhinishwa."

Kama lengo ni hilo unalosema basi kifungu hiki hakijaweka hayo unayosema wewe kwa sababu hii ni kama vile ina-*defeat* ile (1) na (2), yaani hii namba tatu hapa haijaweka mazingira kwamba zile ambazo hazitakuwa na, yaani zile ambazo hazitakuwa kwenye (1) na (2) ndiyo Waziri apewe sasa, kama sivyo hii (1) na (2) inakuwa kama vile haina maana tena. Eti Mwanasheria Mkuu wa Serikali umeitazama hiyo?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimeitazama.

**MWENYEKITI:** Ukisoma (1), ukasoma (2) halafu ukaja kusoma (3) ni kama tatu inafuta.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu moja imeelezea kwa kuzingatia viwango vilivyowekwa na kuidhinishwa, (2) inatoa wajibu nani wa kuviidhinisha ambapo hapo ndiyo kuna vyombo husika vya Serikali. Sasa (3) kuna ambavyo sasa bila kujali huko ambavyo havikuidhinishwa sasa lazima vitungiwe Kanuni.

**MWENYEKITI:** Ambavyo, samahani sentensi ya mwisho umesemaje?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, yale maneno ya mwisho; "bila viwango vya ununuzi vilivyoidhinishwa," kwa sababu huku mwanzo kuna viwango vilivyoidhinishwa.

**MWENYEKITI:** Jamani utungaji wa sheria kwa Kiswahili hapa ndiyo tutajua changamoto yake, yaani mimi hiki cha tatu kwa kweli sijakielewa hata kinamaanisha nini. Ukisoma moja na mbili ni kama vile kinatoa, yaani kimetoa nguvu kwa mkono wa kushoto kinachukua kwa mkono wa kulia.

Mheshimiwa Waziri uzuri nimesema tangu mwanzo kwamba Kiswahili kinanipiga chenga.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazo bidhaa ambazo tumekubaliana kwamba taasisi husika ndani ya Serikali zitaidhinisha kwamba kwa manunuzi bei ya hivi vitu, bei kikomo zitakuwa hizi na hizi. Tukaelezea kwamba zitakuwepo bidhaa nyingine ambazo hazitaangukia katika eneo hilo. Kwa hiyo, tulisema hizo bidhaa nyingine ambazo hazikupata viwango vilivyoidhinishwa kwamba bei zake ziwe hizi, na zenyewe zinatakiwa zitengenezewe utaratibu wake wa namna ya kununua kikanuni, ni hicho tu tunachokiweka, siyo kutunga ambayo iko nje

ya sheria, iko ndani ya sheria lakini tunasema tunatengeneza mwongozo kwa zile ambazo hazijatajwa bei zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mathalani tumeorodhesha simenti, tumeorodhesha kalamu, labda sasa hatukutaja vikombe kwa hiyo inabidi vitengenezewe kanuni yake ambayo inajitegemea.

**MWENYEKITI:** Shida haya maneno hapa chini yanasema "Kwa matumizi ya Serikali bila viwango vya ununuzi vilivyoidhinisha." yaani hakuna mahali panapoashiria kwamba bidhaa hiyo itakuwa ni ile ambayo haiko kwenye moja wala mbili, ndiyo changamoto ya hii tatu. Lakini kama nilivyosema tangu mwanzo inanipa wakati mgumu sana hii sheria yetu ya Kiswahili, labda tusubiri siku tisini zikiisha wakileta ya Kiingereza basi tutajua nini cha kubadilisha lakini hiki kifungu kidogo cha (3) kwa namna kinavyosomeka hapa hakioneshi kwamba, ni kama vile Waziri atatengeneza Kanuni ambazo zitakuwa zinapoka tena yale madaraka ya (1) na (2). Yaani yale makatazo ya (1) na (2) au maagizo ya (1) na (2) yataondolewa na hizi Kanuni atakazotunga Mheshimiwa Waziri hapo. Kwa hiyo, kidogo inaleta hiyo changamoto lakini sasa mimi ndiyo Mwenyekiti na nimesema dhahiri kwenye kifungu hiki Kiswahili kimenipiga chenga kidogo. Naona Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali unataka kunisaidia.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ingekuwa lugha ya Kiingereza inge-*attempt* hizi *sub (1) and (2)* kuongelea bidhaa ambazo zina *specified* halafu (3) kwa bidhaa ambazo hazina *specification.*

**MWENYEKITI:** Haya Waheshimiwa Wabunge, itakapotokea changamoto Bunge ndiyo hili hili marekebisho yataletwa tusiwe na wasiwasi. Haya Mheshimiwa Mpina.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii Ibara ya 78(3) mimi nakushauri ifutwe halafu hayo mengine hayo kama tutaletewa baadae ndiyo iwe hivyo, lakini tusitoe mwanya hili Bunge kumpa Waziri mamlaka makubwa yaku-*alter down* hiki tunachokitunga hapa.

**MWENYEKITI:** Uzuri wake ni mmoja tu, kwamba anaenda na yeye kuweka Kanuni, yaani hakai nayo haya madaraka halafu akawa anasubiria jambo litokee, anatengeneza Kanuni ambazo hizo Kanuni zitaletwa kwenye Kamati yatu ile. Siyo kabla ya matumizi akishatengeneza tu si huwa zinaletwa hapa mbele, Kamati yetu itaenda izitazame. Kwa hiyo, anaenda kuweka na yeye kwenye Kanuni. Hoja ilikuwa ni kwamba hizi Kanuni anazoenda kutengeneza zisiwe sasa zinaondoa umuhimu wa (1) na (2).

Mheshimiwa Mpina sasa tusiwe na wasiwasi haya madaraka haendi kukaa nayo anaenda kuyatungia Kanuni, ndiyo inavyosema hapa ama situmeelewana? Mheshimiwa Waziri, ndiyo inavyosema hapa anaweza kutengeneza Kanuni za ununuzi, kwa hiyo zile Kanuni Kamati yetu ya Sheria Ndogo itazitazama wakati utakapowadia. Lakini ni jambo ambalo hata ninyi mnapoenda upande wa Serikali mkawe mnakisoma kwa Pamoja, naamini kitakapoletwa kwenye tafsiri kitatuweka mazingira mazuri zaidi.

Wahesimiwa Wabunge, napaswa kumpa Mheshimiwa Mpina ametoa tena ushauri wa kufutwa kwa hiyo toa hoja Mheshimiwa Mpina.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa hoja Bunge liniunge mkono tufute hiki kipengele tusiingie kwenye hii rekodi ya kuharibu sheria za nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**SPIKA:** Haya hoja haijaungwa mkono.

Ibara ya 78

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 79

**SPIKA:** Mheshimiwa Mpina.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa napendekeza hiki kifungu cha 79 kifutwe chote kwa sababu tusiliingize hili Taifa kununua vitu chakavu, vitu ambavyo vinahusu maisha ya watu. Tukanunue treni chakavu, tukanunue meli chakavu, tukanunue ndege. Vitu hivi vyote vinaenda kubeba maisha ya watu, sasa kama Taifa tusiingie huko. Kwa sababu hata sasa hivi hata usimamizi tu wa hizi mpya si tumelalamika sasa hivi majuzi hata ndege mpya tulizozinunua tumelalamika kwamba kuna baadhi ya ndege zilikuwa na kasoro, sasa leo huu ujasiri wa kwenda kununua ndege zilizotumika, ndege chakavu tunautoa wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda ni mfupi lakini ninachoomba ni kwamba Bunge lako liridhie tuondoe haya mambo ya uchakavu, tuende tukanunue vitu vipya badala ya kununua hivi vitu vichakavu ambavyo vinaweza kutuletea matatizo makubwa. Kwanza tuna matatizo makubwa hata ubora wake utau-*assess* vipi, kama ni Ndege unanunua hiyo thamani utaipata wapi ya uchakavu, ubora utau-*assess* vipi, *guarantee* ya hiyo Ndege au hiyo Meli utaipata wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama tunapigwa vipya tuje tuingie tena kwenye vichakavu? Sikushauri Bunge lako liingie kwenye *record* ya kutunga sheria mbaya lakini ya kutunga sheria ambayo mwisho wa siku itaenda kuleta madhara makubwa kwa Watanzania. Hii Ibara ya 79 tuifute kabisa na tutaendelea ku-*invite* hata watu wengine wataleta hata wa madawa watasema hata *CT-Scan* na zenyewe tuwe tunanunua zilizotumika, hata majokofu ya hospitali yenyewe tununue yaliyotumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Daktari wangu aliwahi kununua jokofu lililotumika akatuibia pale Halmashauri baadae na yeye Mwenyezi Mungu akamchukua akapelekwa akaoza na yeye kama walivyokuwa wanaloza wengine. Tusitende hii dhambi kwa Watanzania tufute hiki kipengele, kama Serikali ina sababu za msingi za kuleta hiki kipengele ilishawishi Bunge kwa njia nyingine kwanza kabla ya kuingiza kwenye sheria.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hiki kifungu cha 79 Serikali imeleta marekebisho imeongeza kifungu kidogo cha (6)

ambacho mwanzo hakikuwepo. Kifungu kidogo cha (6) kinasema; "Kanuni zitakazotengenezwa kwa madhumuni ya utekelezaji wa kifungu hiki zitaainisha miongoni mwa masuala mengine sifa na vigezo vitakavyozingatiwa na taasisi nunuzi wakati wa ununuzi wa vichwa na mabehewa ya treni, meli au ndege zilizotumika."

Waheshimiwa Wabunge, ukisoma kifungu kidogo cha (3) kinasema; "Baada ya kupokea maombi kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2) Waziri ataunda Kamati Maalum ya ushauri wa kiufundi itakayokuwa na watu wenye taaluma, ujuzi na uzoefu unaohusiana na ununuzi husika."

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge nadhani tutoe fursa, nakumbuka sijui kama sote tunakumbuka si kuna mabehewa yalinunuliwa ama, si kuna mabehewa yalinunuliwa? Nadhani sasa hiki Kifungu ndiyo kinatoa nafasi ya siyo tu kwa ajili ya mabehewa na vitu vingine ambavyo vitaonekana ni bora, kama sisi tunavyonunua magari yale.

Waheshimiwa Wabunge, sisi si tunanunua magari jamani ambayo yametumika ama? Naona kuna watu wanatingisha vichwa kuashiria kwamba wanaendesha magari mapya wote. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba Waheshimiwa Wabunge tusikilizane vizuri ili tuelewane vizuri kwenye jambo hili. Iko hivi, kama ambavyo umetuongoza tunapitia kipengele kimoja baada ya kingine, kwa sababu hii sheria hatufanyi tu marekebisho tunatunga sheria mpya. Sasa hiki kifungu tunachokiongelea namba 79 siyo kifungu kipya ni kifungu kilikuwepo kwenye sheria ya zamani, si kwamba sasa Serikali inataka kutunga sheria kuruhusu mabehewa yaliyo-*used,* vichwa vilivyo-*used* na vyote kama ilivyoelekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki ni kifungu ambacho kilikuwepo kwenye sheria ya zamani na kimekuwa kikitumika, sasa tumeweka kipengele cha (6) Kipya ambacho tunataka kubainisha kwenye Kanuni usimamizi wa karibu zaidi. Hapa tunatunga sheria ambazo zitakuwa sheria za nchi na masuala haya tunayoyatungia sheria

yanahusisha Serikali na yanahusisha sekta binafsi lakini pia tunaongelea vitu ambavyo ni vikubwa ndiyo uliokuwa msingi zamani walipoweka hii sheria, yaani tunaongelea vile vitu ambavyo ni vikubwa, ukizima kabisha dirisha la kupata vitu vya aina hiyo, kuna wakati vitu hivyo vitapatikana lakini sheria itakuwa umefunga mikono na hujaweka dirisha lolote la kupitia hivyo. Kwa hiyo, hata kwenye maeneo mengine tumeweka hivyo, kikiwa kinaonekana hakina uhitaji hakitumiki lakini kuna baadhi ya vitu ambavyo ukiziba kabisa dirisha hilo *I mean* katika *actual cost* tunaweza tukatengeneza matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kifungu hiki kilikuwepo tunaongezea Kanuni ambayo itaweka usimamizi wa karibu zaidi ambao ndiyo uliokuwa unafafanua na katika siku zilizopita, miaka iliyopita hiki kimekuwa kikitumika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *AG* hiki ni kifungu cha ngapi? Naangalia hapa, 79 kwenye hii sheria mpya ile sheria ya zamani ilikuwa inasemaje, uko nayo hapo, ama huna, kilikuwepo hiki? Mwenyekiti wa Kamati.

**MHE. DANIEL B. SILLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye sheria ya zamani ni kifungu namba 66.

**MWENYEKITI:** Namba?

**MHE. DANIEL B. SILLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namba 66.

**MWENYEKITI:** Namba 66 ahsante. Haya Waheshimiwa Wabunge, kifungu hiki kama alivyotuongoza hapo Mwenyekiti namba 66, kipo kwenye sheria yetu ile ya zamani kama alivyosema Mheshimiwa Waziri, halafu hii sheria tunayotunga leo inachofanya ni kuleta maboresho ya kutengeneza hiki Kifungu kuongeza kifungu kidogo cha (6). Kwamba sasa kisiwe tu vile Kifungu kilivyo kiongezeke kwamba ziwekwe sifa na vigezo kwenye Kanuni ambazo Waziri atatunga.

Mwanzoni hakukuwa na hilo takwa sasa Mheshimiwa Mpina anapendekeza Kifungu chote tufute, mimi nafikiri kulikuwa na hoja za msingi sana kwa nini hiki Kifungu kilikuwepo na kama

nilivyosema nadhani hiki ndiyo kilitupa mwanya lakini sasa tulikuwa hatuna Kanuni, kilitupa mwanya wa kupata yale mabehewa ambayo yataanza kufanya kazi muda siyo mrefu, sijui kama yameshaanza lakini yataanza kufanya kazi muda si mrefu.

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu hapa tumeshaambiwa kama nilivyowasema kwamba Kifungu Kidogo cha (3) kinasema Waziri ataunda Kamati maalum ya kushauri. Kwa hiyo, maana yake ni wataalam wapo huko na wakati mwingine mtu anakuwa amechoka jambo, ni kama ambavyo tunaweza kuwahi vitu ambavyo kuna watu hapa wananitazama kwa sura fulani, kuna mtumba unaweza kuwa mpya pia. Kwa hiyo, watu tusijenge picha ile kana kwamba kitakuja kitu ambacho ndiyo kimechoka yaani kimetumika mpaka basi, Wataalam hapa wametajwa jamani kwamba wataenda kutazama na mimi nafikiri tuafiki hilo tutasubiri Kanuni Waziri akishazitunga na haya maboresho ni mazuri, kwa maana ya utekelezaji wa hii sheria kwa maana ya utekelezaji wa hii sheria sasa ama Kifungu hiki.

Haya, nasikia neno hapana, uzuri anayesema hapana hajaleta marekebisho, Mheshimiwa Mpina toa hoja.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja, hoja hii tuijadili ili tufute kabisa hiki kifungu.

**SPIKA:** Haya, hoja haijaungwa mkono mliosimama mko watano.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 80

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila na mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 81

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 82
Ibara ya 83
Ibara ya 84
Ibara ya 85
Ibara ya 86
Ibara ya 87
Ibara ya 88
Ibara ya 89

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila na mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 90

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 91
Ibara ya 92
Ibara ya 93

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila na mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 94

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mpina.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hili eneo la *variations* tumekuwa tukifanyiwa mchezo mkubwa sana, tenda nyingine zinaenda mpaka mara mbili, mara tatu ya zabuni ilivyokuwa. Kwanza kiwango kile kilichokuwa kinasomwa cha asilimia 30 ni kikubwa na mimi hapa nilikuwa nimependekeza iwe angalau asilimia 15 lakini pia wapate kibali cha *PPRA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupata kibali cha *PPRA* wala siyo kazi ngumu kama ilivyojaribu kuelezwa hapa, kwa sababu mfumo wote wa manunuzi uko kwenye mfumo, kwa hiyo, vyombo vyote hivi vya Serikali vitawasiliana kupitia mifumo, kwa hiyo siyo jambo ambalo litachelewesha, eti kupata *approval* ya *PPRA*. Hii tujiridhishe kwa sababu mtu mwenyewe uliyempa kazi ya ujenzi ni huyo huyo anayeona umuhimu wa *variations* ni huyo huyo sasa lazima uweke jicho la msimamizi la *oversight* ili *PPRA* waweze ku-*approve* hizi *variations,* hiyo itatusaidia kupunguza hasara ya Serikali ambayo tunaingia sasa hivi

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri Serikali wao wenyewe wanakiri, ukisoma ukomo wa bajeti, wanakiri kabisa kwamba hili swala la *variation* linawasumbua kwa taasisi nyingi za Serikali zinavyoweza kufanya *variation* na kupandisha gharama za ujenzi *unnecessary.*

**SPIKA:** Ahsante sana. Serikali imeleta marekebisho Mheshimiwa Mpina umeyaona marekebisho ambayo serikali imeleta?

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ya asilimia 15 nayakubali na ndiyo niliyoyapendekeza pia. Kwa hiyo, hiyo nimekubaliana nayo, lakini sasa *variation* zozote zile zipate kibali cha *PPRA.*

**SPIKA:** Ufafanuzi Serikali, Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeweka ule wigo ambao na Mheshimiwa Mpina amekubali. Naomba na kwenye hili nimshawishi, tuna *lines of command*, tuna utaratibu wa ufanyaji kazi ndani ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye masuala ya mikataba, mshauri wa Serikali kwenye masuala yote ya mikataba ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kwa hiyo, kama jambo linahusisha masuala ya kimkataba *custodian,* na Mheshimiwa Mpina alikuwa kwenye Serikali anajua, *custodian* wa masuala ya mikataba ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kwa hiyo, likitaka kufanyika

badiliko lolote la masuala ya kimkataba linapelekwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. *PPRA* wao wataendelea kusimamia masuala ambayo yanahusisha masuala ya kimanunuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukibadili utaratibu kwamba suala la mkataba badala ya kwenda kufanyiwa *vetting* kwa Mwanasheria Mkuu tukapeleka *PPRA* kuna eneo ambalo tutakuwa tunakosea ile *flow* ambayo inahusika kwa sababu mwisho wa siku kukitokea *conflict* yoyote ambayo inahusisha masuala ya kimkataba anayeshtakiwa ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo ya kimkataba sisi tunapendekeza kama ile ambayo tumekubaliana asilimia iendelee vilevile, lakini masuala ambayo yanahusiana na *vetting* na masuala ambayo yanahusiana na kupata kibali cha kuendelea yaendelee kupita kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa sababu ndiyo *best practice* duniani kote, *custodian* wa masuala ya kimkataba ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Ikumbukwe hii sheria ambayo tunatunga inawahusu *PPRA* moja kwa moja, hili jambo wao wataendelea kusimamia yale ambayo sheria inawataka wasimamie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuomba Mheshimiwa Mpina akubaliane na huu utaratibu, *PPRA* wataendelea kuhusika kwa sababu hizi ni taratibu zinazohusisha manunuzi, lakini mikataba iendelee kwenda kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mpina, umeelewa?

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu ya usimamizi wa utekelezaji wa mikataba ni kazi ya *PPRA*. Majukumu ya kuangalia *compliance* katika manunuzi ni kazi ya *PPRA*. Hayo ndiyo majukumu ya *PPRA*, sasa nitasikitika kama Waziri hajui *function* za taasisi yake ya *PPRA*. Majukumu haya ni ya kwake *PPRA* na mimi ninachotaka ni *intervention* ya *PPRA* iwahi mapema ili tusiendelee kupoteza fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *variations* umetangaza *tender* ya shilingi bilioni 100 na mpaka *tender* inamalizika ina shilingi bilioni

200 sasa kwani kuwapa *PPRA* mamlaka ya ku-*approve* hizo *variations* kuna tatizo gani? Kwa nini *CAG* asiwe ana-*approve* kwenye *consolidated fund?* Kwa nini ana-*approve?* Yeye ndiyo *oversight* katika eneo hilo lakini ana-*approve* fedha zinapotoka ili azione zinaenda wapi…

**MWENYEKITI:** …Mheshimiwa Mpina, toa hoja.

**MHE. LUHAGA J. MPINA: M***heshimiwa Mwenyekiti, natoa hoja. Bunge lako pamoja na kwamba limechoka lakini likatae hii... (Kicheko)* **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mpina, ngoja tuelewane vizuri, yaani tumechoka kwa sababu tumekaa muda mrefu leo au unamaanisha nini? Washa kisemeo. *(Kicheko)*

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tuiache hiyo, naomba hii Ibara hii…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ngoja, ngoja, acha unamaanisha nini?

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamaanisha kwamba Bunge lako hapa kwenye kipindi cha Kamati kwa sasa, kwa bahati mbaya kumetokea marekebisho mengi katika sheria na bahati nzuri hata wewe mwenyewe umesema kwamba ni kwa mara ya kwanza Bunge hili linajadili sheria iliyoandikwa kwa Kiswahili. Kwa hiyo, kila mtu amechoka kufikiri kutoka kwenye Kiingereza kuja kwenye Kiswahili. Kwa hiyo, nilipokuwa nasema…

**MWENYEKITI:** Hapana, hapana, ngoja kwanza Mheshimiwa. Futa hayo maneno kwanza, Bunge halijachoka lipo hapa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, si mnaona pale dakika zilizobaki, lakini kwa sababu tupo kwenye utungaji wa sheria ndiyo maana hatuwezi kupitisha haya mafungu, ndiyo maana tunakusikiliza hata wewe, la sivyo ningekuwa nimeshakatisha mjadala saa nyingi kabisa. Tunatunga sheria na unaona kila mtu ametulia

humu ndani kuashiria kwamba tuko vizuri. Sasa ukisema tena Bunge…, hiyo lugha hebu futa kwanza, sitaki hata kuirejea.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayaondoa hayo maneno.

**MWENYEKITI:** Shukrani na ahsante sana. *(Makofi)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 95
Ibara ya 96
Ibara ya 97
Ibara ya 98
Ibara ya 99
Ibara ya 100
Ibara ya 101

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 102
Ibara ya 103

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 104
Ibara ya 105
Ibara ya 106

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 107

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 108
Ibara ya 109
Ibara ya 110
Ibara ya 111
Ibara ya 112
Ibara ya 113
Ibara ya 114
Ibara ya 115
Ibara ya 116
Ibara ya 117

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 118
Ibara ya 119
Ibara ya 120

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 121
Ibara ya 122

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 123

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 124
Ibara ya 125

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 126
Ibara ya 127

Ibara ya 128

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 129
Ibara ya 130

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya marekebisho yale ambayo tumeshayafanya namba ya vifungu inabadilika kwa sababu kuna kifungu kipya cha 62 kiliongezwa na Serikali. Kwa hiyo, kile kifungu kilichokuwa 62 sasa kitakuwa cha 63 na hivyo tutaendelea badala ya kuishia 130 tutaishia 131.

Waheshimiwa Wabunge, marekebisho hayo ya namba za vifungu yanaafikiwa?

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imekamilisha kazi yake.

*(Bunge Lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Mtoa hoja, taarifa.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imepitia Muswada wa Sheria ya Ununuzi wa Umma wa mwaka 2023 kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na marekebisho yake.

Mheshimiwa Spika naomba kutoa hoja kwamba taarifa hiyo sasa ikubaliwe rasmi.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa nitawahoji, Waheshimiwa Wabunge wanaoafiki hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha kuhusu Muswada wa Sheria ya ya Ununuzi wa Umma wa mwaka 2023 waseme ndiyo, wasioafiki waseme siyo.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wote mmeafiki kwa hiyo waliosema ndiyo wameshinda na ndiyo wote, kwa hiyo muswada wetu umeshahojiwa na umepitishwa.

Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria kwa ajili ya kuweka masharti bora ya Usimamizi wa Ununuzi wa Umma na Ugavi kwa lengo la kutatua changamoto zilizobainika katika utekelezaji wa masharti na taratibu za ununuzi na ugavi**

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

*(Muswada wa Sheria ya Ununuzi wa Umma wa Mwaka 2023 Ulipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muswada umesomwa kwa mara ya tatu na unakamilisha utaratibu wetu kama Bunge wa kutunga sheria. Kwa hiyo, sisi tumemaliza kwa sehemu yetu na hivyo tutampelekea Mheshimiwa Rais ili na yeye afanye kwa sehemu yake kama Katiba inavyotaka halafu tutawaletea mrejesho Waheshimiwa Wabunge kama Mheshimiwa Rais atakuwa ameridhia sheria hii. *(Makofi)*

Natumia fursa hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa namna ambavyo mmeshiriki katika zoezi la utungaji wa sheria hii muhimu sana ambayo Serikali imeleta muswada ili sisi tuweze kuangalia yale mambo ambayo tumekuwa tukiyasema mara nyingi humu Bungeni na Serikali imeweza kufanya hivyo nawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yenu mingi ambayo imepelekea muswada huu kuwa katika hali hii uliyopo.

Pia, naishukuru sana Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti. Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na wajumbe wote tunawashukuru sana kwa kufanya kazi nzuri sana kwa niaba yetu sisi sote. Mmefanya kazi nzuri na kwa kweli tunawapongeza na kuwashukuru pia.

Pia nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote chini ya Wizara hii kwa kuendelea kuwa wasikivu katika mawazo ambayo Waheshimiwa Wabunge huwa wanatoa katika vipindi mbalimbali na hata kipindi hiki ambacho mmeleta marekebisho haya bado Wabunge wameendelea kutoa mawazo yao na mmeyafanyia kazi na mmeleta marekebisho. Tunawapongeza sana kwa kazi nzuri ambayo mmeifanya ya kushirikiana vizuri na Bunge katika utungaji wa sheria hii.

Tunawatakia kila la kheri katika utekelezaji na mengine Waheshimiwa Wabunge wameyachangia wakati wa mjadala nayo mtaendelea kuyachukua muone namna ambayo Serikali inaweza kuendelea kuimarisha utendaji kazi wake kwenye hili eneo la manunuzi. Tunawatakia kila la kheri katika utekelezaji wa sheria hii.

Waheshimiwa Wabunge, tukishamaliza sisi kutunga sheria kazi yetu haiishii hapo, sheria hii ni kati ya sheria ambazo zinahitaji kanuni nyingi sana zikatungwe ili iweze kufanya kazi kwa ufanisi. Kwa hiyo, kazi yetu kama Bunge bado itaendelea ya kuangalia hizi kanuni ambazo sheria imemruhusu Waziri Kwenda kutunga na kuangalia namna ambavyo zinakidhi yale matakwa ambayo sheria imesema.

Kwa hiyo, itakuwa ni kazi ya Kamati yetu ya Sheria Ndogo, kwa muktadha ule wa kuzitazama kanuni ambazo zimeshaanza kufanyiwa kazi na siyo ile ya kuleta kabla kwa sababu Katiba imeturuhusu kukasimu madaraka hayo na sisi tumekasimu kwa Waziri kama tulivyotunga sheria hii.

Pamoja na hayo, Mheshimiwa Waziri kwa sababu umeshayaona maeneo mbalimbali ambayo Wabunge walikuwa wakiyaeleza kama vile kuonesha wasiwasi, kanuni hizo zikishatengenezwa uzitazame kwa maana ya kuangalia ule wasiwasi uliokuwa unaelezwa na Wabunge. Pia zitakapofika kwenye Kamati yetu basi itawaletea mawazo yao na ninyi naamini mtayafanyia kazi kama ambavyo mmeyafanyia kazi mawazo mengine ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kusema hayo, nilikiri leo na ninaendelea kukiri kwamba kutunga sheria kwa Kiswahili siyo masihara. Kuna kifungu humu kwenye hii sheria kinachohusu manunuzi ya bidhaa za afya, baada ya yale marekebisho ambayo mmeyafanya, sijajua kwa Kiingereza kitasomeka namna gani, lakini kwa Kiswahili kinasomeka kana kwamba kimekaa pale, lakini mambo yote yaliyowekwa pale yanataraji kwenda kuwekewa utaratibu fulani. Kwa hiyo, mtaenda mtazame vizuri hicho kifungu kama kitahitaji marekebisho ili tuweze kuharakisha ule ununuzi wa madawa ambayo yanahitajika kwa haraka na tusijekuwa tumetunga sheria ambayo itaweka mlolongo mrefu halafu zile dawa zikawa hazipatikani kama ambavyo tumekuwa tukisema huko nyuma. *(Makofi)*

Kwa hiyo, hiki kifungu, nimekiona mahsusi kwa sababu kinahusu kuokoa maisha ya watu, kwa hiyo, ni muhimu mkakitazame kwa sura hiyo. Kama kitaleta sura nyingine basi Bunge ndiyo kazi yake kutunga sheria, hatutasita kukibadili kama kitaleta changamoto. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunawatakia kila la kheri katika utekelezaji wa hayo yote.

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimemuahidi Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, aliomba mwongozo kabla hatujahitimisha

kipindi chetu cha kwanza siku ya leo. Sasa nimpe nafasi aeleze ni jambo gani analotaka kulizungumza.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nimeomba Mwongozo kwa Kanuni ya 76 sitaisoma kutokana na muda.

Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako, kumekuwa na utaratibu unaotumika humu ndani na hasa leo imekuwa zaidi. Mheshimiwa Waziri Mkuu anapokuwa amekaa kwenye kiti chake, kuna Wabunge wanaenda wanakaa kwa muda mrefu sana. Mimi ninaamini Waziri Mkuu ni msimamizi wa shughuli za Kibunge pia, kuna mambo anahitaji kuyasikiliza. Pia kama mwanadamu ana mambo yake binafsi anaweza kuhitaji kuyafanya pale kwenye kiti chake alichokaa.

Mheshimiwa Spika, si hivyo tu, Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu sijajua kwa sababu ni mgeni watu wanaenda kumpa pongezi, siku ya leo siku nzima ni kama hospitali, watu wamekuwa wakikaa pale toka asubuhi mpaka ulivyokuwa ukifunga Bunge lako saa saba. *(Makofi)*

Sasa mimi naomba mwongozo wako, najua kabisa wanao wajibu wa kuongea na Wabunge, tunayo nafasi, hata mimi wakati mwingine huwa ninaenda. Je, mwongozo unasemaje, mtu anapoweza kukaa hata zaidi ya dakika 40 akiongea na Waziri kwa muda mrefu na akitoka anakuja na mwingine na mwingine. Naomba Mwongozo wako.

Mheshimiwa Spika, wakati mwingine Mheshimiwa Waziri Mkuu anapotoka kwenye kiti chake anapotoka nje hatujui ana dharura gani, njiani anapotembea, na umekuwa ukionya, wanamsimamisha kwa muda, sasa yeye ni mtu mzima hawezi kusema anakimbia kwa sababu gani kutoka nje au inakuaje.

Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako niweze kuelewa, utaratibu wa Kibunge unasemaje? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, amesimama hapa Mheshimiwa Sophia Mwakagenda akiomba Mwongozo kuhusu Mheshimiwa Waziri Mkuu na namna ambavyo Wabunge tunatumia muda wake mwingi akiwa hapa Bungeni na sasa imetokea kwa Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, naye vivyo hivyo. Hili jambo nadhani nilishaeleza kwa kirefu sana huko nyuma na sikusudii kueleza kwa kirefu siku ya leo.

Waheshimiwa Wabunge, nilishatoa katazo la kumzuia Mheshimiwa Waziri Mkuu anapoingia au anapotoka, lakini inaonekana hilo katazo Wabunge aidha hawanielewi ama najaribu kutazama viti upande anaopita havina watu sasa kwa hiyo sijui nitarudia mara ngapi ili watu waelewe kwamba ni katazo. Kwa sababu kama nilivyowahi kusema huko nyuma anaweza kuwa ameitwa kwa haraka, sasa wewe ukimsimamisha hapo na yeye ni mstaarabu anaona hawezi kukupita, kwa nini usikae? Muache Waziri Mkuu aende na arejee, ndiyo maana kiti kimewekwa pale. Kama una jambo nenda hapo. Wengine mnasimama huko njiani mnaanza kusema hoja zenu.

Waheshimiwa Wabunge, naomba sana pamoja na upole wa Waziri Mkuu na Naibu Waziri Mkuu tusiichukulie sasa kwamba unaweza ukapiga naye *story* kama vile, tuheshimu nafasi hizo, ni kubwa sana na sisi Wabunge ni lazima tuoneshe mfano. Kwa hiyo, tusimsimamishe Mheshimiwa Waziri Mkuu huko njiani. *(Makofi)*

Pia pale kwenye kiti nilishawahi kutoa mwongozo. Tusitumie muda mrefu sana kwa sababu ana wasaidizi na ana ofisi. Sasa mtu atasema, Mheshimiwa Waziri Mkuu hata nilikuja pale kwenye kiti chako nikakuambia hoja yangu, ndiyo maana kapewa wasaidizi, ili unapomueleza hoja yako awepo wa kufuatilia. Sasa pale atafuatilia nani? Unataka umwambie kisima kimepasuka, barabara imeanguka na mambo kama hayo sasa hapo atafuatiliaje? *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nadhani Mwongozo nilishautoa huko nyuma, kwa hiyo, alichokisema kichukuliwe hivyo hivyo kwamba ni jambo ambalo tuwasaidie viongozi wetu hawa kwanza waweze kufuatilia mjadala Bungeni. Wanapokuwa ofisini wanawaza yale mengine, humu ndani wanataka wasikie

Waheshimiwa Wabunge mnasema nini, msichukue muda mrefu sana, la sivyo utaniweka kwenye wakati mgumu wa kuanza kukuambia toka. Baada ya kuwaacha kidogo wenyewe mmeshaanza kuona kuna changamoto.

Ninawaomba tulifanyie kazi hilo kwa kadri tuwezavyo ili tusiwaweke viongozi wetu kwenye mazingira magumu maana yeye hawezi kukufukuza pale kwamba bwana nenda. Mwingine anaenda pale anashika na simu yake anaanza kuchati akiwa amekaa pale. Kwa hiyo, mazingira kidogo tunayaweka magumu kwa viongozi wetu hawa kutaka watujibishe ama waseme jambo, tusifanye hivyo.

Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana kwa kazi nzuri mliyoifanya siku ya leo na sasa ninaahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 2.00 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa, Tarehe 8 Septemba, 2023 Saa Tatu Asubuhi)*